BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Thelathini – Tarehe 27 Mei, 2016

(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Tukae. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI: Hati za kuwasilisha Mezani.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI: Maswali.

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Tutaanza na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Na. 249

Ufufuaji wa Viwanda Nchini

MHE. RASHID A. SHANGAZI (K.n.y. MHE. JAMAL KASSIM ALI) aliuliza:-

Serikali katika kipindi hiki imejipanga kufufua viwanda vyetu:-

Je, katika mipango hiyo mizuri, Serikali imejipanga vipi kusaidia wananchi kuweza kuanzisha viwanda hivyo?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jamal Kassim Ali, Mbunge wa Magomeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kufufua viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo havifanyi kazi ili kuongeza ajira kwa vijana na pato la Taifa. Kupitia Wizara yangu na kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina tunafuatilia mikataba ya viwanda vilivyobinafsishwa ili kuona utekelezaji wa mikataba ya mauzo kama kufanya uperembaji wa kina ili kujiridhisha kabla ya kuvirejesha kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inaendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji kwa wazawa na tunahimiza Halmashauri za Wilaya zote nchini pamoja na Mamlaka za Mikoa kutenga maeneo katika wilaya, vijiji, kata ili yaweze kutumika kwa ajili ya uwekezaji. Serikali imejipanga kuwezesha upatikanaji wa maeneo ya kujenga viwanda, kuhamasisha uwekezaji katika viwanda, kushauri kuhusu upatikanaji wa mitaji na teknolojia ya kisasa, kuwaibua wanaviwanda, kuwalea na kuwaendeleza kupitia viatamizi *(incubators)* lakini kadhalika kutoa ushauri wa kitalaam na kujenga miundombinu wezeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji wazawa wanashauriwa kutafuta wabia wenye mitaji au kuungana nao na kuomba mikopo katika benki mbalimbali hususan *TIB.* Pia, Taasisi za Serikali za *TBS, TIC, TIRDO* na Benki ya Wakulima, zinaelekezwa kutoa maelekezo na huduma inayotakiwa ili kufanikisha wazalendo kuwekeza katika viwanda.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shangazi swali la nyongeza.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa, Serikali ya Awamu ya Tano imejipambanua kwamba itakuwa ni Serikali ya viwanda, je, Selikali ina mpango gani wa kuanza kufufua viwanda hivi ambavyo vilikufa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Kiwanda cha Chai cha Mponde kilichoko katika Wilaya ya Lushoto, Jimbo la Bumbuli, kimefungwa kwa takribani miaka mitatu sasa na mpaka sasa hakijaanza uzalishaji. Mara ya mwisho wakati Msajili wa Hazina anakuja pale alituambia kwamba zimeandaliwa shilingi bilioni nne kwa ajili ya kuanzisha shughuli za uzalishaji na kwenye randama ya Wizara ya Fedha na Wizara ya Viwanda na Biashara fedha hiyo hatujaiona. Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu kufunguliwa kwa kiwanda hiki?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Shangazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Serikali imedhamiria kujenga viwanda na hasa kuanzia viwanda vidogo sana, viwanda vidogo, viwanda vya kati pamoja na viwanda vikubwa. Mikakati ambayo Serikali inaichukuwa kwa sasa ni pamoja na kutengeneza mazingira wezeshi ikiwa ni pamoja na kuimarisha miundombinu ili kuwawezesha Watanzania kuwekeza zaidi. Mkakati wa pili ni kufanya utafiti hasa kwa viwanda ambavyo vimedhoofika au vimekufa ili kuviweka katika mazingira mazuri ili kutafuta wawekezaji wengine kwa ajili ya kuviendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo, nimhakikishie Mheshimiwa Shangazi tu kwamba Serikali inafanya mikakati mingine ya ziada ikiwa ni pamoja na kutoa mikopo kama mnavyoona kwamba Serikali itatoa mikopo shilingi milioni 50 kila kijiji ili kuwawezesha Watanzania waweze kufanya pia biashara kuendesha viwanda vidogo vidogo. Pamoja na hayo, Serikali imeweka mazingira ya kisera na kisheria ili kuhakikisha kwamba sasa tasnia ya viwanda inaimarishwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusiana na Kiwanda cha Chai cha Lushoto, ni kweli kabisa kiwanda hiki kimedhoofu na siyo Lushoto tu, viwanda vingi vimekufa sehemu mbalimbali. Mkakati wa Serikali uliopo ni kuhakikisha

kwamba inatafuta wawekezaji binafsi ili waweze kujadiliana na wenye kiwanda hicho ili wawekezaji hao waweze kukiimarisha Kiwanda cha Lushoto na kianze kufanya kazi kama kawaida.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nadhani tuendelee. Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, kwa hiyo, tusubiri ya kwake ya Nishati.

Na. 250

Kiwanda cha Manonga na Kiwanda cha Nyuzi - Tabora

MHE. MWANNE I. MCHEMBA (K.n.y. MHE. SEIF K. S. GULAMALI) aliuliza:-

(a) Je ni lini Serikali itakwenda kuona hali ya Kiwanda cha Manonga na kukifanya kiweze kufanya kazi na kutoa ajira kwa vijana wa Mkoa wa Tabora?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kukiangalia upya Kiwanda cha Nyuzi Tabora ili uzalishaji uweze kuanza?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mbunge wa Manonga, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji yupo tayari kwenda Manonga na kutembelea Kiwanda cha Manonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imedhamiria kukifufua Kiwanda cha Manonga *Ginnery* ili kiweze kufanya kazi na kutoa ajira kwa vijana wa Mkoa wa Tabora. Pamoja na jitahadi za Wizara yangu na Msajili wa Hazina, mkakati wa kufufua sekta ya pamba pamoja na nguo *(cotton to clothing strategy)* utaongeza uzalishaji wa pamba. Chini ya mkakati huo tunalenga sasa kuongeza uzalishaji wa pamba kwa tija lakini wingi wa pamba utapelekea pia kutosheleza mahitaji na matumizi ya *ginneries* ikiwemo ikiwemo *Ginnery* ya Manonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Tabotex kilichopo Mkoani Tabora kimekuwa kikifanya shughuli za usokotaji nyuzi tangu mwaka 1978 chini ya umiliki wa Serikali. Ilipofika Aprili, 2004, Serikali ilikibinafsisha kiwanda hicho kwa kampuni za *Noble Azania Investment Limited* na *Rajani Industries Limited*. Kiwanda hicho hakijafungwa bali kimesimamisha uzalishaji kutokana na changamoto ya soko la nyuzi ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha *Tabotex* kilisimamisha uzalishaji Mei, 2015 kutokana na kuwa na akiba *(stock)* kubwa ya nyuzi zilizozalishwa mwaka 2013 ambapo hadi sasa zinaendelea kuuzwa. Soko kubwa la nyuzi za *Tabotex* ni soko la nje huku kiwango kidogo kikiuzwa katika soko la ndani. Kawaida wanunuzi wakubwa wa nyuzi ni viwanda vinavyofanya shughuli za ufumaji wa vitambaa lakini viwanda vyote vinavyofanya kazi ya ufumaji vitambaa nchini vikiwemo *21st Century, Sunflag Limited,* Urafiki, *NIDA* na *Musoma Textile* vina mitambo yake ya kusokota nyuzi, hivyo soko la ndani la *Tabotex* kuachwa kwa wafumaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hilo sasa, kiwanda hicho sasa kinatafuta mwekezaji ambaye atakuwa tayari kuingia nacho ubia kwa kupanua wigo wa uzalishaji na kukufua shughuli za ufumaji vitambaa *(weaving)* hadi ushonaji. Wadau tushirikiane ili tupate mshirika atakayeweza kuboresha shughuli za kiwanda cha *Tabotex*.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanne Mchemba swali la nyongeza.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hivi karibuni kulikuwa wawekezaji kutoka China ambao walitarajia kufika Mkoa wa Tabora tarehe 22 na safari yao kuahirishwa *Air Port* baada ya kuwa na dosari ndogo ndogo za *visa*. Je, ni lini sasa wawezekezaji hao ambao wataanzia kusimamia na kuangalia maeneo ya Kiwanda cha Tumbaku pamoja na Manonga safari yao itakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, kwa kuwa Kiwanda cha Nyuzi kina historia ndefu na mpaka sasa hivi ninavyosema kiwanda hicho hakifanyi kazi na wameondoa mitambo yote ambayo ilikuwepo pale. Je, Serikali iko tayari kufuatilia mitambo hiyo ambayo imeng'olewa pale? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Kiwanda cha Manonga kwamba kulikuwa na Wachina wanakuja, wameishia *Air Port* kwa sababu ya masuala ya *Immigration* na mambo mengine, ni lini sasa watakuja. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kuwasiliana nao ili kuona lini watakuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la pili kuhusiana na Kiwanda cha Nyuzi kwamba Serikali iko tayari kufuatilia sasa kuhakikisha kwamba kinafanya kazi. Nimhakikishie kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Serikali iko tayari kufuatilia na kuhakikisha kwamba kinafanya kazi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Masoud swali fupi.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nina swali moja dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vilivyobinafsishwa ni kikwazo cha maenedeleo katika maeneo mengi. Katika hotuba ya Mheshimiwa alisema kuna viwanda 34 ambavyo vilibinafsishwa na Serikali ina mkakati wa kuweza kuvifufua. Pia kwenye majibu yako Mheshimiwa Naibu Waziri umesema kwamba mnapitia upya mikataba. Je, katika mikataba hiyo, mna mkakati gani wa ziada kuhakikisha kwamba mikataba ya Viwanda vya Korosho vya Lindi na Mtwara ambavyo vilibinafsishwa na hadi leo kuna tatizo kubwa la kupatikana kwa maendeleo katika mikoa hiyo? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ya ziada ambayo Serikali inaifanya, cha kwanza kabisa, viwanda vingi vilikufa kwenye miaka ya 1990 na 1998. Jambo la pili, viwanda vingi vilikufa kwa sababu ya kukosekana kwa malighafi au kuwepo kwa malighafi lakini kupungua kwa soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha tatu ni Sera ya Ubinafsishaji. Sasa mikakati ya kikatiba, kisheria na kimkataba, kwanza ni kutazama sasa hali halisi ya soko la dunia lakini hali halisi ya viwanda vingine na ku-*review* mikataba hiyo ya

kiuwekezaji. Hatua ya pili, ni kutazama sera yetu sasa ya uchumi ambapo tunaelekea kwenye uchumi wa viwanda na kutazama sasa mikataba yetu iwe namna gani ili kuvifufua viwanda hivyo.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango.

Na. 251

Malipo ya Wastaafu wa Iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki

MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA aliuliza:-

Je, Serikali imeshalipa stahiki za wastaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suzana, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshalipa stahili za wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki iliyovunjika Juni, 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya 2005 na 2010, Serikali iliwalipa wastaafu 31,519 kati ya wastaafu 31,831 wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Serikali ililipa jumla ya shilingi bilioni 115.3. Wastaafu waliolipwa stahili zao ni wale ambao walijitokeza na kuthibitishwa na waliokuwa waajiri wao yaani mashirika waliyokuwa wakiyafanyia kazi. Aidha, katika kipindi cha 2011 mpaka 2013, Serikali iliendelea kuwalipa wale ambao walikuwa hawajalipwa *(on a case by case basis)* ambapo wastaafu 269 walilipwa kiasi cha shilingi bilioni 1.58 na kufanya jumla ya wastaafu waliolipwa kufikia 31,788 na kiasi kilicholipwa kufikia shilingi bilioni 116. 88.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kupokea madai mapya lilisitishwa tarehe 13 Desemba, 2013 kwa mujibu wa makubaliano kati ya wawakilishi wa wastaafu wakiwa na Wanasheria wao kwa upande mmoja na Serikali kwa upande mwingine.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Suzana Chogisasi Mgonukulima, swali la nyongeza.

MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri hasa kwa baadhi ya wastaafu hao kusitishiwa zoezi wakati walikuwa watumishi wa halali. Hii inaashiria kuwa Serikali haikuwa na orodha sahihi ya wastaafu hao. Pia stahiki walizolipwa ilikuwa ni kusafirishia mizigo na wala siyo kiinua mgongo. Je, Serikali itawalipa lini kiinua mgongo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imeomba fedha ya kulipa madeni kwenye bajeti ya mwaka 2016, je, madeni hayo ni pamoja na ya wastaafu hao? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme kwamba hawa watumishi wa iliyokuwa Afrika Mashariki walipokuwa wanastaafu kazi, mafao yao ya kustaafu yalikuwa yanakokotolewa na kuunganishwa na kipindi ambacho walikuwa wanafanyia kazi Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kipindi chote walichofanyia kazi kwenye mashirika husika. Pamoja na kulipwa mafao yao kwa namna hiyo, walikwenda wakafungua kesi Na.93 ya 2003, wakidai walipwe mafao ya utumishi waliyotumikia kipindi wakiwa Jumuiya ya Mashariki. Serikali iliwaomba tufanye mazungumzo nje ya Mahakama wakakubali na tulifanya mazungumzo na 2005 Serikali ndipo ilikubali kuwalipa wafanyakazi 31,831. Mwezi wa Septemba, tulifikia makubaliano (*Deed of Settlement)* kwamba baada ya kuwalipa wastaafu hao hapatakuwa na madai mengine tena na ndiyo tuliwalipa kama nilivyoeleza katika jibu la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, swali la ni lini tutawalipa kiinua mgongo tulishamaliza na Serikali haidaiwi tena. Pia ni muhimu nieleze kabisa kwamba pamoja na kufikia *Deed of Settlement* bado tulitoa muda wa zaidi ya miaka saba ambapo wastaafu walikuwa wanakuja wanalipwa *on a case by case basis.* Kwa hiyo, Serikali hatudaiwi tena na wastaafu hao.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Faida Bakar.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba wastaafu wa Afrika Mashariki hakuna tena na Serikali haidaiwi tena lakini mimi nasema Serikali inadaiwa, wako wengi. Mimi mwenyewe nina ushahidi, kuna mzee mmoja kule Pemba alikuwa anafanya kazi *Custom,* anaitwa Mzee Mohamed Kombo Maalim, alikuwa Askari wa *Custom,* mpaka kafariki hajalipwa mafao yake, ni mzee wetu kabisa. Sasa naomba kusema kwamba Mheshimiwa Waziri asitudanganye, aseme ukweli na sisi atujibu hapa, hawa waliobakia watalipwa lini? Wapo, hawajalipwa, nina ushahidi kamili! *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, hawa ambao hawakuridhika walienda tena Mahakamani wakafungua kesi, Shauri la Rufaa Na. 73 la 2013. Mahakama ya Rufaa imeamua tarehe 29 Januari, 2016, mwaka huu, kwamba madai hayo waliyokuwa wanadai kwamba wamepunjwa hayakuwa halali na hayapo tena. Kwa hiyo, ile ndiyo mwisho wa safari…

MBUNGE FULANI: Wako ambao hawajalipwa kabisa.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Sasa hii ni Mahakama ya Rufaa, ndiyo mwisho wake pale.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Huyu hajaenda Mahakamani, kafariki!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Faida zima *microphone* tafadhali!

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Aah, aah!

NAIBU SPIKA: Naomba uzime *microphone!*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini.

Na. 252

Usambazaji wa Umeme Kupitia *REA*

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI (K.n.y. MHE. LAMECK O. AIRO) aliuliza:-

Usambazaji wa umeme kupitia *REA* ulikusudiwa kufikishwa kwenye vijiji na senta 54 kwenye Awamu ya II na ingewezesha upatikanaji wa umeme asilimia 25-30, kwani upatikanaji wa umeme kabla ya mpango huo ulikuwa ni asilimia 5 na kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya umeme kwa maendeleo ya wananchi wa Rorya umeme wa asilimia 25 bado ni wa chini na hata hivyo bado mradi unasuasua:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kasi ya usambazaji umeme katika Wilaya ya Rorya?

(b) Je, ni lini Mpango wa *REA II* utakamilika na kuanza *REA III*?

(c) Je, *REA III* ina vijiji na senta ngapi ndani ya Wilaya ya Rorya?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rorya, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa *REA* Awamu ya II kwa Wilaya ya Rorya ulitarajia kufikisha huduma ya umeme katika vijiji 44. Mradi huu upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo ujenzi wa njia kubwa ya umeme msongo wa kilovoti 33 na ufungaji wa transfoma umekamilika kwa asilimia 95 na wateja zaidi ya 300 katika vijiji 16 wameunganishiwa umeme kwa sasa. Ili kuhakikisha mradi unakamilika kwa muda uliopangwa, Serikali imeongeza kasi ya usimamizi wa karibu pamoja na kumwelekeza Mkandarasi *Derm Electric* kukamilisha kazi hizo kwa wakati.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa *REA,* Awamu ya II utakamilika mwishoni mwa Juni, 2016. Vijiji vitakavyobaki katika *REA* Awamu ya II vitaunganishiwa umeme kupitia *REA* Awamu ya III itakayoanza Julai, 2016.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Rorya, vijiji vipatavyo 56, sekondari nne na kanisa moja vinatarajiwa kupatiwa umeme katika Mpango wa *REA* Awamu ya III.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chegeni swali la nyongeza.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na kazi nzuri aliyofanya katika Jimbo la Rorya, naomba tu nimuulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile ahadi ya Serikali kupitia *REA III* itakamilisha mradi kabambe wa kuweka umeme katika Jimbo la Rorya kuanzia tarehe 1 Julai, 2016. Je, Waziri anawahakikishiaje wananchi wa Rorya kwamba katika *REA III,* vijiji vyote vilivyobakia kupata umeme vitapata umeme huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa vile Mpango wa *REA III* uko mpaka Jimbo la Busega na kuna Kituo cha Afya cha Lukungu pale Lamadi hakina umeme na kimeshapatiwa tayari vifaa kutoka Shirika la *AMREF*. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kunihakikishia kwamba kupitia *REA III* Kituo hiki cha Afya cha Lukungu na chenyewe kitapata umeme huo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Nishati na Madini.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chegeni aliyeuliza kwa niaba ya Mheshimiwa Mbunge wa Rorya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa *REA II* tunatarajia itakamilisha kazi zake mwisho wa Juni, 2016. Nichukue nafasi hii, siyo kwa Jimbo la Rorya tu lakini na kwa Wabunge wengine, nimhakikishie Mbunge wa Rorya kwamba vijiji vyote ambavyo vilikuwa katika *REA* Awamu ya II ambavyo havitakamilishwa, pamoja na kwamba tunataka vikamilishwe, vitaingizwa katika *REA* Awamu ya III. Ni mpago wa Serikali kwamba vijiji vyote hapa nchini ambavyo havijapata umeme katika *REA* Awamu ya II vitapatiwa umeme katika *REA* Awamu ya III inayoanza Julai, 2016. Nirekebishe kidogo swali la Mheshimiwa, amesema tarehe 1 Julai siyo kukamilisha, tarehe 1 Julai sasa ndiyo tunaanza *REA* Awamu ya III itakayoendelea kwa miaka mitatu, minne hadi mitano, ile Awamu ya II ndiyo itakamilika Juni, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusiana na Jimbo la Busega kupatiwa umeme wa uhakika *REA* Awamu ya III, ni kweli viko vijiji vya Mheshimiwa Mbunge wa Busega, Mheshimiwa Dkt. Chegeni ambavyo vilikuwa viunganishwe umeme kwenye *REA* Awamu ya II lakini havijapata umeme ikiwa ni pamoja na Hospitali ya Lukungu katika Mji wa Lamadi. Tunatambua eneo la Lamadi ni eneo la kibiashara kwenye Jimbo la Mheshimiwa wa Busega, eneo hilo litapatiwa umeme pamoja na vituo vingine na Kituo cha Afya cha Lukungu kitapatiwa umeme kwenye *REA* Awamu ya III. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Msabaha.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nimuulize Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa huu umeme wa *REA* wananchi wengi hawajapata elimu ya kusaidiana na Serikali katika kutoa maeneo ya kuweka huu umeme wa *REA*. Je, Serikali mna mpango gani kuhakikisha mnakwenda kijijini kutoa hii elimu ili wananchi watoe maeneo haya ya kupitisha umeme wa *REA?*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa *REA* wanavyofanya kazi, elimu inayotolewa inatolewa kwa kiwango kidogo. Nichukue nafasi hii kutamka rasmi kwamba kuanzia tarehe 1 Julai, wafanyakazi wote wa *REA* pamoja na *TANESCO* watakuwa sasa wanawafuata wateja badala ya wao kufuatwa, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili tunawaelekeza sasa kutoa elimu sahihi kwa ajili ya taratibu za uunganishaji umeme pamoja na ada zinazotakiwa kulipwa. Kwa sasa wananchi wataelimishwa kwamba hawatakiwi kuweka mchango wowote kwenye maombi ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, wananchi wataeleweshwa kuhusu gharama za *service levy* kwamba zimeondolewa, kwamba huduma ya kuhudumiwa umeme sasa imeondolewa. Kwa hiyo, jitihada za Serikali za kuhakikisha kwamba wananchi wanapata elimu zitaendelea. Zilikuwa zikifanyika lakini sasa tutaongeza nguvu zaidi kwa kuwafanya watumishi wa *TANESCO* na *REA* kufanya kazi kibiashara kwa kuwafuata wateja na kuwapa elimu badala ya wao kufuatwa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Oscar Mukasa.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wakandarasi wa *REA* wanalalamika hawajalipwa pesa mpaka juzi na hili linaweza kuathiri uanzaji wa Awamu ya III kwa sababu shughuli ya Awamu ya II haijakamilika, Serikali inatoa kauli gani?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nipate ufafanuzi vizuri, tunataka tuwatambue wakandarasi wote wanaolalamika kwamba hawajalipwa pesa ili tujue wanalalamikia nini, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini inawezekana kukawa na malalamiko kwamba baadhi ya wakandarasi hawajalipwa pesa lakini kwa takwimu tulizonazo wakandarasi kwa mara ya mwisho, miezi miwili iliyopita tumewalipa pesa kwa ajili ya kuanza kazi. Inawezekana kuna baadhi ya wakandarasi nao wanaweka pia *subcontractors,* inawezekana wanaolalamika ni wale *subcontractors*. Napenda nimhakikishie kwamba suala hili tutalifanyia kazi. Nimelichukua, nitakaa na Mheshimiwa Mbunge tuone ni mkandarasi gani analalamika tuanze kulifanyia kazi mara moja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Martha Umbulla.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Nishati ya umeme ni nishati muhimu sana hasa kwa maendeleo ya elimu. Hivi sasa sekondari zetu nyingi za kata, hasa kwa mikoa ya pembezoni kama Manyara na kwingineko hakuna umeme kabisa. Je, ni kwa nini

usambazaji huu wa umeme vijijini unaofanywa na *REA* usilenge kwanza sekondari hizi za kata ambazo zina hali mbaya na ambazo zinahitaji kuboreshwa kielimu na kuboreshewa mazingira ya kusoma? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumebaini kwamba taasisi nyingi za jamii kwenye kuunganishiwa umeme zimekuwa zikisahaulika. Hata hivyo, niseme kipaumbele cha *REA* Awamu ya II, kipaumbele cha *REA* Awamu ya III itakayaoanza vinalenga sanasana kwa kuanzia kuzipatia umeme taasisi za jamii zikiwemo shule, zahanati na taasisi nyingine, hilo ni la kwanza. Niombe sana Wabunge tushirikiane sasa na wataalam wetu wa *REA* na *TANESCO* huko vijijini kuwaelekeza wanapoanza kazi waanze na taasisi za jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe tu kuwaambia Waheshimiwa Wabunge, vipaumbele kwa kawaida kabla ya matumizi ya nyumbani tunaanza na taasisi za jamii. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutatembea na wewe kama ambavyo huwa unatembea siku zote, tutembee kwa karibu ikiwezekana siku nzima Mheshimiwa Mbunge, tuongelee hospitali yako ambayo haijapata umeme tuipelekee umeme kwa haraka iwezekanavyo. Naomba uvumilie tukitoka hapa, Mheshimiwa Naibu Spika naomba unipe fursa ya kukaa na Mheshimiwa Mbunge, tukitafakari namna ya kupeleka umeme kwenye maeneo aliyozungumzia. *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, hiyo fursa umenyimwa. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 253

Manufaa ya Mgodi wa Bulyankulu kwa Wananchi Jirani

MHE. ELIAS J. KWANDIKWA (K.n.y. MHE. EZEKIEL M. MAIGE) aliuliza:-

Kilio kikubwa cha wananchi waishio jirani na Mgodi wa Bulyankulu ni kunufaika na mgodi huo:-

(a) Je, ni kiasi gani cha pesa Mgodi wa Bulyankulu ulitumia katika miradi ya ujirani mwema?

(b) Je, kwa nini mgodi huo hautekelezi miradi yake kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ambako kuna wataalam na gharama za utekelezaji miradi ni ndogo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2015 Mgodi wa Bulyankulu kwa kutumia "*Maendeleo Fund*" ulitumia takribani dola za Marekani milioni 1.98, sawa na takribani shilingi bilioni 4.4 kwa ajili ya miradi ya ujirani mwema iliyotolewa na Kampuni hiyo ya Bulyankulu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni za Migodi huwa na utaratibu wa kutekeleza shughuli zake kwa kuajiri wafanyakazi kulingana na mahitaji yao na kwa kuzingatia sheria za nchi. Pamoja na hayo, kampuni hizo huruhusiwa kuajiri wakandarasi wafanyakazi katika taaluma za ujuzi ambao haupo nchini. Hadi sasa kampuni imeajiri wafanyakazi hapa nchini wapatao 1,168, kati yao wafanyakazi 517 wanatoka katika maeneo yanayozunguka mgodi huo. Aidha, miradi husika hutekelezwa kwa kushindanisha wakandarasi na wataalamu kutoka sehemu mbalimbali nchini wakiwemo kutoka Halmashauri husika na hasa ya Msalala.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tutachukua hali hii kama ombi rasmi la Mheshimiwa Mbunge wa Msalala ili kulitafakari na kulifanyia kazi na kukaa na wakandarasi pamoja na mgodi unaomiliki shughuli za Mgodi wa Bulyankulu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kwandikwa swali la nyongeza.

MHE. ELIAS J. KWANDIKWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa yapo mazungumzo yanayoendelea kwa ajili ya ujirani mwema kati ya mgodi na vijiji vinavyozunguka ikiwemo Kijiji cha Bugarama na kwa kuwa kijiji hiki kina shida ya maji na wana mpango wa kupata maji kupitia mgodi huu. Je, Serikali iko tayari kuratibu mazungumzao haya?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri kwamba Mgodi wa Bulyankulu umekuwa ukitoa pia huduma za jamii katika maeneo ya Ilogi, Kakora, Runguya na maeneo mengine lakini hivi karibuni mgodi umekuwa ukifanya mazungumzo na vijiji vya jirani na tumekuwa tukiendelea kuratibu shughuli za migodi pamoja na wananchi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko tayari, itaendelea kuratibu mazungumzo mpaka suluhisho la wananchi kunufaika na mgodi huo zipatikane kama kawaida.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Atupele Mwakibete swali la nyongeza.

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Mkoa wa Mbeya umebarikiwa sana kuwa na madini pamoja na vyanzo mbalimbali vya umeme. Nataka nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa mfano, kuna vyanzo vya umeme vya jotoardhi kule Busokelo lakini pamoja na *Lake Ngozi*, kuna makaa ya mawe, kuna maporomoko ya maji na vitu vingine katika sehemu nyingine mbalimbali. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini vyanzo hivi vitaanza kufanya kazi ili wananchi wa Mbeya na Tanzania kwa ujumla ipate umeme wa kutosha? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, na mimi nasikiliza kwa bidii hayo majibu yako. *(Kicheko/Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa, kati ya mikoa hapa nchini iliyojaliwa kwa kuwa na rasilimali za madini pamoja na maporomoko ya maji ni pamoja na Mkoa wa Mbeya na hasa Mbeya Vijijini. Nikubaliane naye, kwa sasa Wizara yetu inafanya utafiti na inakamilisha utafiti wa jotoardhi *(geothermal)* ambapo sasa tumegundua madini hayo yatakuwa na megawati 20 kwa kuanzia lakini baadaye tutakwenda hadi megawati 100, hiyo ni kwa jotoardhi. Bado tunafanya upembuzi yakinifu katika makaa ya mawe pamoja na maporomoko ya maji katika mito hiyo na hasa katika Mto Ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hatua tunazochukua ni kukamilisha utafiti huo yakinifu na kadri itakavyowezekana tukipata fedha, shughuli ya kutekeleza miradi hiyo itaanza. Mradi wa *geothermal* unaanza kutekelezwa mwezi Julai, 2017.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri uzitafute hizo fedha kwa bidii sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwakagenda swali la nyongeza.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda Waziri atuambie, kwa migodi kama ya Kiwira ambayo tayari inazalisha, je, tunapata kiasi gani kama Halmashauri?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nifanye masahisho kidogo, Mgodi wa Kiwira haujaanza kazi rasmi, uko katika kukamilisha *detailed design* na hatua za kumpata mkandarasi kwa ajili ya kuanza ujenzi. Hata hivyo, mgodi huo utakapoanza, Halmashauri zote zinazohusika zitanufaika na mambo yafuatayo. La kwanza, Halmashauri zitakuwa na uwezo wa kukusanya *service levy* ambayo ni asilimia 0.3. Kadhalika zitaweza kupata mrabaha ambao utaingia Serikali kuu. Pia, mradi wa Kiwira unakadiriwa kuajiri wafanyakazi zaidi ya 1,000 utakapoanza kufanya kazi. Kwa hiyo, wananchi wa Mbeya na Watanzania wengine wataendelea kunufaika na kupata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika mradi huo utakuwa sasa na kipengele kinachowalazimisha wakandarasi na wamiliki wa migodi kuanza kuwashirikisha Watanzania kwa kununua bidhaa zao pamoja na huduma za jamii ili huduma za jamii zianzie maeneo yanayozunguka mgodi huo. Kwa hiyo, napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge Mradi wa Kiwira utakuwa na manufaa makubwa sana kwa Taifa lakini pia kwa wananchi wanaozunguka mgodi huo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kiula.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri swali dogo. Kwa sababu Mkalama kuna wachimbaji wadogo wadogo wa madini ya shaba, ni lini Wizara itawasaidia wachimbaji wadogowadogo? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba eneo la Mkalama lina madini na siyo shaba tu, yapo madini ya shaba, madini ya ujenzi na madini mengine ya viwandani. Huduma ambazo zitatolewa na Serikali kwa wachimbaji wadogo ni kote nchini ikiwemo pia wachimbaji wadogowadogo wa Mkalama, ni kama ifuatavyo. Hatua ya kwanza kama tulivyosema kwenye bajeti yetu, Waheshimiwa Wabunge niwapongeze sana kwa sababu mmepitisha shilingi bilioni 6.68 kwa ajili ya ruzuku ya wachimbaji wadogo wadogo na ruzuku hiyo itatumika pia kwa wananchi wa Mkalama Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini manufaa mengine ambayo pia Serikali imejizatiti ni pamoja na kuyafanyia utafiti maeneo yote. Sasa hivi Wakala wa Jiolojia Tanzania anapita maeneo yote na kuyafanyia utafiti ili kubaini maeneo ambayo yanaweza kuchimbwa na wachimbaji wadogo kwa tija. Jambo lingine tunalofanya kama Serikali kusaidiwa wachimbaji wadogowadogo ni pamoja na kutoa elimu wezeshi na ushauri kwa ajili ya kuufanya uchimbaji mdogo uwe wa tija zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi tumesogeza sasa huduma zote za ugani huko wachimbaji wadogo waliko. Tumefungua ofisi za madini karibu kila mkoa ili kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata ushauri nasaha kwa masuala ya afya migodini pamoja na mazingira. Kwa hiyo, huduma za wafanyakazi, huduma za wachimbaji wadogo, zitaendelea kama kawaida na kama ambavyo nimeeleza.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 254

Ujenzi wa Barabara ya Kawe kwa Kiwango cha Lami

MHE. HALIMA J. MDEE aliuliza:-

Serikali iliwaahidi wananchi wa Jimbo la Kawe kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Chuo Kikuu cha Ardhi - Makongo - Goba na barabara ya Tegeta Kibaoni - Wazo Hill – Madale:-

Je, ni lini ujenzi huo utakamilika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Chuo Kikuu cha Ardhi - Makongo - Goba pamoja na barabara ya Tegeta Kibaoni - Wazo Hill - Madale Goba ni kati ya barabara ambazo zimo kwenye mpango wa Serikali wa ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara za kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam ambao utekelezaji wake ulianza mwaka 2010 na unagharamiwa na Serikali za Tanzania kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ambazo ujenzi wa kiwango cha lami umekamilika ni *Ubungo Bus Terminal* - Kigogo *Roundabout* ambayo ni kilomita 6.4, Ubungo Maziwa - Mabibo *External* kilomita 0.65 na *Jet Corner* - Vituka - *Davis Corner* ambayo ni kilomita10.3. Aidha, barabara zinazoendelea kujengwa ni pamoja na Tangibovu - Goba kilomita 9, Kimara Baruti - Msewe - Changanyikeni kilomita 2.6, Kimara - Kilungule - *External* kilomita 9 na Tabata Dampo - Kigogo kilomita 2.25.

Mheshimiwa Naibu Spika, usanifu wa kina wa barabara ya Tegeta Kibaoni - Wazo Hill -Madale - Goba na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi umekamilika. Aidha, usanifu wa kina wa barabara ya Chuo Kikuu cha Ardhi - Makongo - Goba utafanyika sambamba na ujenzi wa barabara hiyo yaani *design and build*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Chuo Kikuu cha Ardhi - Makongo - Goba na Tegeta Kibaoni - Wazo Hill - Madale - Goba umepangwa kuanza katika mwaka wa fedha 2016/2017.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima Mdee swali la nyongeza.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwenye majibu ya Waziri anasema uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi umekamilika. Labda tu nimpe taarifa Mheshimiwa Naibu Waziri hizi barabara kwa miaka ya fedha miwili mfululizo, 2014/2015, 2015/2016 zilitengewa fedha, zikatangazwa, tatizo ilikuwa fedha zilizotolewa na wakandarasi walichokuwa wakihitaji zilikuwa ni ndogo hivyo licha ya matangazo mara tatu hakuna kilichofanyika. Ukiangalia bajeti ya ujenzi zimetengwa kiasi kilekile cha fedha, barabara ya *Mlimani City* - Goba imetengewa shilingi bilioni 2.5, fedha ambazo mwaka jana ilishindikana, halikadhalika Tegeta Kibaoni - Goba. Nataka tu Naibu Waziri aniambie kiukweli tu kabisa, anawahakikishia vitu wananchi wa Jimbo la Kawe kwamba kwa

bajeti hii iliyotengwa ujenzi utaanza kufanyika kwa mwaka huu wa fedha? Hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili barabara muhimu sana ya *New Bagamoyo Road*, tunafahamu kwamba kwa miaka miwili iliyopita pia zilitengwa shilingi bilioni 88, zilitolewa na Wajapan *through JICA*. Madhumuni yalikuwa ni kujenga barabara ya Mwenge - Tegeta (*double road),* kujenga barabara ya Mwenge - Morocco *(double roads)*, *88 billion* akiwa Waziri wa Ujenzi ni Magufuli. Sasa leo kile kipande cha Mwenge - Morocco inaonekana kama kimekufa kuna ukarabati wa kienyeji unaendelea pale. Nilitaka Naibu Waziri aniambie zile shilingi bilioni 88 zimekwenda wapi na kile kinachoendelea pale Mwenge - Morocco ndiyo *permanent* ama ni *temporary* kukidhi mahitaji ya sasa ya barabara? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge wa Kawe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Kawe na wananchi wake wote wa Kawe kwamba nilichokieleza katika jibu langu la msingi kuhusu kuanza kwa ujenzi wa hizi barabara mbili alizozitaja ni sahihi na tutajenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili kwamba shilingi bilioni 88 zilikwenda wapi, nadhani anafahamu kwamba hiyo *double road* anayoongelea kuna sehemu yake imeshajengwa, kilichobaki ni kama anavyosema ni hiki kipande cha kati ya Mwenge - Morocco, upande ule mwingine umeshajengwa na hizo hela ndiko zilikoenda. Zimekwenda huko, zimetumika kujenga barabara hiyo na namhakikishia kazi inayoendelea sasa hivi pale, inaendelea kwa kiwango. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Edwin Sannda.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Tunashukuru sana kwa kazi ya barabara inayoendelea kutoka Dodoma - Kondoa - Babati ingawa inakwenda kwa kasi ya kusuasua. Tatizo moja kubwa wakati wa ujenzi kuna alama na maelekezo mbalimbali yanayotakiwa yawepo wakati wa ujenzi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sannda swali lako ni la nyongeza, lifanye fupi tafadhali.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Barabara hii hizi alama zinapungua maeneo mengine hakuna kabisa, kwa hiyo, unakuta watu wanapotea kilomita kadhaa halafu ndiyo urudi tena. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wanawasimamia wakandarasi hawa waweke hizi alama ili kuondoa ajali na upotevu wa muda wa namna hii? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wote wa maeneo yote ya wakandarasi watatu wa kuanzia hapa Dodoma mpaka mwisho kabisa, wa *CHICO*, namuelekeza *Regional Manager* wa Dodoma asimamie kuhakikisha kwamba alama za barabarani zinazowaongoza wananchi wanaopita na magari yao ziwe zinawekwa na kusimamiwa muda wote zisiwe zinaondolewa ili wananchi wale wanaopita na magari yao wasipate shida ya kupoteapotea au kutumbukia kwenye mitaro. Namuelekeza atekeleze hilo na mimi mwenyewe nitafuatilia.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecil Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Swali la Mheshimiwa Mdee linafanana kabisa na suala ambalo liko katika Jimbo la Ndanda hasa katika maeneo ya Lukuledi - Chikunja - Nachingwea. Barabara ile siku za karibuni itajengwa kwa kiwango cha lami lakini tunaomba kufahamu fidia ya watu wale itafanyika kwa njia gani na ni umbali gani toka katikati ya barabara mpaka mwisho wa hifadhi ya barabara? Watu wale wanahitaji kufahamu jambo hili, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge swali la nyongeza la kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema hiyo barabara hatujaanza kuijenga na tumeiwekea bajeti mwaka huu unaokuja wa 2016/2017. Nadhani unafahamu kwamba tunafuata ile Sheria ya 1967 ya *Road Reserve* ambayo sasa hivi tunaongelea kila upande kutokea katikati ya barabara wale wote ambao wako ndani ya mita 60 na wale ambao wako nje ya mita 60 wana haki

tofauti. Wale ambao wako nje ya *road reserve* wana haki ya kulipwa fidia na wale ambao waliifuata barabara, nadhani kama sheria inavyosema na kama tulivyopitisha humu Bungeni hawana haki ya kulipwa fidia. Kwa hiyo, huo ndiyo umbali ambao umwekwa kisheria na ni sisi wenyewe tulipitisha humu ndani. Sisi kazi yetu ni kuisimamia tu, hapa kazi tu. *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Phillipo Mulugo.

MHE. PHILIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi niweze kuuliza swali lanyongeza. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Songwe naomba niiulize Serikali. Rais Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alipokuja Songwe ambapo sasa ni Wilaya mpya aliahidi ujenzi wa barabara ya lami kutoka Mbalizi - Mkwajuni - Makongorosi na tayari Serikali 2013 imeshafanya upembuzi yakinifu lakini baada ya hapo hakuna kinachoendelea. Je, Serikali ni lini itaanza sasa ujenzi wa lami wa barabara hiyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mulugo, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliwasiliana na Mheshimiwa Mulugo kuhusu barabara hii. Najua unaifuatilia sana, ni haki yako kuifuatilia na ni wajibu wako na sisi ni wajibu wetu kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu barabara hii iko katika Ilani. Naomba tu kumhakikishia kwamba kama ambavyo tumeitaja katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kama ambavyo wewe unafuatilia utekelezwaji wa Ilani hiyo, tutatekeleza katika kipindi hiki cha miaka mitano.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 255

Chuo cha *Marine Institute* Kuanzisha Kozi ya Gesi na Mafuta

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA aliuliza:-

Ili Watanzania wanufaike katika ajira zinazotokana na shughuli za uchimbaji wa gesi na mafuta wanatakiwa kuwa na cheti cha *Basic Off Shore Safety Certificate* ambacho kwa sasa hakipatikani katika vyuo vya hapa nchini:-

Je, ni lini Serikali itakiwezesha Chuo cha *DMI (Dar es Salaam Marine Institute)* kianze kutoa kozi hizi ili wananchi wote waweze kupata cheti hiki ili waweze kuajiriwa katika shughuli za gesi na mafuta?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Bandari kinachosimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya mafuta na gesi kutoka hapa nchini kikiwemo Chuo cha DMI yaani *Dar es Salaam Marine Institute* na Norway, kinakamilisha maandalizi ya kuanza kutoa mafunzo na kujenga miundombinu inayotakiwa ili kuendesha mafunzo ya usalama katika sekta ya mafuta na gesi. Kutolewa kwa mafunzo hayo hapa nchini kutaongeza fursa ya ajira kwa wahitimu wetu kufanya kazi katika sekta ya mafuta na gesi lakini pia kupata wanafunzi kutoka nchi jirani zenye viwanda vya mafuta na gesi kama Uganda, Sudan na Kenya. Tunategemea ifikapo Disemba, 2016 mafunzo hayo yatakuwa yameanza kutolewa na Chuo cha Usimamizi wa Bandari. Mafunzo yatatolewa kwa kufuata mitaala ya kimataifa na hivyo wahitimu watapewa vyeti vinavyotambuliwa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Chuo cha *DMI (Dar es Salaam Maritime Institute)* kitaendelea kufanya maandalizi muhimu ya kumpata mtaalamu wa kufanya tathmini ya vifaa vya kufundisha kama vile helikopta *dunker*, bwawa la kuogelea, *smoke house* na kadhalika ili kuanzisha mafunzo hayo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mtolea swali la Nyongeza.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Upatikanaji wa gesi na mafuta katika nchi hii ulileta matumaini kwa Watanzania kwamba sasa watapata fursa ya kupata ajira katika shughuli hizo. Kwa kuwa Serikali inakiri kabisa kwamba ni muhimu hii kozi kuwa inatolewa hapa nchini ili Watanzania waweze kupata uwezo wa kuajirika au kupata ajira katika sekta ya mafuta na gesi na mpaka leo Serikali ndiyo bado iko kwenye mchakato wa kuanzisha kozi hii. Nataka kufahamu, Serikali kwa nini ilianzisha uchimbaji wa gesi na utafutaji wa mafuta hapa nchini wakati bado haijajenga uwezo kwa Watanzania kutumia fursa hizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika sheria zinazosimamia shughuli za bandari inazitaka meli zikishaweka gati kwenye bandari zetu theluthi mbili ya wafanyakazi wanaoenda kutoa huduma kwenye zile meli wawe ni Watanzania. Kwa sasa meli zote zinazoingia zinakuja na wafanyakazi wake na hivyo kuwakosesha ajira Watanzania wanaotegemea ajira kwenye bandari zetu. Je, ni lini Wizara hii itaivunja hii Bodi ya *SUMATRA* na kuiunda tena upya ili iweze kusimamia majukumu yake? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea, Mbunge wa Temeke kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea na kwa kweli Watanzania wote wanafahamu kwamba Chuo cha Bandari tunachokiongelea pamoja na *DMI* ni hatua ya nyongeza. Mafunzo kwa ajili ya utaalam wa masuala ya mafuta na gesi yalishaanza kutolewa muda mrefu katika Chuo cha Dodoma pamoja na Chuo cha Madini na wahitimu wameshaanza kutoka. Kwa hiyo, nachomueleza Mheshimiwa Mbunge ni kwamba katika chuo hiki tunaongeza mafunzo. Kitu ambacho ni kipya katika chuo hiki ni yale mafunzo ya usalama ambayo yatafanyika katika Chuo cha *DMI* na wenzetu wa Norway wametuahidi kutuimarisha katika eneo hili ili tuwe nchi ya pili kwa Afrika kutoa mafunzo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la pili, hata sisi tumepata malalamiko kutoka kwa Mabaharia na kwa kweli tumehangaika nao sana na nadhani wanatuelewa kwamba tafsiri ya ile sheria unayoongelea haiko hivyo kama inavyotafsiriwa. Tunaomba tuipitie hiyo sheria upya pamoja na Sheria ya SUMATRA ili tukipate kile tunachokitaka yaani sisi, Mabaharia na Waheshimiwa Wabunge.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbatia swali la nyongeza.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Waziri anaonaje akishirikiana na Wizara ya Elimu wanafunzi wote wanaosoma masomo ya sayansi kwa *A level* wapate somo la *health and safety* ili iwe ni *general* kwa *public* ikiwepo sisi Wabunge kupewa elimu kama moto ukitokea kwenye Bunge hili tahadhari inakuaje, milango ikoje na mambo mengine yakoje humu ndani? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Waziri wangu Kivuli wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa umakini kabisa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaongea na mtaalamu kati ya wataalamu wachache tulionao nchini. Tumechukua hoja yake na tutawasiliana na Wizara ya Elimu na namuomba ashiriki kama ambavyo amekuwa akitushirikisha katika mambo mengine ya elimu ili tuweze kufikia huko kwenye eneo ambalo yeye amebobea. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 256

Ujenzi wa Barabara ya Tanga – Pangani – Saadani kwa Kiwango cha Lami

MHE. JUMAA H. AWESO aliuliza:-

Ujenzi wa barabara ya Tanga – Pangani - Saadani yenye kilometa 178 kwa kiwango cha lami ni ahadi ya muda mrefu ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne na Rais wa Awamu ya Tano:-

Je, ni lini sasa ujenzi huo utaanza hasa ikizingatiwa kuwa ahadi hiyo ni ya muda mrefu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Mbunge wa Pangani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara wa Tanga - Pangani - Bagamoyo yenye urefu wa kilometa 178 ni sehemu ya Mradi wa Kikanda wa barabara ya Malindi – Mombasa - Lunga Lunga/Tanga - Bagamoyo. Mradi huu wa Kikanda unaratibiwa na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Tanga – Pangani – Bagamoyo kwa kiwango cha lami ilianza Januari, 2011 na kukamilika Novemba, 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, inaendelea na juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Benki ya Maendeleo ya Afrika tayari imeonesha nia ya kutoa fedha kwa ajili ya kugharamia ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii. Taratibu za kumpata mkandarasi zitaanza baada ya kupatikana kwa fedha za ujenzi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aweso swali la nyongeza.

MHE. JUMAA H. AWESO: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nami nipate fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia barabara ya Tanga – Pangani - Saadani ndipo tunapozungumzia uchumi na siasa ya Pangani. Kwa kuwa katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri imeeleza kwamba *African Bank* wameonesha nia ya kutoa fedha kwa ajili ya barabara hii, je, Serikali imefikia wapi katika ufuatiliaji kuhakikisha kwamba *African Bank* wanatoa fedha hizi ili wananchi wa vijiji vya Choba, Pangani Mjini, Bweni, Mwela pamoja na Makorola na Sakura wanalipwa fidia ili wajue hatma ya maisha yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa malengo ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inakusanya mapato na Wilaya ya Pangani ni miongoni mwa Wilaya ambazo zimejaliwa na Mwenyezi Mungu kuwa na Mbunga ya Saadani ambayo ni pekee Afrika mbuga ambayo imepakana na bahari. Kwa nini sasa Serikali isitenge fedha zake za ndani kuhakikisha kwamba inajenga barabara hii kwa haraka ili kukusanya mapato kupitia Mbuga hii ya Saadani? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Aweso anafahamu kwamba katika maeneo ya kwanza niliyotembelea ni Pangani na ilikuwa ni ziara ya kuifuatilia barabara hii pamoja na ile gati. Anafahamu baada ya hapo Waziri wangu naye alikwenda kwa ajili ya kufuatilia barabara hii pamoja na gati. Kwa hiyo, kwa namna wananchi wa Pangani walivyotupokea tukiwa na yeye, nina uhakika wanafahamu nia yetu ya kuhakikisha barabara hii inajengwa ni ya dhati na tutahakikisha fedha hizi ambazo wenzetu wa *African Development Bank* wanataka kutoa tutazifuatilia. Hivi ninavyoongea, kuna kikao Zambia

kuhusiana na miradi ya *African Development Bank*. Kwa hiyo, namhakikishia tunafuatilia na tuna uhakika hatimaye tutazipata fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi huu hatuwaachii *African Development Bank* peke yake na sisi kama Serikali tutatenga fedha, moja kwa ajili ya masuala ya fidia lakini vilevile na masuala ya ujenzi. Kuna kiwango ambacho sisi kama nchi ni lazima tutenge. Kwa hiyo, hata Tanzania kama Serikali inawajibika katika kuhakikisha barabara hii inajengwa. Namhakikishia kama ambavyo tumemwonesha na wananchi wake wameona tutalifuatilia hili mpaka lifikie mwisho.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Tunajua kuna Halmashauri nyingi mpya na kutangaza Halmashauri mpya ina maana kama Halmashauri ilikuwa moja kuna mgawanyo wa vyanzo vya mapato na kadhalika. Hizi Halmashauri mpya nyingi vyanzo vyake vya mapato ni vidogo ikiwepo Halmashauri ya Mji wa Bunda na huko ambako wewe pia una *interest* nako barabara nyingi hazipitiki.

Nataka kujua Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wanapeleka fedha za kutosha kwenye Halmashauri hizi mpya kupitia *TANROADS* Mikoa ili waweze kuhakikisha barabara zinapitika ikiweko na barabara yangu kutoka Rwahabu – Kinyabwiga na barabara ya kutoka Tairo – Gushingwamara? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Bunda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimeeleza huko nyuma kwamba *TANROADS* Mkoa siyo wa *TANROARD* Taifa na wale Wahandisi wa Halmashauri wote sasa nchi nzima, wakae na kuhakikisha zile barabara ambazo zimekatika sasa tunazirudishia, hii ni pamoja na Mfuko wa Barabara ambako fedha zinatoka. Tunajua hizi barabara zingine ni za Halmashauri, zingine za Mkoa na zingine za Kitaifa lakini hii ni dharura, kwa hiyo wote tunashirikiana kwa pamoja ili tuweze kufungua mawasiliano pale ambapo yamekatika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Flatei Massay.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa ahadi za Rais, zimekuwa zikitolewa na

moja ya Mji wetu wa Haydom, Mbulu na Dongobesh tumeahidiwa kujengwa barabara ya lami kwa kilometa tano. Je, lini Serikali inatekeleza ahadi hii ya Mheshimiwa Rais?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anafahamu na nimeshajibu hoja hiyo huko nyuma kama mara mbili hivi. Najua kwa nini anarudia, ni kutokana na umuhimu wa barabara hiyo, lile eneo halina lami kabisa kama ilivyo kwa Mbunge wa Loliondo. Niliwaambia kwamba ahadi ya Rais wa Awamu ya Tano na Awamu ya Nne, ni lazima tutazitekeleza kwa sababu ndiyo wajibu tuliopewa katika Wizara yetu. Lini hasa? Naomba atuachie kwani siyo rahisi kutoa tarehe hapa Bungeni. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dongo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio changu cha zaidi ya miaka minne katika Bunge hili ni kuhusu barabara ya mchepuko kutoka Uyole - Songwe Airport kupitia Mbalizi kimekuwa kirefu na nimekuwa nikielezea ni kwa nini. Naishukuru Serikali kwenye bajeti yake Mheshimiwa Waziri amesema kwa kilometa 40 hizi upembuzi yakinifu utaanza. Nilitaka Mheshimiwa Waziri atoe tamko hapa upembuzi yakinifu huu utaanza lini kutokana na adha hii ya Wanambeya ambayo tumekuwa tukiipata kwa muda mrefu? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa anafahamu kwamba hilo eneo analoliongelea ndilo eneo ambalo na mimi kila wakati napita nikienda kuwatembelea wakwe zangu. Nakuomba sana Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa, utuamini siyo kwa sababu hiyo, utuamini kwa sababu tumedhamiria na ndiyo dhamana yetu ya kutekeleza ahadi zote za

Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne ambaye aliitolea ahadi barabara hii na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano ambaye naye aliitolea ahadi. Mimi nakuomba utuamini mwaka huu wa fedha unaokuja kuanzia Julai, 2016 mpaka Juni, 2017 kama huo upembuzi yakinifu hautafanyika, ninakuhakikishia dada yako atarudi. *(Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Tumefika mwisho wa kipindi cha maswali na majibu.

Waheshimiwa Wabunge, naleta kwenu matangazo yaliyotufikia Mezani. Tangazo la kwanza linahusu wageni. Tunao wageni wa Naibu Spika, wageni 106 ambao ni viongozi mbalimbali CCM kutoka Mkoa wa Mbeya na Songwe. Tunao viongozi nane wa CCM kutoka Mkoani ambao wanaongozwa na Ndugu Zongo Lobe Zongo. Naona wageni wetu wamesimama wote kwa pamoja, naona niwataje kwa makundi *(Makofi)*

Tunao viongozi nane wa CCM kutoka Mkoani wakiongozwa na Ndugu Zonge Lobe Zonge ambaye ni Katibu wa Mkoa. Tunao pia viongozi tisa wa CCM kutoka Wilaya ya Mbeya Mjini wakiongozwa na Ndugu Ephraim Mwaitenda ambaye ni Mwenyekiti wa Wilaya. Viongozi 11 wa CCM kutoka Mbeya Vijijini wakiongozwa na Ndugu Ipiana Seme. Viongozi 11 wa CCM kutoka Wilaya ya Mbarali wakiongozwa na Ndugu Mathayo Mwongomo. Viongozi 10 wa CCM kutoka Wilaya ya Kyela wakiongozwa na Ndugu, Hanta Mwakifuna. Viongozi 10 wa CCM Wilaya ya Rungwe wakiongozwa na Ndugu Ally Mwakalindile. Viongozi 11 wa CCM kutoka Wilaya ya Ileje wakiongozwa na Ndugu Hebron Kibona. Viongozi 11 wa CCM kutoka Wilaya ya Mbozi wakiongozwa na Ndugu Aloyce Mdalivuma. Viongozi 10 wa CCM kutoka Wilaya ya Chunya wakiongozwa na Ndugu Kapala Makelele. Viongozi 11 wa CCM kutoka Wilaya ya Momba wakiongozwa na Ndugu Eliachim Simpasa. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, viongozi hawa kutoka Mikoa hii miwili wameongozana na wenyeji wao kutoka Wilaya ya Dodoma Mjini ambao ni Ndugu Paulo Lwamo, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Dodoma Mjini. Ameongozana na Ndugu Salum Kali, Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Wilaya. Yupo mgeni mwingine ambaye ni Kamanda wa UVCCM wa Mkoa wa Mbeya, Ndugu Yona Sonelo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni hawa wameongozana na Ndugu wa Naibu Spika ambao nitawataja na watasimama kwa pamoja. Ndugu Best Mwansasu, Ndugu Philemon Mwansasu, Ndugu Bitisa Mwansasu, Ndugu Odima Mwansasu, Ndugu Saul Mwaisenye, Ndugu Shadrack Mwakombe, Ndugu Charles Mwakipesile, Ndugu Maryprisca Mahundi, Ndugu Mary Dominic Nyagawa, Ndugu Gunza Mwasote, Ndugu George Kazumba, Ndugu Yesayah Nicholaus na Ndugu Elias Ndabila. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni watano wa Mheshimiwa William Olenasha, Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi ambao ni Ndugu Lengai Olesabaya, Ndugu Lucas Nsomi, Ndugu Victor Njau, Ndugu Aron Lukumai na Ndugu Eliamani Mollel. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Alex Ghashaza ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni, Ndugu Josephat Gwamagobe na Ndugu Idan Joseph. *(Makofi)*

Tunao pia wageni saba wa Mheshimiwa Esther Mmasi ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 16 wa Mheshimiwa Allan Joseph Kiula ambao ni viongozi wa CCM na Madiwani wa Wilaya ya Singida. Wameongoza na Ernesta Richard, Katibu wa CCM Wilaya na Ndugu James Mkwega, Mwenyekiti wa Halmashauri. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Qambalo Willy ambao ni watoto wa Mheshimiwa, Ndugu Irene Qambalo, Ndugu Irene Leo na Ndugu Aloyce Willy. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Riziki Mngwali ambaye ni mwanaye anayeitwa Ndugu Solomon Mwaisumbe kutoka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliokuja kwa ajili ya kujifunza Bungeni, wanafunzi 45 wanaosoma mwaka wa pili kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe Morogoro wanaochukua Shahada ya Utawala katika Utunzaji wa Kumbukumbu za Nyaraka. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 100 kutoka Chuo Kikuu cha St. John cha Dodoma. Karibuni Sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni waliotufikia Bungeni siku ya leo kama wapo wengine sijapata orodha wataongezeka baadaye.

Tangazo lingine ni lile ambalo lilitangazwa jana linarudiwa tena. Waheshimiwa Wabunge mnakumbushwa kwamba leo tarehe 27 Mei, 2016, saa saba na nusu mchana kutakuwa na warsha kwa Wabunge wote kuhusu magonjwa yasiyoambukizwa itakayofanyika katika ukumbi wa Msekwa.

Aidha, kesho Jumamosi mnakumbushwa tena kwamba kuanzia saa nne asubuhi kutakuwa na zoezi la upimaji wa hiari wa afya. Mnaombwa msikose

tafadhali kwenye Zahanati ya Bunge na vipimo hivi ni bure kwa Wabunge wote. *(Makofi)*

Tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club*, anawatangazia kwamba kesho saa kumi kutakuwa na mechi ya kirafiki kati ya Waheshimiwa Wabunge na Benki ya *NMB* kwa michezo ya *football* na *netball*, wote mnakaribishwa.

Pia Mwenyekiti anawatangazia kwamba leo baada ya kuahirisha Bunge mchana saa saba, Kamati Tendaji ya muda ya Bunge *Sports Club* wanaombwa kukutana Ukumbi wa Msekwa C ili kupitia Katiba kwa malengo ya kufanya maandalizi ya uchaguzi wa viongozi wa *club*.

Pia anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wanamichezo wote kwamba nafasi mbalimbali za uongozi, watu wataanza kugombea, lakini wachukue fomu siku ya Jumatatu tarehe 30 Mei, 2016 saa nne asubuhi, Ofisi ya Katibu wa Timu ambaye ni Ndugu Mbilinyi. Mwisho wa kuchukua fomu itakuwa tarehe 31 Mei, 2016. Uchaguzi utafanyika Jumatano tarehe 1 Juni, 2016. Kwa hiyo, mnakumbushwa hizo tarehe mziweke vizuri kwa wale Wabunge ambao ni wanamichezo.

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunayo miongozo miwili hapa. Mwongozo wa kwanza uliombwa na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko kutokana na maelezo ya Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu malipo ya posho za Askari Magereza.

Waheshimiwa Wabunge, jana tarehe 26 Mei, 2016 katika kikao cha 29 cha Mkutano wa Tatu wa Bunge nilitoa nafasi kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aweze kutoa maelezo ya ufafanuzi kuhusu mwongozo aliokuwa ameomba Mheshimiwa Esther Matiko kuhusu ucheleweshaji wa malipo ya posho za Askari Magereza.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alitoa maelezo ya ufafanuzi kuhusiana na mwongozo huo. Katika maelezo yake, alieleza kuwa posho ya chakula kwa Askari Magereza yaani *ration allowance* ilicheleweshwa kwa Machi na Aprili na sababu ya kuchelewa kulipa ni baada ya Serikali kuongeza kiwango cha malipo ya posho hizo kutoka Sh.180,000 mpaka Sh.300,000. Ongezeko hilo lilifanyika mwezi Oktoba wakati tayari bajeti ya fedha kwa mwaka 2015/2016 ilikuwa imeshapitishwa. Hivyo walikuwa wakifanya taratibu za kuomba kibali Hazina ili kufanyike uhamisho wa fedha yaani *reallocation* kwa ajili ya kupata fedha za malipo ya posho hizo. Hata hivyo, alieleza kuwa malipo ya posho hizo kwa mwezi Machi na Aprili tayari

yameshafanyika. Kwa posho ya Mei na Juni, Naibu Waziri alieleza kama ifuatavyo:-

"*Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Aprili, 2016 Jeshi la Magereza pia liliomba uhamisho wa fedha za nje ya bajeti ya Jeshi la Magereza kwa ajili ya kulipa Askari wake posho hiyo kwa mwezi Mei na Juni, 2016. Taratibu za kuwalipa posho hizo za chakula Askari wa Magereza kwa mwezi Mei 2016 zimeshakamilishwa na Hazina na zitakuwa zimelipwa ama kukamilika kulipwa wakati wowote wiki hii*".

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu malipo ya Posho ya Pango ya Nyumba ya Askari Magereza, Naibu Waziri alieleza kuwa posho hiyo hulipwa kupitia orodha ya malipo ya mshahara kwa kutumia mfumo shirikishi wa taarifa za kiutumishi yaani *LAWSON*. Mpaka sasa wapo Maafisa na Askari 3,241 ambao tayari wanalipwa posho hizo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya Naibu Waziri kutoa ufafanuzi huo Mheshimiwa Matiko akaomba mwongozo kuhusiana na maelezo hayo ya Naibu Waziri. Alidai kuwa Naibu Waziri aliongea uwongo kwa kuwa posho ya Aprili Askari Magereza walilipwa tarehe 5 Mei, 2016 badala ya tarehe 14 mpaka 16 ya mwezi Aprili. Mheshimiwa Matiko aliendelea kusema kuwa posho ya pango ilizuiwa kwa miaka mitatu ikifanyiwa marekebisho na Askari hawajaanza kulipwa.

Waheshimiwa Wabunge, katika mwongozo huo nitajielekza kwenye hoja ya Mheshimiwa Matiko kuwa Naibu Waziri alitoa maelezo ya uwongo Bungeni. Nikianza na hoja ya posho ya chakula, Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* zinaonyesha wazi kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alisema kuwa baada ya uhamisho wa fedha kufanyika posho za chakula za Machi na Aprili, 2016 zililipwa ipasavyo. Hoja ya msingi hapa ni kwamba posho hizo zililipwa sababu za ucheleweshaji alizitoa kuwa ni maombi ya kibali Hazina kwa ajili ya kuhamisha fedha hizo. Hivyo ni wazi kuwa hakuna uwongo wowote aliosema Naibu Waziri. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hoja ya pili ya Mheshimiwa Matiko kuhusu malipo ya posho ya pango nayo ilijibiwa kikamilifu na Naibu Waziri. Alieleza kuwa mpaka sasa wapo Maafisa na Askari 3,241 ambao tayari wameanza kulipwa posho hizo. Mheshimiwa Naibu Waziri jana ametoa vielelezo kuunga mkono maelezo yake. Alileta kwa Spika nyaraka zinazothibitisha kufanyika kwa malipo hayo, *allowance rent payment report*. Taarifa hiyo inaonyesha kuwa hadi kufikia Aprili, 2016 jumla ya watumishi 3,241 wa Jeshi la Magereza wameomba kulipwa posho ya pango. Maafisa na Askari ambao tayari wanapokea posho hii ni 2,860 ambao ni asilimia 88.2, ambao maombi yao yanafanyiwa kazi ni watumishi 381 sawa na asilimia 11.8.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na maelezo hayo ya ufafanuzi ya Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na uthibitisho wa nyaraka alizozileta ni uamuzi wa Kiti kuwa maelezo hayo ni sahihi na aliyatoa kwa ufasaha na kwa ukamilifu. Hakuna uwongo wowote aliotoa Bungeni kama Mheshimiwa Matiko alivyodai. Hivyo kwa uamuzi huu suala hili nalifunga rasmi na hakutakuwa na mjadala tena kuhusiana na suala hilo. Huo ndio mwongozo wa Spika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge mwongozo mwingine ni wa Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko kwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwamba hakujibiwa swali lake kwa ufasaha.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 26 Mei, 2016 katika kikao cha 29 wakati wa kipindi cha maswali na majibu, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko aliuliza swali namba 244 kwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi swali hilo lilijibiwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Hata hivyo, Mheshimiwa Nsanzugwanko hakuridhishwa na majibu yaliyotolewa na Naibu Waziri hasa sehemu (a) ya swali hilo na hivyo kuomba kwamba swali hilo litafutiwe majibu ya ufasaha. Swali hili linasomeka kama ifuatavyo, nanukuu:-

"Mkoa wa Kigoma ni kati ya mikoa mitatu inayopata mvua nyingi katika nchi yetu kwa wastani wa takribani milimita 1,300 kwa mwaka ikifuatiwa na Mkoa wa Katavi:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali haifanyi jitihada za kuwekeza katika kilimo ili kunufaika na uwepo mzuri wa hali ya hewa?"

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu swali hilo kama ifuatavyo, nanukuu:-

"Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa katika Mkoa wa Kigoma zinaendelea tafiti mbalimbali za kilimo kwa kushirikiana na wadau wengine kama vile kampuni ya Kigoma Sugar kwa zao la miwa na Belgium Technical Cooperation kwa zao la chai kabla ya kuanza kuhamasisha sekta binafsi kwa uzalishaji mkubwa. Aidha, Mkoa wa Kigoma upo katika mpango wa BRN (Big Result Now) katika kilimo cha miwa (sugar cluster) ambapo katika mpango huo mashamba makubwa mawili yameshatambuliwa na wawekezaji kama vile Kigoma Sugar wameshaonyesha nia ya kuzalisha sukari kwa kushirikiana na wakulima wadogo".

Waheshimiwa Wabunge, kwa nukuu hiyo kutoka kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* ni wazi kuwa majibu ya Naibu Waziri yanaonyesha jitihada zinazofanywa za uwekezaji katika kilimo Mkoani Kigoma. Hivyo, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 46(1) nimeridhika kuwa swali hilo

limejibiwa kikamilifu na Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Huo ndiyo mwongozo wangu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI: Hoja za Serikali kwamba Bunge sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 – Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunao wachangiaji, *list* zimeshaletwa hapa na vyama, tutaanza na Mheshimiwa Grace Victor Tendega

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwongozo.

NAIBU SPIKA: Halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe. Naomba mkae Waheshimiwa, tafadhali. Mheshimiwa Grace Victor Tendega endelea.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza napenda kukushukuru kwa kupata nafasi hii na pia napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kupata fursa hii ya kuchangia katika Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Kambi ya Upinzani kwa asilimia 100. Ninavyounga mkono, naomba ninukuu maneno ya Hayati Baba wa Taifa katika kitabu chake cha Binadamu na Maendeleo alipokuwa akizungumzia faida ya elimu katika nchi. Naomba ninukuu baadhi ya mistari, anasema:- *"Tunatumia fedha nyingi sana zisizolingana na uwezo wetu kuwasomesha watu wachache ili baadaye na wao walete faida kubwa kiasi hicho hicho katika nchi. Tunatumia fedha nyingi kutafuta faida katika akili ya mwanadamu kama vilevile tunavyotumia fedha kununua trekta na kama vilevile ambavyo tukinunua trekta tunatarajia kufanya kazi kubwa zaidi kuliko kazi ya mtu na jembe la mkono". (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunaona elimu ni gharama tujaribu ujinga, walikwishazungumza watu wengi. Elimu ya nchi hii imewekwa rehani. Watanzania walio wengi hawaoni umuhimu wa kupeleka watoto wao katika

shule zetu za Serikali kwa sababu ya matokeo ambayo tunayaona sasa hivi. Watoto wengi wamekuwa wakimaliza shule bila hata kujua kusoma na kuandika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri wa Elimu aweze kunisikiliza kwa makini. Hakuna elimu bora bila kujali Walimu. Walimu ndiyo wanaofanya elimu hii ikawa bora zaidi hata kama shule ikiwa haina madawati mengi, haina miundombinu mizuri zaidi lakini Walimu wakawa wameboreshwa vizuri wanaweza wakafanya elimu hii ikawa bora hivyo vingine vinasaidia kuwa bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii imewatelekeza Walimu. Tumesema tunahitaji Walimu wa Sayansi katika nchi hii lakini tuna vyuo vya ualimu visivyo na maabara. Nitavitaja baadhi muone kama vyuo vya ualimu ambavyo vinafundisha Walimu wa Sayansi havina maabara unategemea nini huko? Kuna Chuo cha Ualimu Vikindu, Chuo cha Ualimu Singa Chini, Chuo cha Ualimu Mpuguso, Chuo cha Ualimu Kitangali na vinginevyo hivi navitaja ni baadhi havina maabara na hakuna vifaa vya maabara. Sasa tunatarajia nini na tunajenga maabara nchi nzima tukitarajia kwamba tutapata Walimu bora ambao watakuja kufundisha watoto wetu lakini kule tunakoandaa Walimu wetu hakuna maabara. Serikali hii inafanya masihara na elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu hao hao wa Sayansi waliahidiwa kupewa mikopo, hapa ninavyozungumza Walimu hao wa Sayansi hawajapata fedha za mikopo mpaka dakika hii. Nina ushahidi nitakuletea orodha ya Walimu Mheshimiwa Waziri kama utahitaji, wengi hawajapata mikopo katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kuzungumzia katika suala la mitaala. Naomba ni *declare interest* mimi ni Mwalimu na pia nilikuwa mkuzaji wa mitaala kabla sijaacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kabisa tunapozungumzia elimu bora tunahitaji mitaala iliyo bora na mitaala ili iwe bora ina *process* zake za uandaaji. Zile hatua zikipindishwa ndiyo tunapata matokeo haya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatakiwa tufanye *research* ili kujua Serikali yetu au nchi yetu inataka Watanzania wawe na elimu ya namna gani ili kuwanufaisha hao Watanzania, ile sera kwanza haipo vizuri. Tulikuwa tuna falsafa ya elimu ya kujitegemea huko nyuma lakini sasa hivi haieleweki na haitafsiriki vizuri kwenye mitaala kwamba tunakwenda na falsafa ipi sasa hivi. Je, bado ni elimu ya kujitegemea mpaka sasa hivi ama tuna nini ambacho kipo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya *process* nyingine zinarukwa, tunatakiwa tuite wadau ili tukubaliane nao ni yapi ambayo tunatakiwa kuyaweka kwenye mitaala. Mheshimiwa Waziri alikuwa ni Mjumbe wa Bodi katika Taasisi ya Elimu Tanzania anaelewa matatizo yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi tulikuwa tukiomba fedha Wizara ya Elimu lakini fedha za kufanyia mambo hayo mengi zinakuwa hakuna, unatarajia upate nini? Unatakiwa ufanye utafiti, uitishe wadau lakini kwa kiasi kikubwa wadau wa nchi nzima unaweza ukaita wadau 60 au 100, hao watasaidia kuweza kujua kwamba nchi hii inahitaji twende katika mrengo upi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika suala hilohilo kuna masuala ya vitabu. Mheshimiwa Waziri amezungumza katika hotuba yake, amezungumzia masuala mengi yanayohusu masuala ya vitabu. Kulikuwa na bodi iliyokuwa inaitwa *EMAC* ambayo walikuwa wanashughulikia vitabu vyetu, ilivunjwa wakarudisha Taasisi ya Elimu Tanzania iweze kufanya kazi hiyo. Hivi ninavyozungumza hapa shule zetu kule hazina vitabu, Wizara imeandaa masuala ya KKK lakini sijui huo usambazaji TAMISEMI unakwenda vipi. Walimu wanakwenda wanafundisha bila vitabu na vitabu vyenyewe vilivyokuwa vimetolewa kwa masomo mengine vinatofautiana, hii ni changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ya 80 kulikuwa na ushindani baina ya shule za Serikali na shule za watu binafsi. Leo hii mnaleta bei elekezi, hivi hawa wenye shule binafsi wangekuwa hawakuweza kuwekeza hivyo wale watoto wetu waliokuwa wanaachwa wangekwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, badala ya kukaa tukaboresha elimu yetu katika shule zetu za Serikali ndipo sasa tuanze kuona kwamba tunaweka bei elekezi baadaye, kwa nini tunaanza kubana watoto wetu wasiweze kusoma katika hizo shule kwa sababu huku waliachwa katika nafasi ya shule za Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu shule za Serikali zinawachukua wale ambao ni bora na hawa shule binafsi zinawachukua wale ambao siyo bora ilivyokuwa zamani. Sasa hivi hata wazazi hawaoni umuhimu huo kwa sababu kule shuleni tunakuta hakuna Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mfano katika Mkoa wangu wa Iringa kuna baadhi ya shule ina Mwalimu mmoja shule nyingine zina Walimu wawili, shule ya sekondari wanatakiwa wafundishwe masomo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kimoja Mheshimiwa Waziri lazima mtambue utahini wa mitihani. Shule X ambayo ina Walimu wa masomo yote na shule Y

ambayo kwa mfano ina Mwalimu mmoja au wawili lakini mwishoni mwa utahini mnatahini mitihani sawa. Hii siyo sawa hata kidogo!

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwaangalie wale ambao wamefundishwa na Mwalimu mmoja somo moja tutahini kwa kile walichofundishwa! Kwa nini mnawafelisha watoto wetu wakati mwingine wakati siyo makosa yao kwa sababu… *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante.

Kabla hajasimama Mheshimiwa Mlowe, Mheshimiwa Mwijage ana wageni wake ambao walisahaulika kusomwa, samahani. Wageni tisa wa Mheshimiwa Savelina Mwijage ambao ni viongozi wa Chama cha Wananchi *(CUF)* kutoka Mkoani Kagera, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza nimshukuru Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kufika hapa ndani saa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwe wazi kwamba mimi nina shule, vilevile ni Mwalimu na nina Kituo cha Watoto Yatima. Hivyo vyote kwangu ni mwiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na suala la watoto yatima, tunaongelea suala la mikopo, kwangu mimi mwenye Kituo cha Watoto Yatima nimekuwa na watoto na vijana zaidi ya 451 ambapo 15 walitakiwa kwenda chuo kikuu kwa njia ya mkopo lakini hawakuweza kufanikiwa, sielewi ni vigezo vipi ambavyo vimekuwa vikitumika kwa ajili ya kupata mikopo. Hivyo naona kuna matatizo kwenye mikopo, Bodi ya Mikopo ina matatizo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri niombe uone namna utakavyofuatilia suala hili na kuhakikisha kwamba vigezo stahiki vinatumika kwa ajili ya mikopo hiyo hasa kwa watoto yatima na watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika suala la Walimu; mimi kama Mwalimu nina uchungu sana, nina uchungu na maisha wanayoishi Walimu kwa sababu mwenyewe nimekuwa katika mazingira hayo magumu. Mwalimu inafika hatua

Afisa Elimu anakuchapa makofi au vibao, mfano, kule Rukwa kuna Mwalimu alichapwa na Afisa Elimu, jamani haki ziko wapi kwa Walimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo haitoshi Walimu wanapangiwa kwenda kufanya kazi maeneo ya mbali. Mfano pale Njombe nina Walimu zaidi ya watano walipangiwa kazi Mwanza. Walimu hawa walikuwa ni wanandoa, lakini unakuta Mwalimu wa kike anapangiwa Mwanza, mume wake anapangiwa Kondoa. Hapa naona vilevile Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inakinzana na Sheria ya Ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sasa tuone namna gani tunawasaidia Walimu kwa kuweka sheria hizi mbili vizuri kwa sababu sasa hivi tunaongelea suala la UKIMWI na Mkoa wangu wa Njombe ninavyoona ndiyo unaoongoza, halafu bado tunawatenganisha Walimu hawa wanandoa, kwa kuwapeleka kukaa maeneo tofauti, tunategemea nini. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, akisaidiana na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, waone namna gani tunawasaidia Walimu hawa, wanandoa naomba wapangwe sehemu moja. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la mitaala; miaka ya nyuma kabla ya mwaka 2005 mitaala ilikuwa imejielekeza zaidi kwenye maarifa, lakini baada ya mwaka 2005 mitaala hii ilibadilishwa na ikaja kuboreshwa mwaka 2013. Mitaala hii imekuwa angamizo kwa kweli, kwa nini imekuwa angamizo? Watoto wetu sasa hivi wanajua kusoma vizuri na kuweza kutoa maana ya vitu fulani au kujieleza lakini hawajui kufanya kazi yoyote ile. Mfano mtu mpaka yuko Chuo Kikuu hajui hata kusonga ugali, mtu yuko chuo kikuu hajui kufua nguo, sasa hiyo ni mitaala ya namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri turudi kwenye mitaala ambayo tulisoma sisi kule nyuma. Mtu kuanzia darasa la nne anajua namna ya kufanya kazi ndani ya nyumba, namna ya kuelekeza hata wadogo hata kama yeye ni mdogo anajua namna ya kuelekeza mdogo wake, anajua kufua nguo, anajua kuosha vyombo, lakini sasa hivi hakuna. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sayansi ya jamii haipo tena, nitoe tu mfano mdogo tu, tukiwa darasa la nne, mimi nikiwa darasa la nne, nilijua hata maana ya pazia, unapoweka pazia ndani ya nyumba, unapoweka kwenye dirisha ugeuzie wapi na maana yake nini, lakini hata ukimuuliza mtu aliyemaliza chuo kikuu hajui hata maana yake, hajui hata lengo la pazia ndani ya nyumba ni lipi. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri, tutumie njia yoyote turudi kwenye mitaala yetu ile tuliyoiacha, elimu tumeipeleka wapi? Sayansikimu tumeipeleka wapi, watoto hawajui kupika. Kwa hivyo, niombe tafadhali, Serikali ilione hili tusaidiane kuhakikisha tunarudi kule nyuma, tuwasaidie, tuokoe Taifa hili linaloangamia. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala linguine, sasa hivi tumeanza kwa nguvu zote na ni jambo jema, kuwahamasisha watu ambao walikopa na wengi wetu humu ndani nafikiri tulikopa, tumesoma kwa mkopo, lakini hebu tujiulize, tunapohamasisha kurudisha hiyo mikopo hao watu wote wamepata ajira! Watu wengi wako mitaani na ndiyo maana inakuwa vigumu kufuatilia kuwa na mapato makubwa yanayotokana na mikopo kwa sababu wengi hawajapata ajira, hivyo tuone ni namna gani tunawafuatilia wale wa mitaani tutumie njia ya kisasa kuweza kuwafutilia hao walioko mitaani na kuhakikisha tunakusanya pesa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tutengeneze mazingira ya wao kuajiriwa na hata kama inawezekana basi, tutumie njia ya kuwafundisha au kuielimisha jamii namna gani iweze kuwa na njia za kujitegemea au ujasiriamali ili waweze kurudisha pesa hizi ambazo wananatakiwa warudishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la uhamisho. Sasa hivi wanahamishwa watumishi toka kona moja hadi nyingine, lakini hawapati pesa za uhamisho. Unakuta Mwalimu anapangiwa kwenda kufundisha mfano Mwanza au Tabora, anafika kule hana hela ya kujikimu, hana sehemu ya kukaa, mwisho wa siku anaanza kuombaomba, huyo ni Mwalimu na huko ni kumdhalilisha Mwalimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo nimwombe Mheshimiwa Waziri, tuwasaidie watu hawa, tunapowapangia tuhakikishe basi pesa ya kujikimu tumeiandaa na mahali pa kukaa tumepaandaa na nyumba za Walimu ziandaliwe. Walimu wengi sasa hivi wamekata tamaa wanahama fani kutokana na ugumu huo wa maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge hoja ya Upinzani kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mlowe ahsante sana kwa mchango wako, naamini ule mchango wako mwingine ulikuwa unatugusa wafanyakazi wote, waume zetu wahamie Dodoma. (*Kicheko)*

Mheshimiwa Hamida Mohammed Abdallah!

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia. Nianze kwa kumpa pole Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi ndugu yetu *Engineer* Stella Manyanya kwa msiba ambao ameupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nichangie hotuba hii ya Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi. Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii ni nzuri, ina mikakati mizuri, yenye utekelezaji wake kwa kipindi hiki tunachokitarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona mambo mengi, mafanikio mengi katika upande huu wa elimu. Tumejenga shule nyingi za msingi, shule za Sekondari, shule za ufundi *VETA*, Vyuo vikuu lakini uwepo wa vyuo vikuu huria katika Mikoa yetu. Vyuo vikuu hivi vilivyopo katika mikoa yetu kwa kiasi kikubwa vimeweza kuwasaidia vijana wengi, watumishi wengi, kuingia katika kujiendeleza na elimu hii ya juu. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio haya tuliyoyapata, lakini kuna changamoto mbalimbali katika miundombinu ya elimu. Waheshimiwa Wabunge wengi sana jana wamechangia katika changamoto mbalimbali zilizopo katika eneo hili la elimu. Pamoja na kutokuwepo kwa Walimu wa kutosha lakini vitendea kazi tumeona ni changamoto kubwa. Tumefanya jitihada kubwa sana katika kuhakikisha shule zetu za sekondari zinakuwa na maabara katika kila eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule hizi zilijengwa kwa changamoto kubwa sana na kwa agizo la Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu iliyopita. Hata hivyo, tumeona maabara hizi zimeendelea kubaki hivi hivi, hazina hata samani ndani ya vyumba vile, matokeo yake vyumba vile vimeendelea kukaa hivi hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu kubwa ni watoto wetu wapate masomo kwa nadharia, lakini kwa vitendo pia. Kwa hiyo, ningependa Mheshimiwa Waziri atakavyofanya majumuisho yake hapa leo, atuambie ni mkakati gani ambao ameuandaa katika kuhakikisha maabara zetu tulizozijenga zinafanya kazi kama ambavyo tumetarajia. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani kubwa sana na Serikali ya Awamu ya Tano yenye kauli mbiu ya Hapa Kazi Tu. Tumeona jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais wetu anavyotekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kuanza kutoa elimu bure kuanzia shule ya awali, shule ya msingi na shule ya sekondari. Vile vile tumeona jitihada kubwa anayofanya katika kutatua kero hii ya madawati na madawati haya yatakuja katika Majimbo yetu. Tunamwombea kila la heri Mheshimiwa Rais wetu, aendelee na jitihada ambazo anazifanya lakini aendelee kutuongoza Watanzania. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona katika shule hizi za ufundi, shule za *VETA*. Sera ya Elimu ilisema kujengwa shule za *VETA* katika kila Wilaya. Nashukuru katika Mkoa wetu wa Lindi, Lindi Manispaa tunayo shule hii ya *VETA,* lakini kutokana na sera hii ya ujenzi wa shule hizi za *VETA* kila Wilaya hatujafanikiwa kwa kiwango ambacho tumekitarajia. Wilaya nyingi zimekosa

kuwa na vyuo hivi vya *VETA*. Kwa hiyo, hii inawafanya vijana wetu wengi wanaomaliza darasa la saba, wanaomaliza *form four* ambao wamefeli kushindwa kuendelea na shule hizi za ufundi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani tulikuwa na shule za ufundi katika shule zetu za msingi hasa pale kwetu katika Mkoa wa Lindi, tulikuwa na shule za msingi ambazo zina shule za ufundi, lakini baada ya sera hii ya kujenga vyuo katika kila Wilaya. shule zile za ufundi zilifungwa. Tunapata shida sana kwa sababu shule hizi za *VETA* hazipo katika kila Wilaya, matokeo yake vijana wetu wanaofeli darasa la sababu, wanashindwa kujiendeleza. Shule zile zilikuwa zinasaidia sana katika kuwafanya vijana wetu wanapata fani mbalimbali na hatimaye wanaweza kujiajiri wenyewe.

Mheshimwa Naibu Spika, napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, shule zile ambazo zilikuwa na shule za ufundi, basi ziweze kuendelea na shule hizo za ufundi ili watoto wetu watakapomaliza darasa la saba na kufeli, basi waendelee kupata elimu hii ya ufundi na hatimaye waweze kujiajiri. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Lindi na Mtwara kielimu kwa muda mrefu tuko nyuma sana. Hii imechangiwa na mambo mbalimbali nitasema jambo moja tu ambalo lilisababisha kuwa nyuma kielimu katika Mikoa hii miwili ya Lindi na Mtwara. Katika harakati za ukombozi wa nchi za Afrika, maeneo ya Mkoa wa Lindi na Mtwara, yalikuwa ni maeneo ya mafunzo ya kivita kwa ajili ya maandalizi ya ukombozi huu wa nchi za Afrika. Kulikuwa na makambi ya South Afrika ya Nelson Mandela, kulikuwa na makambi ya Msumbiji ya Samora Mashelu, lakini kulikuwa na makambi ya nchi za Zimbabwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa hii ya Lindi na Mtwara lilikuwa ni eneo linaloitwa *danger zone,* kwa hiyo, kwa kweli Serikali haikuweza kujenga shule kama ambavyo tulitarajia na kufanya watoto wa mikoa hii miwili waweze kuwa nyuma kielimu. Kwa hiyo, naiomba Serikali, pamoja na jitihada hizi kubwa tulizozifanya za kujenga shule za sekondari kila Kata, lakini tuna changamoto kubwa sana ya ukosefu wa Walimu katika shule zetu. Suala la Walimu kila Mbunge aliyesimama amelizungumzia, pamoja na kuwa na maslahi duni, lakini tumekuwa na ukosefu mkubwa sana wa Walimu hasa Walimu wa sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wetu wa Lindi, mahitaji ya Walimu wa sayansi yalikuwa 726, lakini waliopo ni 262 na pungufu ni 464. Upungufu huu ni mkubwa sana, maana hata nusu ya mahitaji yetu kwa walimu hatukupata. Kwa kweli Serikali haijatutendea haki maana tutaendelea kuwa nyuma mwaka hadi mwaka kwa kiwango hiki cha Walimu tuliowapata. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu atutazame kwa jicho la huruma sana katika Mkoa wa Lindi kuhakikisha tunaongezewa idadi ya Walimu hii hasa wa sayansi ili watoto wetu waendelee kupata elimu iliyo bora kwa kipindi hiki tunachokitarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la maslahi ya walimu limeongelewa karibu na Wabunge wote waliozungumza tangu jana hadi leo, lakini mafao ya Walimu wastaafu pia yamekuwa ni tatizo, kwa hiyo naiomba Serikali yangu sikivu, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuwaangalia Walimu hao wastaafu…

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hamida muda wako umekwisha, tunaendelea.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Edwin Sannda atafuatiwa na Mheshimiwa Stella Ikupa Alex na Mheshimiwa Amina Mollel ajiandae.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, kwanza kabisa pamoja na kazi kubwa, kazi nzuri inayofanywa na Waziri pamoja na timu yake yote, lakini napenda kusema kwamba, naona bajeti hii haija-*reflect* ile safari tunayotaka kwenda, haija-*reflect* mapinduzi ya elimu ambayo tunataka kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumzia tunakwenda kwenye uchumi wa kati, uchumi wa kati tukasema tunahitaji mapinduzi ya viwanda, lakini kunahitajika mapinduzi mengi tu, mojawapo ni mapinduzi ya elimu, tuweze kweli kweli kupata *transformational change*. Sasa kama safari ni hatua, tuone kabisa hatua inayokwenda, kama nakwenda tuseme Kondoa, basi naona nimetokea Dodoma naona nimefika Aneti, nione nimefika Chemba, mwisho wa siku nifike Kelema na hatimaye nifike Kondoa. lakini kwa bajeti hii na malengo yetu ya muda mrefu ambayo tunataka kuyafikia, kwa kweli Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yako, nafikiri kuna kazi kubwa sana ya kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri inabidi tuamue sasa kuwekeza kwenye elimu kwa kiwango kikubwa kweli kweli. Huu uwekezaji tulioufanya sasa hivi katika bajeti, naona hautatufikisha pale tunapotaka kwenda, hiyo nilipenda nianze kuzungumzia kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye hoja mahususi katika bajeti nzima ya elimu. Kwanza napenda kuongelea wanafunzi. Suala la mfumo, muundo na kanuni za ufundishaji na kwa maana ya kutoa mitaala naona haimjengi mwanafunzi wa Kitanzania katika kwenda kuingia umahiri katika soko la ushindani kwa maana ya *competence*. Sisi hatuko wenyewe, dunia siku hizi ni

kijiji na inatakiwa wanafunzi wetu wanapotoka huko nje waweze kushindana katika soko duniani, waweze kujiamini, wajenge uelewa badala ya kujenga kukariri na kufaulu mitihani, wajenge uwezo wa kujieleza, matokeo yake wanapofika huko mbele wana uwezo mkubwa wa kupambana na ku-*survive*, wanasema *survival for the fittest*. Sasa kama elimu yetu haitujengi kwenda kuwa *fit* duniani itatukwamisha sana, tutakuta tu tunaendelea ku-*import knowledge* kutoka kwa wenzetu, lakini wa kwetu sisi hawatoki kwenda nje nao wakafanye vitu vyao huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri ni wakati muafaka kabisa Wizara ikae na kujiuliza, hivi tatizo liko wapi? Tujiulize sana na tufanye tafiti za kutosha sana, tunao Wataalam, tujiulize tatizo liko wapi? Kwa nini *output*, kwa nini *products* za wanafunzi wetu siyo mahiri? Kwa nini hatuko *competent* sana *on average*? Wapo watu wazuri, wanatokea wazuri, lakini *on average* elimu yetu hairidhishi. Kwa hiyo katika hili, ningesisitiza sana uwekezaji *investment* ifanywe kubwa sana kwenye *RND* kuweza kuhakikisha tunainua ubora wa elimu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nataka nizungumzie kwa upande wa Walimu. Hapa hasa ndiyo kwenye kasheshe. Ifike mahali sasa ile dhana iliyopo kwamba Ualimu ni kazi ambayo ni dhaifu, mtu huwezi kujivunia, hatuwezi kuikimbilia, tubadilike kabisa. Ifike mahali Ualimu uheshimike, mtu unapoamua kwenda kusomea Ualimu una-*proud* kwamba mimi ni Mwalimu. Mwalimu awe na uhakika wa ajira, lakini awe na uhakika wanasema maslahi mazuri, *very well paid,* waweze kuwa *motivated* vizuri sana, waweze kuwa na *incentives* kubwa, lakini mazingira pia ya kazi lazima yawe tofauti sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaowachukua hawa kuwa Walimu, siyo ile ya sasa hivi labda tunakwenda mpaka *division* tofauti tofauti, Walimu wanatakiwa kuwa *top scores, top performance* ndiyo wawe Walimu na mwisho wa siku na kama maslahi yako mazuri na wanalipwa vizuri, kila mtu atakuwa ana *pride* kusema akawe Mwalimu na watu wengi watakimbilia kwenda kufundisha. Ualimu uwe ni kazi ya *bright students*. Tukifanya hivyo kweli tutakuwa tumefanya *transformational change*, mwisho wa siku Walimu wetu kama ni wazuri, *obviously products* zao zitakuwa ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, napenda kuchangia kwenye suala zima la *polytechnic*, Vyuo vya Ufundi. Hapo zamani tulikuwa na Vyuo vya Ufundi Dar *Tech*, chuo ambacho nilisoma mimi, Chuo cha Ardhi kilikuwa kinatoa Wataalam, Mafundi, lakini sasa hivi vile vyuo vyote tumevigeuza vinapanda hadhi vinakuwa Vyuo Vikuu. Sasa kama kila mtu atavaa tai, kila mtu anataka kuwa meneja, kila mtu anataka kuwa na *degree,* nani atakwenda *site* kusimamia kazi? Nani ataingia maabara kuhakikisha kazi za kitaalam zinafanywa vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka kuwa na Vyuo Vikuu vingi, ni sawa tuwe na Vyuo Vikuu vingi, lakini *polytechnic* ni muhimu sana kuhakikisha kazi za kitaalam zinafanywa. Rai yangu kwa Serikali, hebu tuache hili suala la *degree* na tai, lakini tuwe na *FTC's* za kutosha. Arusha *tech* ziimarishwe, ziwe bora zaidi, ziwe *equipped*, ziwe *resourced* ili watu wetu wanaotoka kule wakienda kazini, wawe na uwezo hasa wa kusimamia *details* za kitaalam. Turudishe *polytechniques* zetu. Kwa hiyo, pamoja na jitihada kubwa ya kuongeza idadi ya Vyuo Vikuu na kutoa *degree*, hebu na suala la *polytechnique* tuliangalie sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tano na la mwisho, napenda kuongelea kuhusiana na wataalam, watu wanao-*qualify*, wamekwishasoma *degree* zao au kama ni *FTC*, wametoka wameingia kwenye soko la ajira, tutengeneze utaratibu mmoja wa kuwekeza kwa hawa watu ili wakapate *exposure programs,* wajifunze, waige utaalam, waige *experience*. Nchi za wenzetu ambazo kwa baadhi ya taaluma zinafanya vizuri. Nitatolea mfano suala la Madaktari, hata Walimu au Wahandisi, lakini nitatolea mfano suala la Madaktari; watu wawe wanatoka tunawapa Mikataba *specific* wameshamaliza shule, lakini anapelekwa mtu zaidi ya miaka mitano mpaka hata kumi, si tunawekeza kwa ajili ya *generation* zijazo? Tunawekeza kwa ajili ya kupata *transformation* ya elimu yetu kwa ujumla wake, watu waje hapa wana uwezo mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tu tumeshuhudia Tanzania zimefanyika *operations* za kwanza kubwa za moyo. Watu wanafunua moyo ule ndani wanazibua mirija iliyoziba, lakini waliokuja kufanya ile *operation* wanatoka India. Kawaida kuna ushirikiano na Australia, Saudi Arabia na Marekani, basi tuwapeleke Madaktari wetu nao wakasome, tuweke mikataba mahususi, watu wakasome, tukishamaliza kuwekeza kwenye elimu hapa, wakimaliza wanakwenda nje, wakirudi *they bring back wealth of experience* ambayo itatusaidia sana kubadilisha mfumo mzima wa uwezo na *knowledge* hapa nchini. Kwa hiyo, nasisitiza sana, katika jambo kubwa tunalotakiwa kulifanya kama Serikali ni kuwekeza kwenye elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumerudia na tunaendelea kuimba kwamba tunakwenda kwenye uchumi wa kati, lakini huu uchumi wa kati bila mapinduzi na *transformation* ya sekta nyingine hizi kama elimu, pia ni mtihani mkubwa tunaweza tusifike. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Elimu kama *pioneer* katika Serikali kwenye suala zima la elimu, hebu tuangalie maeneo yote haya, kuanzia mitaala, kuufanya Ualimu uwe ni kazi ya kujivunia, shule zetu za *polytechnique* pamoja na hawa wataalam tuweze…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Sanda. Mheshimiwa Stella Ikupa Alex atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Mollel. Mheshimiwa Joram Ismail Hongoli naye ajiandae.

MHE. STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ajili ya ulinzi, rehema na fadhila zake kwangu pamoja na familia yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda niitumie nafasi hii kumpa pole sana Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineer* Stella Manyanya kwa kuondokewa na mama yake mpendwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba niitumie tena fursa hii kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa jinsi ambavyo imetekeleza kwa haraka sana ahadi yake ya elimu bure kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha nne. Kama tunavyofahamu kwamba, hata mbuyu ulianza kama mchicha, pamoja na changamoto zilizopo lakini Serikali yetu inastahili kupewa pongezi kwa jinsi ambavyo imefanya na kwa jinsi ambavyo inaendelea kutatua changamoto ambazo zimejitokeza ikiwemo changamoto ya madawati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee tatizo la ufaulu wa msomo ya sayansi, *biology* pamoja na *mathematics*. Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake ameliongelea hili, lakini naomba niongelee kwa msisitizo. Kweli kumekuwa kuna tatizo kubwa la ufaulu wa masomo haya kwa watoto wetu, tatizo ambalo linasababishwa na Walimu lakini pia ukosefu wa maabara pamoja na vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kwa upande wa Walimu, iangalie watu ambao wanakwenda kuchukua *course* ya Ualimu, wawe ni wale watu ambao wamefaulu sana katika haya masomo yaani *chemistry*, *biology* na *physics*. Inakuwa inatia simanzi sana kuona kwamba Mwalimu ambaye labda yeye alipata 'D' lakini ndiyo huyo anayekwenda kusoma Ualimu wa *physics* au Ualimu wa *chemistry*. Kwa hiyo, naishauri sana Serikali iliangalie hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niongelee suala zima la ukosefu wa maabara pamoja na vifaa katika hizi maabara. Inatia simanzi sana kuona kwamba vyumba vipo, lakini vifaa vya maabara hakuna tatizo ambalo linapelekea wanafunzi kufundishwa *theory,* lakini baadaye inabidi aende akafanye *practically*, vifaa hamna vya kumwezesha mwanafunzi huyu kufanya hizi *practical,* mwisho wa siku anaingia kwenye chumba cha mtihani anakutana na swali hata ambalo ni rahisi la *titration* anashindwa kufanya, anakutana na kifaa kama *test tube,* anashindwa kugundua kama hiki kifaa kinaitwa *test tube*.

Kwa hiyo, niiombe sana Serikali iliangalie hili, iangalie uwezekano mkubwa wa kuweka vifaa kwenye hizi maabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niongelee suala zima la changamoto ya elimu kwa wanafunzi ama watoto wenye ulemavu. Changamoto ziko nyingi sana, lakini naomba niongelee changamoto chache kwa sababu ya muda. Kuna changamoto kubwa ya Walimu kwa watoto hawa wenye ulemavu. Changamoto hii ni ya muda mrefu na ni changamoto kubwa. Niiombe sana Serikali kwa habari ya Walimu wa kundi hili maalum, wawachukue wale Walimu ambao wana uweledi wa kuwafundisha watoto hawa ndiyo ambao wakachukue *course* hii ya kufundisha watoto wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niiombe Serikali itoe motisha kwa sababu kiukweli kufundisha makundi maalum ni kazi. Kwa hiyo, itoe motisha kwa maana ya *pakages* za mishahara ziwe kubwa tofauti na Walimu wa wanaofundisha watoto wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niongelee suala zima la changamoto ya miundombinu kwa watoto wenye ulemavu ama wanafunzi wenye ulemavu. Changamoto hii ni kubwa kuanzia *primary school* mpaka vyuoni. Naomba nitolee mfano mdogo wa Chuo Kikuu cha *UDOM*, hiki chuo ni kipya, kimejengwa miaka ya hivi karibuni, lakini cha kushangaza miundombinu yake si rafiki kwa wanafunzi wenye ulemavu. Kwa hiyo, niiombe Serikali iangalie suala zima la kuboresha miundombinu kwa wanafunzi ama watoto wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna changamoto ya uhaba wa shule za haya makundi maalum. Shule ni chache sana ukilinganisha na uhitaji. Kwa mfano, unaweza ukakuta labda shule inapatikana Dar es Salaam, lakini mtoto yuko Mtwara, ama yuko Mwanza ama yuko mahali ambako panakuwa hapana shule, inakuwa ni ngumu sana kwa sababu tuelewe kwamba wazazi wengi wenye watoto hawa wana kipato cha chini. Kwa hiyo, inakuwa ni ngumu mzazi huyu kumleta mtoto wake shule halafu aje amfuate, ukizingatia kwamba pia kulikuwa kuna ile pesa ambayo inatolewa kwa ajili ya kumwezesha mzazi mwenye mtoto mwenye ulemavu kuweza kumpeleka mtoto wake shuleni, hizi pesa siku hizi hazitolewi tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niiombe sana Serikali izirudishe hizi pesa, iwapatie wazazi wenye watoto wenye ulemavu pamoja na walezi ili waweze kusafiri kuwapeleka watoto hawa kwenye maeneo ambayo yana shule maalum. Pia niiombe Serikali kuboresha sana hizi shule ambazo zipo kwenye maeneo, kwamba watakapoziboresha hizi shule katika maeneo husika, itaondoa huu usumbufu wa wazazi kusafiria huduma hii ya shule kwenda mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala zima la changamoto ya vifaa saidizi kwa watoto wenye ulemavu. Unaweza ukakuta kwamba mtoto ana uwezo wa kwenda shule, wa kusoma lakini sasa changamoto yake aidha ni *wheel chair* au ni *brail* au ni vifaa vingine vinavyofanana na hivyo. Changamoto hii ni kubwa sana na inawafanya watoto wengi washindwe kwenda shule kwa sababu ya ukosefu wa hivi vifaa saidizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Wizara ya Elimu, ishirikiane na TAMISEMI pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu kuwabaini watoto ambao kweli wana uhitaji wa hivi vifaa saidizi na waweze kupatiwa hivi vifaa tofauti na sasa hivi, vifaa hivi vinaweza vikawa vinatolewa lakini haviwafikii wale walengwa, kwa maana kwamba utakuta mtu yule aliyenacho ndiye anaongezewa, kwamba mtu ambaye ana uwezo wa kupata hiki kifaa ndiye huyo ambaye anapewa tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi hili la utambuzi linawezekana kabisa kwa sababu mimi mwenyewe binafsi nimeshawahi kufanya hilo zoezi. Ni juzi tu hapa nilimtumia Mwenyekiti wangu wa Serikali za Mitaa, nikamwambia kwamba naomba nifahamu idadi ya walemavu waliopo kwenye mtaa huu pamoja na changamoto zao na ilikuwa ni *within a week* yule Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa alinipatia orodha ya hawa watu wenye ulemavu pamoja na changamoto zao. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara ya Elimu ishirikiane na Ofisi ya Waziri Mkuu inayoshughulikia Bunge, Sera, Ajira na Walemavu pamoja na TAMISEMI kuwabaini watoto hawa na kuweza kuwapatia hii huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niongelee suala la hivi Vyuo vya *VETA*. Kumekuwa kuna ongezeko kubwa la ombaomba wenye ulemavu pamoja na tegemezi. Niiombe sana Serikali, ili kupunguza hili wimbi la ombaomba wenye ulemavu, iwasaidie kwa kuwawezesha kusoma katika hivi vyuo vya *VETA* ikiwezekana iwe ni bure kabisa ili waweze kupata ujuzi wa kuweza kumudu maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niongelee na niiombe Serikali kwa habari ya suala zima la lugha ya alama. Kumekuwa kuna changamoto kubwa ambayo tumekuwa tukiiongea kila siku, uhitaji wa Wakalimani wa lugha za alama, lakini nashauri kwamba lugha hii ya alama ifundishwe kama somo mashuleni, kwa maana kwamba mtoto huyu ambaye anasoma sasa hivi darasa la kwanza, anafika *form six,* ndiye mtoto ambaye tunamtegemea kwamba aje kuwa Daktari amuhudumie mtu ambaye ni kiziwi, aje kuwa ni Polisi, aje kuwa ni Nesi ambaye atamzalisha mtu ambaye ni kiziwi. Pia itasaidia hata kwenye jumuiya zetu kwamba unakutana na mtu ambaye ni kiziwi, lakini kwa sababu ulishasoma hii lugha ya alama inakuwa ni rahisi ku-*communicate* naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niongelee suala zima la Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu ambao ulianzishwa kwa Sheria namba 9 ya mwaka 2010. Mfuko huu upo lakini umekuwa hautengewi fedha wala haupatiwi fedha. Niiombe Serikali sana kwamba sasa umefika wakati Mfuko huu utengewe na kupatiwa pesa, pesa hizi zitasaidia kwa habari ya mahitaji ya watoto wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuongelea msongamano wa watoto kule Buhangija. Kule kumekuwa kuna msongamano mkubwa wa hawa watoto, naishauri Serikali kwamba ifanye kuwatawanya kwa yale maeneo ambayo yako *safe* ambapo kwa mfano, kama Dar es Salaam, Arusha, Kilimanjaro ni mikoa ambayo iko *safe* ambayo haijaripotiwa na haya matukio ya mauaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Amina Mollel, Mheshimiwa Joram Hongoli ajiandae halafu atafuatiwa na Mheshimiwa James Mbatia.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwepo hapa, niishukuru pia familia yangu walitambua umuhimu wa mimi kupata elimu ndiyo maana nikawepo hapa, lakini vile vile naomba nimpongeze Waziri mwenye Wizara husika Mheshimiwa Waziri Ndalichako kwa jitihada zake za kuhakikisha kwamba tunaboresha elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nianze kwa kunukuu. Kama tunavyofahamu elimu ni maarifa na maarifa ni maisha. Maana yake jamii ikipata elimu, watoto wakipata elimu ,basi watakuwa na maisha bora. Natambua jitihada za Serikali katika kuboresha elimu tangu uhuru. Kwa mfano, mwaka 1961-1984 kwa falsafa ya Elimu ya Kujitegemea; lakini vile vile Sera ya Elimu mwaka 1995 ambapo Serikali ilikuja na Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi; mwaka 2002-2006 ikaja na MMEM na MMES na mwaka 2014 Sera ya Elimu imeasisiwa, lakini pamoja na jitihada hizo za Serikali bado elimu bora kwa Watanzania na nalenga hasa kundi la watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimnukuu mtu ambaye ni miongoni wa watu wenye ulemavu ambao wamefanikiwa sana, Bwana Nicolaus James maarufu kwa jina la Nick Vujicic ambaye yeye ni mlemavu kutoka nchini Australia, hana miguu, hana mikono, lakini pamoja na yote hayo mafanikio yake ni makubwa na ni mfano wa kuigwa na walemavu wote duniani kutokana na jitihada zake. Hata hivyo, Bwana Nicolaus James au Nick Vujicic yeye

amefanikiwa kutokana na Serikali yake kutambua kwamba kuwa na ulemavu siyo kulemaa, kwa maana hiyo iliboresha miundombinu na kuhakikisha kwamba Bwaba Nicolaus Vujicic anapata elimu, ili elimu ndiyo iwe mtaji katika maisha yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nizungumzie changamoto za watu wenye ulemavu na hasa watoto wenye ulemavu kwa hapa nchini Tanzania. Hii sio kwamba kwa nchi hii ya Tanzania tu, ni Afrika yote, lakini kwa sababu mimi ni Mtanzania naomba nizungumzie nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze kwa kusema kwamba; kama familia yangu isingetambua umuhimu wa mimi kupata elimu, leo hii nisingekuwa hapa, lakini walitambua umuhimu wa elimu ndiyo maana leo niko hapa na pengine isingekuwa hivyo, ningekuwa ombaomba mitaani. Kwa maana hiyo, siyo walemavu wote wanaoomba wanapenda, yote hiyo ni kutokana na maisha, ni kutokana na wao kutokupata elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kibaya zaidi najiuliza swali; ni kwa nini watoto wengi wenye ulemavu wanatoka katika familia maskini? Hili ndilo ambalo linatukosesha sisi elimu kwa sababu katika familia kama kuna watoto watatu na yupo mtoto mwenye ulemavu, familia itaona ni afadhali iwapeleke watoto wasio na ulemavu ili wakapate elimu na kwa maana hiyo yule mwenye ulemavu anabaki nyumbani. Kwa maana hiyo, huyu ambaye ana ulemavu, asipopata elimu ndiyo tunamuandaa na kumpeleka katika kundi la kuwa ombaomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina furaha kwa sababu mama Ndalichako ni mwananmke na wanasema "uchungu wa mwana, aujuaye mzazi" na hasa mama! Wewe ni mama! Nakuomba kwa moyo wangu wote, angalia watoto wenye ulemavu. Waandalie mazingira mazuri ili waweze kupata elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa naibu Spika, changamoto ni nyingi. Miundombinu sio rafiki kwa maana hiyo hata anapokwenda shule bado ni shida huyu mtoto! Ukienda vijijini watoto wanatembea kilometa saba, kama ni mtoto mwenye ulemavu atawezaje kutembea kilometa saba kwenda kupata elimu? Kwa hiyo hii inakuwa ni changamoto, hawezi kwenda kupata elimu!

Mheshimiwa Naibu Spika, yuko mtoto mmoja aliamua yeye kila siku awe anambeba mdogo wake, kumpeleka shule kwa sababu alijua hii ndiyo njia ya kumsaidia mdogo wake! Lakini alifika mahali kwa sababu yule binti anakua na uzito, alishindwa. Kwa hiyo, yule kijana alishindwa kumsaidia mdogo wake na mdogo wake akaishia hapo hakupata tena elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda katika shule zetu, mfano watoto wenye ulemavu wasioona, hawa wanahitaji vifaa ambavyo vinawawezesha mfano mashine za *braille,* katika shule nyingi hakuna hizo mashine. Huyu mtoto ili aweze kupata elimu inakuwa ni vigumu kwake. Naiomba Serikali kuhakikisha kwamba hivi vifaa vinapatikana na kwa sababu Waziri wa Fedha yuko hapa viko vifaa ambavyo ni muhimu vya kupunguziwa kodi au vikaondolewa kodi kabisa ili kuhakikisha watoto wenye ulemavu wanapata elimu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vyuo vyetu na vyuo vya ualimu, kwa nini Serikali isione umuhimu wa lugha za alama zikafundishwa ili Walimu wote wanapotoka shule wawe na ufahamu wa lugha hizi za alama, kwa sababu wakijua hivyo, mwanafunzi mwenye uziwi kule kijijini hatakuwa na haja ya kutafuta shule nyingine. Ndiyo maana ukienda hata katika vyuo vikuu ni nadra sana kuwakuta wanafunzi viziwi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa sababu hakuna Walimu wenye utaalam huo. Kwa hiyo, naomba sana Serikali kuhakikisha kwamba mitaala ya lugha za alama inafundishwa Walimu wote waweze kufahamu, lakini pia kuna ubaya gani kuingiza katika *syllabus* ili hata hawa wanafunzi wengine waweze kuwasiliana kwa sababu watajua kwa kujifunza hizi lugha za alama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko shule za binafsi na hapa Serikali tungeweza pia kuzitumia hizi shule za binafsi kwa kupunguza baadhi ya kodi ili watoto wenye ulemavu na wao wakapata nafasi. Ukimpunguzia kodi, atawachukua watoto, watano, wane; tayari hawa watoto wamepata elimu! Katika vyuo vyetu sio rafiki na hasa vyuo binafsi na hata Chuo Kikuu cha Dar es Salaam chenyewe ukinipeleka hata mimi pale mazingira sio rafiki ili niweze kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuhakikishe kwamba vyuo vyetu vyote na hii sheria ipo na nakumbuka mwaka 2013/2014, Waziri Lukuvi wakati huo tukiadhimisha siku ya watu wenye ulemavu duniani pale Iringa, alilizungumzia hili kuhakikisha kwamba majengo yote yanakuwa rafiki. Nashangaa ni kwa nini mpaka leo hii baadhi ya majengo hayaangalii hilo, lakini pia katika Vyuo Vikuu, tunawaandaa vipi hawa wanafunzi katika suala la mikopo? Wengine hawawezi hata kufuatilia. Tuwe na tangazo maalum, tuwaelekeze wanafunzi wanaomaliza elimu ya *form six* kuhakikisha kwamba wanapotaka kwenda kujiunga utaratibu mzuri umeandaliwa kwa ajili yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ni mengi, changamoto ni nyingi, lakini nimalizie kwa kusema kwamba; elimu ndiyo ufunguo wa maisha. Ukimwezesha mtoto mweye ulemavu, umemkomboa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga hoja mkono. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante! Nilisema kwamba Mheshimiwa Hongoli angefuata, naomba usubiri kidogo kwa sababu Mheshimiwa Mbatia ana dharura.

Mheshimiwa Mbatia! Halafu Mheshimiwa Hongoli atafuata na Mheshimiwa Riziki ajiandae.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utambulisho wa mwanadamu ni utu wake! Je mifumo yetu ya elimu inajali utu wa mwanadamu? Utu ndiyo msingi mkuu wa haki za binadamu. Lengo la nne la maendeleo endelevu ya dunia linasema *ensure inclusive and equitable, quality education and promote lifelong learning opportunities for all*; elimu shirikishi, sawa, bora kwa wote! Meli ya elimu Tanzania inazama, sisi tunaosafiri ndani ya meli hiyo hatujitambui, *both quality and quantity of education are being eroded*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania pole pole tunaondolewa kwenye mkondo muhimu wa maendeleo. Leo ni Ijumaa, Mtume Muhammad *(S.A.W.)* anasema "mwenye kutaka akhera na asome, mwenye kutaka dunia na asome, na mwenye kutaka vyote na asome! Elimu ni kitu chake kilichompotea Muislam, popote akipatapo na akichukue"

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma Biblia Takatafu Mithali 4:13, "Mtafute sana Elimu usimuache aende zake, yeye ndiyo uzima wako" popote umtafute! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeanza na hayo kwa sababu leo hii tunazungumzia ada elekezi. Ada elekezi maana yake nini? Serikali iingie kwenye ushindani, wala sio suala; ada elekezi, mabasi ya njano, kodi zisizotabirika kwenye sekta ya elimu! Mambo haya tuliongea na Mheshimiwa Rais Mstaafu wakati tunachangia BAKWATA mwaka juzi, shule ya Sekondari Al-Haramain pale Dar es Salaam na tukakubaliana kimsingi kodi kwenye sekta ya elimu ziondolewe, elimu ni huduma sio mambo ya kutoa kodi kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii niyapongeze Mashirika ya Dini kwa kazi nzuri wanayofanya na hasa Dayosisi ya Moshi, Askofu Fredrick Shoo, Askofu Isaack Amani na kazi wanazofanya zote hizo wanafanya kwa niaba ya Serikali wakiwepo Sekta Binafsi. Kwa hiyo, haya mambo ya ada elekezi na nini naomba wala tusipoteze muda, badala yake Serikali itoe ruzuku kwenye Mashirika ya Dini, kwenye Sekta Binafsi, wayape nguvu ili waweze kutoa elimu, Taifa letu likielimika, Taifa linafaidika kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto za Walimu, mafao yao, Walimu kukaa mbali na familia zao na wewe umelisemea vizuri sana, tunaomba watu wote waje karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, deni la Walimu sio suala la kuzungumzia tena! Leo hii Wizara ya Elimu inalijua vizuri. Juzi nilikuwa natoa vyetu, ukitoa vyeti *leaving certificate* vimeandikwa TAMISEMI, *Academic certificate,* Wizara ya Elimu, sasa watu hawa wanajichanganya, ni vitu gani vya ajabu sana! Jina la Wizara yenyewe, danadana tangu tumepata uhuru mpaka leo hatujui hata jina la Wizara ni kitu gani. Waziri akiingia kwenye Wizara ndiyo mfumo yaani Waziri ndiyo mfumo, aliyofanya Shukuru Kawambwa umekuja kuyapindua yote, utakayofanya sasa hivi wewe akija mwingine anayapindua yote, akija mwingine anayapindua yote, hili linakuwa tatizo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya *BRN* yamekwenda wapi leo hii? Yaani ni vitu vya ajabu tu! Miaka kumi mambo hayaeleweki. Jimbo la Vunjo tuna shule za msingi 128, shule 102 ziko hoi bin taabani, je, ni karne ya kuzungumzia mambo ya mifumo ya vyuo? Nilikuwa nasoma mitaala ya elimu ya awali, naunga mkono wale wote waliozungumzia walemavu. Ukisoma lile lengo la 326 kuhusu madarasa ya vyuo na namna ya walemavu kuweza kupata haki zao, leo hii ziko kwenye hali gani? *With due respect* hali inazidi kuwa mbaya, mbaya, mbaya! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vitabu; Sera ya vitabu ya mwaka 91; Sekta ya Binafsi waandikie vitabu, Taasisi wakague vitabu, *EMAC* imevunjwa hapa Bungeni tarehe 5 Juni, 2013, siku ya Jumatano, Bunge hili tumevunja *EMAC,* nani anahariri vitabu leo hii? Afadhali magazeti yanahaririwa vizuri kuliko vitabu vya shule za msingi na nitatoa mfano hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo tulilonalo hapa ni itikadi zetu za siasa na Mwenyezi Mungu atatulaani kwa hilo. Tulikuja hapa mwaka 2013 na hoja ya elimu, ninayo hapa! Yote tunayozungumza kwenye Bunge hili nimeisoma hii jana mpaka saa nane na nusu za usiku, yamo humu ndani, lakini itikadi zikaingia hapa, mpaka na Kiti kikaingia kwenye mambo ya itikadi, tukashindwa Wabunge kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu leo jioni Wabunge wachukue nafasi yao ya kuisimamia Serikali wakati wa Kamati ya Matumizi kama Serikali hii haitashika adabu! Naomba sana *with due respect,* ninayo kwa mfano Mheshimiwa Ndalichako, Sera ya Elimu hii hapa! Iliyozinduliwa mwaka jana na Rais mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete, imetumia zaidi ya bilioni 50, ukisoma ukurasa wa 22 inaelezea mtaala unafundishwa elimu ya msingi, yaani mtaala unafundishwa! Ukisoma ukurasa wa 27 unasema mtaala ni mwongozo mpana, hata hawajui maana ya mtaala ni nini, Sera ya Elimu hapa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakala hizi zililetwa mezani hapa mwaka 2013. Nikahukumiwa kwamba nimesema uongo, wanaonesha kwamba ni Taasisi ya Elimu Mitaala ya 2005, lakini hapa hapa Mungu si Abdallah sio Athumani, leo hii mmeweka kwenye *website* yenu toleo la 2007, leo hii mmeweka kwenye *website* yenu! Yaani kwamba Serikali ilidanganya Bunge hili kuleta mitaala ya uongo ya kugushi ndani ya Bunge hili! Tunamdanganya nani? Huwa tunamdanganya nani? Tanzania ni yetu sote, leo hii ndiyo mitaala iliyo kwenye *Website* yenu. Hii mitaala mliyoenda, anakiri Bhalalusesa - Kamishna wa Elimu na ulikuwa kwenye ile Kamati kwenye Bodi ya Spika, Bhalalusesa umenisikitisha sana Kamishna wa Elimu – umesema uongo kwenye mitaala hii hapa na *evidence* zote ninazo. *(Makofi)*

Mitaala ya elimu ya msingi Bhalalusesa unasema mmefanya *editing,* lakini hebu nikuambie, malengo ya elimu Tanzania, lengo la tatu, sentensi moja ina 'na' 'na' 'na' mara saba, mtaala wa elimu wa shule ya msingi hapa. Malengo ya 2020 - 2025 ukisoma hata *copy and paste* mtaala wa shule ya msingi na awali ni tofauti, ku-*copy* tu lengo la elimu! Malengo ya elimu Tanzania leo hii, mtaala wa awali ni tofauti na ya sekondari, ni tofauti na ya diploma ni tofauti na Walimu, tunamdanganya nani? Ku-*copy* mitaala ya elimu nchini, mtaala mmoja ni tofauti na mwingine. Mtaala wa awali yako 10, mtaala huu mwingine yako mengi tu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetoka Vunjo, kwa sababu ya muda tunazungumzia vitabu, vitabu ninavyo hivi hapa! Ukisoma kitabu cha juzi hiki hapa nimechukua Vunjo, kina mhuri wa *EMAC* japo tulishaivunja *EMAC*! Angalia ukurasa wa kule mwisho jedwali, juzi nimekikuta shule ya msingi Kochakilo, 2X7=15! Hii hapa! Nimeichukua!

Mheshimiwa Naibu Spika, chukua kitabu cha hisababti darasa la kwanza, pale mwanzoni kabisa wanasema namba nzima ni moja hadi 99, hiki hapa! Hii ndiyo sumu tunayowalisha Watanzania leo hii. Ukiangalia cha Kiingereza, *chapter four* ndiyo inaanza na a,e,i,o,u wakati huku mwanzoni wanaanza na sentensi, vitu vya ajabu tu! Ukisoma cha Kiswahili cha ajabu, usiku nilikuwa nasoma kitabu cha sayansi, kitabu cha sayansi, hapa tunatukana watoto huku, ukurasa wa 67 tunafundisha watoto wa miaka minane namna ya kujamiiana, mambo ya ngono, ndiyo maadili tunayowafundisha watoto wetu leo hii na imewekewa mihuri ya *EMAC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hoja ya elimu nilisema nini? Tulisema, ukiangalia mambo yote, angalia hisabati, angali akila kitu, ukiangalia vitabu vyote hivi hapa, nimechukua vichache tu lakini jana usiku nikasema ; Ewe Mungu tunapeleka wapi Taifa hili. Tulisema udhaifu uliopo katika sekta ya elimu unahusiana na mfumo wa utoaji wa elimu, ndicho kirusi kilichoambukiza udhaifu kwenye sekta nyingine zote katika Taifa letu. Sababu ya msingi ya kusema

mambo yote, maendeleo ya Taifa lolote, kijamii, kiteknolojia, kiuchumi na kisiasa ni tunda la mfumo wake wa elimu. Uhai wa taifa lolote lile hutegemea wingi wa matumizi ya wananchi wake walioelimika na mwisho tulisema hapa hapa kwamba; elimu ndiyo mapigo ya moyo ya Taifa letu, mapigo ya moyo yakienda kinyume na asili yake, uhai huweza kupotea, tunao wajibu wa kutunza uhai huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa namwomba sana Rais Mheshimiwa Magufuli afumue Wizara yote ya Elimu. Kama kuna ufisadi wa kupita ni Wizara ya Elimu na watendaji wa Wizara ya Elimu, hasa Taasisi ya Elimu yaani ndiyo hovyo kupindukia ndani ya Taifa la Tanzania. *We are eroding our education*, tunaua Taifa letu, tunambabaisha nani? Tunamdanganya nani? Labda tuondoe *Hansard,* tufungiane humu ndani, wenyewe tu tuondoe na *media*, tuelezane ukweli wa Taifa hili, la sivyo tunaangamiza Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nahitimisha. Mtume Muhammad anatuasa anasema: "Ukiona uovu unatendeka, zuia, ukishindwa kuzuia, kemea, ukishindwa kukemea onesha basi hata chuki" na Zaburi moja inasema…

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Mbatia! Nilikuwa nasubiri umalizie sentensi

MHE. JAMES F. MBATIA: … inasema: "Kheri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki…… *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli. Atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nami nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, John Pombe Magufuli kwa kuanza kutekeleza Sera ya Elimu ya mwaka 2014, hasa kwa kuondoa au kwa kufanya elimu ya msingi na sekondari iwe elimu bure. Hii imewasaidia Watanzania wengi ambao walikuwa wanashindwa kupeleka watoto wao shule za msingi na sekondari kuweza kupata elimu. Kwa hiyo, imeongeza *access to primary and secondary school education*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto ambazo Wabunge wameendelea kuzisema, lakini kwanza tumefungua *access,* tumewawezesha Watanzania wote waweze kupata fursa ya kupata elimu ya shule ya msingi na sekondari. Hizi changamoto nyingine tutaendelea kuzitatua kadri muda utakavyokuwa unaendelea. Kwa hiyo, lazima uanze kwanza kuweka fursa, lakini baadaye katika fursa unakuwa na changamoto nyingine nyingi ambazo tumesema kuna changamoto za miundombinu, changamoto za *resources* mbalimbali ambazo tutaendelea kuzifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Waziri wa Elimu kwa kuteuliwa kuongoza Wizara hii, namwamini, yupo makini na atatufikisha pale ambapo tunatakiwa tufike, lakini pia nimpongeze Naibu wake wa Elimu, Mheshimiwa Stella Manyanya na nimpe pole kwa msiba aliopata wa mama yake. Mungu aendelee kumrehemu na aendelee kumpa nguvu katika kipindi hiki ili arudi kutekeleza majukumu muhimu sana ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika nianze kusema jambo moja linalowakera sana Walimu hasa madai ya Walimu. Pamoja na mambo mengine yote jambo la madai ya Walimu, ndiyo pengine yanachangia kuathiri kiasi kikubwa kufisha elimu au inachangia kwa kiasi kikubwa katika utoaji wa elimu. Walimu wanapokuwa wanadai nyongeza ya mishahara, wanapodai kupandishwa madaraja, hii inawakatisha tamaa. Kwa hiyo, muda mwingi wanakuwa wanawaza kuongezewa mishahara, muda mwingi wanawaza madai yao mbalimbali na changamoto mbalimbali, kwa hiyo, wanaenda kazini wakiwa wamevunjika moyo wa kufanya kazi, hivyo hawafanyi kazi vizuri. Pamoja na kwamba tumeajiri Walimu wengi lakini ukifika kwenye mashule tuna Walimu wengi sana, lakini wanaoingia darasani ni wachache, lakini katika wachache wanaofundisha ni wachache sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wengi wanaingia wakiwa wamekata tamaa, wanaingia wakiwa wanawaza maisha, wanawaza mishahara yao, anawaza atarudije nyumbani, anawaza ataishi namna gani kule nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe Wizara zinazohusika hasa, Wizara ya TAMISEMI, ihakikishe kwamba madaraja ya Walimu yanapanda kwa wakati na zile stahiki zao kwa maana ya madai yao ya likizo, madai yao ya mishahara mbalimbali na madai mengine yanatekelezwa kwa wakati ili Walimu wawe na moyo wa kufundusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunajua huwezi kuwa unafanya kazi vizuri zaidi, kama unakuwa na madai mbalimbali, kama unakuwa unalaumu vitu mbalimbali ambavyo hujatekelezewa. Kwa hiyo, niombe Wizara ya TAMISEMI wakishirikiana na Elimu pia, tuweze kuhakikisha kwamba, madai ya Walimu yanalipwa kwa wakati na pia madaraja ya Walimu yanapandishwa kwa wakati. Kuna huu upandishwaji wa madaraja baada ya miaka kadhaa, Walimu wengi wanaokwenda kusoma mara nyingi wamekuwa wakichelewesheswa sana kupanda madaraja yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wamekuwa wakirudi nyuma, akiondoka kwenda kusoma, akirudi anakuta Mwalimu aliyemwacha ambaye ana elimu ndogo kuliko yeye amepandishwa daraja na yeye anabakia nyuma. Kwa hiyo, hili nalo linakatisha sana tamaa Walimu. Kwa hiyo, niombe madaraja ya Walimu yaende sambamba na muda aliyofanya kazi lakini sambamba pia

na elimu yake aliyoipata ili angalau tuweze kuwamotisha hao Walimu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niseme jambo moja lingine ambalo wamesema Waheshimiwa Wabunge wengi sana juu ya mikopo ya elimu ya juu. Hili nalo limekuwa ni tatizo kubwa wale walengwa ambao wanatakiwa kupewa mikopo wamekuwa hawapati, hasa watoto wa maskini wanaoishi huko Vijijini, wanapewa wakati mwingine asilimia ndogo, asilimia 40 au wakati mwingine asilimia 30 na mwisho wa siku wanashindwa kulipa ada wanabaki wakihangaika tu na wengine imefika mpaka wakati mabinti zetu wanaanza kutafuta njia nyingine za kuweza kupata fedha za kujikimu wanapokuwa chuoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tuombe uwekwe utaratibu mzuri kama tulivyosema kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, wanafunzi wote watakaokuwa wamedahiliwa kwenda chuo kikuu kwa kuwa wana sifa ya kusoma chuo kikuu wapewe mikopo asilimia 100 na kwa sababu ni mkopo wapewe wote kuliko kuweka haya madaraja kwa maana wengine wanapewa asilimia 80, wengine 70, wengine 60 na 40; hiyo inaleta matatizo na inaleta migomo na maandamano yasiyo na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuombe Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Elimu alisimamie hili, wanafunzi wote wanaokuwa wamedahiliwa kwenda chuo kikuu, basi wapewe mikopo asilimia 100 ili tupunguze baadhi ya matatizo ambayo wamekuwa wakipata hawa wanafunzi wa vyuo vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema na Wabunge wengi wamesema juu ya changamoto za Walimu wa sayansi kwamba Walimu wa sayansi hawapo au wapo wachache, kwa mfano kwenye Jimbo langu la Lupembe Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, tuna upungufu wa Walimu wa sayansi 93 na wakati huo huo tuna upungufu wa Walimu 158 wa shule za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunasema kwamba, tunataka twende kwenye uchumi wa kati, uchumi wa viwanda, hatuwezi kwenda kwenye uchumi huo kama hatutakuwa na Walimu wa sayansi wa kutosha. Kwa hiyo, naomba kwanza kabisa tuanze kuwahamasisha wanafunzi wetu toka shule za misingi waweze kupenda masomo ya sayansi. Walimu wa shule ya msingi wawa-*encourage* watoto waweze kupenda hisabati, waweze kupenda masomo ya sayansi na hatimaye wakifika sekondari waanze kupenda kusoma masomo ya sayansi, ni uamuzi tu, tuwaweze hawa Walimu wanaofundisha, tuwawezeshe Wakuu wa Shule pia ili waweze kusimamia vizuri kuhakikisha kwamba katika shule zao wanafunzi wanafaulu masomo ya sayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ku-*declare interest* nami ni Mwalimu, nimekuwa Mkuu wa Shule, shuleni kwangu wanafunzi hakuna *option,*

wanasoma masomo yote yale ya msingi, yote yale tisa na wanafaulu zaidi sayansi hata kuliko *art*. Kwa hiyo, tukiamua tukaweka miundombinu vizuri, tukaweka mazingira mazuri, wanafunzi wanaweza wakafaulu vizuri masomo ya sayansi na hatimaye tukapata wanafunzi wanaokwenda vyuo vikuu kusomea masomo ya sayansi, kwa hiyo, tutaweza kutokomeza jambo hilo, tutaweza kusaidia kupunguza uhaba wa Walimu wa kuanzisha utaratibu wa kuweza kuwahamasisha watoto wa shule za sekondari waweze kupenda masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja kama nilivyosema, la nyumba za Walimu, katika shule zetu nyingi hasa za Kata tuna uhaba mkubwa sana wa nyumba za Walimu, hata katika Jimbo langu tuna uhaba mkubwa sana wa nyumba za Walimu. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI watakavyopanga katika ujenzi wa zile nyumba zile 30 ambazo zinachukua Walimu wengi na mimi wanifikirie kule kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shule mbili hazina hata nyumba za Walimu kabisa, shule ya Ndinga na shule ya Mrunga kule, kwa hiyo, mnisaidie ili niweze kupata hizi nyumba angalau na Walimu wangu waweze kukaa katika maeneo ya shule na hivyo kufundisha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna jambo linguine, wamesema la Mdhibiti wa Ubora, zamani tulikuwa tunaita Kitengo cha Ukaguzi, lakini niseme kwamba Mkaguzi wa kwanza ni mkuu wa shule, tumwezeshe mkuu wa shule aweze kusimamia shule yake vizuri na hatimaye tuwezeshe Kitengo cha Udhibiti Ubora cha Halmashauri au cha Wilaya ili waweze kuhakikisha kwamba wanafanya kazi zao vizuri na Wakaguzi wa Kanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi wakaguzi hawana fedha kabisa, hawana fedha za mafuta, wanashindwa kwenda kwenye mashule kwenda kukagua. Sasa huwezi kuamini kwamba kama Mkaguzi hawezi kufika kwenye shule kwenda kufannya ukaguzi, je, huko shuleni kutakuwa na kitu gani? Atajuaje ubora kama upo kwenye shule hizo husika. Kwa hiyo, tuombe Wizara husika nazo ziwawezeshe hawa Wadhibiti Ubora kwa maana ya Wakaguzi wetu wa Halmashauri, Wakaguzi wetu wa Knda, lakini pia tumwezeshe Mkuu wa Shule aweze kusimamia vizuri taaluma kwenye shule yake kwa kuwa yeye ni mkaguzi wa kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, iliwekwa ile pesa ya majukumu, sh. 200,000/= kwa Walimu wakuu; Sh. 250,000/= kwa Wakuu wa Shule na sh. 300, 000 kwa Wakuu wa Vyuo. Tukiwapa hizi fedha wataweza kusimamia taaluma vizuri, wataweza kukagua vizuri na kuhakikisha kwamba Walimu wao wanafundisha

vizuri. Ilivyo sasa hivi unaweza ukafika Mkaguzi wa Halmashauri au wa Kanda akafikiri Mwalimu anafundisha vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanachofanya darasani kule wanatoa *notes*, wanatoa kazi, wanasahihishana mle darasani, halafu mwisho wa siku akija Mkaguzi, anaangalia madaftari anakuta kuna mazoezi ya kutosha, anaangalia *lesson plan* na *schemes of work* zimekaa vizuri, lakini kumbe kinachoendelea darasani sicho hicho kilichopo kwenye hivi vitabu mbalimbali. Kwa hiyo, tuwawezeshe kwanza Wakuu wa Shule ambao wako jirani na baadaye Idara nzima ya Ukaguzi ili tuweze kuboresha elimu.

NAIBU SPIKA: Asante sana muda wako umekwisha.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Riziki Shahali Mngwali atafuatiwa na Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mheshimiwa Subira Mgalu ajiandae.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na ardhi, aliyetujalia sote hapa uhai na uzima na kutuwezesha kufanya hili tunalolifanya. Baada ya hapo nitoe shukrani za kipekee kwa wazazi wangu wawili Mwenyezi Mungu awarehemu huko waliko na awahurumie kama wao walivyonihurumia mimi nilipokuwa mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee kabisa naomba niyatambue, niyashukuru na niyaenzi malezi ya Walimu wangu wa darasa la kwanza mpaka la saba kama ifuatavyo:-

Mama Clara wa darasa la kwanza na la pili; Mrs Mganga wa darasa la tatu; Mrs. Makundi wa darasa la nne; Mrs Matata wa darasa la tano; Miss Komba wa darasa la sita; na Mr. Mabula wa darasa la saba waliongozwa na ma-*head* waaminifu, mama Kehemere, Mzee Mwamugunda na Mzee Lukoo. Naomba kwa namna ya kipekee niwaenzi Walimu wangu Wakuu wa Kisutu sekondari 1974-1977 marehemu mama Chale, mpenzi wangu mama Tegisa, Mama yangu Mrs. Munuo na Miss Kassim. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaenzi pia Walimu wangu Wakuu wa Korogwe Sekondari mama Msemakweli na Mwalimu Chisongela, kwa malezi yenu nimefika hapa, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuzungumzia mada hii kwa kuangalia Taasisi zilizomo na nianze na *NECTA*. Katika mambo yanayotia

uchungu kwenye Taasisi hii ni *credibility* yake. Hii ni Taasisi ambayo *it makes or destroys* Mtanzania. *NECTA* inatoa maamuzi mwanafunzi anapotoa mitihani yake lakini je, kweli Taasisi hii ina uadilifu wa kutosha kuweza kufanya kazi hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa ruhusa yako niwasome watoto hawa halafu nitakwambia kwa nini. Kuna hafidhi Hassan Arkam Salum, Nassoro Shaban, Ali Alhabi, Abdulhamid Ahmed, Zamha Abdallah Rashid, Damtu Mohamed Tahir, Fatma Vuai Muhidini, Mwanaharusi Ally, Sabrina Suleiman Ally, Ruwaida Ally Ahmed. Hawa watoto walidhalilishwa mbele ya umma wa Tanzania katika watoto waliofutiwa matokeo yao, hawakufanya vizuri, wamekopia mitihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyezi Mungu alichowajalia watoto hawa ni kwamba wazazi wao wana uwezo. Walichofanya wazazi wa watoto hawa, waliwapeleka Arusha *Modern* na pale wakaamua wafanyiwe mitihani ya *Cambridge*, mtoto Hafidhi Hassan Ali, alitoka na *distinction* lakini kama vile haitoshi, ule mtihani wake wa Kiswahili ulipewa *A** na *A** kwa Cambridge ni kwamba iko *beyond* 89. Hasa ni *Global wise* na hiyo *A** yake ya Kiswahili ni *globaly, worldwide* huyu mtoto alitoka Arusha *modern,* lakini kwa mfumo wetu kwa *assessment* ya *NECTA* huyu mtoto kama mzazi wake asingekuwa na uwezo tungeshamsahau sasa hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na hawa wote waliomfuatia katika orodha hii walipata *merit*. Kwa hiyo, ni watoto na naombeni m-*google* muangalie *how Cambridge* wanaweka hizo *classification* zake, *distinction, merit* na *pass* halafu muone sisi tunaingia wapi pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hilo halitoshi kwa *NECTA,* lingine ni kwamba hawa *NECTA* wakishakufelisha ukitaka kukata rufaa ukate kwao, mlisikia wapi? Mahakama ya Mwanzo, hiyo hiyo Mahakama ya Hakimu Mkazi na Mahakama ya Rufaa ni hiyo hiyo, tunafanyaje haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nina kesi mbili ambazo walifelishwa niseme na wakakata rufaa. Uzuri hawa walipata msaada wa Walimu wao wenyewe, kama huyu kijana mmoja yeye alipofanya mitihani ya A-*level* pale Benjamin Mkapa, wazazi wake wakasema haiwezekani Abdulkarim afeli, kupata *division* III ni Walimu wake waliomsimamia na ziliposahihishwa akapata *division one,* sasa hivi ni Mhasibu, yuko Arusha *Municipality,* hiyo ndio *NECTA* yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa *NECTA* katika kasoro nyingine wasifanye kazi kwa uzoefu. Nimepata bahati mbaya ya kupoteza vyeti vyangu, vya O-*Level* na A-*Level,* lakini baadaye nikapa hamu ya kwenda kujiendeleza nifanye *PhD* nilipokwenda shuleni Vietnam, Taasisi zetu za elimu ya juu na *NECTA*, chuo

kikuu wananidai mimi vyeti vyangu vya *form* IV na *Form* VI nikawaambia ninyi mnisamehe kwa sababu *degree* yangu ya kwanza niliipata hapa chuoni kwenu na mlini-*admit* kwa *credential* zangu za O-*level* na A-*level,* lakini wakaniambia tunakuweka lakini hutopata cheti, huto-*graduate* mpaka utuletee.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokwenda *NECTA* wananiambia niende shule yangu ya O-*level,* niende na shule yangu ya A-*level* wakathibitishe kama mimi nilikuwa mwanafunzi wao pale. Mimi nimeondoka Kisutu 1977, nimeondoka Korogwe *Girls* 1980. Mwalimu gani ambaye ataweza kuthibitisha zaidi kuwepo kwangu mimi kuliko *NECTA* ambao wao waliitambua shule, wakanitambua mimi, wakanipa *examination number*. Haya mambo gani ya kufanya kazi kwa uzoefu? *NECTA* wabadilike katika utendaji kazi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo linaingia kwenye Wizara hii pia ni suala la Mheshimiwa Kuchauka alichangia siku moja akasema, uwekwe msisitizo katika kufundisha jiografia na historia, lakini nimekuwa nikisema mara kadhaa hapa kwamba, watendaji wetu wanatakiwa wapate dozi ya *know your country*. Hii nairudia tena leo hapa kwa mfano mdogo kwamba, watu hawa watakapoijua nchi yao, watajua makundi maalum yaliko yanayotengeneza ile jamii kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo watakapofikiria kupanga shughuli maalum kama hizi za michezo kwa mfano, UMISHUMTA sijui, UMISETA na hata SHIMIWI, hawawezi wakayapanga mwezi wa Ramadhani kwa sababu wanajua kuna kundi kubwa la jamii ya Watanzania kushiriki kwao michezo ile itakuwa muhali, basi hata hili nalo jamani tuambiwe, wakati kalenda tunaZIpata mwezi Januari au hata kabla tukaona mle na huwa wanaweka *star* kabisa kwamba tarehe hizi inaweza ikawa *Idd el fitri,* kwa hiyo maana yake mwezi *before* ndiYo Ramadhani, sasa mambo kama hayo yazingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichangie katika, mimi nimeliita *the big scandle in town*, hili tuliloambiwa hapa, la *TCU na Saint* Joseph. Hili limetokea kwa haya ambayo Wabunge wengi wamesema na kaka yangu Mheshimiwa Mbatia amemalizia kusema na amekuwa akilisema miaka mingi ya kuchezea elimu yetu na mfumo wetu wa mafunzo katika nchi hii, mahodari wa kuunda Taasisi, kuzipa majina, halafu tukakoroga yale majukumu yake, mwisho wa yote hatupati chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri na kwa namna alivyom-*introduce best half* wake jana mimi nakuwa wifi, kwa hiyo, nisikilize kwa umakini zaidi, siyo tu Mbunge lakini wifi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ajijulishe kuhusu kitu kilitwa *NAMDEC* ilikuwepo huko, *National Managament Development something* ikaundwa *HEAC,* lakini

baadaye nikadhani baada ya kuunda *TCU* na *NECTA* na *VETA,* nikajua sasa ule mkorogo tuliokuwa nao kwenye *NAMDEC* na ile *HEAC* kwa maana ya *Higher Education Accreditation Council* yatakwisha, kwa nini? Kwa sababu zile Taasisi za mwanzo zilikuwa zinachanganya chuo kikuu kimo, kisichokuwa chuo kikuu kimo, lakini ukishasema *TCU (Tanzania Commission For Unviversity)* ukasema *NACTE* sijui *National Technical Edecucation something; VETA Vocational Education* yashajulikana, lakini tunafanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi zilizokuwa chini ya *NACTE* na zenyewe zinakwenda zinataka kutoa *degree* zijiite chuo kikuu; Taasisi zile za chuo kikuu zenyewe nazo zinashuka mpaka chini zinataka kutoa vyeti, sasa ni nini? *NACTE* kwa mfumo wao wanasema wao ni *competency based* kwa maana nyingine wanatutengenezea hawa watu wa *hands on,* wale wataoshughulika *practically* na wao ndio maana kwao… *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Riziki muda wako umekwisha.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Aaah dakika kumi

NAIBU SPIKA: Kengele zimeshagongwa mbili tayari

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Naibu Spika, basi nakushukuru. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jasson Rweikiza atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Mgalu, Mheshimiwa Dkt. haji Mponda ajiandae atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nipende kusema kwamba Serikali ya CCM inafanya vizuri kwenye eneo la elimu au Sekta ya Elimu kuna mafanikio makubwa sana tumeyapata kila mtu anayajua, lakini kwa vile kuna watu ambao wanajifanya hawayajui ni bora nirudie kidogo kwa ufupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kila Kata ina shule ya sekondari, nyingine mbili, nyingine tatu Kata moja. Kila Kijiji kina shule ya msingi, haya ni mafanikio makubwa; vyuo vya elimu ya juu mwaka 2005 kila mwaka tulidahili wanafunzi 36,000m leo tunadahili wanafunzi 150,000 vyuo vya elimu ya juum haya ni mafanikio makubwa. Leo tumesema elimu bure kuanzia darasa la kwanza hadi la kumi na mbilim haya ni mafanikio makubwa. Niipongeze Serikali, Wizara ya Elimu na CCM kwa ujumla, kazi nzuri, tumeweka misingi mizuri katika kuboresha elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado kuna kazi ya kufanya, tuboreshe, tumeweka misingi mizuri sasa tuiboreshe. Shule binafsi zinafanya vizuri sana wamesema wenzangu jana hapa na mimi ni mmoja wa wamiliki wa shule binafsi, nitangaze maslahi, lakini shule binafsi zinafanya kazi nzuri sana. Niishauri Wizara isaidie shule hizi za binafsi, isizione kama zinafanya dhambi au kosa, zione kama ni mshirika katika kutoa elimu nzuri kusaidia kuelimisha Watanzania. Kwa hiyo, haya mambo ya ada elekezi wamesema Wabunge wengi, nisirudie, hayana maana, tuwaachie wenye shule wafanye shughuli zile, watoe elimu bora, ndio wanaoujua mzigo wanaobeba, mambo ya kupaka mabasi rangi ya njano tuachane nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake tusiwape masharti magumu na yakiwa magumu watashindwa, tutashindwa na mimi nikiwemo, tuwawezeshe ili tuweze kufanya kazi nzuri tuboreshe elimu. Kuhusu kodi wamesema Wabunge hapa kuna mzigo wa kodi haubebeki, watashindwa, tutashindwa kutoa elimu nzuri ambayo kwa kweli ndiyo msingi mzuri wa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ni kila kitu amesema Mbunge Mheshimiwa Mbatia, elimu ndio roho ya Taifa, ni kweli na mimi naungana naye elimu ndiyo roho ya Taifa, tushirikiane katika kuboresha elimu. Shule binafsi mwaka jana kidato cha nne katika wanafunzi 100 bora, wa kwanza wa pili mpaka wa 100, wanafunzi 97 wametoka shule binafsi. Serikali ni watoto watatu, hawa utawabeza kweli? Sasa hapa ni kuwapunguzia mzigo wa kodi na mzigo wa masharti, maana watashindwa na tutadidimiza elimu, tutadidimiza maendeleo ya Taifa hili. Nasema tuboreshe elimu, tupambane, tusonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Bukoba Vijijini tuna Sekondari kama nilivyosema za Kata, za wananchi na nyingine 31, lakini hatuna Sekondari ya juu, *A Level,* hata moja. Imeainishwa moja ya *Mahoro Secondary School* miaka mingi, lakini hakuna kilichofanyika. Niiombe Wizara, hii shule nayo iboreshwe ipate madarasa ya *Form Five* na *Form Six* ili hawa vijana kutoka shule 31 hizi waende kupata elimu pale, elimu ya *A Level,* tuzidi kupiga hatua twende mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Nne ilikazania sana ujenzi wa maabara, jambo zuri sana. Tukajenga maabara kila shule ina majengo ya maabara, lakini hayajakamilika! Sasa naona mkazo umepungua pale, yale majengo mengine yamefika nusu, mengine kwenye linta pale, mengine yameezekwa, mengine hayajakamilika! Tusiyaache haya, yatabomoka, tumechanga pesa kwa tabu sana; kila mwananchi amechangia, hata mimi nimechangia hela nyingi sana kwenye majengo haya ya maabara, tusiyaache yakaporomoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itafute namna ya kusaidia kwa kusaidiana na wananchi hawa waliozijenga hizi maabara zikamilike, ziwe nyumba kamili, ziwekwe vifaa vya sayansi, zitumike kama ilivyokusudiwa; ndiyo maendeleo yenyewe ya elimu kila shule iwe na maabara iliyokamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuko kwenye kazi kubwa ya kuhakikisha kila shule inakuwa na madawati, shule za msingi na sekondari zina upungufu mkubwa sana wa madawati. Kazi inafanyika nishukuru, nimeona hapa katika taarifa Wizara ya Maliasili na Utalii imesema itatoa mchango wa madawati 168,500 nawapongeza, lakini hayatoshi, waongeze kwa sababu, pale nasikia kuna shilingi bilioni sita kwenye Wizara hiyo ya Maliasili na Utalii kwa ajili ya kusaidia jamii. Hizo shilingi bilioni sita ziende kwenye madawati, ndiyo jamii yenyewe na Wizara nyingine zifanye ziige mfano wa Wizara ya Maliasili na Utalii na taasisi nyingine ziige mfano huu, kama Bunge hili limetoa shilingi bilioni sita kwenye madawati na wengine waige mfano huo, ili baada ya muda mfupi madawati yatoshe, vijana hawa wasome katika mazingira mazuri, wasikae chini kwenye vumbi, wakae kwenye madawati ili waweze kusoma vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari, kwangu mimi wana madai mengi sana, mafao yao hawalipwi. Mwalimu anahamishwa kituo anaambiwa nenda utalipwa baadaye! Anakaa miaka miwili au mitatu hajalipwa! Hili muliangalie wapate mafao yao. Mwalimu anapandishwa daraja haongezwi mshahara!

Mheshimiwa Naibu Spika, nina Mwalimu mmoja pale amekaa miaka 16 hajapanda daraja, tangu ameajiriwa hadi leo miaka 16, hajapanda daraja! Hajapewa *warning* kwamba, haendi kazini, anafanya kazi vizuri, miaka 16 hajapanda daraja! Mnamkatisha tamaa, hawezi kufundisha vizuri! Walimu waangaliwe, wapewe motisha inayotakiwa ili waweze kufanya kazi vizuri. Hawa ndiyo wanaotoa elimu, ndiyo wafundishaji, ndiyo wasimamiaji wa sekta nzima ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nizungumzie suala la juzi la wanafunzi wa *Saint Joseph,* wale karibu 500. Nasema hawa wasaidiwe wasifukuzwe, 55 ni wengi. Halafu wamekuwa *admitted* pale wamedahiliwa kwa vigezo vilivyokuwepo! *TCU* hata kama walikosea, lakini makosa yao siyo makubwa kiasi hicho. Kwa sababu, kama tunasema mtu ana *D* nne, wamesoma *Certificate* wakapanda *Diploma,* sasa wanafanya *Degree;* ndivyo hata *CBE* inavyofanya. *CBE* mtu anaingia ametoka *Form Four* ana *D* tatu, anasoma *Certificate* anamaliza, anaingia *Diploma* anamaliza, si anaingia *Degree,* kwa nini hawa watendewe tofauti? Wasaidiwe wapate msaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbona tulichukua *UPE* miaka ya 70, walikuwa darasa la saba, wakapata mafunzo ya miezi mitatu wakawa Walimu wa *UPE*,

mpaka leo ni Walimu wanafundisha shuleni. Baadaye tukachukua hawa vijana wa *Form Six,* wanaitwa *Voda Faster* sijui, wakapewa miezi mitatu kozi ya Ualimu, hadi leo ni Walimu wanafundisha! Sembuse hawa ambao wamefaulu vizuri *D* nne! Wameingia kwenye *Certificate* wamemaliza, wamesoma *Dilpoma,* leo wanasoma *Degree* mnawafukuza! Msiwafukuze, tumelipa hela nyingi Watanzania kwenye kodi zetu, wamesoma miaka mitatu, miaka minne na wengine miaka miwili. Wasaidiwe warudi chuoni wamalize ili wasaidie kupunguza pengo la upungufu wa Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Subira Mgalu atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda, Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu ajiandae, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbarouk Mussa Bakar.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa fursa asubuhi ya leo kuweza kuchangia bajeti ya Wizara yetu hii ya Elimu, Sayansi na Mafunzo ya Ufundi. Nianze moja kwa moja, kwanza kuwapongeza Walimu wote nchini Tanzania kwa kazi kubwa wanayofanya. Kipekee niwashukuru Walimu hao kuanzia Shule ya Msingi, Sekondari *Mtwara Girls* na *Ndanda High School,* Chuoni *IFM*, *Mzumbe University* na Walimu wa Bodi ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu kwa namna ambavyo wamenisaidia, nimepata fursa ya kusimama ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba leo, kabla hata sijachangia niliwasiliana na wanafunzi niliosoma nao ambao pia ni Walimu ambapo, changamoto nitakazozichangia hapa na ni maombi yao, ni maombi yaliyotokana na Walimu wenyewe baada ya kuwasiliana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, anafanya kazi vizuri; hatua alizochukua dhidi ya Bodi ya Mikopo, hatua alizozichukua dhidi ya *TCU,* binafsi naziunga mkono. Pia, nampa pole sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kufiwa na mama yake mzazi, Mwenyezi Mungu ampe subira na wepesi katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nina matumaini sana ya Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa kuwa, naamini inaongozwa na Rais wetu aliyepata kuwa Mwalimu, Waziri Mkuu aliyepata kuwa Mwalimu, *First Lady* aliyepata kuwa Mwalimu, Walimu wana matumaini makubwa sana katika Awamu hii kwamba, jitihada zilizoanzishwa katika Awamu mbalimbali changamoto zao nyingi zitapata fursa ya kutatuliwa katika Awamu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nipongeze kwa utekelezaji wa suala zima la Waraka Namba Tano (5) wa Elimu Bure ambao umeanza mwaka jana Disemba,

2015 mpaka sasa. Nipongeze dhamira ya Serikali ya kutenga kiasi cha bilioni 18 kila mwezi kukabiliana na majukumu mazima ya kutoa elimu kwa Shule za Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mkoa wa Pwani suala hili limetusaidia, ongezeko la uandikishaji kwa ngazi ya mkoa limefikia 150%. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile 50% ya watoto walioongezeka katika Elimu ya Awali na Msingi ni wazi kuwa kuna wazazi ambao ilikuwa inashindikana kabisa kupeleka watoto wao kutokana na changamoto mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwanzo wa hesabu moja. Natambua Roma haikujengwa kwa siku moja. Katika utaratibu mzima wa utoaji wa elimu bure, naiomba Wizara iangalie, isije ikawa utekelezaji wa elimu bure imewapa Walimu Wakuu mzigo mkubwa na Walimu wenyewe bado wanalalamika mishahara bado ni midogo na marupurupu yao mengine; kwa nini nasema hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji huu wa elimu bure, kuna kipengele cha utawala. Utakuta shule inawezekana ina wanafunzi wachache, lakini gharama za utawala ni moja; kama ni bei ya shajara ni moja, masuala ya mitihani ni mamoja, lakini utakuta ile 10% hasa kwa shule ambazo zina mazingira magumu, mfano shule za Kata ya Kibindu Wilaya ya Bagamoyo, Shule za *Delta,* Kiongoroni, Mbuchi, Msala, Maparoni Wilaya ya Rufiji! Shule za Wilaya ya Kisarawe zilizopo Vikumburu, Dololo, Kimaramisale, Mafia, Visiwa vya Jibondo, Chole, Mkuranga, Visiwa vya Kwale, Koma, mazingira yao ni magumu kiasi kwa mfano Visiwa vya Rufiji, kuja Makao Makuu ya Wilaya Utete, Mwalimu anatumia 50,000/= nauli. Zilikuwepo boti kwa ajili ya kuwasaidia walimu hawa, lakini zile boti zimeharibika, lakini anaenda kufuatilia *cheque* kwa ajili ya masuala ya utawala. Kwa mfano kuna shule iko Msala na inapokea 40,000/= asilimia 10 ni 4,000/=, lakini afuatilie hiyo hela mpaka Utete ni 40,000!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iangalie mazingira haya magumu na iwatendee haki Walimu, wamelalamika! Walimu sasa wanatumia pesa zao mifukoni kwa ajili ya uendeshaji wa shule. Vile vile suala hili limeathiri masuala ya mitihani; kifungu cha mitihani hakitoshelezi, kwa hiyo, baadhi ya mitihani imepunguzwa! Labda shule zilipanga utaratibu *mock* ya Kikata, *mock* ya Wilaya, mitihani ya kila mwezi, ya kila wiki na mitihani hii ilikuwa inasaidia ufaulu. Kwa hiyo, nadhani Wizara iangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Walimu niliowasiliana nao wameomba hiki Chama cha Walimu Tanzania, wamesema chama hiki kimeshasimama, kina miliki jengo, kinafungua benki! Masuala ya kuwakata asilimia ya mishahara yao kwa ajili ya kuchangia chama ambacho kimeshasimama, kina uwezo, naomba Wizara mfuatilie, Walimu wanalalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini chama hiki hakipo wazi! Sisi tumekaa Wilayani, hatuoni msaada mkubwa kwa Walimu wetu, lakini mara nyingi utakuta kwenye masuala ya michakato ya kisiasa kiko mbele, lakini siyo katika kuwasaidia Walimu! Nadhani michango waliyochangia Walimu ingewezekana Chama cha Walimu kingethubutu, sasa hivi kinamiliki benki, kinamiliki jengo kubwa Dar-es-Salaam, kingethubutu hata kuwapunguzia makali ya maisha walimu ambao ni wanachama wao. Kwa hiyo, hilo nalo walimu waliniomba, lakini wamesema sasa hivi chama kimesimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Walimu wameiomba jitihada za kuimarisha miundombinu. Bajeti ya miaka iliyopita, hususan mwaka jana, kulikuwa na kifungu waziwazi cha ujenzi wa nyumba zao kama 500 kila mwaka. Nimejaribu sana kuangalia kwenye bajeti ya mwaka huu sioni vizuri, hakionekani waziwazi, lakini bado kuna changamoto kubwa ya miundombinu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Walimu wameniomba, kuna Walimu waliajiriwa Juni, 2015 mpaka leo bado hawajalipwa pesa zao za kujikimu na pesa zao za nauli, inawakatisha tamaa. Walimu pia, wameniomba Serikali iendelee na jitihada za kulipa madeni yao; wanatambua hata mwaka jana mwezi wa 10 baadhi ya madeni yao yamelipwa, lakini kwa kuwa yanajilimbikiza kwa muda mrefu, Walimu wameomba pia suala hili litekelezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu pia wameniomba niwasilishe, utekelezaji wa Waraka wa Posho za Viongozi, sijaliona waziwazi kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri! Walimu Waratibu wa Elimu Kata walipangiwa sh. 250,000/=, Wakuu wa Shule walipangiwa sh. 200,000/=, hizi zinaweza zikawasaidia, naomba hilo nalo litazamwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Pwani tunalo tatizo, baadhi ya shule zetu zina Walimu mmoja mmoja. Mfano Shule ya Gundumu Kata ya Talawanda, Shule ya Kwa Ikonji, Pera, Kata ya Kibindu ina Mwalimu mmoja, lakini shule hizi zina madarasa kuanzia la kwanza mpaka la saba. Kwa mfano kwenye Shule ya Gundumu kuna Walimu wawili wanajitolea kwa sh. 50,000/= lakini tangu Disemba hawajalipwa! Kwa hiyo, mimi binafsi kama Mbunge wao nimeona niwasaidie, nilichukue jukumu hilo ili niweze kuona jinsi Serikali itakavyotusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia suala la Bodi ya Elimu. Kwanza nakubaliana na hatua zilizochukuliwa dhidi ya *TCU*, lakini pia nasikitika hela zaidi ya milioni 700 zilizotumika kwa vijana wale na mimi binafsi siyo Mwalimu, lakini nikiangalia maelezo ya Mheshimiwa Waziri na vigezo walivyovitumia kuwadahili wale na nikirejea maelezo ya Kamati yetu ya Huduma za Jamii, ukurasa wa 11 kwamba, Kamati imebaini kuwa, vijana wengi wenye alama za kuwawezesha

kuendelea na masomo ya elimu ya juu wameshindwa kuendelea kutokana na hela hizi za mikopo kuwa si nyingi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kama wapo vijana wenye elimu, wenye vigezo, wako mitaani wanakosa fursa ya mikopo, tufike hatua ya kuwadahili wanafunzi wenye *Arts* kusoma masomo ya sayansi kwa ajili ya kuja kutufundishia watoto wetu! Kwenye suala hili kwa kweli, naunga mkono. Nimesema mimi siyo Mwalimu, lakini naamini Profesa Ndalichako amejiridhisha, naamini na Tume aliyoiunda itafanya kazi nzuri, lakini hatua lazima zichukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, nimalizie kwa kuomba huu ujenzi wa miundombinu, hasa kwenye shule ambazo, kwa mfano tuna Shule ya Mlegele Kisarawe, tuna Shule ya Kidugalo, Tondoroni, Sofu na Kola; shule hizi zina vyumba viwili viwili vya madarasa, lakini zina madarasa kuanzia la kwanza mpaka la saba! Kwa hiyo, utakuta changamoto katika miundombinu ya elimu, bado ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, niiombe Serikali, maoni ya Kamati yetu ya Huduma za Jamii ni mazuri sana, hasa uwekezaji kwenye Sekta ya Elimu. Tunapoliandaa Taifa letu kuwa Taifa la kipato cha kati na Taifa la viwanda, tunatarajia kufufua Viwanda vya Nguo, Viwanda vya Kusindika Korosho, tusipoandaa wataalam na tukawekeza zaidi katika Wizara hii, hasa miundombinu yake. Tunaweza tukawa na kila kitu, lakini Taifa litakalokosa wafanyakazi wenye elimu inawezekana hata hii azma nzima tusiitimize. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda, Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu na Mheshimiwa Mbarouk Mussa Bakar wajiandae.

MHE. DKT. HADJI H. MPONDA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa wingi wa afya ambayo inaniwezesha leo kusimama hapa na kutoa mchango katika mada ambayo tunaizungumzia. Vile vile naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi leo ya upendeleo ili nami nitoe mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na pongezi za dhati kabisa, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Profesa Ndalichako na timu yako, mmeanza vizuri. Mmeanza vizuri wala msitikisike, mikakati mnayoweka tuna imani mnaweza mkatutoa hapa tulipo. Pia, niipongeze Kamati mahiri, Kamati ya

Huduma za Jamii; Kamati hii mchango wao na upembuzi waliofanya kwa kweli umesaidia, pengine utaboresha zaidi hii sekta ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wamelalamika, wametoa maoni yao na ushauri; kwa kifupi picha iliyojitokeza hapa, hali ya elimu sio nzuri. Mchango wangu utajikita huko huko na kutoa mfano wa hali halisi. Mheshimiwa Waziri matokeo ya mwaka jana ya vijana wetu wa Kidato cha IV, Wilaya yangu ya Malinyi ni miongoni mwa zile shule 10 ambazo hazikufanya vizuri, Wilaya yangu imetoa shule tatu, zile shule ambazo zimeshika mkia. Matokeo haya yalitusikitisha, yalitushtua, kama wadau wa elimu tulirudi tukakaa chini, kulikoni? Tulijua, lakini imebidi kama wanasayansi twende kwa kina zaidi. Tumeongea na Bodi za shule, tumeongea na Walimu, tumeongea na wananchi, baadaye tumebaini yafuatayo ambayo yanalinganalingana na wenzangu, lakini yangu ni mabaya zaidi na ndiyo maana yamekuja kutokea matokeo yale. Tuna upungufu mkubwa wa Walimu, hususan Walimu wa Masomo ya Sayansi. Tunahitaji Walimu 72, lakini hali ilivyo sasa hivi kule hata kama walimu hawa wakija changamoto nyingine nitazieleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la mabweni; hizi Shule za Sekondari za Kata ambazo ndiyo nyingi katika Jimbo langu, katika Wilaya hii Mpya ya Malinyi zinachachukua wanafunzi kutoka vijiji mbalimbali. Shule nyingine ya Kata kati ya vijiji vitano mpaka kumi, lakini vijiji hivi viko mbali na hizo shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Shule ya Sekondari Ngoeranga, wanafunzi wengine wanatoka Kijiji cha Kilosampepo, kilometa 22! Kwenda na kurudi mtoto huyu maana yake kwa siku atembee kilometa 44! Kwa hiyo, kulikuwa na dhana pale na ingeweza kuleta jibu hilo, mabweni. Hata hivyo, nimeona azimio la Mheshimiwa Waziri la uboreshaji wa mazingira ya kufundishia na mazingira ya kujifundishia, lakini mmeelekeza mboreshe hizo shule kongwe.

Nashauri waanze kule kwenye matatizo kweli kweli ambapo kama wanaweza wakayarekebisha matatizo haya, hizo shule kongwe tayari wako pazuri! Mheshimiwa Waziri tumeongea, ameonesha dhamira, naomba asirudi nyuma kwamba, baada ya Bunge hili, pamoja na Mkurugenzi wa *TEA* watakwenda Wilaya ya Malinyi, waje wayaone haya mambo ambayo mtayazungumza, yamechangia sisi kuwa wa mwisho katika matokeo ya mtihani wa kidato cha nne mwaka jana. Hawa walimu niliosema hata kama wakiletwa, nyumba ni changamoto. Shule nyingine hazina kabisa nyumba ya Mwalimu na shule hizi ziko vijijini wakati mwingine hata hizo nyumba za kupanga, aghalabu, hazipatikani kirahisi. Shule hizi kwa mazingira yalivyo kule tunapakana na mito mingi, tunahitaji madaraja, tunahitaji na barabara, navyo ni kikwazo, Walimu na wanafunzi hawa kufika kwa wakati hasa kipindi cha masika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliliona tena tatizo lingine, mfumo wetu huu wa elimu, mtoto huyu anaanza darasa la kwanza mpaka la saba anajifunza Kiswahili, anapoingia *form one* Kiingereza, hapo ndio shughuli. Masomo yote ni ya Kiingereza, kwa hiyo ukiangalia ufaulu wao *form two* wanakwenda vizuri lakini wanapoingia *form three, form four* ni hatari.

Mheshimwa Naibu Spika, sasa mimi nashauri, kwa nini sasa kama hizi shule binafsi wanaweka *pre-form one* mwaka mzima ni bora tuchelewe lakini tufike. Kwa hiyo, vyema watoto hawa kabla hawajaendelea kuanza *form one* walio-*pass* darasa la saba waanze *pre-form one* kwa mwaka mzima, wawezeshwe masomo ambayo yanawasumbua, masoma haya ni kiingereza masomo ya hisabati na sayansi. Baada ya hapo ndio waingie kidato cha kwanza mpaka la nne. Hili linawezekana, nimeongea na Mheshimiwa Waziri ukawa unasitasita ukasema sijui kama itawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba Wabunge wenzangu tukubaliane, ndio maana nimesema chelewa lakini ufike, hawa tunawawahisha wa miaka minne matokeo yake wanakuja kuishia wengi wao asilimia karibu 30 ya watoto wetu mitihani ya *form four* wanapata *division zero*.

Mheshimwia Naibu Spika, haya tuliweza kuwezesha sasa tunapitisha hii bajeti, naona wengine mtakwenda mtafika hatua hii mtaigomea, hamtaki kupitisha hii bajeti. Lakini mimi nawashauri na kwanza naomba nishauri Kamati ya Bajeti hii fedha iliyotengwa ni ndogo sana katika Wizara hii, hii sekta ya elimu ni nyeti, ni muhimu sana, tunaomba ile wiki ya kujadili na Serikali Kamati ya Bajeti makae muongeze fedha hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ukiangalia bajeti hii muundo wake yaani ile *structure* asilimia 17 ndio inazungumzia elimu ya msingi na elimu ya sekondari, asilimia 48 elimu ya vyuo vikuu, wapi na wapi! Kama kweli tunataka twende uchumi huu wa viwanda wafanyakazi wengi watatakiwa ni hawa wa elimu ya kawaida, elimu hii ya *form four*, kwa hiyo ingekuwa vyema zaidi tungeboresha hii bajeti, hiyo*structure* tuweke fedha nyingi zaidi tuziwekeze kwenye elimu ya misingi na elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamelalamikia, wamechangia wameonesha hoja yao, na mimi naungana nao sula la maslahi ya walimu. Wala nisitafune tafune kwa kwali walimu wanaonewa, mafao yao yanasua sua.

Kwa nini wafanyakazi wengine malipo yao pamoja na sisi Wabunge yanaenda chapu chapu kwa nini hawa walimu bado kilia siku sauti ni hiyo hiyo, kila siku wanalalamika lakini kama ni kusikilizwa kidogo kidogo.

Mheshimwa Naibu Spika, naomba nimalizie kuhusu *COSTECH* (Taasisi ya Sayansi na Teknolojia). Tunasema tunataka tuipeleke nchi hii kuwa ya viwanda, uchumi wa kati, kuwa nchi ya teknolojia ya kisasa, lakini hatufiki huko kama hatuwezi tukawezesha taasisi hii kufanya kazi zake kikamilifu. Maana wao ndio wanatengeneza, wanasimamia suala zima la utafiti na utafiti majibu yake ndio yanatoa ushuhuda au *evidence*, ushuhuda huu ndio unaotufanya sisi watunga sera, sisi wasimamizi wa hii Serikali namna gani unaweza kuishauri vizuri kwa kutegemea matokeo ya utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti iliyowekwa hapa ni 0.04% ni kidogo mno na mimi nakumbuka utaratibu wetu tulikubaliana *COSTECH* itengewe bajeti ya asilimia moja ya bajeti ya Serikali. Sasa leo kiko wapi? Tunawashauri Serikali na Kamati hii ya Bajeti mrudi mpitie bajeti ya *COSTECH* kama kwa fedha hii hawawzi wakafanya chochote matokeo yake tunalaumu ndio tunaruka ruka kwa sababu wakati mwingine tunakosa vigezo, ushahidi kwenye mipango yetu na sera tunazozipanga. Nakushukuru kwa kunipa nafasi tena na naunga mkono hoja asate.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mhehimiwa Grace Sindato Kiwelu, naona Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk
ametoka, kwa hiyo, tuendelee Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbarouk Musa Bakari, Mheshimiwa Martha Umbulla ajiandae.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia Wizara hii muhimu sana katika Taifa letu. Nichukue nafasi hii kuwashukuru walimu wangu wote walionisaidia kufika mahali hapa leo, ninawashukuru sana, lakini niwapongeze walimu wote nchini kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na mazingira magumu waliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, urithi pekee tunaoweza kuutoa kwa watoto wetu ni elimu, na kwa maana hiyo ni lazima elimu hiyo iwe bora na isiwe bora elimu. Na ili elimu hiyo iwe bora ni lazima tuhakikishe tunatatua matatizo ya walimu, wamesema Waheshimiwa Wabunge hapa, matatizo waliyonayo walimu wetu, liko tatizo la upandishwaji wa madaraja, tatizo hili limekuwa ni tatizo sugu, walimu wetu kila mwaka Wabunge wakija hapa wanalisemea hilo lakini bado tatizo hili linaendelea kuwepo.

Nikuombe dada yangu Mheshimiwa Waziri wa Elimu, ninamba tuangalie walimu hao, lakini wanadai kwamba pamoja na hao wanaobahatika kupandishwa hawaangalii umri wa mtu kuuingia kazini, anaweza akaingia wa mwaka huu akampita daraja aliyefanyakazi zaidi ya miaka kumi, sasa yapo malalamiko hayo ninaomba myatazame.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwingine ni tatizo la ucheleweshwaji wa mishahara. Walimu hawa kwanza nimesema wanakaa kwenye mazingira magumu, mazingira hayo yanawasababishia kushindwa hata kuzihudumia famila zao. Mshahara mnawacheleweshea, walimu wanaokaa mbali na miji wanafunga safari kufuata mishahara, wanatumia muda mirefu kufuatilia mishahara yao na watoto wetu wanakosa vipindi. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, akikisheni mishahara ya walimu hawa inafika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine Mheshimiwa Waziri ni unyanyaswaji wa walimu. Wamesema wenzangu hapa, walimu wanapigwa makofi na Maafisa Elimu, wananyanyasika sana walimu hawa. Lakini lingine wako walimu wanaoonekana kuwa upande wa pili wakionekana na upinzani wanaandikiwa barua za onyo, lakini wale wanokuwa upande wa wapinzani wetu wao wanaonekana wanafanya sahihi. *(Makofi)*

Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, angalieni masuala haya tusiwagawe watanzania kwa itikadi za kisiasa, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni suala la nyumba. Suala la nyumba maeneo mengi bado ni tatizo hasa wale wanaokwenda maeneo yenye mazingira magumu amesema mchangiaji aliyemaliza hakuna hata nyumba za kupangisha. Na hili ni tatizo kubwa sana hasa kwa watoto wetu wa kike, unajikuta wanapewa nyumba na Wenyeviti wa Vijiji mwisho wanakuwa wake zao. *(Makofi)*

Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri hakikisheni suala la nyumba kwa walimu wetu mnalifanyia kazi haraka ili waweze kupata hizo nyumba za kuishi na hao wanaokaa mbali tuwape basi *transport allowance*, wanakaa mbali sana na maeneo ya vituo vyao vya kazi. Lakini na posho ya pango, watumishi wa Wizara nyingine wanapata, kwa nini walimu? Walimu wametufikisha hapa ndugu zangu tuwekeze kwa walimu kama kweli tunataka kuboresha elimu ya Taifa letu. Tutafanya mengine yote lakini tusipowekeza kwa walimu wetu kuhakikisha wanapata maisha mazuri, fedha zao wanapata kwa wakati itakuwa ni kazi bure.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la elimu bure. Waraka Namba 6 ulieleza yake mambo mliyoyaeleza pale, lakini niseme kwa kifupi, wamesema pia wenzangu, wakuu wa shule mnawapa wakati mgumu sana, ile fedha ya OC mnayotuma kwanza ni fedha kidogo, haitoshelezi, leo shule nyingi zina madeni ya umeme, maji, walinzi wanadai, leo tumechongesha madawati tumesaidiwa na *TANAPA*, tuna vifaa ambavyo vinahitaji vilindwe na walinzi. Leo walinzi hawajalipwa mishahara wanaondoka kwenye mashule yetu, viti vikiibiwa tutakuwa wageni wa nani.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia shule nyinge wamekatiwa maji, Mheshimiwa Waziri wewe ni Mwanamke wamesema Wabunge wenzangu mtoto wa kike bila maji hawezi kusoma. Leo shule zimekatiwa maji, watoto hawa wa kike tunawasaidiaje, watakimbia shule mwisho mnakwenda kuwakamata wazazi wao kuwaweka ndani, lakini Serikali ya Chama cha Mapinduzi mmeshindwa kutimiza wajibu wenu kwenye hizi shule. Hakikisheni mnapeleka fedha za kutosha, leo chakula kipatikane mashuleni hasa yale maeneo yenye mazingira magumu. Watoto hawaendi shule kwa sababu hakuna chakula na hata wanakwenda wanasinzia madarasani, walimu wanashindwa kufundisha kwa sababu watoto wetu wana njaa. Wazazi wameshindwa kuchangia kwa sababu hawana kipato cha kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi walipelekwa shule kwa sababu walijua chakula kinapatikana hasa yale maeneo ya wafugaji, leo chakula hakuna watoto wemeondoka mashuleni, lakini hata wale wanao-*supply* chakula kwenye mashule yetu hawajalipwa mpaka leo wanadai na wengi wao wamechukua mikopo kwenye mabenki, leo tunataka kuwatafutia vifo watu hawa kwa sababu mabenki yatakwenda kutaifisha mali zao. Niombe sana Mheshimiwa Waziri hakikisheni suala hili mnalifanyia kazi, walipeni wazabuni ili waweze kutimiza wajibu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nisemehe shule zenye mahitaji maalum. Kwa hapa nimshukuru sana Waziri wa TAMISEMI nililisema hili kwenye Wizara yake na tuliwasiliana, niwaombeni sana shule hizi zina mahitaji mengi muhimu. Tunawahitaji watoto wetu hawa wenye ulemavu, tunajua wanao uwezo lakini miundombinu ya shule hizo bado ni tatizo, ukiingia kwenye vyoo ni tatizo, vifaa vya kujisomea bado ni tatizo. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri fuatilieni watoto hawa wenye ulemavu, wanaouwezo wa kuwa viongozi katika Taifa hili. Ni jana tu nimetoka kutuma dawa katika ile shule ya watoto wenye ulemavu Njia Panda, hawana hata fedha za dawa, kwa hiyo niombe sana akikisheni shule hizi mnaziangalia kwa jicho la kipekee.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni suala la Ujenzi wa maabara. Tatizo la Serikali hii badala ya kuanza jambo la kwanza tunaanza la mwisho kwenda la kwanza. Maabara hizi zilijengwa, wananchi walipata wakati mgumu sana, walinyang'anywa mbuzi, walinyang'anywa kuku, maabara hizi zimekamilika leo, hakuna walimu, hakuna vifaa, tuwaeleweje Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Ninaomba sana na kwenye hotuba yako umesema vifaa vitaanza kununuliwa 2018 kama sikosei, sasa ni kwa nini tusingeanza kuandaa walimu, tukaviandaa vifaa alafu tukajenga hizo maabara. Leo watoto wetu wanakosa walimu, wanasayansi tutawapata wapi, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri ulifanyie kazi suala hilo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni ombi kutoka kwa mdogo wangu hapa ameniomba, wana Chuo cha Maendeleo ya Jamii kule Tarime, anaomba sana chuo kile mkibadilishe kiwe chuo cha *VETA*. Kwa sababu kama tumeshindwa kuvijenga bora tukatumia vyuo hivi au majengo haya yaliyopo kufungua vyuo vya *VETA* ili watoto wetu hawa wakaendelee kupata elimu hii ya ufundi kupitia vyuo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni suala la polisi Wilaya ya Siha walisimamia mtihani wa kidato cha nne mwaka jana. Lakini mpaka leo hawajalipwa fedha zao. Nikuuombe sana Mheshimiwa Waziri na ni Wizara yako ilitakiwa iwalipe, tunaomba mkawalipe polisi wale fedha zao na ukizingatia nao bado wako kwenye mazingira magumu fedha zao hawazipatai kwa wakati, kazi hii walishaifanya, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri mkalifanyie kazi suala hili ili polisi hao waweze kupata fedha zao.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunao upungufu mkubwa sana wa walimu wa Sayansi katika Wilaya yetu ya Siha. Ninaomba sana tuhakikishe tunawekeza kwa walimu hawa, kuna hiyo taarifa tuliyoipata ya mgomo wa *UDOM*. Walimu hawa hawafundishwi, zaidi ya wiki mbili sasa, walimu hawa wangetusaidia kuziba hilo pengo la walimu wa sayansi. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri fanyia kazi suala hili watoto wetu warudi darasani wakafundishwe ili wakafundishe watoto wetu. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mussa Mbarouk Bakari, atafuatiwa na Mheshimwiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma ajiandae

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Naibu Spika, labda na mimi niungane na wenzangu katika kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa alivyotuwezesha kutupa afya njema tukaweza kuwemo katika Bunge letu leo hii siku ya tarehe 27 Mei, siku ya Ijumaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine nirudie kuwapongeza wapigakura wa Jimbo langu la Tanga Mjini. Kama nilivyosema kwa kubadilisha historia ya Tanzania na kuweza kumleta Bungeni Mbunge kutoka Kambi ya Upinzani kwa mara ya kwanza. Lakini vilevile niseme kwamba katika Wizara ya Elimu naunga mkono hoja iliyotolewa na Kambi ya Upinzani asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo nianze kuchangia kama ifuatavyo; moyo na *engine* ya nchi ni elimu na ndio maana wanataaluma wakasema *education is a life of nation*. Lakini vilevile nimnukuu aliyekuwa Rais wa Afrika ya Kusini Mzee Nelson Mandela, alisema kwamba *education is the most powerful weapon which you can use to change the world* yaani elimu ni silaha nzito ambayo inaweza ikaibadilisha dunia lakini sisi Tanzania imekuwa ni kunyume na ninasema hivyo kwa sababu leo ukienda katika Wizara ya Elimu

kuanzia elimu ya *nursery* kuna matatizo, ukienda katika elimu ya msingi kuna matatizo, elimu ya sekondari kuna matatizo, ukienda kwenye vyuo vikuu ndio kabisa, sasa tujiulize hivi kweli miaka 55 baada ya Uhuru mpaka leo sisi Watanzania tunajadili madawati!

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano wenzetu nchi ya India baada ya kupata Uhuru miaka 40 tayari Wahindi walikuwa wanaweza kutengeneza pikipiki aina ya Rajdoot, tayari walikuwa wanaweza kutengeneza magari aina ya Mahindra, tayari walikuwa wanaweza kutengeneza matreni, tayari wahindi baada ya miaka 40 waliweza kutengeneza vyombo vinavyokwenda *aerospace* katika anga za juu. Lakini leo Tanzania twajadili madawati, twajadili matundu ya vyoo, mashuleni vyakula hakuna *it is a shame*. Hii ni aibu, nchi kama Tanzania yenye rasilimali zote ambazo Mwenyenzi Mungu ametujalia lakini tumeshindwa kuisimamia vizuri elimu, tumeshindwa kuiweka misingi mizuri ya kielimu matokeo yake Tanzania tunakuwa na wa mwisho katika nchi tano za Jumuiya ya Afika Mashariki na kama sio ya mwisho basi labda tutakuwa tumeishinda *Southern Sudan. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunashindwa na Burundi, Rwanda,Uganda na Kenya. Leo Burundi waliokuwa na vita ya wenyewe kwa wenyewe wakauana watu milioni mbili lakini wana *system* ya *one child onelaptop*,sisi Tanzania ambao tunajisifi tuna eneo kubwa la nchi, tuna uchumi imara lakini tumeshindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi niseme na niishauri Serikali tusichanganye siasa na elimu. Tunaposema elimu bure basi iwe bure kweli, lakini kama tunawacheza shere Watanzania Mwenyenzi Mungu atakuja kutuhukumu kesho. Leo tumesema elimu bure, lakini hivi ni kweli elimu ni bure?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda shule za msingi leo hata maji ya kunywa watoto hakuna, kama pana nyumba ya jirani wakimbilie nyumba ya jirani kwenda kunywa maji. Leo watoto wa kike Ashakum si matusi anapokwenda kujisaidia lazima apate maji, shule zimekatwa maji, wanategemea kwenda katika nyumba za jirani, kama kuna muhuni, mvuta bangi huko mtoto wa kike ndio anaenda kubakwa huko huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi wenzetu hamuoni kwamba haya ni matatizo. Sisi wapinzani tuna akili gani na ninyi wenzetu wa Chama Tawala mna akili gani. Miaka 55 baada ya Uhuru leo, tunajadili matundu ya vyoo, na ukiangalia hata katika matangazo ya Haki Elimu, mwalimu anakwenda kwenye choo na wanafunzi wamepanga mstari wanasukumana, choo hakina bati, hakijapauliwa, mwalimu anakanyaga mawe, lakini tunaambiana hapa ukitaka kuwa Rais lazima upitie kwa mwalimu, ukitaka kuwa Mbunge lazima upitie kwa

kwa mwalimu, ukitaka kuwa Waziri Mkuu upitie kwa mwalimu. Tuna wacheza Watanzania shere, tuwaambieni ukweli kama tumeshindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme kitu kimoja tu kwenye suala la elimu ya *nursery,* Mheshimiwa Waziri lazima ukasimamie vizuri kwa sababu elimu ya *nursery* tumeweka utaratibu kwamba mtoto haanzi *standard one* mpaka apite *nursery school*, lakini hivi Serikali imeangalia ufundishaji na mitaala ya kwenye *nursery school?* Hakuna kitu kila mwenye *nursery school* yake ana mitaala yake ana utaratibu wake wa kufundisha. Hii ni hatari kwa sababu mwingine anaweza akawa ana uwezo mzuri wa kufundisha, mwingine hana uwezo mzuri matokeo yake sasa wazazi wanapoteza fedha lakini watoto wakitoka huko kwa sababu msingi sio mzuri hakuna kitu wanapofika *standard one*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hilo halitoshi kwenye elimu ya msingi, hapa pana matatizo makubwa. Kwenye elimu ya msingi katika nchi yetu kumekuwa na utaratibu kwamba kwanza watoto wanakwenda shuleni wakati mwingine hata chakula mtoto hajapata nyumbani. Sasa matokeo yake mtoto anakwenda na njaa, na mtu mwenye njaa hafundishiki, matokeo yake mimi nilikuwa naishauri Serikali ikibidi lazima tupeleke bajeti ya chakula katika shule zetu za msingi, hata na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mtoto anapotoka nyumbani, anapokwenda shuleni na njaa hata mwalimu afundishe namna gani anakuwa haelewi. Amesema mwanafalsafa mmoja anaitwa Bob Marley, *the hungry man is angry man,* kwamba mtu mwenye njaa anakuwa na hasira, haelewi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi niseme tupeleke bajeti kubwa ya chakula katika shule za msingi na sekondari na vyuo. Hata wale wanaotu-*supply* vyakula katika vyuo vyetu na shule zetu basi walipwe kama alivyotangulia kusema msemaji aliyetangulia, kwa sababu wengine wanapelekwa mahakamani, wametoa zabuni za vyakula Serikali haijawalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine kwenye sekondari kuna matatizo makubwa, kuna suala zima la ukosefu wa walimu wa sayansi. Hakuna walimu wa *mathematics, biology, physics* na *chemistry*. Matokeo yake mtoto anamaliza *form four* hata ukimuuliza *what is bunsen burner* hajui, ukimuuliza *what is test tube* hajui, na matokeo yake wanakosa katika *theory* na *practical* zote wanakosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimtake Waziri ahakikishe maabara zinazojengwa zinaambatana pamoja na vifaa. Tusiseme tu kisiasa kwamba tunajenga maabara kumbe vifaa hakuna na matokeo yake hata wanaokuwa wanachukua masomo ya sayansi, kwa mfano wanaosoma *PGM* ndio hao

tunaotegemea kwamba watakuja kuwa marubani. Lakini kwa ukosefu wa vifaa sasa tunakosa ma-*pilot* katika ndege zetu, matokeo yake tunaajiri wageni tunapeleka ajira katika nchi nyingine, mimi niseme lazima tujikite katika elimu iliyo bora kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda kwenye suala zima la vyuo vikuu. Vyuo vikuu kuna matatizo, na matatizo ni hayo ya mikopo, lakini hata na matatizo na uwezo wa wanafunzi wenyewe wengine wanaopelekwa. Lakini hata baadhi ya walimu pia nao uwezo wao sio mkubwa sana, matokeo yake sasa wanafunzi wetu wa vyuo vikuu wamekuwa nao elimu yao ikishindanishwa na nchi nyinine inakuwa sio bora.

Pia yupo Makamu Mkuu wa Chuo kimoja alisema, hata wanafunzi wa chuo kikuu hawawezi kuandika barua ya kuomba kazi, kwa kiingereza kwa sababu msingi ulikuwa ni mbovu, leo mtoto anakwenda shule ya msingi na njaa, leo mtoto anakuwa hana chakula, matokeo yake anateseka na njaa mpaka mchana, anatoka shule hana alichoelewa.

NAIBU SPIKA: Ahsante muda wako umekwisha, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma ajiandae.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uzima na kuweza kusimama hapa kuchangia hoja
hii ya Wizara ya Elimu. Naomba na mimi nichukue fursa kama wenzangu nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu Profesa Ndalichako, na Naibu Wake Mheshimiwa Stella Manyanya, aidha nimpe pole kwa msiba wa mama yetu na Mungu ampe subira.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ni ufunguo wa maisha na lazima Watanzania wapate elimu itakayowafungua katika maisha yao. Aidha, niipongeze sana Serikali ya Awamu ya Tano, kwa sababu imekwisha anza kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata elimu wote na wanakuwa na ufunguo wa maisha kwa sababu ya kuanza mfumo wa elimu bure kuanzia shule ya msingi hadi sekondari kidato cha nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya msingi pamoja na sekondari hadi kidato cha nne ni kama msingi wa nyumba, na kama msingi wa nyumba ni imara basi elimu yetu ya msingi na sekondari itakapokuwa imara tutakuwa na elimu iliyo bora hadi vyuo vikuu na hatimaye Watanzania wote watakuwa na elimu bora Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini elimu bora pia inatokana na walimu walio bora, na wenye moyo wa kufundisha kwa sababu walimu ndio watakaoweza kuboresha elimu yetu na kwa hivyo ni lazima tuhakikishe kwamba changamoto zote zinazokabili elimu ya msingi na elimu ya sekondari tuweze kuzitatua ili dhamira yetu ya kuboresha elimu kuanzia msingi na sekondari iweze kutimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze kuzungumzia mazingira wezeshi kwa ajili ya walimu wetu hasa wa sekondari za kata. Walimu wetu wa sekondari za kata wako katika mazingira magumu sana, hasa sisi ambao tunatoka katika mikoa ya pembezoni. Walimu wengi wa sekondari hizi za kata wako katika maeneo ambayo hakuna umeme, maji, huduma mbali mbali za jamii, hospitali ziko mbali na hatimaye hata mitandao hizi ambazo vijana wengi wanazitumia hazipo; na kwa hivyo utaona changamoto nyingi zinazowakabili vijana hawa walimu ili waweze kufanya kazi katika Sekondari hizo ama maeneo hayo, inahitajika ushawishi ili waweze kuendelea kufanya kazi katika shule ama maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilikuwa naiomba Serikali kwamba iweze kuangalia uwezekano wa kuwapa walimu wa sekondari za kata, na maeneo mengine yenye mazingira ambazo ni mbaya, waweze kupata *hardship allowance* ili iweze kuwapa motisha. Hili ni muhimu sana, najua walimu wengi wote wana matatizo ya hapa na pale, lakini hawa ambao wako katika sekondari hizi zenye mazingira ambayo sio wezeshi n wanahitaji uangalizi ama huruma ya Serikali kwa kuweza kuwapa motisha waweze kufundisha kwa sababu elimu bora kama ambavyo nilianza ni pamoja na mwalimu ambaye atakuwa na moyo wa kufundisha baada ya kuwezeshwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia mengi yameisha zungumzwa. Lakini ni suala zima la kutenga maeneo ya shule ambayo yatawezesha kilimo ya mashamba na bustani. Tuki-*refer* elimu za hapo awali, shule zetu nyingi zinakuwa na mashamba ama maeneo ambayo wanafunzi wanalima na kilimo hicho kinaweza kikasaidia pia kuwapatia chakula cha mchana, ama matunda ambayo yatawajenga wanafunzi wetu kiakili, kimwili na kiafya. Kwa hiyo, najua changamoto ya ardhi ambayo inakumba nchi yetu hasa kwa maeneo ya mjini lakini bado kwa maeneo ya mikoani tuna ardhi ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo uanzishwaji wa shule ziende sambamba na maeneo ambayo wanafunzi watapata kulima na kuweza kujijenga kimwili na kiafya. Lakini vilevile kupata chakula kwa bei nafuu. Tukisema wazazi waendelee kuchanga kwa ajili ya chakula cha mchana cha wanafunzi, bado ni mzigo na kwa hivyo tutafute namna rahisi ya kuweza kuwapatia wanafunzi wetu chakula cha mchana, kupunguza pia utoro shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia upungufu wa walimu wa sayansi. Hili limezungumzwa sana. Lakini mkoa wetu wa Manyara una upungufu mkubwa sana wa walimu wa sayansi, najua pengine na maeneo mengine lakini ya kwetu lazima niisemee, hatuna walimu kabisa wa masomo ya sayansi, kwa hivyo tunaomba Serikali iweze kuangalia inapo-*allocate* walimu, iweze kufikiria maeneo ambayo tayari kuna upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali itafute kila mbinu, jinsi ambavyo ilipata mbinu ya kujenga maabara nchi nzima, tukaweza kujenga kwa kipindi kifupi. Hiyo ni hatua ya kwanza na tumemaliza, na mimi naipongeza Serikali, wanaoibeza wana lao, lakini tayari tuna maabara zetu, nina hakika kwamba walimu wa sayansi watapatikana. Serikali iweke juhudi ya hali ya juu, kuhakikisha kwamba walimu wa sayansi wanapatikana ili waweze kufundisha masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa maabara umefanikiwa, lakini ninajua kwamba suala hili lilikuwa suala kama la zimamoto na imetumia fedha ambazo zilikuwa zimekusudiwa kwa madhumuni mengine. Kwa mfano, huko katika Wilaya yetu ya Mbulu ama Mkoa wetu wa Manyara, maabara tumezijenga katika Wilaya zote, lakini tumetumia fedha ambazo zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya miradi kwa hiyo baadhi ya miradi sasa hivi imekwama kwa kukosa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kulikuwa na ujenzi wa madaraja muhimu sana katika maeneo ya vijijini kama Daraja la Gunyoda kule Mbulu, ujenzi wa kituo cha afya kule Endagikoti, Mbulu, tayari miradi hii na miradi mingi ya umwagiliaji imekwama kwa sababu ya kukosa fedha, kwa sababu fedha zile zilikuwa *diverted* kwenda kujenga maabara. Naiomba Serikali iweze kuangalia hili na ihakikishe kwamba fedha hizi zinarudishwa ili miradi hii ya maendeleo iweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia suala zima la matatizo ya walimu wastaafu. Hili ni tatizo sugu na wengi wamelizungumzia, lakini ni kilio cha wastaafu walimu wengi ni lazima Serikali iwe sikivu, wananchi wanapolalamika kwa kipindi kirefu na kilio hiki cha wastaafu ambao hawapati stahili zao ni cha muda mrefu sana. Walimu wengi kipindi kile cha kupandisha madaraja kiliposimamishwa, wengi walikuwa wanaendelea kufanya kazi na huko wanastahili na wanapaswa kupandishwa daraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa suala hili lilikuja kufikia kupandishwa madaraja wakati wengi wameshastaafu vilevile, ninaiomba Wizara iangalie walimu ambao tayari walistahili kupandishwa na wamekaa katika cheo kimoja zaidi ya miaka 15, lakini hadi wanastaafu hawakuweza kupata stahili zao. Na sasa wako wengine ambao wamesimama kwa kipindi kirefu, mishahara yao

inatofautiana na walimu ambao walikuwa nao wameajiliwa hata baada yao, lakini wana mishahara ambayo ni midogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa muda wako umekwisha. Namuita Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja hii leo. Namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa nguvu kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuweza kutoa mchango wangu kwa Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi. Naanza kwa kuunga mkono hoja, napongeza juhudi na kazi nzuri inayofanywa na Profesa Joyce Ndalichako na timu yake akiwemo *Engineer* Stella Manyanya, pamoja na timu nzima ya Wizara na wakati huo huo nampa pole Mheshimiwa Stella Manyanya kwa kuondokewa na mama yake mzazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara hii ya Elimu ina umuhimu wake kipekee, hapo hapo naunganisha na kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kupitisha lile azimio la kupatia elimu bure kuanzia darasa la kwanza mpaka sekondari. Jambo hili lina maana sana, kwa sababu linatoa nafasi na fursa kwa wanyonge wengi kupata elimu kwa watoto wao. Wote tunajua umuhimu wa elimu, kwa hiyo zinahitajika juhudi zetu za pamoja kuunga mkono Wizara hii, ili vijana wetu wote wapate elimu stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa elimu mpaka sekondari, ni bure kwa hivyo ningependekeza kwamba kidato cha tano na cha sita, vilevile tufanye jitihada, ili iweze kuwa bure vilevile. Kwa kuwa pale kuna watoto wa wanyonge wengi, ambao wameweza kupita kuanzia kutoka kwenye shule za kata mpaka wakafika pale.

Kwa hiyo, Serikali ifanye vile inavyoweza katika kuongeza ukusanyaji wake wa kodi au mbinu nyingine inakojua itapata pesa ili vijana hawa wasije wakakwazwa. Kwa kuwa vijana wa chuo kikuu wanapata mkopo, na hawa nao wapate, kwa kuwa *form five* na *six*ndio chimbuko la wataalam wetu, naamini juhudi za ukusanyaji wa kodi zitatuwezesha kufika hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia iangalie na ipitie ihakikishe kwamba angalau Wilaya zote zina shule za *A-level* za kutosha, kwa mfano Wilaya kubwa kama Rufiji ina shule moja tu ya*A-level* pale Mkongo na hii Wilaya ni kubwa kuliko Mkoa mzima wa Kilimanjaro, kwa hivyo Wizara ifanye *ranking* kuhakikisha kwamba Wilaya zote zina shule hizi la *A-level*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Nne, ilifanya juhudi kubwa kusimamia kujenga shule za sekondari za kata katika Kata zote, na maabara na madarasa. Hili jambo limefanikiwa kwa juhudi za wananchi na Serikali pamoja.

Dhana ya elimu bure inapata mtikisiko kidogo, hii dhana imelenga kuondolea wazazi wanyonge, kuweza kuwasaidia vijana wao wapate elimu, maeneo mengi maabara zimesimama kujengwa, madarasa yamepungua kasi ya kujengwa, maeneo mengi wazazi wamepunguza kasi ya kujitolea kushiriki kwa kisingizio kwamba elimu ni ya bure, naomba sana tusiieleleze Serikali, tuendelee na *spirit* ile ile ya kuunga mkono jitihada za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuendelee kusisitiza wananchi waendelee kuelimishwa umuhimu wa kutimiza wajibu wao, tunakiri kwamba katika jambo hili la elimu bure ziko changamoto, na hilo ni jambo la kawaida kwa sababu jambo lolote la maendeleo huwa linavikwazo vikwazo, lakini tutashinda na tutafika tunakokwendea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijazungumza zaidi kuhusu masuala ya shule hizi za kata, naomba kwa ruhusa yako nizungumzie kidogo kuhusiana na sheria. Naomba nitanabaishe kuhusiana na Sheria za Shule za Kata, Sheria ya Elimu Namba 25 kama ilivyorekebishwa mwaka 1978, kwa Sheria Namba 10 ya mwaka 1995, imeweka utaratibu wa Kikanuni wa kuanzishwa shule za sekondari na msingi, kwa utaratibu wa sasa, tuna shule za kata ina maana sheria hii haizungumzii shule za kata, kwa hivyo kunahitajika marekebisho ya sheria, kujumiuisha shule ya kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile sheria na kanuni inayounda bodi za shule, inatoa maelekezo ya uteuzi wa wajumbe wa bodi katika mkoa; kwa kuwa sasa tuna shule za kata, tunahitaji malekebisho ya Kanuni ili tuweze kutoa wajumbe hao wa bodi kutoka kwenye kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilijitahidi sana kuanzisha Sekondari karibu 3,500 za kata kama sikosei, sasa niiulize Serikali hii inashindwaje kujenga vituo vya *VETA*kwa kila Wilaya ili hawa vijana wetu ambao ni wengi wakapate elimu ya amali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia ina vitu ambavyo tunategemea vijana wetu wafanye. Lakini tulifuta somo la elimu na elimu ya kujitegemea, kwa mfano kila Ijumaa iliku wakati wa mchana watu wanakwenda kufanya mambo ya bustani, kama ilivyokuwa *setup* ya Mwalimu Nyerere wakati ule. Sasa vijana hawa wanapomaliza, wanaishia kwenda kucheza *pool* kwa sababu ile elimu ya bustani haipo, kwa mfano siku hizi kuna elimu ya bustani katika sehemu ndogo inaitwa *permaculture* ingeweza ikaanzishwa kwenye shule mbalimbali kule,

watu wakajipatia mboga, viazi na vitu vidogo vidogo. Kwa hiyo lazima tuchanganue zaidi kutafuta, utaalamu na teknolojia sasa wa kuweza kuzalisha katika sehemu ndogo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijamaliziwa muda wangu, basi niombe Wizara ya hii ilekebishe *curriculum,*ili tuweze kupata masomo ya kilimo na biashara, michezo, ufundi, katika ngazi zote na masomo haya yatiliwe mkazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala kubwa sana la kupata mimba wasichana, hili ni suala linaleta matatizo, linaleta unyonge, kwa sababu Wizara ifikirie na izingatie kwa kina kwa uharaka ikiwezekana kuwarudisha watoto hawa kwenye madarasa. Hatusemi hivyo kama tunawatia washawasha ili wakapate mimba laa! Ilamimba nyingine zinakuja ni kwa *accident,* nyingine ni kwa kubwakwa, kwa hivyo tufikirie, unapomuadhibu kijana huyu asiendelee kusoma, umemuadhibu na mtoto atakayezaliwa, umeiathiri familia yake nzima, umeongeza umaskini, hujauondoa umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini uadhibu mtoto ambaye hana makosa, na yule ambaye mhusika mwingine mara nyingi anakwenda wanaposema wazungu anakwenda *scot free,* kwa sababu huwezi kumpata na hivyo anapata nafasi ya kwenda kufanya uharibifu, kuwawekea mimba watoto wengine.

Sasa tuone Wizara, sisi Wizara ya Elimu kule Zanzibar kwa mfano wameliona hili na wasichana wanaopata mimba kwa bahati mbaya, wanaendelea na masomo yao na imeonekana kwamba wengine hawa wanatokea kuwa wataalam wakubwa, wakatoa na mfano mzuri katika jamii, na mchango mzuri katika jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wizara yangu wakati nilipokuwa nahudumu kama Waziri, nilifika Bahamas. Nikatembelea darasa zima nikakuta watoto wote ambao wana miaka 16 hivi nakuendelea wote darasa zima wana mimba matumbo kiasi hiki. Lakini wameandaliwa darasa lao na wanafundishwa, kwa sababu huwezi kum-*penalized* huyu mtu, ile mimba inatokana na hali ya maumbile, saa nyingine huna nguvu za kumshinda mwanaume. Mimi baba yangu alisema usiende ukaa faragha na mwanaume itakuwa taabu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo kidogo hapa, tangazo la kwanza kuna wageni walitangazwa asubuhi, lakini walikuwa bado wako getini,na hawa ni wageni wa Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza ambao ni Josephat, Gwamagobe na Aidan Joseph, karibuni sana.

Halafu nitayasoma kwenu majina ya wachangiaji wa mchana, tunao Mheshimwa Joel Mwaka Makanyaga, Mheshimiwa Moshi Suleiman Kakoso, Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka, Mheshimiwa Aisharose Matembe, Mheshimia Omary Mgumba, Mheshimiwa Leonidas Gama, Mheshimiwa Emmanuel Papian, Mheshimiwa Salum Rehani, Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mheshimiwa Juma Kombo Hamad na Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe.

Waheshimiwa Wabunge, kwa dakika hiyo moja iliyobaki, tukumbushane Kanuni ya 99(14), inatukataza wakati wa mjadala wa bajeti kutoa salamu za pongezi. Kwanza zinasema kutoa maneno yoyote ya utambulisho, salamu za pongezi au shukrani kwa Mbunge au Waziri. Kwa hiyo tuzingatie hiyo Kanuni.

Kanuni nyingine ni ya 147, kuhusu lugha inayotumika humu ndani, kiingereza au kiswahili, na Kanuni ndogo ya pili inasema, tujitahidi tusichanganye lugha zote mbili. Tujitahidi tusichanganye lugha zote mbili, wakati wa kutoa michango.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi leo jioni.

(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia

MWENYEKITI: Tukae, Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI: Hoja za Serikali,Kwamba Bunge sasa lilikubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa mwaka wa fedha 2016/2017, majadiliano yanaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017 - Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa nafikiri kuna majina yalishasomwa na ninayo hapa. Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, ajiandae Mheshimiwa Kakosa, ajiandae Aisharose Matembe.

MHE. JOEL M. MAKANYAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamechangia wachangiaji wengi na mimi niko ndani yao yaliyozungumzwa kwa hakika ni yale ambayo na mimi ningependa niyazungumze kwa undani. Lakini nataka nijiweke kimsingi katika kukubaliana nao kwamba elimu ndiyo kila kitu, ndiyo msingi wa maendeleo bila kuwa na elimu bora Taifa halitapiga hatua yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuwa na elimu bora safari yetu ya kuelekea Tanzania ya uchumi wa kati itakuwa ni ndoto kwa sababu huko tunazungumzia kuwa na viwanda pamoja na kwamba tunapuzungumzia Tanzania ya viwanda maana yake tunazungumzia *industrialization*. Tukienda katika historia wenzetu wamepita huko miaka ya 1800 wakati sisi tuko kwenye *primitive,* lakini leo sisi tunazungumzia *industrialization* basi tuifanye iwe kweli kwa maana ya kwamba iwe elimu bora ndiyo maana wachangiaji wote wanapiga kelele elimu iwe bora tuweze kwenda jinsi tunavyotaka sisi Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme machache, kwanza nimevutiwa sana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hotuba imesheheni kila kitu ambacho kinahitajika kutufanya sisi tuweze kusonga mbele katika nyanja ya elimu na kwa hiyo kuweza kutubeba sisi kutupeleka katika Tanzania ya uchumi wa kati. Lakini tatizo liko wapi, tunapopiga kelele na elimu kuwa siyo bora, elimu duni tatizo liko wapi, mipango mizuri tunayo, mikakati mizuri tunaiweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu ili tuweze kufika tunakotaka, tunahitaji kuwa na elimu bora inayozingatia usawa kwa wanafunzi wote. Tunapozungumzia elimu bora tunazungumzia elimu yenye mitaala iliyosimama na *syllabus* zilizosimama, zisizobadilika badilika, hii ni sera hatuwezi kuwa na sera ya kutufikisha popote inayobadilika badilika kila wakati. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi naona sehemu moja ambayo inaleta shida kwetu ni hapo kwamba sera zetu mitaala yetu *syllabus* zetu zinabadilika na zinabadilika na watu. Leo yuko Mama Ndalichako anakuja kivyake, kesho anakuja Mwaka anakuja kivyake, keshokutwa anakuja Mheshimiwa Zungu anakuja kivyake hatuwezi kusonga mbele hata siku moja, tunatakiwa tuwe na sera iliyosimama, haijalishi leo yuko nani, kesho yuko nani ili tuweze kuwa na elimu bora.

Pili, tunahitaji kuwa na walimu bora, walimu bora utawapata wapi? Lazima uwapate vyuoni je wanadahiliwa vipi kuingia vyuoni. Tumesikia hapa tatizo la udahili wa vyuoni. Tumesikia hatua zilizochukuliwa na Mheshimiwa Waziri kwa wale waliotufikisha pabaya pamoja na kwamba tunalia hawa wanafunzi waliofutiwa masomo kwa kweli tunaomba Serikali iwafikirie mara mbili

mbili, kuwapoteze muda mwingi na sasa waende wakaanze upya na hawajui waanzie wapi kwa kweli siyo sahihi. Tunaiomba Serikali iwafikirie kwa sababu halikuwa tatizo lao tunajua kuna namna yoyote inaweza ikafanyika ili nao waweze kujikwamua kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini udahili vyuo vya walimu viko vipi huko wanakosoma walimu kukoje vyuo viko sawasawa au wanakwenda kupitisha muda tu miaka miwili, mitatu wanatoka wanakuja kufundisha? Hayo ni mambo ya msingi katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na elimu bora. Mazingira ya kufundishia yako vipi? Madarasa yako vipi, madarasa yasiyokuwa na sakafu, madarasa ambayo darasa moja linaingia wanafunzi mia moja naa mpaka mwalimu anakosa pa kusimama, hilo ni darasa ambalo mwalimu anaweza akafundisha kweli? Tunajua mwalimu anapofundisha ana *standard* awe na wanafunzi wangapi darasani, aweze kuwapitia hata wale walio *slow learners* kuwavuta waende na wenzao. Sasa mwalimu anapokuwa na darasa limejaa hata pa kupita haoni atawasaidia vipi hao wengine *slow learners* na hata hao *first learners* hawawezi ku-*learn* chochote katika darasa ambalo limesheheni wanafunzi kiasi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia vifaa vya kufundishia, viko mashuleni kweli? Maana yake sisi ndiyo tunaotoka huko vijijini, ndiyo tunaotoka huko kwenye majimbo yetu, shule zina vifaa vya kufundishia? Serikali ina mpango gani katika hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia maslahi bora ya walimu. Ukishakuwa na mwalimu bora lazima awe na maslahi bora maslahi bora ya mwalimu ni pamoja na mshahara wake uwe mzuri, tunazungumzia kwamba ukitaka kuwa Mbunge lazima utapita kwa mwalimu, ukitaka kuwa Rais lazima upite kwa mwalimu, ukitaka kuwa daktari lazima upite kwa mwalimu, lakini huyu mwalimu ukishapita umemuacha hapo nyuma, leo kuna mwalimu aliyenifundisha mimi pengine nikianza kumgeukia nyuma ninachokipata mimi kama mshahara wangu ukilinganisha na cha mwalimu hakuna heshima hata dakika moja. Wanavunjika moyo, wanaona kwamba kazi hiyo ni kazi ya kudharaulika sana, hebu tuifanye kazi ya walimu kuwa kazi ya heshima kwa kuwaangalia kwenye maslahi yao kwa upande wa mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na mishahara hiyo waliyonayo stahili zao wanazostahili wanazipata inavyostahili? Mwalimu anahamishwa, hapati hela ya uhamisho. Mwalimu anatakiwa kwenda kwenye semina au walimu wanatusaidia kwenye kusahihisha mitihani pesa za kusahihisha mitihani hawazipati kwa wakati unaostahili. Hivi tunawaangalie kweli walimu kwa karibu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la nyumba za walimu. Walimu huko vijijini mkienda utawaonea huruma, wanakaa kwenye vibanda ambavyo huwezi kuamini, sasa tunaanza kuwaambia walimu wakipangiwa shule wakienda wakiripoti wanaondoka, hata mimi ningeondoka, anakwenda kuingia kwenye kibanda ambacho huwezi kuamini, kweli mwalimu ametoka chuoni anakuja kuwafundisha wanafunzi anaingia kwenye kibanda hamna taa *okay* mambo ya taa siyo tatizo watanunua siku hizi kuna mambo ya *solar* kuna nini, lakini kibanda kimejibana kidogo kidogo tu, kitanda hakuna nafasi ya kuweka kitanda cha sita kwa sita hakiingi kweli jamani? Hii siyo sawasawa hebu tuwaangalie kwa karibu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho na muhimu katika ubora wa elimu ni hili la kuzikagua shule. Shule hazikaguliwi kabisa, ukienda shuleni ulianza mara mwisho wamekaguliwa lini utacheka, hazikaguliwi na hiki ndicho chanzo kikubwa cha elimu kushuka pamoja na walimu kuwa wamekataa tamaa lakini kama wanajua kuna mtu anawafuatilia nyuma basi hata kawoga kidogo kanakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu naomba haya masuala Mheshimiwa Waziri ayachukue pamoja na mengine mengi waliyozungumza wenzangu ayachukue na Serikali iyafanyie kazi kama kweli inataka kufanya Tanzania tuwe na elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili usawa kwa wanafunzi. Tuna wanafunzi wengine wenye mahitaji maalum, mahitaji maalum…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kakoso jiandae Mheshimiwa Aisharose Matembe, karibu Mheshimiwa Aisharose Matembe, Mheshimiwa Omary Mgumba.

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu katika bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi.

Awali ya yote namshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, mwingi wa neema ambaye ameniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza sana Rais wetu mpendwa Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuliongoza Taifa hili. *(Makofi)*

Vilevile nampongeza Makamu wa Rais Mheshimiwa Mama Samia Suluhu, Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Baraza la Mawaziri kwa namna ambavyo wanajituma kuhakikisha kero za Watanzania zinapungua au zinakwisha kabisa. Ninapenda kuwatia moyo waendelee kukaza buti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuwashukuru sana wananchi wa Mkoa wa Singida hususan wanawake na vijana kwa kuniamini na kunichagua kwa kura nyingi za ndio napenda kuwahakikishia kwa heshima hii kubwa waliyonipa sitawaungusha na wala sitaanguka katika kuwatumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo najielekeza moja kwa moja katika kuchangia. Mwanafalsa mmoja John Dew aliwahi kusema *education is not preparation for life, education is life itself,* akimaanisha kuwa elimu siyo maandalizi ya maisha, elimu ni maisha yenyewe, hivyo basi, elimu ndiyo msingi mkuu katika kuyamudu maisha ya kila siku na ndiyo mkombozi wa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inatajwa kuwa na elimu ya kiwango cha chini ukilinganisha na nchi nyingine za Afrika Mashariki, hii ni kutokana na ukweli kwamba elimu inayotolewa haikidhi viwango vya ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu inayotolewa katika vyuo na shule zetu za Serikali haimuandai kijana kujiamini, kuwa mbunifu, kuwa ni mwenye uwezo wa kubembua mambo, kuwa na *communication skills,* kuweza kujiajiri au kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kijana aliyemaliza elimu ya kidato cha nne kutoka nchini Kenya au Uganda akija Tanzania anapata ajira bila wasiwasi wowote, hii ni kwa sababu elimu aliyopata ni bora, inamwezesha kujiamini, inamwezesha kujielezea kwa ufasaha kwa lugha ya kiingereza ambayo hapa nchini kwetu ni lugha ya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo sababu kadhaa ambazo zinachangia kushuka kwa kiwango cha elimu katika shule zetu za Serikali. Sababu hizi nitazitaja kama ifuatavyo:-

Kwanza, ni utayarishaji wa mitaala ambayo haiendani na wakati na mazingira ya sasa. Mitaala ambayo inakosa *skills* ambazo zingeweza kumsaidia mwanafunzi kujiamini au kujitegemea baada ya kumaliza elimu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zimeonyesha kwamba kuna changamoto za utayarishaji na utekelezaji wa mitaala bila kufanyiwa majaribio jambo linalopelekea walimu wengi kukosa stadi za maisha, kukosa maarifa ya kufundishia. Mfano katika Taifa la Netherland mtaala wake unasisitiza

kufundisha elimu ya ujasiriamali kuanzia shule za sekondari. Hivyo basi, ningeishauri Serikali kutizama upya mitaala ambayo itazingatia uchambuzi wa kina wa kumwezesha kijana kuweza kujitegemea na kujiamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili inayochangia kushuka kwa kiwango cha elimu, ni uhaba wa vitendea kazi na *teaching methodology* ambazo kimsingi hazimjengi mwanafunzi kujitegemea au kujiamini. Shule zetu nyingi za Serikali zinafundisha kwa nadharia zaidi kuliko vitendo. Wenzetu wa dunia ya kwanza wanasema *practice makes perfect*. Unapomfundisha mwanafunzi kwa nadharia na vitendo unamwezesha mwanafunzi huyo kulielewa somo hilo vizuri zaidi. Hivyo kuna haja ya msingi ya kurudisha elimu ya vitendo katika shule zetu za msingi na sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, ukimfundisha mwanafunzi mapishi ya keki kwa nadhari na baadaye ukaweza kumuonyesha namna ya keki hiyo inavyopikwa ataelewa zaidi. Kusoma kwa nadharia tu ni sawa na kuwa-*feed* wanafunzi kitu ambacho hawana *reference* nacho. Hivyo basi, ningeomba sana elimu ya vitendo ilirudishwe kama zamani ilivyokuwa ikifundishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo linachangia elimu yetu kuendelea kuwa duni ni kukosekana kwa uwiano kati ya mwalimu na wanafunzi darasani katika shule zetu wanafunzi katika darasa moja wanaweza kufikia idadi ya wanafunzi 35 mpaka 50, idadi hii inamuwia mwalimu ugumu kuweza kufanya *assessment* kwa kila mwanafunzi. Matokeo yake anaangalia tatizo la mwanafunzi mmoja na kulitolea suluhu kwa wanafunzi wote darasani. Tofauti ya darasa lenye wanafunzi kumi mpaka kumi tano, ni rahisi mwalimu *assessment* ya kila mwanafunzi na kujua wana tatizo gani pindi atakapomaliza kufundisha na kuona namna gani ya kuwasaidia hao wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutomuandaa mwalimu vema ili afundishe kuendana na wakati wa sasa nayo ni sababu inayochangia kuporomoka kwa elimu yetu. Ajira ya ualimu imewekwa katika kundi la kitu ambacho hakina thamani. Leo hii wanaochukuliwa kujiunga na ajira hii ni wahitimu waliopata daraja la nne katika kidato cha nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine maslahi ya walimu ni duni. Mwalimu kwa kweli hawamjali mwalimu, mwalimu huyu hana nyumba ya kuishi, anaishi katika mazingira duni, mshahara wake ni mdogo na wala haumkidhi mahitaji yake na wakati mwingine haufiki kwa wakati. Ningeiomba Serikali yangu kuwaangalia walimu na kuangalia maslahi yao upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unategemea nini kwa mwalimu kama huyo na atakuwa kweli na morali ya kufundisha si ata-*beep* tu kutimiza wajibu wake na

kuondoka zake. Ndiyo maana kiwango cha elimu kimeendelea kushuka kutoka asilimia 22.3 mwaka 1985 na kufikia asilimia 49.6 mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali kuja na mpango utakaowawezesha walimu kupata *training* za mara kwa mara na semina zinazolenga mahitaji ya sasa ili kuwawezesha kufundisha kwa ufanisi na ufasaha katika dhama hizi za sayansi na teknolojia. Lakini pia vilevile walimu watakaokuwa wamejiendeleza wapewe *incentives* kulingana na madaraja yao, hii itasaidia sana kupunguza madai ya uhamisho ya mara kwa mara na kuwafanya walimu watulie katika maeneo yao ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba katika shule zetu za Serikali hatuna programu za kuhamasisha watoto wapende kusoma vitabu, wanafunzi wetu hawana tabia ya kujisomea vitabu, lakini pia vitabu vyenyewe hakuna vya kutosha. Serikali ione umuhimu wa kuanzisha programu au iwena *slogan* maalum ambayo itawahamasisha wanafunzi wetu na katika kila mkoa uwe na *e-library* ambayo wanafunzi watapata ku-*access* vitabu mbalimbali zikiwemo *story books* ambazo zitaweza kuwasaidia katika ku-*improve english language* ambayo ni *medium of instruction in secondary schools.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida ni miongoni mwa mikoa yenye changamoto nyingi katika sekta ya elimu. Mkoa wa Singida una jumla ya shule 542, kwa wastani kwa mwaka watoto 25,000 humaliza shule ya msingi ukilinganisha na ufaulisha watoto 13,383 kwa mkoa mzima. Ukilinganisha idadi hii ya wananfunzi waliomaliza shule za msingi hailingani kabisa na wale wanaondelea na masomo ya shule za sekondari. Zaidi ya vijana 10,000 wanakaa mitaani… *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Gama, ajiandae Mheshimiwa Tunza Issa Malapo.

MHE. LEONIDAS T. GAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba nichukue nafasi hii kama walivyofanya wenzangu nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na uwasilishaji wake mzuri. Mimi nilikuwa na tatizo moja ambalo niliomba Serikali iangalie kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vyuo vilivyofungwa ni pamoja na chuo changu cha *St. Joseph,* Songea ambacho kilikuwa na maeneo mawili; eneo la kwanza ni eneo la *campus* ya kilimo na eneo la pili ni *campus* ya teknolojia. Hiki chuo kimefungwa, lakini sina tatizo na sababu za msingi ila nilichokuwa nakiona ni kwamba uamuzi huu umechukuliwa mkubwa mno, haulingani na mazingira halisi, sisi sote tunataka vijana wetu wapate elimu na kwa sisi Songea kile chuo cha *St. Joseph* ndio chuo kikuu pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo zipo sababu za msingi zilizosemwa na kubaliana nazo lakini vilevile ningeomba nishauri, kwa mfano suala la udahili wa wanafunzi ambao hawajafikia viwango, Mheshimiwa Waziri ametuambia hapa kwamba vijana 424 wamefutiwa udahili wao. Lakini hawa vijana 424 ni kati ya vijana 3,585. Ukiangalia takwimu hizi maana yake waliokiuka taratibu ni asilimia 11.8; kwa hiyo vijana asilimia 88.2 hawana tatizo lolote. Kwa hiyo, haiwezi kufika mahali hiyo ikawa moja ya sababu ya kufunga vyuo au kuvifuta vyuo. Ukiangalia sababu hizi sio sababu zinazotokana na vijana ni sababu zinazotokana na utawala wa chuo, utawala wa uongozi wa *TCU* na viongozi wengine wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo huwezi ukafika mahali makosa ya kiwizara yakaenda kutoa adhabu kwa chuo ambacho chenyewe kilikuwa haina kosa. Lakini yako matatizo ambayo yamesemwa kutokana na vyuo hivi na hasa chuo changu; matatizo ya uongozi, matatizo ya utawala na matatizo ya kitaaluma. Sitaki kubishana na Mheshimiwa Waziri ni kweli makosa hayo yanajitokeza lakini ufumbuzi wa makosa hayo sio kufuta chuo, ufumbuzi wa makosa hayo ni pale ambapo una kitaka chuo au taratibu zilizokosewa ziweze kurekebishwa. Na kama kurekebishwa hakuwezekani zipo taratibu za kudhibiti uongozi uliopo; lakini sasa ukiangalia uamuzi wetu wa kufuta hivi vyuo umekuja kuwahukumu moja kwa moja wahusika kwenye vyuo ambao ni wanafunzi wetu na utawala kwa ujumla wa chuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikwambie kwamba siku zote wanasema ukiwa na mtoto umemuogesha kwenye dishi (beseni), maji yakichafuka unachofanya ni kuyatupa maji, huwezi kuondoa dishi na mtoto ukaenda kuwamwaga kwa sababu maji yamechafuka, huo sio utaratibu.

Kwa hiyo, kama makosa yalifanywa na uongozi na kama makosa yalifanywa na Wizara yenyewe kwa kutumia vyombo vyake kule kilichotakiwa ni kuona namna gani tunaadhibu wale waliohusika na wala sio vijana waliokuwa wanasoma au utawala wa chuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi taratibu zilizotumika kukifuta kile chuo maana kimefutwa, sio kimefungwa, kimefutwa usajili wake, hati yake ya kuongoza kile chuo imefutwa rasmi. Kwa hiyo, uaratibu uliotumika katika kukifuta chuo hiko haukuwa sahihi na kuna sababu kadhaa. Kwanza uamuzi wenyewe wa kukifuta chuo ni wa ghafla mno haukuwa na taarifa yoyote, *notice* yoyote ya kuwajulisha kwamba baada ya hapa tunafuta chuo, ni uamuzi ambao umetokana na taarifa walizozipokea, wakaamua hata uongozi umepata taarifa za kufutwa chuo kutokana na vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, tumewaadhibu watu wengine ambao hawana hatia, kulikuwa na wanachuo kutoka makundi mbalimbali,

tumeamua kuwahamishia vyuo vingine, lakini kuna watu walikuwa wanasoma kama *part time* pale anatoka kazini anakwenda kufanya masomo, kwa hiyo maana yake kumuhamishia maeneo mengine kwanza unamuingiza kwenye migogoro ya kulipa ada, vilevile unamuingiza kwenye migogoro ya kiutumishi kati yake yeye na ofisi yake.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri maeneo hayo yote yangeangaliwa kabla ya kutoa uamuzi huo. Athari yake ni nini? Kwanza sisi wenyewe kama Kanda ya Kusini tumeathirika sana, tumeathirika sisi kama Mkoa wa Kusini lakini vilevile na wanafunzi hawa wameathirika sana kisaikolojia, kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, matokeo yake huwezi ukategemea vijana hawa wanakohamishiwa wakaenda kufanya vizuri katika taratibu zao za kimasomo kwa sababu athari hiyo imekuwa kubwa sana na imewaumiza sana vijana wale. Lakini vilevile kimkoa sisi tumekosa mambo mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chuo hiki pamoja na shughuli nyingine walizokuwa wanafanya, lakini vijana hawa ndio walikuwa wakiwa kwenye *field* wanakwenda kwenye taasisi zetu mbalimbali za kielimu; walikuwa wanajitolea kwenye vyuo, wanajitolea kwenye shule, wanafanya tafiti mbalimbali ambazo zilisaidia kuwezesha mkoa kuinua kiuchumi.

Lakini sio hilo tu, hata hali ya kiuchumi ya wananchi katika maeneo yale ilikua kutokana na kuwepo kwa chuo hiki, wananchi wengi walifanya shughuli zao, wananchi wengi walijenga nyumba mbalimbali ambazo kuwepo kwa wanachuo hawa kulisaidia sana kuinua uchumi wa wananchi na kusababisha mzunguko wa fedha kwa jamii ya Songea Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, athari hizi zimetukuta wote, kwa hiyo tunaomba Serikali kwa sababu mmeshatoa adhabu kwa *TCU,* nilikuwa naiomba Serikali ione uwezekano wa kuamua kukirudisha chuo hiki cha Songea pamoja na masharti ambayo mnaona yatafaa ili waweze kuyarekebisha. Lakini kukifuta moja kwa moja naona sio sahihi na haitakuwa kuwatendea haki wanafunzi na ndugu zetu wa Songea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tuna maswali ambayo tunajiuliza, je, kwa nini *TCU* iliamua kutokutoa notice kwa chuo? Lakini la pili kwa nini *TCU* haikutoa muda na nafasi ya chuo kufanya marekebisho yale ambayo waliyapata?

Vilevile tunajiuliza je, kwani Serikali haina namna bora nyingine ya ufungaji wa chuo lazima kukifunga chuo kwa *ambush* maana kimefungwa kile chuo utafikiri tupo jeshini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri tuangalie. Lakini vilevile tunajiuliza sana sisi Songea kwamba kile chuo kilichokuwa na matatizo kwa mujibu wa maelezo ya Wizara na *TCU*, ni kile chuo cha *campus* ya kilimo lakini chuo cha TEHAMA hakikukuwa na tatizo, kwa nini katika kufuta vimefutwa vyuo vyote viwili wakati *campus* ya TEHAMA haikuwa na matatizo.

Kwa hiyo, nilitaka niiombe Serikali yangu tukufu ione utaratibu wa kufanya ukaguzi, kutoa ushauri, kutoa maelekezo ili ifike mahali yale ya msingi yaweze kuondolewa na wakati huo huo kutoa haki kwa kile chuo kiweze kuanza tena usaili ili kuwarudisha wanafunzi katika chuo kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya uongozi wa chuo kile na kwa niaba ya uongozi wa Songea kwa ujumla tupo tayari kupokea. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, ajiandae Mheshimiwa Juma Kombo Hamadi.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika Wizara hii ya Elimu, mimi nitajikita zaidi kwenye vyuo vya ualimu kwa sababu nina *experience* huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vya ualimu wamebadilisha mtaala kwa mfano chuo ambacho kilikuwa kinafundisha *diploma* ya ualimu wa ngazi ya sekondari unakuta sasa hivi kimepangiwa *diploma* katika ngazi ya elimu ya awali. Mtaala huo umebadilishwa sijui kwa vigezo vipi, sijui kwa tafiti zipi sasa mbaya zaidi mtaala umebadilishwa, wakufunzi hawajui nini wanachotakiwa kufundisha, mtu anapewa kozi pale mwezi mmoja ama miwili unatafuta *material* hujui uanzie wapi, hakuna kitabu, hakuna rejea na kama rejea zipo zimeandikwa kwa lugha ya kiingereza lakini wale watoto tunatakiwa tufundishe kwa lugha ya kiswahili; shida sio kutafsiri lakini ipi ni tafsiri sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukichezea elimu utafikiri ni kitu ambacho hakina msingi. Sera ya Elimu inasema elimu bure, Sera ya mwaka 2014 tumekubali elimu bure maana yake ni nini? Serikali inajinasibu wanafunzi wengi wanasajiliwa shuleni, shule za msingi lakini nataka niwaambie jambo la kusikitisha Mheshimiwa Ndalichako pita kwenye vyuo vya ualimu, nenda kaangalie *capacity* ya chuo ni wanafunzi 450 unakuta waliosajiliwa ni wanachuo 50; maana yake ni nini? Baada ya muda wanafunzi wale wa shule za msingi wataongezeka kuwa wengi lakini walimu hakuna, tunatengeneza kitu gani? Tusifanye vitu kwa siasa wakati tunaongezea wanafunzi pia tuhakikishe walimu idadi yao inaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naongea kwa ushahidi nenda Chuo cha Ualimu Mtwara Kawaida kaangalie *capacity* ya chuo na kaangalie wanafunzi

ambao wapo chuoni, lakini unakuta pale kuna walimu wengi wapo tunasema *misuse of resources.(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaitwa Wizara ya Elimu, Teknolojia na huko inaendelea. Jambo la kusikitisha sana tunapoenda kwenye vyuo vya ualimu mtandao wa *internet* hakuna wa uhakika, maana yake mwalimu huyo hana vitabu vya uhakika, mtandao wa *internet* hakuna na kulikuwepo na programu inaitwa *ICT implementation in teacher education*.

Mheshimiwa Waziri unapokuja kuhitimisha naomba nipate ufafanuzi programu ile imefikia wapi, ukienda kwenye vyuo vya ualimu utakuta kuna kompyuta nyingi ni mbovu, mtandao wa *internet* hakuna kabisa, naongea kwa ushahidi, walimu wale mnataka wafanye kitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia elimu hatuwezi kumuacha mwalimu. Wakufunzi wa vyuo vya ualimu na vyuo vya ualimu kwa ujumla wake vimeingia kwenye mfumo wa *NACTE* ingawa mimi sijui na sioni utekelezaji wake, lakini mfumo ule wa *NACTE* una stahiki zake lakini mpaka leo tunapoongea baadhi ya wakufunzi wa vyuo vya ualimu wanalipwa kwa stahiki za Wizara ya Elimu, wanafanya kazi mpaka muda wa ziada kwa sababu ule mfumo una mambo yake, mwisho wa siku mtu analipwa kama bado anahudumiwa na Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunataka ufafanuzi wale watu wapo katika mlengo gani, kama mmeamua kuwapeleka *NACTE* wapelekeni *NACTE* na stahiki zao zote na kama mnaamua wabakie Wizara ya Elimu basi wabakie na stahiki zao zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza vyuo vya ualimu ni vichache siji tatizo ni nini, mnashindwa kukaa mkajua mahitaji ya wakufunzi mnashindwa kuboresha miundombinu, ukienda kwenye Chuo cha Ualimu Mtwara Kawaida nakiongelea kwa *experience*, mabwenini kule hali ni mbaya, unamfundisha nini mwalimu? Hali ni mbaya, miundombinu mibovu, madarasa yapo hayaeleweki yaani ule utanashati wa mwalimu unapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atueleze kwenye vyuo vyote vya ualimu kulikuwa na shule za mazoezi, shule ya msingi ya mazoezi na shule ya sekondari ya mazoezi, lakini zile shule zote sasa hivi zimerudi TAMISEMI. Sasa naomba kupata ufafanuzi kila kitu ambacho kilifanya muanzishe shule shule za mazoezi ambazo sisi tuliokuwa tunafundisha kule tuliona umuhimu wake kwa nini sasa hivi shule hizo zimerudishwa kupelekwa TAMISEMI?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ule umuhimu umepotea ama kuna kuna kitu gani hapo kilichopo katikati? Tunaomba ufafanuzi kwa sababu mwenyewe nimesoma shule ya mazoezi ya msingi na katika miongoni mwa shule ambazo zilikuwa zinafanya vizuri ni shule za mazoezi na pia wale wanachuo wa ualimu walikuwa wanaenda kufanya *practice* kwenye shule za mazoezi. Lakini sasa hivi, ukitaka kuitumia ile shule ni lazima uende ukaombe kibali TAMISEMI na vitu kama hivyo, kwa hiyo kuna mzunguko mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo. Mheshimiwa Waziri juzi nimekuona ukiitumbua *TCU,* mimi nasema umechelewa sana kwasababu malalamiko yalikuwa mengi ya muda mrefu. Watoto wa maskini ambao wana stahiki ya kupata mikopo hawapati, watu wanapeana mikopo kwa kujuana, tunaomba hilo suala ulifuatilie na wale wote waliohusika wawajibike na wale ambao walishindwa kusoma kwa sababu ya mikopo na sifa wanazo tunaomba wasome kwa sababu ni haki yao ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenzangu asubuhi hapa ametoka kuongea, kuna vyuo vinafundisha masomo ya sayansi lakini havina maabara, Vyuo vya Ualimu. Tunategemea tunazalisha watu wa namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo mwalimu leo unamfundisha kwa *alternative to practical*, unataka akifika shuleni umejenga maabara kwa kuwakimbiza wazazi, kwa michango mbalimbali, unataka akafundishe *real practical, is it possible? If it is not possible we should be more serious* ili elimu yetu tuione inapaa.

Mimi kila siku nasema masomo ya sayansi sio magumu ila mfumo wa elimu ya Tanzania ndio unapelekea masomo ya sayansi yawe magumu, masomo ya sayansi *is very simple,* ukipata mazingira wezeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaeongea hapa nimesoma *PCB* na nimefaulu kwani hao wanaofeli wamekosa kitu gani? Ni mfumo mbovu, mazingira mabovu, tunatakiwa tuone namna ya kuweka miundombinu yetu vizuri ili watoto wetu wasome kila mtu ana uwezo wa kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti …

MWENYEKITI: Ahsante

MHE. TUNZA I. MALAPO: Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni jioni hii nawatangaza mapema kwa sababu ni timu za mipira za *NMB* na wanahitaji

kwenda kufanya mazoezi wasilalamike kuwa tunawafanyia makusudi ili wafungwe kesho. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wafanyakazi 39 wa *NMB* ambao watashiriki mchezo wa kesho na timu ya Bunge, wafanyakazi hao ni timu ya mpira ya miguu wakiongozwa na ndugu Staton Chilongo, timu ya mpira wa pete ikiongozwa na Josephine Kulwa pamoja na Joseline Kamuhanda, ahsante. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Halima Mdee ambao ni wawakilishi wa *Makongo Hill Society* ndugu Martin Mosha na ndugu Peter Mtungi. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Zacharia Paul Isaya ambao ni watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, ahsanteni. *(Makofi)*

Sasa namuita Mheshimiwa Kombo na Mheshimiwa Zitto jiandae.

MHE. JUMA KOMBO HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema mchana huu na kupata fursa hii ya kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara muhimu, Wizara ya ELimu.

Pili kwa sababu ni mara ya mwanzo kabisa nichukue fursa hii pia kuwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Wingwi kwa kunipatia ushindi mkubwa wa asilimia 90 dhidi ya mgombea mwenzangu. Pia nikishukuru chama changu, Chama cha Wananchi (CUF) kwa kuniamini kabisa na kunipa fursa hii, nakiahidi kwamba sitakiangusha, nitakitumikia kwa nguvu zangu zote kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nianze kwa kusema kwamba ili tufanikiwe na ili tuendelee tunahitaji tuwekeze kwenye suala zima la elimu. Kinachoonekana hapa bado kama vile hatujakuwa tayari kuwekeza katika suala zima la elimu. Kinachoonekana hapa ni kama vile tunakuja kutaniana, kwa sababu kile ambacho kimezungumzwa mwaka wa jana, kile ambacho kimezungumzwa mwaka wa juzi ndicho kile kile kinachopigiwa kelele, hakiongezeki wala hakipungui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambayo ili zungumzwa mwaka wa jana tulipaswa leo tuje tuione angalau imetatuliwa kiasi fulani ili tuondoke pale tulipokuwa mwaka wa jana na sasa tuzungumzie kitu kingine. Lakini hadi sasa wenzangu wengi wamezungumza hapa, tunapiga kelele kwa matundu ya vyoo, tunapiga kelele ukosefu wa madawati na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninamuomba Mheshimiwa Waziri, kwa nia njema kabisa, hebu fuatilia zile hotuba mbili, hotuba ya Kambi ya Upinzani

pamoja na hotuba ya Kamati. Kama utazifuata vizuri basi zimetoa mwanga mzuri wa kukuongoza kufikia kule Watanzania tunakokuhitaji. Na wala sioni sababu ya kwamba usifuate mawazo yale ya vitabu vile viwili, ni vitabu ambavyo vimezungumza vizuri, vimetoa mapendekezo mazuri, vimetoa maelekezo mazuri ambayo yatatutoa hapa tulipo na kuelekea pale tunapopahitaji.

Ninakuomba sana mama yangu, kwamba kwa hili bora tu ulifuate ili maelekezo yale ukichanganya na uliyo nayo wewe mwenyewe basi utapata kitu cha kushika na mwakani utatueleza kitu kipya kabisa hapa kwenye Bunge lako hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uwekezaji huu yamezungumzwa mengi, lakini lazima tukubali kugharamia, lazima tukubali kuchagua vijana tuwapeleke wakasomee taaluma mbalimbali ili waje waisaidie Tanzania; nchi nyingi zimefanya hivyo. Hata China pale ilipo leo kwanza ilianza zaidi miaka kumi kula hasara kwenda kuwasomesha vijana nje ya nchi kusoma kwa ajili ya taaluma fulani ili kwenda kuisaidia nchi yao. Sasa na sisi si aibu wala si fedheha.

Leo kuna mtu alitoa mfano hapa, mpaka leo tunategemea marubani, tunagemea ma-*captain* wa meli zile ambazo ziko hapa ndani ya nchi yetu ukienda pale unawakuta wote ni wageni. Kwa nini tusiende tukasomeshe wakwetu? Hivi kuna ugumu gani kuwa rubani? Hivi kuna ugumu gani kuwa *captain* wa meli? Hivi kuna ugumu gani kuwa meneja wa kiwanda fulani au mtandao fulani ambaye huyu atakuwa ni mzalendo wa nchi yetu? Naomba kumshauri Mheshimiwa Waziri afuate yale mawazo, naamini atatukwamua katika hatua hii na tutakwenda katika hatua nyingine nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo ninaomba kulizungumzia hapa ni suala la mikopo. Suala la mikopo limekuwa na malalamiko makubwa na ya muda mrefu hasa kwa upande wa Zanzibar. Mimi nikuombe kitu kimoja katika hili, nikuombe wakati utakapokuja, au ujiandae kuanzia sasa, kama utakuwa hujajiandaa basi ujiandae vizuri ili kuwe na utaratibu maalum wa utoaji wa mikopo. Suala la elimu ya juu, suala la Bodi ya Mikopo ni suala la Muungano, Wazanzibari wanahusika katika suala hili, hawapaswi kama vile kuchotewa, kama vile ni waalikwa. Zanzibar si mualikwa katika ile Bodi ya Mikopo, Zanzibar ni mshirika kwa sababu suala la elimu ya juu Kikatiba, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni suala la Muungano.

Sasa mimi nikuombe tu kwamba uandae utaratibu mzuri, wakati unakwenda kufanya udahili unatuletea hapa bajeti, unaisoma bajeti. Ukionesha kwamba fungu hili ndilo la mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu utuambie basi katika fungu hili kiasi hiki ndicho kinachokwenda kwa wanafunzi

watakaodahiliwa watokao Zanzibar. Sioni kama kuna dhambi, sioni kama kuna tatizo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba sana Mheshimiwa Waziri sana kwamba hili ulifanye ili kuondoa haya malalamiko ya muda mrefu. Utakapotuambia, pengine fungu la mikopo lina milioni 40, lakini hizi Shilingi 200,000 zitakwenda kwa wanafunzi wa Zanzibar, wewe utakuwa umejiondoa kwenye malalamiko, na umeitoa wizara kwenye malalamiko. Tutajua tuna wanafunzi wangapi kutoka Zanzibar ambao watapata mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Tanzania.Nitakuomba sana hili ulichukue, ulifikirie na ulipatie maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ambalo ninaomba kulizungumzia hapa ni suala la uwekezaji hasa katika vyuo vikuu. Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu, na Serikali hapa ilifanya jambo kubwa na lenye nia njema kabisa. Suala la uanzishwaji wa sekondari katika kila kata lilikuwa ni suala muhimu, limetekelezwa na Serikali kwa kiasi fulani, hivyo hivyo, lakini lipo na limetekelezwa. Sasa, kuna ukanda huu wa Kusini, baada ya kuanzishwa sekondari hizi za kata imepelekea wanafunzi wengi kujiunga na sekondari za *O-Level* na *A-Level*. Udahili wa wanafunzi kwenda vyuo vikuu umeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini miaka mingi mmekuwa mkisema Chuo cha Ualimu kilichoko Mtwara mtakigeuza kiwe Chuo Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mpaka leo suala hili halijachukuliwa hatua yoyote. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri, kwa heshima zote mama yangu Ndalichako ukija hapa utueleze, kile chuo ni lini kitachukuliwa hatua ya kugeuzwa sasa kuwa Chuo cha Ualimu na sasa kiende kwenye kuwa chuo kishiriki kisaidie ule ukanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mikoa mitatu, Lindi, Mtwara na Ruvuma, huu ni ukanda mmoja, mikoa hii imefuatana kabisa, lakini hakuna hata chuo kikuu kimoja cha Serikali. Tunakuomba sana suala hili lichukuliwe hatua na ni vyema utakapokuja hapa sasa utuambie ni lini suala hili litachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema kwamba hakuna elimu bora bila huduma bora za walimu. Muda umefika sasa kuwaonea huruma walimu, wamehangaika muda mrefu sana. Imefika muda sasa kuboresha maslahi ya walimu katika nyanja zote, ukae pamoja na TAMISEMI uboreshe, uone kwa namna gani mtashirikiana kuikwamua kada hii ya walimu katika sekta au katika maslahi ya walimu. Walimu hawa ni wetu, ni Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wamekuwa wakisema, hata wewe leo usingekuwa Waziri wa Elimu kama hujapitia kwa walimu. Ulianza darasa la

kwanza mpaka ulipofika, waliokuwezesha hapo ni walimu. Hebu wahurumie walimu, waonee huruma walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba mchango wangu kwa leo uwe huo, ninaamini kwamba mawazo yangu haya yatasaidia kwa namna moja ama nyingine kufikia pale tunapopahitaji, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Zitto, ajiandae Mheshimiwa Omary Mgumba na Mheshimiwa Profesa Tibaijuka.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ninashukuru kwa kupata fursa ya kutoa mchango wangu kidogo katika makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara muhimu kabisa katika nchi na nchi yoyote ile duniani. Ukitazama kipimo cha maendeleo *(Human Development Index)* theluthi mbili zinachukuliwa na elimu na afya (afya theluthi moja, elimu theluthi moja).

Kwa hiyo, tukiweza kutatua matatizo haya mawili, afya na elimu, maana yake ni kwamba tunakuwa tumetatua theluthi mbili ya changamoto zetu za maendeleo katika nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wenzangu wazungumzia falsafa tuliyokuwa nayo, falsafa ya elimu ya kujitegemea na mimi swali ambalo ninapenda tujiulize sisi kama nchi, falsafa yetu ya elimu sasa ni nini? Tunataka tuzalishe watoto wa namna gani? Tunataka tujenge Taifa la namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunazungumzia viwanda, lakini tunajua hali yetu ya elimu ilivyo. Watoto ambao tunawazalisha sasa wataendana na Tanzania ya viwanda ambayo tunataka kuijenga? Haya ni maswali ambayo tusipopata majibu yake humu Bungeni kwa miaka mitano tutakuwa tunakuja, tunazungumza, tunapitisha bajeti, tunaondoka hali inabaki ni ile ile. Kwa sababu kelele hizi ambazo zinasikia leo na jana ni kelele ambazo zimepigwa sana huko nyuma. Iliwahi kufikia nchi hii asilimia 20 ya bajeti ilikwenda kwenye elimu, mwaka 2008. Lakini ukiangalia uwekezaji tulioufanya kwenye elimu na ubora ambao tunaupata kwenye elimu haviendani kabisa. Na hapo ndipo ambapo tunapaswa kuangalia ni namna gani ambavyo tunafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya kujitegemea ilitaka kujenga taifa kujenga Taifa moja. Elimu ya sasa tunataka kujenga nini? Haya ni mambo ambayo ni lazima tujiulize kama nchi na tuyapatie majawabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunavyozungumza katika watoto ambao wanamaliza darasa la saba asilimia 50 walipofanyiwa utafiti, *50 percent* walikuwa hawawezi kupiga hesabu ya sita jumlisha tatu. *50 percent*

walishindwa kupiga hesabu ya saba mara nane. Na haya si maneno yangu, ni utafiti ambao umefanywa na vyombo mbalimbali. *(Makofi)*

Kwa hiyo tuna tatizo kubwa kwamba siku zote tunaangalia *inputs.* Bajeti, majengo, *enrolments*, hatuangalii *outcomes* ni nini. Na kwa hiyo ningemshauri Mheshimiwa Waziri kwamba sasa hivi tuanze kuji-*focus*, na si Waziri peke yake, sisi viongozi, wazazi na kadhalika tu-*focus* tuangalie kwenye matokeo ya elimu. Watoto wetu hawasomi, lakini si hivyo tu, walimu pia hawafundishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Benki ya Dunia na *REPOA* wametoa taarifa inaitwa *Social Delivery Indicators.* Inaonesha kwamba ukienda ghafla kwenye shule zetu bila kutoa taarifa, *the so called* ziara za kushtukiza asilimia 49 ya walimu hawapo shuleni kabisa. Kwa hiyo, tunapozungumza tunataka tuwekeze kufanya walimu wawe *motivated,* wawe na hamasa wafanye kazi, tuwalipe vizuri lazima pia tuwaambie walimu wawajibike kufundisha watoto wetu. Kwa sababu takwimu zetu ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo nusu ya walimu hawaingii darasani maana yake ni kwamba hiyo inayoitwa mishahara hewa hii ndiyo mishahara hewa kweli kweli, kwa sababu nusu ya walimu hawafundishi, maana yake mishahara ambayo tunailipa, tunailipa bila watu kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri, kwanza *salary scale* ya walimu tuibadilishe. *Salary scale* ya walimu tuiweke sawa sawa na angalau nusu ya *salary scale* ya Wabunge. Na tusim-*judge* mwalimu kwamba huyu anafundisha *primary,* huyu anafundisha sekondari, huyu anafundisha chuo kikuu, walmu wote *salary scales* zao zifanane, mishahara yao itofautiane kulingana na muda ambao wamefundisha na kulingana na kiwango cha elimu ambacho wanacho. Kwa maana hiyo ni kwamba tutakuwa tuna walimu wazuri, *dedicated,* ambao wanaanzia chini kabisa kwenda mpaka ngazi ya juu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vikuu vyetu ndiko hali mbaya kabisa. Juzi kuna taarifa imetoka inaonesha kwamba kuna vyuo vikuu bora 30 Afrika, Tanzania hatumo. Hata Makerere na Nairobi ambao tulikuwa tunawazidi sasa hivi wanatuzidi. Lakini hii inatokana na nini? Ni kwa sababu ukiangalia bajeti ya elimu, hivi vitabu vya bajeti ya elimu tukivishika utaona *development budget* kubwa sana, zaidi ya shilingi bilioni 500, lakini *80 percent of that* ni mikopo. *It is distorting* na ndiyo maana Kamati imependekeza kwamba fedha za mikopo ya wanafunzi zitoke hazina ziende Bodi ya Mikopo moja kwa moja, zisipite kwenye vitabu vya Wizara kwa sababu inaonekana vibaya, bajeti inaonekana ni kubwa wakati haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu nchi kama hii *0.001 percent* ya bajeti yetu ndiyo inakwenda kwenye *research and development*, vyuo vikuu vinafanya kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna *commitment* ambayo tumeweka, kuna *commitment* kwenye *Five Years Development Plan*, kuna *commitment* za matamko ya viongozi kwamba tutaweka asilimia moja ya Pato la Taifa kwenye *research and development,* kwa nini hatufanyi? Vyuo vikuu vyetu haviwezi kufanya *research and development*. Nilikuwa naomba nisisitize hili, na niwaombe Waheshimiwa Wabunge. Takwimu za *GDP* tunazijua. Waziri wa Fedha anaweza akatuambia *GDP* ya sasa hivi ni ngapi. Tuangalie bajeti. Leo hii tunatenga 500 *billion* kwenda kununua ndege, *500 billion*, *500 billion* kwenda kununua ndege, atakayerusha hizo ndege ni nani? Atakayezitengeneza hizo ndege ni nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *one percent* ya *GDP* ni bilioni *59* tu. Tunyofoe kule, tuwaombe watu wa Kamati ya Bajeti wakae tunyofoe kule, tuweke kwa ajili ya *reseach and development*, watu wetu wafanye kazi ya utafiti tuweze kuzalisha na tuweze kuitengeneza nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia kwenye ufundi. Na Wabunge wengi wamezungumza hili. Kwa hiyo ni *consensus*, lakini nimeangalia bajeti hapa, tunazungumza kuhusu *VETA* kila Wilaya, tunazungumza kuhusu vyuo vya ufundi katika Mikoa, bajeti ha-*reflect*. Bajeti yetu hai-*reflect* hizi *VETA* tunazozitaka. Lakini tuna zaidi ya *50 percent* ya watoto ambao wanamaliza kidato cha nne hawaendelei na elimu ya juu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa naomba tuwekeze kwenye *VETA*, tuwekeze kwenye vyuo vya ufundi mchundo na mimi hapa ninakuja kuomba ombi langu rasmi Mheshimiwa Waziri, naomba Chuo cha Ufundi Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma ni lango la Magharibi la nchi hii, Kigoma ndiyo *center* ya nchi zote za Maziwa Makuu. Ukitaka kufundisha watu utengenezaji wa boti *Kigoma fits*, ukitaka kufundisha watu *maritine Kigoma fits*, ukitaka kufundisha watu namna ya kuvua kisasa *Kigoma fits*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri katika mipango ambayo tunakwenda kuifanya kwa ajili ya kufungua vyuo vya ufundi yva kutosha tupate chuo cha ufundi pale ili tuweze kusaidia, kama jinsi ambavyo wengine wameweza kuomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba kusisitiza kwamba tuwekeze kwenye matokeo, tuangalie namna gani ya kuboresha watoto wetu waweze kusoma. Watoto wetu hawasomi.

Naomba tuji-*focus* huko, tuondokane na *inputs*, tumeshawekeza sana kwenye *inputs*, tumeshawekeza sana huko, naomba sasa hivi tujikite sasa hivi kwenye *outcomes* na ili tuwe na *outcomes* nzuri ni lazima tuwe na mwalimu ambaye yuko *motivated*, na ni lazima tuwe na mwalimu ambaye yuko *accountable*, nashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mgumba, ajiandae Profesa Tibaijuka.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nitoe mchango wangu katika Wizara hii ya Elimu.

Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa nafasi hiyo aliyokuwa nayo. Kama ni mchezaji huyu ni wa kulipwa. Kwa sababu wachezaji *local* tulikuwepo Wabunge wa CCM wengi lakini kwa mamlaka yake Mheshimiwa Rais alisajili wachezaji wa kulipwa, wewe ni mmojawapo na alikupeleka katika Wizara hii si kwa bahati mbaya. Mimi nasema kama ni upele umepata mwenye kucha, hongera sana mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite kwenye mchango wangu ingawa wenzangu wengi wamesema lakini na mimi nirudie tu, hasa kwenye ubora wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamesemwa, ukiangalia na *records* za nyuma bajeti ya elimu inaongezeka mwaka hadi mwaka, miundombinu inajengwa tukiwashirikisha wazazi, wananchi kwa mfumo uliopo sasa hivi wa *D by D,* walimu wanaongezeka, Serikali inajitahidi kuajiri walimu wengi na wanafunzi pia wameongezeka, kwa maana hata mwaka huu baada ya elimu bure tumeona wameongezeka wengi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa, *output* ya elimu na kiwango cha elimu kila siku kinashuka! Sasa ni suala la kujiuliza, kama vitu vyote hivi vinaongezeka, pesa zinaongezeka, madarasa yanaongezeka, vitabu vinaongezeka, lakini elimu inarudi nyuma; tatizo tumejikwaa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni shahidi; yeye mwenyewe amesema kwamba, yeye ni zao la shule za Serikali, *Tabora Girls* na ametokea huko. Jambo moja tu, hata yeye mwenyewe akienda *Tabora Girls* leo, ile aliyosoma yeye. Ndiyo leo inafanana na *Tabora Girls?* Elimu aliyopata pale *Tabora Girls*, ndiyo ile inayotolewa pale leo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana mwanzo nimesema, upele umempata mwenye kucha kwa sababu umepata elimu bora na kupitia Serikali hiyo hiyo, sasa umepewa jukumu la kusimamia Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa kabisa ambalo naliona kwa upeo wangu; moja ni kukosa uzalendo na kuzipenda shule hizi hasa kwa sisi viongozi. Nasema hili kwa sababu tulikuwa na Serikali yetu ya CCM ya Awamu ya Kwanza, tulikuwa na Awamu ya Pili na Awamu ya Tatu. Wengine sisi tulianza Awamu ya Pili mpaka ya Tatu, tulikuwa tunasoma huko na watoto wa viongozi. Wote! Yaani mtu akichaguliwa kwenda Shule ya Sekondari ya Serikali ni sherehe kijijini au kwenye familia. Leo hii mtu akichaguliwa kwenda Shule ya Sekondari ya Serikali, ni kilio! Anaambiwa mwanangu nitakutafutia *Private* uende. Tena mbaya zaidi, hata viongozi wenyewe waliokuwa hata Serikalini, watoto wao wanaosomesha kwenye Shule za Serikali wanahesabika! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unategemea nini kama wewe mwenye jukumu la kusimamia na kuboresha hiyo elimu, watoto wako wote hawasomi pale? Wanasoma Ulaya na shule zile ambazo ni za *private*, zinatoa elimu bora. Kwa hiyo, wewe mwenyewe kiongozi unakubali kwamba zile shule zetu za Serikali hazitoi elimu bora. Sasa nawaomba, ili tuweze kuziboresha kwa ukweli hizi shule, kwanza sisi viongozi turudishe watoto huko; kwa sababu tunajifahamu, hata kule vijijini kwetu, ukisikia kesho mwenge unakuja, ndiyo barabara inachongwa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kurudisha watoto wetu waende huko, hata Walimu, kwa sababu utakuwa unapata mrejesho kama kiongozi au Waziri, kila mtoto anapokuja kama anapata elimu bora au sivyo. Hata wale Walimu wa kule lazima wataboresha mazingira ya elimu kwa sababu wanajua mkubwa atafahamu. Kwa hiyo, ukosefu wa ubora wa elimu, *output* tunapata ndogo ni kutokana na sisi wenyewe dhambi hii tumeibeba. Kama ile ile ya kutokuthamini vyetu, tunathamini vya wageni, sasa tunathamini hata shule nyingine za *private* na nyingine, tunaacha za kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika suala la ada elekezi, nawezekana nikatofautiana kidogo na wengine. Wengi hapa walikuwa wanazungumza; walikuwa wanasema kwamba, Serikali haina haki ya kuweka ada elekezi katika suala la elimu. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, hili suala la ada elekezi ni mjadala mpana.

Kama sisi humu humu Wabunge tulikuwa tunaisema Serikali hii hii, nitoe mfano mmoja hasa wa sukari; tumesema bei elekezi ya sukari ni shilingi 1,800/=. Kwanini Serikali hamsimamii bei iuzwe 1,800/=? Leo mazao ya wakulima iwe pamba, iwe korosho, iwe tumbaku yanawekewa bei elekezi; mafuta

yanawekewa bei elekezi, umeme una bei elekezi, kwanini shule zisiwe na bei elekezi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali wateja wake ni wananchi masikini wa Taifa hili, zaidi ya asilimia 70 wanaishi vijijini, kama tukiacha tu tuseme, watu hawa hizi shule ni za kwao, wamekopa, ndiyo ile kwamba tumegeuza elimu ni biashara badala ya huduma. Kwa hiyo, ni vizuri, kwa sababu hata kwenye mazao, pande mbili za wadau wanakaa; wanunuzi, wazalishaji, wakulima na wadau wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa Serikali, wakae na wadau wa wamiliki wa shule na wazazi na Serikali yenyewe wapange bei elekezi kutoka na ubora wa shule, wazi-*categorize* katika *qualities* zake. Kwa sababu tunakubali kweli kuna shule nyingine zina hali ya juu zaidi, nyingine ni za kati, nyingine ni za chini, lakini zote bei haziwezi kufanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hapa, kuna hoja ambayo ilikuja upande wa pili kule na ilitolewa mfano wa Shule ya Sekondari ya Almuntazir wanazungumza kwamba imepandishwa bei imekuwa kubwa kutoka shilingi1,600, 000/= mpaka shilingi milioni 1,900,000/=. Mimi nikajiuliza, yaani labda ni *factor* gani imetumika kuichagua shule hii moja badala kutolea shule nyingi? Kwa sababu kuna shule nyingine nyingi zina ada kubwa zaidi kuliko hii ya Almuntazir. Kuna shule zina ada mpaka shilingi milioni 70, nyingine shilingi milioni 35, nyingine shilingi milioni 20, nyingine shilingi milioni tano, nyingine shilingi milioni tatu; lakini amekuja kuichagua Almuntazir yenye shilingi 1,900,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri tutende haki, tunapotoa maoni yetu, tuweke maoni ya jumla, tusionekane kama tunabagua jamii fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, niongelee kuhusu Jimbo langu. Sisi ni Halmashauri ya Morogoro na jukumu moja la Wizara hii, linasema kwamba, ni kusimamia elimu ya ufundi. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri, ukija hapa uniambie umejipanga vipi katika kutuunga mkono katika Chuo cha *VETA* katika Halmashauri yetu ya Morogoro Vijijini? Kwa sababu eneo tunalo, wananchi wameshajitolea, lakini tatizo tu hatujapata kushikwa mkono na Serikali kwa miaka mingi na Chuo hicho hatuna. Hii inasababisha wanafunzi wengi wanaoishia Kidato cha Nne na cha Sita kukosa nafasi ya kuendelea na elimu ya ufundi baada kukosa nafasi ya Chuo Kikuu.

MWENYEKITI: Ahsante! Mheshimiwa Tibaijuka na Mheshimiwa Emmanuel Papian ajiandae. *(Makofi)*

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kabisa kwa kusema kwamba naunga mkono hoja. Nampongeza sana mdogo wangu Mheshimiwa Profesa Ndalichako, amekaa vizuri na yameshasemwa mengi kwamba yeye ni mchezaji wa kukodisha. Nami nakubaliana na usemi huo. Maana yake ni kichwa, ametafutwa na sasa hivi nadhani nazi imepata mkunaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposimama hapa, baada ya kuyasema hayo, pia, nitoe masikitiko yangu makubwa kwa Naibu Waziri wake ambaye amempoteza mama na Waswahili wanasema, "aisifuye mvua, imemunyea." Kwa hiyo, najua machungu anayopita, Mungu ailaze roho ya mama yetu, mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasimama hapa kwanza kabisa kama mdau wa elimu. Watu wengi wameshasema, wengine wanasema ni mgongano wa masilahi. Mimi sina mgongano wa masilahi ila *I am interested party*. Katika hili la elimu, natangaza kabisa, hii ni sekta ambayo Mwenyezi Mungu akinijalia maisha, ninalia nayo, nakufa nayo, nahangaika nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hiyo, maana yake Waheshimiwa Wabunge wote ambao mko ndani hapa, ni kwa sababu wazazi wetu katika nyakati mbalimbali na mazingira mbalimbali walitupeleka shule, ndiyo maana tuko hapa. Ni ufunguo wa maisha. Kwa hiyo, hii sekta ambayo tunaijadili leo, tunazungumza mustakabali wa Taifa hili na watoto wetu. Kwa hiyo, hapa ni lazima wachangie kwa uchungu; na wachangiaji wengi nasikia wanazungumza mambo yanatoka rohoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda ni mfupi, siyo rafiki. Naomba nianze kwa kumwomba Mheshimiwa Waziri aangalie Waraka Na. 6 wa Elimu wa Mwaka 2015. Mheshimiwa Waziri unajua kwamba nilishawahi kuzungumza kwamba Waraka huu umeandikwa vizuri, lakini unatakiwa kuboreshwa. Ulivyoandikwa, sasa hivi ulivyokaa, sisi ambao tunawakilisha wananchi wetu katika mazingira ambayo bado elimu ni changamoto, unatuletea sintofahamu. Kwa sababu nimeona katika hotuba yako umefafanua jukumu la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, napongeza sana kwamba, Mheshimiwa Rais ameona yafaa kwamba Serikali ijaribu kutoa elimu bure kwa maana ya kwamba Serikali inagharamia elimu. Elimu unaposema iko bure inamaanisha, Serikali ndiyo inalipia elimu, wazazi wanakuwa wamepunguziwa mzigo. Kwa sababu kwamwe elimu haijawahi kuwa bure, lazima mlipaji apatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hiyo basi, naomba nikupeleke kwenye Jimbo la Muleba Kusini ambalo limenituma hapa. Mheshimiwa Waziri, Waraka ule ulivyosimama, utakaposimama kujibu, naomba unipunguzie matatizo niliyonayo Muleba Kusini. Pale tuna Shule za Sekondari. Kwa mfano, tuna sekondari 44, wanafunzi 15,378, lakini hali ya shule zile bado madarasa hayatoshi, madawati hayatoshi, nyumba za Walimu hazitoshi, mabweni usizungumze, Maabara tunahangaika nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hiyo, ni muhimu sana Waraka ukatambua pia kwamba kwa kuwa sera yetu ya elimu ni bure, inamaanisha kwamba wazazi ndio wanatolewa mzigo wa kulazimisha watoto kushindwa kuja shule, lakini jamii inachangia. Nataka niseme kabisa kwamba ule Waraka una walakini sana kwa sababu unafanya kazi yetu iwe ngumu. Sijui wenzangu vipi, lakini Muleba Kusini watu wote wanashikilia elimu ni bure, hawataki kuchanga. Hawataki kuchanga katika hali ambayo Serikali Kuu haina fedha za kutosha kuweza kuenea na wengine wameshasema. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kusudi tusijirudishe nyuma, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri, utakaposimama kujibu, ujaribu kutuelezea, utakavyotusaidia katika hili. Elimu ni bure, lakini pia lazima jamii ya Watanzania ilipe. Ni vizuri kwa sababu mwisho wa siku mtoto ni mali ya jamii, siyo mali ya mzazi. Mtoto ni mali ya jamaii, hilo nadhani nimelimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimeshasema kwamba, mimi nimekuwa mdau wa elimu kwa muda mrefu; mimi ni Mwanaharakati wa Haki za akina mama, katika hilo wala sirudi nyuma, wala siombi radhi kwa mtu yeyote, ninasonga mbele. Sasa Wanawake ukiangalia, tumepiga hatua, lakini katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nimeona hapa katika lile jedwali.

Katika udahili wa Vyuo Vikuu, bado wasichana ni asilimia 50. Bado hawajaweza kuwafikia wale wavulana. 7, 700 wasichana, wavulana wanaingia kwenye 15, 000 na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaona kwamba, bado changamoto ya mtoto wa kike bado iko unapozidi kupanda ngazi, ngazi za chini tuko sawasawa. Sasa shule zetu za Kata zimeleta mafanikio makubwa sana. Kama maendeleo yote, zimeleta changamoto! Shule za Kata ndizo tunataka kuhangaika nazo kwa sababu ndiyo mkombozi wa Taifa letu. Sasa hivi naipongeza Serikali ya CCM, imefanikisha kupunguza tatizo la Walimu katika shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nikupe mrejesho Mheshimiwa Waziri. Nikichukuwa Muleba tu, nilishasema ina shule za sekondari 44, ina wanafunzi 15,000 na Walimu wamepatikana. Katika Hesabu, tuna upungufu wa

Walimu 86; na kuna shule 13 za sekondari Muleba, hazina Mwalimu wa Hesabu hata mmoja.

Katika hali hiyo, kama tunavyozungumza, shule ambayo haina Mwalimu wa Hesabu ni hatari sana. Naomba Mheshimiwa Waziri jambo hilo aliangalie, kama hajalifanyia kazi, lifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Biology,* Muleba kuna shule nane hazina Mwalimu wa *Biology*, upungufu Walimu 47. Shule nane hazina Mwalimu wa *Chemistry*. Huwezi kutoa Mkemia pale! Huwezi kutoa Daktari pale! Shule 57 hazina walimu hao. *Physics,* hiyo ndiyo zahama kabisa! Walimu 80 wanakosekana. Shule 18 hazina Mwalimu wa *Physics* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naendelea; Kiswahili, Muleba tumeletewa Walimu wa Kiswahili 85 wa ziada. Walimu 85 wa ziada wa Kiswahili, Walimu 80 wa ziada wa Historia, Walimu 30 wa ziada wa Jiografia. Napendekeza kwamba, haya ni maendeleo, lakini maendeleo yanataka mrejesho *from the field*. Nataka nipendekeze kwamba, baadhi ya Walimu hawa wangeweza kufanyiwa *retraining* wakatusaidia katika masomo mengine ambayo hayapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza pia kwamba Walimu hawa wanaweza wakapelekwa Shule za Msingi. Hii kasumba kwamba wanaotoka Chuo Kikuu wataishia Shule za Sekondari, nayo tuondokane nao. Pia nataka kusema kwamba shule inapokuwa haina Mwalimu wa Hesabu, hiyo ni *crisis*. Mwalimu Nyerere, sisi tulifundishwa na wamarekani, tulifundishwa na Walimu kutoka India. Mimi nafikiria kwamba…

(Hapa kengele lililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kengele ya kwanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini ni kengele ya kwanza. Niombe tu Mheshimiwa Waziri utakapo simama au utakapojiandaa na timu yako nzuri ya Makatibu Wakuu waliobobea katika elimu, mwangalie namna ya kutafuta misaada kutoka nje. Nadhani hatuwatendei watoto haki. Mtoto anamaliza *Form Four* hajawahi kukutana na Mwalimu wa Hesabu! Kwa kweli hapo tutakuwa hatuwatendei haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamesema mengi kuhusu shule binafisi. Mimi ninashiriki katika Taasisi zinazoendesha shule binafisi. Yameshasemwa mengi; elimu ni ya ghali, inaweza ikawa bure kwa sababu Serikali nzuri inaisimamia, lakini elimu ni ya ghali. Sasa hizi shule ambazo tunataka, wazazi wanafanya bidii, wanajiongeza. Nafikiria ifike mahali wazazi na wenyewe

tutambue mchango wao. Sisi kama viongozi kusimama hapa na kusema tunaweka ada elekezi wakati wazazi wako tayari kulipa, kwani wazazi ni wajinga? Kwani wazazi hawana akili? *(Makafi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia mtu, akasema kwamba Sukari ni pendekezo, lakini huwezi kulinganisha elimu na sukari; ni bidhaa tofauti. Ni bidhaa tofauti kabisa, ziko katika masoko tofauti na mtu yeyote anayeelewa elimu, anajua kwamba elimu ni huduma. Katika shule nzuri, elimu ni huduma, haiwezi kuwa biashara. Wengi wanasema; mimi nikitaka biashara nitauza Bia na kaka yangu Rugemalila, sitahangaika! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitaka biashara sitahangaika na shule; shule siyo biashara. Ukitaka biashara unakwenda kwenye *fast moving items;* unauza bia, unauza nini na mambo yanakuwa mazuri. Elimu ni huduma! Sasa wale wanaotoa huduma, tuwatambue mchango wao, tuwaenzi. Katika nchi nyingine, wana utaratibu wa kupeleka fedha katika shule binafsi. Sasa sisi tuna utaratibu huu kidogo ambao unaweza kusema ni aibu kwa Taifa watu wa *TRA* kwenda kushinda kwenye shule wanatafuta kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo hayatusaidii, nayazungumza kwa dhati kabisa kwa sababu *program* tulionayo ni nzuri. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba hilo nilichangie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la haraka kama muda utaniruhusu, nizungumzie pia umuhimu…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Asante. Mheshimiwa Papian na Mheshimiwa Salum Rehani ajiandae.

MHE. EMMANUEL P. JOHN: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na kazi nzuri, ambayo inaifanya baada ya kuteuliwa na Mheshimiwa Rais. Napenda kushauri mambo machache yafuatayo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kwenye elimu Serikali imefanya mambo mengi, lakini na mengi yamezungumzwa humu ndani ambayo yanaelekeza ni jinsi gani ambavyo elimu inaweza kwenda na jinsi gani iwe na watu wote wametoa ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kumshauri Mheshimiwa Waziri kwamba aanze na *Primary Schools*. Ile mitaala ya *Primary Schools* ya zamani tuliyoizoea airudishie ule mfumo kwamba ukikuta Kitabu cha Darasa la Kwanza anachokisoma Mwanafunzi aliyeko Nkasi Tanzania, kule Rukwa, Sumbawanga, kitabu hicho hicho tukikute Lindi cha Darasa la Kwanza, kinachofanana na kinachosomeka vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Waziri *a-plan Primary Schools* kwanza, asiende haraka! Sekondari pumzika, Vyuo pumzika, taratibu tu, kule kunakwenda kuna Makamishina, kuna watu wanafanya, wewe nenda na *Primary Schools,* jenga misingi; hakikisha Walimu wanafundisha, hakikisha shule zinakaguliwa, hakikisha kuna utaratibu wa elimu kwa zile ambazo ni Sekondari, za Kiingereza *Primary Schools* wawe na mitaala inayofanana. Zile za Kiswahili zirudi vile vile kama zamani. Sayansikimu; mtoto afundishwe kutengeneza mwiko, chungu, afundishwe kupika, kulima; tunataka hiyo ianze *Primary School* bila haraka kwa mwaka huu. *(Makofi)*

Mwaka kesho wewe nenda *Secondary School, Form One* mpaka *Form Six,* panga mambo vizuri, usiwe na haraka, pesa hazitoshi na sisi ndiyo wakusanyaji, hazipo! Hicho kidogo kinachopatikana, mwaka kesho *plan for Secondary School, Form One* mpaka *Form Six*. Mwaka unaofuata, *plan* kwa ajili ya vyuo, nenda tena mpaka Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri awatafute wale Walimu wa zamani waliokuwa wanafundisha zile shule za *primary;* kaa nao, zungumza nao wakupe *tactics* na *the way* kuingia katika huu mfumo wa kutengeneza elimu bora kama ile ya zamani ambayo tunahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri akae na Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje. Tunao Mabalozi nje, wafanye kazi ya kutafuta *scholarships* kwa ajili ya wanafunzi wetu waende wakasome nje. Kila mwaka Balozi yeyote kwenye nchi aliyomo ambayo ina uwezo, aweze kuita na kutafuta wafadhili wasaidie watoto wetu wakasome nje. Lengo kuu la kusomesha watoto wetu nje, Watanzania wamejifunga; Watanzania wako magereza, wamefungwa; hawatoki nje! Wanafikiri hapa panaweza. Waende nje wakapigwe, wapigwe baridi, wapate shida, walale njaa, wakirudi Tanzania watashughulika na uwekezaji. Mheshimiwa Waziri, hebu jitahidi zungumza na hao watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, hawa wawekezaji mnaowaona ni kwa sababu wameona fursa huku, tupeleke watoto wetu kule. Wale watoto ukikaa nao ukiwaambia nenda kasome au nenda *Netherlands*, ukimaliza *degree* shawishi mfadhili ndugu yako mwingine apate nafasi umlete huko huko. Mkibaki huko, sawa; mkirudi Tanzania, sawa. Tutakuwa tumetengeneza

Watanzania kwenye *exposure* ya dunia hii nao watoke nje wakaone vilivyoko huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mkaguzi mmoja Kiteto alikuja ametoka kwenye kanda, ana gari, hana mafuta, hana nini. Nikamuuliza, sasa vipi? Anasema sasa nitakagua nini? Anataka kukagua na anayeombwa mafuta ni Mkurugenzi na akienda kuomba Mkurugenzi mafuta Mkurugenzi haiwezekani akamnyima mafuta kwa sababu anakwenda kumkagua; akimkagua anamletea madudu; akimletea madudu, hawataelewana. Matokeo yake anakosa mafuta, anakaa mezani analipwa mshahara bure. Hii ndiyo mishahara hewa ambayo tunazungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba hawa Wakaguzi waanze na *Primary School* wakutengenezee kitabu, wakuletee ujue matatizo ya *Primary School* kwa nchi nzima kwa mwaka huu ili ujue sasa shida za ku-*tackle* matatizo ya *Primary School* yanaanzia wapi na yanakwenda wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiteto tuna shule za mabweni chache, lakini watoto wetu kwa sababu ya maeneo ya kifugaji, ni mbali. Shule nyingine ni kilometa 14, shule nyingine 15, sasa watoto kwenda shuleni ni ngumu.

Nakuomba, kuna shule za Dongo za sekondari, tunaomba hizi shule za bweni, za kifugaji basi mtusaidie waweze kusoma kwa maana ya kupata hela ya chakula ili wale watoto tuweze kuwa-*accommodate* kule kwa sababu wakirudi majumbani mwisho wa siku wanaolewa. Kule kuna ndoa ambayo Mkuu wa Shule akipewa ng'ombe mmoja anaachia mtoto anakwenda anaolewa na anaolewa *underage*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba zile shule zangu za Dongo, kuna Engusero, kuna *Resoit Secondary School*, kuna *Rarakin Primary School*. Hizi shule tunaomba zipate msaada wa kupata hela ya chakula ili watoto waweze kulala bwenini na wote tuwabebe wakae huko wasiweze kutoka kwenda kuolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Rais, ali-*plan* na sasa tumefikia, changamoto zipo, ni nyingi, lakini tuna hakika kwa kushirikiana tutaweza. Naomba niseme, Bunge hili lilikwenda likazuia kidogo fimbo za makalio kidogo na kwenye mikono, hebu turudishe fimbo watoto wajue kwamba jamani kuna malezi. Turudishe bakora kidogo kwenye mikono; Walimu wanadharaulika! Wakisema, hawasikiki! Hebu turudishe huo utaratibu jamani, turudi tulikotoka. Sisi ni Waafrika. Ni lazima kuwa na nyenzo kidogo twende, hatutafika! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hebu ajitahidi aangalie namna ya kuliweka hili, fimbo zirudi kidogo. Aombe huko juu fimbo zirudi halafu watoto waanze kuogopa, hata wawahi shuleni wakasome wakiambiwa wasome; wakikemewa wakimbie, wakiitwa waje wanakimbia. *Discipline* iwepo. Walimu wanatukanwa shuleni na mtoto wa Darasa la Tano na wazazi twende tukaseme. Waheshimiwa Wabunge nanyi semeni huko tushinikize hili tuondoe tabia utovu wa nidhamu, halafu watoto warudishiwe fimbo kidogo halafu mambo yasonge mbele.

Mheshimiwa Waziri, naomba kusema kwamba nakushukuru lakini anza na *primary* mwaka huu, umalize matatizo ya *primary;* mwaka kesho sekondari, mwaka kesho kutwa vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Salum Rehani na Mheshimiwa Dkt. Immaculate na Mheshimiwa Susan Lyimo wajiandae.

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nilitaka nitoe shukrani kwa uwasilishaji wa hotuba hii ya Waziri kuhusu bajeti ya elimu. Nilikuwa na mambo ambayo yananisikitisha na hasa kuhusiana na mfumo mzima wa elimu unavyokwenda hapa Tanzania. Kwa kiufupi kusema ukweli, hakuna *consistency* ambayo tunaiona inatolewa kwa elimu yetu katika *level* zote. Tuchukulie mfano kule Zanzibar, safari hii wamesema wameanza kufanya mitihani ya Darasa la Sita. Ukitoka Darasa la Sita unaaza *Form One*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto hawa wanaoanza shule miaka minne, miaka mitano anaanza Darasa la Kwanza, akifika Darasa la Sita, ana umri gani? Halafu arukishwe aende *Form One*. Mtu huyo huyo anatakiwa afanye *Common Exam Form Four,* ambayo inasimamiwa na *NECTA*. Huku Tanzania Bara Darasa la Saba, lakini *Form Four* wanafanya *Common Exam*. Sasa hizi elimu tunaiga mifumo ya nje ambayo kwa kweli haijafanyiwa uchunguzi na utafiti wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya utafiti katika Jimbo langu la Uzini na nilikuwa naandaa *strategic plan*. *Preliminary survey* niliyokuwa nimeifanya matatizo niliyoyakuta ndani ya lile Jimbo, kuna tofauti kubwa baina ya shule na shule ndani ya Jimbo, achilia mbali ndani ya Wilaya. Tofauti nyingine iliyokuwepo, ni baina ya shule za *private* na shule za Serikali, *there is no common syllabus*. Kila mmoja anaangalia mazingira ya uboreshaji wa elimu kwa eneo lake.

Sasa kwenye Serikali unajiuliza, tofauti ya *syllabus* hii ya Serikali inatofautiana baina ya shule moja na shule nyingine, lakini kubwa linatokana na kwamba hakuna *monitoring,* ufuatiliaji haupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakaguzi ndio wanaoweza kupita katika zile shule wakaweza kuhakikisha kwamba *syllabus* inayofundishwa pale ni sahihi. Shule zetu nyingi nyingine zinatumia mitaala inayotoka *Cambridge,* nyingine zinatumia mitaala ya Kenya nyingine zinatumia mitaala waliyotengeneza wenyewe kulingana na mazingira yao; ndiyo maana unakuta *level* ya upasishaji inakuwa tofauti baina ya eneo moja na lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kama tuna *Common Exam,* lazima tuwe na mtaala mmoja na *flow* iwe inaeleweka kutoka chini kuja juu. *Flow* yetu iliyokuwepo ndiyo kitu kinachotutesa. Kila mmoja anakwenda njia yake. Nchi hii hatutafika kwa kila mmoja kwenda vile anavyoona yeye. Leo ukienda *St. Mary's* na shule nyingine za *mission* zina miongozo na mitaala yao na kiwango chao cha elimu kinachotolewa ni tofauti kabisa na shule nyingine za *private,* lakini halikadhalika shule nyingine hizi za vipaji maalum zina miongozo yake na mitaala yake mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba tukae pamoja, kama ni *NECTA* na wadau wake wengine ili kuweza kutoa *common syllabus* itakayoweza kufuatwa, lakini vilevile ile *consistency* ya madarasa tukubaliane, kwa sababu wale Wazanzibari wanasema wao wakiona *flow* imekwenda vizuri mwakani nao Tanzania Bara inataka kuanza mwisho Darasa la Sita, haieleweki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoamua jambo, tujiandae kwanza, tufikiri hawa wanafunzi kweli tunataka kuwapa kitu gani na kwa *level* gani? Mtoto akimaliza Shule ya Msingi, Darasa la Sita, huyo anamaliza *Form Four* bado mdogo sana na uwezo wa kukabili mtihani wa *Form Four* unakuwa haupo. Sasa nashauri kwamba mkutane viongozi wa elimu wa sehemu hizi mbili ili kuwe na mustakabali mzuri wa kuweza kuendesha hizi shughuli na mambo yaweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo linakwaza kwenye elimu ni suala zima la ukosefu wa Walimu husika kwa masomo husika. Shule zetu nyingi Walimu wamekuwa wanabambikiziwa masomo ambayo hawana ujuzi nayo. Mwalimu amesomea *arts* kwa vile hakuna Mwalimu wa *science,* anapewa *science* anaambiwa bwana utaziba kiraka.

Vilevile Mwalimu amesoma *science* sekondari, pengine *Form Two* au *Form Three,* lakini leo ndiyo unamweka Mwalimu huyo aweze kufanya *practicals* za *chemistry* na *physics* kwa wananfunzi wa *Form Four.* Sasa kwa kufanya hivi, tunaziba viraka. Hii siyo elimu ambayo tunategemea kwamba itaweza

kuwasaidia Watanzania. Kuwepo na utaratibu maalumu wa kuajiriwa Walimu wapelekwe katika maeneo maalum ili kuwe na uwiano wa utoaji wa elimu. Vinginevyo bado tutaendelea hapa kuhangaika na kutengeneza bajeti na kushauri lakini hakuna kinachoendelea. Elimu inaporomoka kwa mfumo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kinachotofautiana, shule nyingi zimejenga maabara, lakini tatizo la vifaa vya maabara limekuwa sugu na haviko katika shule chungu nzima. Na leo tuna lengo la kuhakikisha kwamba tunainua elimu ya sayansi katika nchi hii. Watu wale waliokuwa wamejenga maabara pengine inawezekana kwa shinikizo, kwamba lazima iwepo maabara pale, hapana walimu, vifaa vile hata kama wanavipeleka walimu waliokuwepo hawana uwezo wa kufanya zile *practical.* Kwa hiyo, mtu anakuwa na majengo na vifaa ambavyo havitumiki. Nakuomba Mheshimiwa Waziri hili nalo ukae na timu yako … *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Immaculate, jiandae Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka kuanza kutoa *inputs* zangu katika Wizara hii kwa kujiuliza: Je, ni mafaniko yapi tunayo katika Sekta ya Elimu, ukiangalia… *okay,* samahani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *inputs* gani tunaziona katika Sekta ya Elimu? Matokeo gani tunayaona katika Sekta ya Elimu kwa kuangalia shughuli za kiuchumi au shughuli za huduma za maendeleo ya jamii? Je, uchumi wetu una-*reflect* elimu tuliyonayo? Au huduma za kijamii kama ni afya, Madaktari wanatuhudumia vile tunavyotakiwa kupata? Sekta nyingine kama za Utalii, *Service Provisions,* zikoje? Je, zina-*reflect* kiwango cha elimu tulichonacho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko ambayo yametolewa na Wajumbe ni mengi hata kwa *Wizara* nyingine zilizopita na hii yote ina-*reflect level* yetu ya elimu ikoje. Kwa hiyo, sitajikita sana katika kusema changamoto ni zipi za miundombinu, lakini changamoto ni zipi ukiziangalia katika *outcome* na jinsi ambavyo ina-*affect* elimu yetu kwa ujumla na uchumi wetu kwa ujumla? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika Sera ya Elimu yenyewe, katika kipengele cha muda wanafunzi wanaoanza shule, hii pia inaweza ikawa na *outcome* au ikaleta *impact* ambayo siyo sahihi. Watoto wadogo, miaka minne, mitano, mitatu, wanaamshwa saa 10.00 au 11.00 alfajiri, wamepumzika saa

ngapi? Akili zikoje? Ukiangalia hata watoto wadogo wa Shule za Msingi Dar es Salaam, miundombinu hairuhusu wale watoto. Wanafika shuleni wamedumaa au hawana hizo akili, hawako *creative*. Kwa hiyo, chochote unachomfundisha yule mtoto hakiwezi kukaa, hiyo tayari ina *impact* katika siku za usoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mitaala au *curriculum* zetu, ni masomo gani yanafundishwa? Kwa elimu ya sasa hivi, je, *curriculum* ipo sawa? Watoto wadogo wa *primary school* au *nursery, content* wanayofundishwa ni sawa? Watoto wanafundishwa mambo makubwa ambayo ni *repetitive,* ya kazi gani? Hii inaleta udumaivu au udumavu. Samahani sijui Kiswahili, hakiko vizuri sana, nayo ni *reflection* ya elimu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *issue* za mitihani ya *primary* au '*O' Level,* mwanafunzi au mtoto huyu anapewa *one time chance,* ambayo si sawa. Mtihani unafanya kwa siku moja mtoto wa Darasa la Saba, miaka yote saba inakuwa *judged* na siku moja. Hii lazima iwe *reflected,* haiko sawa. Au mtoto wa *Form Four* au *Form Six,* miaka yote hiyo minne au miwili aliyosoma inakuwa *judged one time* na chochote kinaweza kikatokea. Kwa hiyo, tunamnyima huyu mtoto nafasi au fursa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niguse kwenye *issue* ya Vyuo Vikuu na *specialization*. Tuna vyuo vya Serikali, naona hapa *list* inaonyesha vyuo 31. Ni chuo gani au vyuo hivi vikuu vime-*specialize* kwenye nini? Chuo Kikuu hakiwezi kuwa na *faculties* saba au nane. Hao wanaofundisha, wanaotoa huduma, hao Walimu wana *qualities* zinazotakiwa?

Kwa hiyo, lazima na hiyo nayo namshauri Mheshimiwa Waziri mhusika mwangalie *specialization* katika vyuo lazima iwe *reflected* inavyotakiwa na wataalamu wanaotakiwa wawepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* nyingine ni miundombinu lakini kwenye njia ya ku-*deliver* elimu au kutoa mafunzo. Ni mbinu gani zinatumika kufundishia? *Style* tuliyonayo sasa hivi shuleni, hasa Shule za Serikali na hasa vijijini ni Mwalimu anaandika *notes* ubaoni na wanafunzi wanafanya kazi ya ku-*copy*. Kinachofuata ni ku-*cram* kile Mwalimu alichofundisha.

Sasa mtoto huyu anayefaulu, asilimia kubwa ni yule mwenye uwezo wa ku-*cram* halafu anakuja kutema baadaye kwenye *exam*. Hii nayo inakuwa *reflected* kwenye Vyuo Vikuu. Wanafunzi wanaokuja hawako *creative,* lakini tunaendelea kuwa na *system* za kukremisha. Sasa kama umejaliwa kukremisha ndiyo *you have a better chance* ya kufaulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vizuri kujiuliza au kujitathmini, tutaendelea hivi mpaka lini? Tutaendelea kusema madarasa hayatoshi, Walimu hawatoshi, miundombinu hafifu lakini tunataka nini? Serikali kama Serikali tuna *strategy* gani ya kusema kwamba elimu yetu i-*focus* kwenye nini ili izae kitu gani? Kwa hiyo, ni lazima tujiulize: Je, ni vipaumbele vipi tulivyonavyo, kama hivyo vipaumbele vipo na tunajiwekea nini katika elimu? Au imekaaje kimkakati ku-*reflect* uchumi wetu na nini tunataka kukijenga katika nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi katika muktadha huo, naomba tujikite na tu-*concentrate* kuangalia kwamba elimu yetu ipo katika *standard* gani na tunataka ku-*achieve* nini na matokeo hayo ya elimu tunataka yaweje? Tu-*focus* kwenye *impact* au *outcome* ya mfumo mzima wa elimu tunataka uwaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu kwa sasa. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Naomba kuchangia Wizara hii muhimu sana kama ambavyo Mheshimiwa Zitto alivyosema, inachangia kwa zaidi ya *one third*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nianze kwa kuzungumza masuala ya *TCU* na niseme kwa kweli uamuzi huo wa kuivunja umechelewa kwa sababu ni kwa muda mrefu sana nimeongelea suala la vyuo hivyo pamoja na Kampala, japo sijajua Kampala inaendeleaje. *TCU,* kwanza niilaumu sana kwa jinsi ambavyo imekuwa ikidahili vijana ambao wanajua kabisa hawana uwezo. Nilikuwa nataka Serikali ituambie nini hatma ya vijana hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hilo kwa sababu kuna vijana 500 waliohamishwa kutoka kwenye Vyuo vya *St. Joseph* Songea na Arusha na hususani Arusha. Hapa nina barua ya *TCU* iliyoandikwa na Profesa Mgaya ikisema kwamba vijana wote waliokuwa kwenye vyuo hivyo, hii ikiwa ni pamoja na wale 500, watapelekwa kwenye vyuo vingine na vijana hao wamekwenda; na kifungu cha tano kinasema kwamba wanafunzi wote ambao ni wanufaika wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, mikopo yao itahamishiwa katika vyuo watakapokuwa wamehamishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninapozungumza, vijana hawa wamehamia *SUA* toka tarehe 28 mwezi wa Tatu wengine wamehamia *UDOM* toka tarehe 9 mwezi wa Nne na wengine wamehamia Mkwawa. Hapa ninapozungumza, vijana hao hawajapewa hata shilingi moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisemi kwamba wasichana wataathirika zaidi, lakini nazungumza kama mzazi. Watoto hawa kama kweli wamekaa miezi miwili *plus* hawajapata kitu chochote, tunategemea tunapa wanafunzi wa namna gani? Vilevile nalaumu sana vyuo hivyo, inawezekanaje Wakuu wa Vyuo hao hawawasiliani na Bodi ya Mikopo ili kujua kwamba hawa watoto wanaweza hata wakasababisha fujo katika vyuo hivyo kutokana na hali waliyonayo? Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri unapokuja utuambie nini hatima ya vijana hawa kutokana na huu mwongozo uliotolewa na *TCU?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba nizungumzie suala la Walimu, sitaenda kwa *details* kwa sababu kila mtu ameliongea. Ni wazi kwamba elimu bora lazima iletwe na Walimu lakini vilevile Walimu hao kinachofuatia ni vitabu na hasa vitabu vya kiada. Ni jambo la kusikitisha sana kuona kwamba ile *change* ya Rada ya shilingi bilioni 75 ambapo najua shilingi bilioni 55 zimeenda kwenye vitabu, lakini vitabu vilivyotengenezwa ni vitabu ambavyo haviwezi kabisa kusaidia watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbatia ametoa mifano nami sina sababu ya kuendelea kutoa mifano, lakini kama mtoto wa Darasa la Kwanza, la Pili na la Tatu hawa ndio watoto ambao kile anachoambiwa ndiyo hicho hicho ataendelea kukiamini maisha yake yote. Sasa kama kitabu nilichonacho hapa kimepigwa chapa mara saba lakini bado kina makosa makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimepigwa chapa mara ya kwanza 2000, 2004, 2006, 2007, 2009 mpaka leo ni mara saba, lakini bado ina makosa lukuki. Unaposema namba nzima ni moja mpaka 99 ni makosa makubwa sana, lakini ukiangalia humu ndani ni aibu. Unamwambia vitu 11 lakini unasema ni 10, kwa hiyo, mtoto yule ataendelea kujua ni kumi kumbe ni 11. Huyu mtoto atajuaje kuhesabu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haishii hapo tu, ndiyo sababu tunasema Wizara ya Elimu ina matatizo makubwa sana. Kwa kweli kwa kuwa Waziri Kivuli wa hii Wizara nimeelewa mambo makubwa mengi ya kipuuzi; inawezekanaje kitabu kitoe ithibati mwaka 2006, lakini kitabu kimepigwa chapa 2007, inawezekanaje? Unawezaje kutoa ithibati kabla ya kitabu? Kwa hiyo, haya ndiyo mambo tunayoyasema. Wizara ina matatizo makubwa sana. Hata ukiangalia hii Sera ya Elimu, ni matatizo makubwa, kwa sababu huwezi kusema mtaala au *curriculum* inafundishwa. Toka lini mtaala ukawa unafundishwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli tuna matatizo makubwa sana. Nami ninaamini hivi vitabu ambavyo vimepitishwa kote huko na kupata ithibati wakati vina matatizo maana yake ni kwamba wana makusudi kabisa ya kuua elimu ya Tanzania, kwa sababu vitabu ukitoka Mwalimu ndiyo kitabu. Kama vitabu vina matatizo, watoto wanapata nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili la elimu kwenye shule zetu za msingi na Vyuo Vikuu, kuna tatizo kubwa sana katika elimu ya juu. Sasa hivi kuna watu wenye *Masters* na *Ph.D* Dar es Salaam na maeneo mengi, kazi yao ni kusaidia wanafunzi kufanya *thesis.*

Kwa hiyo, unakuta mwananfunzi anamaliza *masters* lakini has *nothing in the brain*. Wanafanya *plagiarism* ya hali ya juu. Naomba kujua kwa Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla, hivi huyu bwana anayeitwa Msema Kweli alipotoa hiki kitabu cha orodha ya Mafisadi sugu wa elimu ambao wengine ni Mawaziri, Wabunge nakadhalika, hivi Wizara ilichukua hatua gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunaona vitu vinatolewa hadharani halafu Wizara haichukui hatua, maana yake ni kwamba wanabariki watu waendelee kusoma bila kuingia darasani. Kwa hiyo, nataka Serikali ituambie, ni lini wanachukua hatua kwa watu ambao wanafanya *masters* na *Ph.D? Y*aani mtu anajiita *Doctor,* kumbe siyo *Doctor,* unaenda kwenye mikutano, aibu tupu! Haelewi chochote, hawezi *language* hawezi nini? Sisi wenyewe ndio tunaoharibu elimu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye mfumo wa elimu. Mfumo wa elimu hapa Tanzania ninavyojua mimi kama Mwalimu unaanza *nursery* kwa mwaka mmoja au miwili, unaenda shule ya msingi miaka saba, unaenda *ordinary level* kwa maana ya Kidato cha Kwanza mpaka cha Nne, halafu unaenda *advance level* Kidato cha Tano na cha Sita *then tertiary level,* miaka mitatu mpaka mitano kutegemeana na na *degree*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo mfumo wetu wa elimu. Kinachonishangaza leo na Mheshimiwa Waziri aje atuambie, ni lini mfumo huu umebadilika kwamba mwanafunzi anamaliza Kidato cha Nne moja kwa moja anaenda Chuo Kikuu? Imeanza lini na kwa utaratibu upi? Kwa hiyo, nataka tuelezwe sasa mfumo wetu wa elimu nionavyo sasa hivi, tumeamua kwamba kutakuwa na elimu msingi ya Darasa la Kwanza mpaka Kidato cha Nne. Nataka kujua tu, kwa nini tuna wanafunzi wanaomaliza Kidato cha Nne wanaenda moja kwa moja Chuo Kikuu kwa ajili ya *degree*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuzungumza ni suala la utafiti wamezungumza wengi lakini niseme kwamba tulishafikiria na kuamua kwamba angalau utafiti upewe *one percent* ya *GDP* ya pato ghafi. Kwa takwimu za pato ghafi la mwaka 2013/2014 ilikuwa ni shilingi trilioni 44, naambiwa sasa hivi limeongezeka sana kama shilingi trilioni 90. Kwa hiyo, niliamini kwamba utafiti na hapa nazungumzia *COSTECH* ambao ndiyo wana mwamvuli wa tafiti zote. Kwamba wangepata sawa na shilingi bilioni 440 kwa pato la Taifa la shilingi trilioni 44.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hawa wamepata *ten billion* sawa na 0.025 ya pato la Taifa. Sasa hawa watu watafanyaje utafiti kama hawapati fedha? Mbaya zaidi, vyuo vyetu vikuu; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa takriban miaka mitatu mfululizo hawajapata fedha za utafiti. Tunategemea kweli nchi hii itaendelea kuwa ya viwanda kama haiwekezi kwenye utafiti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mweyekiti, kwa hiyo nilikuwa nadhani tuna… *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chegeni na Mheshimiwa Gulamali ajiandae.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu. Kazi yake ni nzuri, tufike mahali Watanzania tuanze sasa kukubaliana. Hii Wizara ya Elimu ina mambo mengi sana, lakini kimuundo wake jinsi ilivyo, mambo mengi tunayozungumza Waheshimiwa Wabunge ni ya TAMISEMI. Ukizungumzia Shule za Msingi, Shule za Sekondari, vyote viko chini ya TAMISEMI na hata ukiangalia suala zima la bajeti yake, sehemu kubwa inagharamia wa *Loan Board* na taasisi nyingine za juu. Yeye amebaki na *function role* ya kutunga sera na kusimamia sera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna haja ya kuangalia vizuri mfumo mzima na muundo wa Wizara hii ili kweli ifanye kazi na tunaposema elimu hapa, basi moja kwa moja iweze ku-*tricle-down* kutoka kwa Wizara ya Elimu kuja mpaka elimu ya chini. Sasa hapa kuna *gap* na hata ukiangalia mazungumzo mengi ya Waheshimiwa Wabunge humu ndani, tunajaribu kuzungumza lakini kimsingi *functionally,* Waziri wa Elimu ana jukumu dogo sana hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kuna haja ya kuangalia muundo mzima wa Wizara hii ili sasa unapozungumzia Wizara ya Elimu, iwe na mantiki yenye kwenda mpaka kwa mwananfunzi wa chekechea. Leo hii unakuta Walimu wanadai stahiki zao, wana matatizo yao, wana mambo chungu nzima, hawana motisha, lakini bado kama Wizara ya Elimu, haina majibu ya haya. Haya peke yake yatajibiwa na Wizara ya TAMISEMI zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna *debate* inaendelea humu ndani, suala la shule binafsi na shule za Serikali. Waheshimiwa Wabunge, naomba nijielekeze kwamba bado suala la ada elekezi ni muhimu zaidi kwa Watanzania wote kwa sababu ukiangalia elimu siku hizi ni biashara. Mheshimiwa Mama Tibaijuka hapa ana shule zake *as a business* na wengine kadha wa kadha *is a business*. Sasa kwenye biashara zamani ilikuwa elimu ni huduma, lakini leo

wanakopa kwenye mabenki wanawekeza kwenye elimu. Ni kama miradi mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa usipokuwa na *regulation policy* hawa watoto wa mkulima watoto wa Mtanzania ambaye hana uwezo wa kuweza kulipa ada, inakuaje? Kwa hiyo, lazima ifike mahali Serikali i-*play role* yake ya kuwasaidia Watanzania wote. Naheshimu kwamba shule za binafsi wacha mwenye kipato cha juu ampeleke mtoto wake kwenye shule ya binafsi alipie hiyo ada, ana uwezo wake; lakini yule ambaye hana uwezo, tunamsaidiaje? Sasa ni wajibu wa Serikali kuweza kuboresha. Lazima Serikali iboreshe. Inaboreshaje? Waheshimiwa Wabunge hapa tuje na mkakati tuseme iboreshe namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoanza kusema Wizara ya Elimu iboreshe, hataboresha huyu! Serikali kupitia TAMISEMI kwa Mheshimiwa Simbachawene, ndiyo tuipe jukumu kubwa la kuboresha Shule za Sekondari na Shule za Msingi ambao ndiyo msingi wa chimbuko la mwanafunzi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunasema kwamba lazima kuwe na ada elekezi, Serikali lazima iweke *policy* hiyo. Hawa watoto ambao wazazi wao hawana uwezo, watasomaje hizi shule? Hawa watoto ambao Serikali hii imejitolea kuchangia kupitia kodi za Watanzania, kwa sababu leo hii Watanzania katika kuboresha zile kodi za Watanzania, zimesaidia sasa kwenye kuboresha shule hizi. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge, katika hili naomba tukubaliane tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, katika hali ya kawaida, mitaala yetu ya elimu bado ina mapungufu makubwa sana. Leo watoto wanapohitimu, hatuwatengenezi katika akili ya kujiajiri au kujitegemea. Tunawatengeneza katika akili ya kuajiriwa kitu ambacho ni tatizo. Kwa hiyo, kuna haja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, naomba mje na mtaala ambao utasaidia wahitimu wanapohitimu iwasaidie kuweza kujitegemeza katika kujenga maisha yao. Bila kufanya hivyo, suala la ajira ni tatizo na bado Watanzania tunazidi kulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii katika *Labour Market* Watanzania tunapoenda ku-*compete* watu wengi hatuwezi kufaulu. Niwape tu mfano. Leo hii Makao Makuu ya Kiswahili yako Zanzibar lakini anaye-*head* ile timu ni Mkenya kwa sababu Mtanzania hakuna aliyefaulu kujua kusema Kiswahili vizuri kuliko Mkenya.

Kwa hiyo, Watanzania tunakwenda kwenye *job Market,* hatuna uwezo wa kutaka kuchukua kazi hizi? Anayefuatia pale ni Mganda. Leo Watanzania

pamoja na kwamba Kiswahili kilizaliwa Tanzania, kikakua Tanzania, kikaanza kukulia nchi jirani kikafia kwingine na kikazikwa kwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Watanzania tunaenda kwenye soko la ajira tuna tatizo kubwa sana, lakini ni kwa sababu ya muundo na mfumo wa elimu yetu. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, wewe una nafasi ya pekee, umekuwa ni mtu ambaye ni mahiri toka ukiwa *NECTA*. Umefanya kazi nzuri. Tumia sasa utalaamu wako huo kuweza kui-*shape* Wizara ya Elimu ili Watanzania wapate wanachokitaka. Leo hii ukiangalia, Tanzania ina wasomi wengi sana lakini wakipelekwa kwenye soko la ajira ni wachache wanaweza ku-*compete* na kupata kazi za Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana hili tuweze kuliangalia. Vile vile kuna suala la mazingira ya elimu na hasa watoto wa kike. Kuna baadhi ya maeneo watoto wa kike wanashindwa kwenda shule kwa sababu hakuna vyoo. Wanashindwa kujisaidia vizuri kwa sababu ni watoto wa kike; wanashindwa kusoma kwa sababu ni watoto wa kike. Naomba tuweke mkazo, Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Simbachawene Waziri wa TAMISEMI, naomba muwe na *link* nzuri na Wizara ya Elimu. Mfanye kazi kwa maelewano mazuri ili kusudi tuwasaidie watoto wa Mtanzania waweze kuhitimu vizuri na wapate elimu inayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilisoma katika shule za *mission Form One* mpaka *Form Six,* ni mdau. Natambua ubora wa shule binafsi, lakini naiomba Serikali hii itusaidie, bado Shule za Serikali zinatakiwa ziboreshwe zaidi ili ziweze ku-*compete* na shule za binafsi. Tusipofanya hivyo tutakuwa tunacheza mchezo ambao ni wa kuigiza. Mzazi anahitaji asomeshe mtoto wake, lakini tunahitaji *quality of education*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima ubora wa elimu tuuzingatie. Tusiwe na wingi tu wa kusema tunaingiza watoto, wanasoma. Tumeanzisha Shule za Kata, zimesaidia sana kuwaelimisha Watanzania, zimesaidia sana mpaka Waheshimiwa Wabunge humu wamesoma Shule za Kata, wako humu ndani. Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aweso huyu ni zao la Shule ya Kata, leo ni Mheshimiwa Mbunge hapa ndani na wengine, lakini watu walidharau wakasema ni yebo yebo, hakuna cha yebo yebo! Hizi shule zimesaidia, naomba tuziboreshe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni madai ya Walimu. Hivi huyu Mwalimu atakuwaje na moyo wa kufundisha? Atakuwaje na moyo wa kumwelimisha mtoto wa Mtanzania…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Gulamali, dakika tano, Mheshimiwa Mariam Kisangi dakika tano na Mheshimiwa Deo Sanga tano.

MHE. SEIF KHAMIS SAID GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Elimu. Kwanza napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa kumpa nafasi hii Waziri dada yetu, Mheshimiwa Dkt. Ndalichako. Mheshimiwa Ndalichako una historia ndefu sana katika Wizara hii ya Elimu. Tunaamini toka hapo kabla hujapata nafasi hii ulikuwa Mtendaji Mkuu wa Baraza la Elimu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua hilo, Mheshimiwa Waziri, sisi kazi yetu kama Wabunge ndani yetu, umoja wetu, ikiwa Wabunge wa Upinzani au Wabunge wa CCM, kwa ujumla wetu, kazi yetu ni kukusaidia wewe Mheshimiwa Waziri. Siyo kukubebesha mizigo ya lawama ambayo haina sababu za msingi. Sisi kazi yetu ni kukusaidia kujua namna gani utaweza kwenda kwenye mfumo wako, kuurekebisha au kuboresha ili watoto wetu wapate elimu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika kumsaidia Mheshimiwa Waziri. Sehemu moja viko vitabu vinavyotolewa shuleni na baadhi wamezungumza wenzangu, unakuta shule 'X' inatumia kitabu fulani na shule 'B' inatumia kitabu fulani; vitabu hivi ni tofauti lakini somo ni moja. Halafu wanakwenda kufanya mtihani mmoja ambao unatofautiana mafunzo ya vitabu vyenyewe. Nakuomba Mheshimiwa Waziri ukaliangalie hili tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwe kitabu kimoja nchi nzima, kama Darasa la Kwanza, kitabu cha Kiswahili cha mwandishi fulani, basi nchi nzima kiwe na mfanano wa *syllabus* zote iwe mfumo mmoja. Isiwe huku *syllabus* tofauti huku *syllabus* tofauti, tukienda kwenye mtihani, watoto hawa wanaenda kukutana na *paper* ambazo hawajawahi kukutana nazo katika kufundishwa kwao. Kwa hiyo, naomba Wizara iangalie hili, wataalamu wanatusikia, wakalifanyie kazi hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, linguine, kuna tatizo la ufujaji wa mitihani. Kuna kipindi fulani ikifika mitihani ya Kidato cha Nne, *Form Six* unasikia mitihani imevuja na kunakovuja mitihani huku kunaathiri sana watoto wote wa nchi nzima waliofanya mitihani. Wako wenye dhamira njema na wale ambao dhamira yao siyo njema. Wanaovujisha mitihani ni Watumishi ambao wanafanya kazi ndani ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilipata kufanya mtihani wa *Form Four* 2004, mtihani ulivuja. Ulipovuja, wakati wengine hatukupata hata hiyo *paper,* tulipoenda kwenye mtihani unakutana na *paper* wanakwambia mikoa mingine ambayo wamepata maendeleo *paper* ile tayari wanayo. Wakaenda kufanya

mtihani wakapata *marks* za juu, kuna watoto ambao wanaenda kufanya hata *paper* hawakuwahi kuiona, lakini Wizara ama wataalamu wanao-*standardize* matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ku-*standardize* matokeo mnapelekea kuwaumiza watoto wengine ambao hawakuweza kupata hata huo mtihani. Hamwangalii nguvu kazi iliyotumika kwa watoto ambao wametoka katika mazingira magumu hasa ya vijijini. Watoto wa Mjini wanapata *paper,* wanajua jinsi gani wanavyozipata katika Wizara. Mwangalie hao watumsihi ambao sio wema, siyo kuwapa maonyo, ni kuwafukuza kazi na ikiwezekana wachukuliwe hatua za kisheria za kufukuzwa kazi na kuwekwa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko tatizo la Walimu. Napenda kuzungumzia Walimu. Walimu wanagawanyika katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu. Yako mazingira mazuri ya Walimu wanayofanyia kazi, lakini yako mazingira ambayo siyo mazuri ambayo Walimu wanafanya kazi. Kwa mfano, katika Wilaya yetu ya Igunga Jimbo letu la Manonga, eneo kubwa ni vijijini. Walimu hawa wanakuja kule vijijini lakini *allowance* zozote zile, *promotions* za kuwafanya waishi mazingira yale, hawapewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iangalie hao Walimu wanaokwenda kufudisha katika maeneo hatarishi, maeneo ambayo siyo rafiki kwao, muwape *promotion* ya kiwango fulani ya fedha ambazo zitaweza kuwashawishi kuweza kumudu kuishi katika mazingira haya. Haiwezekani mshahara na posho ufanane kwa kila kitu. Mwalimu anayefundisha Chomachankola na Mwalimu wa Shule ya Msingi anayefundisha Temeke au Kinondoni. Haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni lazima mliangalie na mlitilie nguvu kuhakikisha kwamba hili tatizo mnalitatua haraka ili ku-*promote* hata Waalimu wanaofundisha Kinondoni wawe wana hamu sasa ya kuja kufundisha Choma, Simbo na maeneo mengineyo ya vijijini. Hii itaweza kurahisisha upatikanaji wa Walimu na kuondoa hii kero ya Walimu; kila wakifika Kijijini wanakaa muda wa mwezi mmoja, wanaomba uhamisho. Anakwambia mama yake mgonjwa…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kisangi, halafu Mheshimiwa Sanga na Mheshimiwa Mwigulu wajiandae.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nami kunipa nafasi. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, wote wanawake. Tunategemea kuona ni jinsi gani

wanawake mnaweza na sisi tuko nyuma yenu, tutawaunga mkono, tuna imani mtafanya vizuri ninyi akina mama ni walezi. Mungu atawasaidia katika kazi yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ni dakika tano, naomba niende moja kwa moja. Mimi kwa vile ni Mbunge ambaye natoka Mkoa wa Dar es Salaam wenye utitiri wa shule za *private*, nitakuwa mkosefu wa fadhila au nitakuwa mnafiki iwapo sitazungumzia suala la ada elekezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kabisa mchango wa sekta binafsi katika maeneo mbalimbali ya maendeleo hususan katika suala zima la elimu. Natambua jinsi gani shule za binafsi zinatubeba kama Mkoa wa Dar es Salaam na kuweza kupata matokeo mazuri. Pia ni wajibu wangu kusema changamoto ambazo wananchi wangu wanazisema kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ada za Shule ya Msingi na Sekondari, mpaka sasa imeambukiza na Vyuo Vikuu, ni tatizo. Ada hizi zinapanda kila baada ya muda. Wazazi hao hao ndio wanaokuja kwangu mimi kama Mbunge. Wengine wanashindwa, wanaomba niwasaidie kuwapeleka Olympio. Olympio shule ni moja Mkoa mzima wa Dar es Salaam, ndiyo shule ya Serikali; Olympio na Diamond. Sasa hawa watoto ambao wanashindwa huku, tutawapeleka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wale wengine wanapata matatizo wazazi wao hali ya uchumi inakuwa mbaya, wanashindwa kuendelea na shule. Pia kumpeleka mtoto wako shule ya *private* mara nyingine siyo wingi wa kipato ulichokuwanacho, ila ni utashi wa kupata elimu.

Kwa hiyo, naomba waelewe hata wenzetu, kwamba tunapokwenda kule, siyo kwamba mimi nina hela nyingi. Vijana wetu ambao ni watoto wetu ambao na wao wana watoto wenzao, wanakwenda kule wanakwama. Nao ndio wanaorudisha huku kwamba jamani hizi ada zenu zinazidi. Mtoto wa chekechea shilingi 3,800,000/=; hivi inakuaje? Ndiyo tunajua huduma anayoipata na nini, lakini tuangalie angalau kidogo. Vijana wangu mimi wa *Clouds* kila siku ndiyo maneno yao, wanasubiri Serikali, ada elekezi, leo mimi Mbunge wao nisimame hapa nisipolizungumzia, kwa kweli sitawatendea haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za binafsi hazikuanza leo wala jana, kwanini wananchi walilipokea? Tena walipoke vizuri. Leo kila mtu anazungumzia suala la ada; hapa kuna jambo. Naiomba kabisa Serikali, ikae na hao wenye shule tuangalie jinsi gani ya kuweka utaratibu mzuri ili shule zetu ziwe angalau na udhibiti wa aina yake. Shule ya Msingi au Sekondari inafika mpaka shilingi milioni tisa. Hivi leo shule ya shilingi milioni tisa, mtoto yule

anaenda; baba yake kafariki, ukienda hawampokei. Wanakushauri ufanye nini, ufanye nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tusema ukweli, pamoja na utoaji wa huduma, lakini na biashara ipo. Kwa hiyo, naiomba kabisa Serikali; kama isingekuwa biashara, isingetofautiana bei. Sasa inakuwa elimu kama inauzwa; hapa unaona shilingi 200/=, hapa shilingi 300/= au shilingi 3,000/=. Siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena, pamoja na mambo yote, tuna shule za *private,* yaani *English Medium* Dar es Salaam mbili; Olympio na Diamond. Hivi Serikali lini italiona hili suala? Kama wananchi sasa hivi wamekuwa wanapenda watoto wao wasome *English Medium* kwanini zisiwekwe katika Wilaya ya Temeke, Kinondoni, lakini na mikoa mingine pia ili wale watoto ambao watakwenda huko wakipata matatizo, warudie kwenye shule hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie *TCU*. *TCU* Mheshimiwa ni matatizo! Hivi leo udahili wa wanafunzi, mimi mtu mzima nataka kusoma Chuo, naambiwa niende *TCU* sijui nikapeleke matakataka gani, vitu kibao! Hivi mambo mengine si wanajichanganya wenyewe! Utakuta mkopo unakuja kwangu, mimi nautaka? Hii yote inakwenda na mfumo mbaya. Wanatakiwa wabadilike, warudishe mambo mengine kwenye kwenye Vyuo Vikuu vyenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuoni tumeweka Uongozi, tunawaamini…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Deo Sanga, halafu Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Angellah na Mheshimiwa Simbachawene wajiandae.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga Mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie angalau kwa dakika tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Waziri mwenye dhamana, Naibu Waziri, Watendaji wote wa Wizara hii ya Elimu, wanafanya kazi nzuri, mwelekeo tumeshauona nadhani tumeuanza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Walimu wa Sayansi ambao Wabunge wenzangu wamelizungumzia sana. Sasa tatizo ambalo naliona, bila kuona namna gani tutalitaua, tutaendelea kuwa na tatizo na Walimu hawa wa Sayansi. Kwa mfano, Walimu hawa kila mwaka wanaopatikana ni wachache; na tatizo kubwa ambalo linajitokeza ni kwamba baadhi ya sisi wazazi; Walimu wenyewe tunawajengea mazingira watoto kwamba somo hili ni gumu. Hili ndiyo tatizo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hebu tuone namna gani tunaanza kujenga misingi huku chini kutoka Shule za Msingi mpaka Sekondari kuona watoto wanapenda somo hili. Tukitengeneza vizuri watoto walipende somo hili, tutamaliza tatizo la Walimu wa Sayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumzia suala la shule binafsi. Shule za watu binafsi, naweza kusema ni sawa na hospitali za watu binafsi ambazo zinahudumia na Serikali inapeleka ruzuku pale. Hata Mwalimu Nyerere wakati ameanza kuambia Taasisi mbalimbali… *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa, naomba utulivu ndani ya ukumbi!

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Mwalimu Nyerere wakati anaanzisha shule za watu binafsi, Taasisi za kidini na kadhalika, ilikuwa ni kuisaidia Serikali. Kwa hiyo, nadhani sasa muda umefika, tuone namna ya kusaidia shule hizi kwa sababu na zenyewe zinatoa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi Shule za Sekondari ambazo tumezianzisha katika Kata mbalimbali, Serikali imefanya kazi nzuri; tusimamie, ziboreshwe zilingane na hizi na baadaye hizi zitajifuta pole pole zenyewe. Hii ya kuelekeza kwamba kuwe na ada elekezi, sioni kama tutakuwa tunafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linguine ni suala la Walimu. Kwenye Halmashauri yangu ya Mji wa Makambako, nilikuwa nadhani TAMISEMI Wizara hii ya Elimu, hebu tuone namna hii ya kuhakiki madeni haya haraka ili Waalimu hawa waweze kupewa stahiki zao. Wenzangu wengi wamesema hapa, Walimu wanafanya kazi nzuri sana; sasa tuone namna ya kuhakiki madeni haya ili waweze kulipwa stahiki zao haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, nirudie tena, shule za watu binafsi zinafanya kazi nzuri, Serikali, isaidie kabisa. Zinafanya kazi nzuri sana. Tuwatie moyo! Mwaka 2015 shule hizi za watu binafsi zimefanya kazi vizuri, zimetoa watoto waliofaulu sayansi vizuri. Sasa kwanini tusiziunge mkono? Kwa nini tusiwasaidie? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii ya Waziri wa Elimu asilimia mia moja kwa mia moja, baada ya kuona haya marekebisho ya ada elekezi yaondolewe. Nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mwigulu.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu na Sekta ya Ualimu. Mtiririko mzima wa kuandaa Walimu una kasoro kubwa sana hasa tangu kuchafuliwa kwao kwenda kwenye Vyuo vya Walimu kwa kuwachagua watu wenye ufaulu wa chini kuingia kwenye Vyuo vya Ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kitendo cha wahitimu kukaa mwaka mzima wakisubiri ajira kinavunja moyo Walimu wetu. Hata hivyo, kitendo cha Walimu kushindwa kuwapandisha madaraja kwa muda mrefu na pale wanapopanda kushindwa kuwapa stahiki zao, nako ni kuvuruga kiwango cha elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu kufanya kazi nje ya ajira yao, mara nyingi Walimu wamekuwa wakitumikia kwenye kazi kama vile sensa, kusimamia uchaguzi, kuwa Watendaji wa Vijiji nakadhalika. Mwalimu anaposimamia uchaguzi na Chama Tawala kikianguka kwenye Kituo husika, basi huyuo Mwalimu Mwalimu ajira yake huwa hatarini. Ninayo majina ya walimu waathirika na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu la Liwale ambako CCM ni Chama cha Upinzani, ushauri wangu ni kwamba tuwaache Walimu wabaki madarasani. Pamoja na changamoto nyingi tunazokabiliana nazo ili kujikwamua kutokana na umasikini uliokithiri mahitaji ya Chuo cha *VETA* Liwale ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na Chuo cha Walimu, kwani Walimu wanaotoka nje ya Mkoa wetu wa Lindi wanashindwa kukaa Liwale. Vilevile tunaomba Kituo cha Chuo cha Utalii ili kukuza utalii Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule za Jimbo la Liwale hazina Wakaguzi na wale wachache waliopo hawana vitendea kazi. Hawana gari hata moja la ukaguzi wala pikipiki. Tunawezaje kuwa na elimu bora, elimu ambayo haisimamiwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupanda kwa madaraja ya Walimu kuzingatie kiwango cha elimu. Hakuna utendaji ulio bora kama Mratibu Kata ni

Form IV, Mwalimu Mkuu *Degree* au Mkuu wa Shule *Diploma*, Mwalimu *Degree*, hapo hakuna uwiano wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Elimu imeshusha kiwango cha elimu nchini. Leo watoto hawana mitihani ya *Mid-term*, mitihani ya wiki, *Mock* – Kata, *Mock* – Wilaya, wala *Mock* – Mkoa. Sasa hivi mtoto hupimwa mara moja tu kwa mwaka mzima. Utajuaje maendeleo ya mtoto anayefanya mtihani mmoja tu kwa mhula?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema mwenye kurehemu. Pia nampongeza Mheshimiwa Spika, yeye binafsi kwa kuwa makini sana kusimamia Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika meneo yafuatayo: maslahi duni ya Walimu, kubadilisha *syllabus* pasi kushauriana na Wizara ya Elimu Zanzibar; *NECTA;* kutolipatia stahiki somo la dini ya Kiislam mashuleni kuhusiana na ufaulu wa wanafunzi; shule za binafsi; mikopo ya elimu ya juu; kufuta mfumo wa *GPA* na kurejesha *divisions;* na elimu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na maslahi duni ya Walimu. Hapa ndipo hasa penye matatizo makubwa sana katika kada ya elimu. Walimu wanalipwa mishahara duni. Hii inapelekea sana Walimu kufanya kazi bila ya utulivu kwa sababu umasikini ni mwingi, wanashindwa hata kujikimu. Ingekuwa vyema maslahi ya Walimu yakaangaliwa upya. Mwalimu wa Tanzania amekuwa kama mshumaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubadilisha *syllabus* bila kushauriana na kupeana taarifa kwa wakati stahiki inasumbua sana. Wizara ya Elimu Zanzibar haishirikishwi wakati wa kubadilisha *syllabus* hasa kwa madarasa ya Kidato cha Kwanza hadi cha Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie chombo cha *NECTA*. Naomba nipatiwe majibu, Zanzibar inashiriki vipi katika chombo hiki? Ni vyema pangejengwa Ofisi ndogo basi ya *NECTA* kule Zanzibar ili kuzuia kwenda Dar es Salaam kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu ambao wanachaguliwa kusimamia mitihani ya *CSEE* wengi wao hawana sifa na kwamba masharti yanayotakiwa hayazingatiwi. Hii hupelekea kuwepo na matatizo mengi sana wakati wa kufanya mitihani hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubadilishaji wa mitihani (matokeo) kutoka *GPA* kwenda *Division* ni vyema ukaangaliwa tena kwa utafiti wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa kwenye shule binafsi. Shule ni nzuri na mimi binafsi ninakubaliana nazo sana. Ila ni vyema Serikali nayo ikazifanye shule zake ziwe na uwezo angalau kama hizi. Maabara za shule za Serikali ni vituko! Walimu wazuri wote wamepotelea katika shule za binafsi, matokeo mazuri yako ndani ya shule binafsi. Kuna nini hapo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasadikika kwamba somo la dini halipatiwi stahiki zake katika ufaulu wa kuendelea Kidato cha Tano. Naomba hapa nipatiwe jibu, ni kweli au la? Kama ni kweli, ni kwanini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mikopo ya wanafunzi wa Vyuo Vikuu ni vipi Zanzibar inapatiwa gawio lake na kwa wakati upi? Pia dhana ya elimu bure haijaeleweka ipasavyo? Ni vyema ikaelezwa vizuri sana na ikaonekana kiutendaji, naomba kuwasilisha.

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi au hotuba nzuri. Pia nimpongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni juu ya ujenzi wa Vyuo vya Ufundi. Katika hotuba ukurasa wa 59 umezungumzia juu ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Geita. Hili nalipongeza na ninashauri ujenzi uanze mara moja kutokana na mahitaji tuliyonayo katika Mkoa wetu. Mkoa una Wilaya tano na hatuna chuo hata kimoja katika Wilaya za pamoja na mpango wa ujenzi wa Chuo cha *VETA* Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe msisitizo pia kwamba Serikali ione umuhimu wa kujenga vyuo hivi katika Wilaya zetu. Sera ya Taifa ni kuwa na *VETA* kila Wilaya. Kwenye bajeti nimeona ujenzi wa *VETA* Wilaya ya Chato, tunapongeza, lakini Serikali ione uwezekanao wa kujenga *VETA* Wilaya ya Geita kulingana na wingi wa watu katika Wilaya yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaomaliza Shule za Msingi na Shule za Sekondari ni wengi ambao hawaendelei na elimu ya juu na hao wanahitaji ujuzi na ufundi stadi ili kuwawezesha kumudu maisha yao kiuchumi na mwisho wa siku wachangie katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ni madeni ya Walimu. Hii ni changamoto sana maana Walimu bado wana madai yao makubwa sana. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita na Mkoa wa Geita madai ni makubwa

na tayari madeni yamehakikiwa. Ili tuboreshe *morale* na ufanisi katika utendaji kazi kwa Walimu ni vema Serikali ikatilia mkazo katika kulipa madeni haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya tatu ni juu ya malalamiko ya wanafunzi wa *UDOM* kitengo cha Diploma ya Ualimu. Ni wiki ya nne sasa hawafundishwi kutokana na mgomo wa Walimu wao. Malalamiko haya yamewasilishwa na viongozi wa wanafunzi katika Kitengo cha Ualimu *UDOM* jana, ambapo walikuja hapa Bungeni kutoa shinikizo kwa Waziri juu ya hatma ya suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri kwa Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho hebu utoe kauli kuhusiana na jambo hili. Naomba ulifuatilie na ulitafutie ufumbuzi.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia Wizara ya Elimu, kwa kuwa elimu ndio jambo la muhimu sana. Bila elimu hakuna Daktali, hakuna *Pilot*, hakuna Mwalimu hakuna Rais, hata viwanda ambavyo tunavisema ni bure, wala barabara, hakuna chochote! Sasa Serikali iwekeze kwenye elimu, tusifanye wimbo elimu bure, tuwekeze kwenye mashule. Bado wanafunzi wanakaa chini, hawana vyoo, hawana maji, hawana vitabu, hasa vitendea kazi vyote hawana. Watoto hawawezi kukaa chini; wataweza kuwa na akili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa tabia kwa Mwalimu, anakaa hadi anastaafu bila hata daraja la kwanza. Heshima ya Walimu iko wapi? Kazi kulalamikia malipo, kulipwa stahiki zao. Kuna wanaostahili toka mwaka 2014 na ni wengi zaidi, unategemea hao Walimu watakuwa na akili ya kufundisha. Serikali ilipe stahiki zao ili tujenge elimu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye shule za binafsi tunaomba Wizara hii iangalie hata kama sheria nyingine ambayo itaweza kusaidia, tunasema watoto wapate elimu bure na karo zinakuwa juu. Hii watasoma watoto wa matajiri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madawati yaliyotajwa na Mheshimiwa Rais, nashauri, kwanini zisitolewe pesa kila Wilaya ya kutengenezewa huko huko kuliko kubebwa na kusambazwa? Je, hiyo gharama nyingine? Ni ushauri wangu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wanaopata ajira wanapangiwa sehemu ya mbali na Wilaya, wanapata shida kufuata malipo yao. Pamoja na hayo, wanapokwenda kufundisha mishahara wanakatwa hapo na nauli anakuwa amejikopa na pesa hakuna. Sasa ninachoomba, Walimu wanapewa ajira na kupelekwa kwenye Wilaya wapewe na mishaara ili iwasadidie huko

wanakokwenda kuanza maisha, hawana nyumba; kama kuna nyumba, hakuna choo; hayo ndiyo elimu bure? Elimu bure iko wapi bila miundombinu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto wa kike akibeba mimba kama wote ni wanafunzi anafukuzwa wa kike tu. Hiyo ni adhabu ya mtu mmoja. Nashauri wote wapate adhabu hata kama sio mwanafunzi mwenzake, wote wape adhabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za watoto wenye mahitaji maalum ziko vibaya sana. Mimi nilishatembelea baadhi ya shule hizo, kuna Mgeza Mseto; kuna Mgeza Viziwi Bukoba Mjini. Kuna shida kweli! Vitendea kazi hawana hasa mahitaji maalum yote, hawana kabisa. Naomba Wizara msiwe mnasikiliza Watendaji tu jamani, hata wewe Waziri una muda, uende na Kamati kuzunguka kuja kubaini matatizo yaliyomo kwenye elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho natoa rai yangu hiyo. Tukirudisha elimu, tutakuwa na utajiri, tumeshatatua matatizo yanayotukwamisha. Huo ndio mchango wangu.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mungu kwa kunipa afya njema na kumwezesha kuchangia hotuba hii. Elimu ni ufunguo wa maisha na Taifa. Ikiwa wananchi wake hawana elimu, basi Taifa hilo haliwezi kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu amesema, anayejua hawi sawa na yule asiyejua. Ni lazima anayejua ana upeo mkubwa wa kuona mbali. Kuhusu Walimu, wana kazi kubwa sana na wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wanapata changamoto nyingi katika mazingira ya kazi, kwanza kufundisha wanafunzi wengi katika Idara moja, upungufu wa vifaa vya kufundishia, ukosefu wa matundu ya vyoo, maji hawana, nyumba za kuishi hawana, usafiri hawana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetangazwa kwamba elimu ni bure, wakati bado miundombinu ni mibovu. Kwanza tuiboreshe. Naishauri Serikali kwamba bajeti ya Wizara hii iongezwe ili iweze kuboresha miundombinu, madarasa yaongezwe ili kupunguza msongamano wa wanafunzi, vyoo, madawati, nyumba za Walimu na mishahara ya Walimu pia iboreshwe ili waweze kutoa hiyo elimu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza, ikiwa mti huutunzi, hauna mbolea wala maji, utawezaje kutangaza tenda ya matunda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wanapofika muda wao wa kustaafu, wanapata usumbufu mkubwa kupewa mafao yao. Wastaafu hao hudai mafao yao mpaka wanafariki hawapati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iwatizame wastaafu hawa kwa jicho la huruma, pale tu wanapostaafu wapewe haki zao mapema ili wapate kuwasaidia katika maisha ya uzeeni na pia wapatiwe bima ya afya angalau waweze kuhudumiwa, kupata matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana kuwa mila potofu ya watoto wa kike kuchezwa unyago ni moja ya kichocheo kikubwa kupata mimba za utotoni, kwa sababu mtoto akishachezwa unyago, hujiona yuko huru na tayari amekamilika na kuingia katika daraja la ukubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipige marufuku kwa mtoto wa kike kuchezwa ikiwa bado ni mwanafunzi ili kupunguza tatizo hili. Vilevile sisi viongozi, wazazi, walezi tukemee kwa kupiga vita jambo hilo ili kumpa nafasi mtoto wa kike aendelee na masomo yake. Baadaye akimaliza kusoma atachezwa kama ndiyo mila zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Zanzibar, elimu ya juu bado kuna usumbufu mkubwa kuhusu mikopo ya wanafunzi. Wanacheleweshwa sana na hivyo kuchelewa kuanza kusoma. Tunaomba Serikali ya Muungano iweze kusimamia ili usumbufu uweze kuondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia, naomba kuwasilisha. Wako mjenzi wa Taifa.

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kwa maandishi katika Wizara hii. Kwanza nianze na suala la wabunifu wa teknolojia katika nchi hii. Nchi hii wapo watu ambao wana ubunifu wa kutumia teknolojia, lakini hawajulikani wala kutambulika na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa Kampuni ya *Young Scientist Tanzania* ambayo huwasaidia kuwaendeleza vijana chipukizi wa ubunifu na teknolojia, Kampuni hii mwaka huu imewapa tuzo vijana wawili wa Shule ya Sekondari Morogoro ambao ni Edmund na John Method. Pia vijana hao Kampuni imewapelekea kusoma *Dublin University* huko *Ireland* kwa ajili ya kuendeleza vipaji vyao vya ubunifu na ufumbuzi wa teknolojia. Nashauri Serikali iwe inafuatilia vijana wabunifu kama hawa ili wanapomaliza masomo yao, Serikali iwashawishi kurudi nchini ili kutumia ujuzi wao kusaidia maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuboresha mishahara ya Walimu pamoja na mazingira ya kufanyia kazi kama vile nyumba, umeme na maji. Hii

itaondoa upungufu wa Walimu mashuleni hususan shule za pembezoni mwa Miji. Walimu wengi wanapopelekwa au kupangiwa na Serikali shule za vijijini huwa hawaendi kutokana na mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inahitaji kuongeza juhudi katika kutoa elimu bora ili kushindana na nchi nyingine duniani. Nasema hivi kwani wanafunzi wengi humaliza Kidato cha Nne ambayo ni elimu ya awali bila kujua kusoma na kuandika vizuri, lakini pia hata kutokuwa na uwezo na kujieleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwasilisha mchango wangu katika sekta hii. Napenda kuwasilisha mawazo yangu juu ya elimu hasa katika kupanga ada elekezi katika shule binafsi. Ni kweli nchi etu imekuwa na utoaji wa elimu ya Serikali na sekta binafsi katika shule za Serikali. Hilo liko wazi katika ada kwani ni bure, lakini shule binafsi ni shule ambazo wazazi hupeleka watoto kwa matakwa yao bila kulazimishwa na mtu yeyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu mimi siyo tatizo kwa ada wapangazo, tatizo langu, naiomba Serikali ifuatilie kwa kina kama ada watoazo ni sawa na huduma wapatazo. Maana haiwezekani ada iwe kubwa lakini mahitaji muhimu hayalingani na gharama wazilipazo. Hivyo tunaiomba Serikali ifuatilie kwa kina kama ada zinaendana na huduma zenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwasilisha mawazo juu ya ada zinazotozwa na Vyuo vyetu katika kozi mbalimbali. Mfano Chuo cha Taifa cha Usafirishaji *NIT* katika fani ya *Aviation,* ada yao ni shilingi milioni 10 ambayo kwa mtoto masikini wa Kitanzania ni bei kubwa sana ambayo hawezi kumudu. Huo ni mfano tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo vyuo vingi mfano *SAUTI* Mwanza, *AMUCTA* Tabora, *Tumaini University, Dar es Salaam* na vinginevyo vimekuwa vikitoza ada kubwa katika fani za sheria na nyinginezo tofauti na ada katika Vyuo vya *UDSM* na *UDOM* huku vyuo hivi vikipata RUZUKU toka Serikalini. Hili halikubaliki, kwani kwa muda fulani wanafunzi wa vyuo hivi waligoma wakidai ada zishuke. Hivyo tunaomba Wizara ilitazame maradufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Wizara kutoa marupurupu ya ziada kwa Walimu wanaofanya kazi katika maeneo hatarishi kama Wilaya za Igunga, Nzega, Uyuyi na nyinginezo ili kupunguza wimbi la Walimu kuhama katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sera ya Elimu, inataka kila Wilaya kuwa na *VETA,* hivyo tuombe Wizara itupe *support* katika hatua tulioifikia ya uanzishaji wa

VETA katika Wilaya yetu ya Igunga. Tumejenga madarasa manne yenye ubora, hivyo basi, katika upungufu wetu tuiombe Wizara itupe ushirikiano katika kufukia azma ya Sera ya Elimu ya Juu na uwepo wa *VETA* katika Wilaya. *VETA* ya Manonga Wilaya ya Igunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya yetu tuna ujenzi wa Maabara ambapo nyingi zimekamilika lakini tatizo ni vifaa vya Maabara. Tunaiomba Wizara katika Jimbo la Manonga itusaidie vifaa vya Maabara ili iturahisishie upatikanaji wake ili wanafunzi wetu waweze kupata huduma hii ya kusoma kwa vitendo. Shule zote Kata ya Chomachenkole, Ziba, Mkinga, Simbo, Mwisi, Chabutua Ichama, Mtobo-Misana, Ngulumwa, Ndebezi, Igoweko, Mwashiku na Sungumizi tunaomba shule hizi zipatiwe vifaa vya kujifunzia ikiwa ni pamoja na vitabu vya *Arts*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapendekezo yetu tunaiomba Wizara itupandishie Shule za Ziba Sekondari pamoja na Mwisi Sekondari ili tuwe na Vidato vya Tano na Sita.

Hili linatokana na shule hizi kwamba ni za Tarafa hapo awali, lakini kutokana na kuwa mazingira ya shule hizo ni mazuri sana ikiwa na ukubwa wa zaidi ya ekari 50 kwa shule ya Mwisi na zaidi ya ekari 10 kwa Shule za Ziba, lakini pia kijiografia shule hizi zimekaa pazuri kwa kuwa tayari kuhudumia wanafunzi wa ndani ya Wilaya hata nje ya Wilaya kutokana na maeneo hayo kuwa na huduma mbalimbali za kijamii. Hivyo, kwa Wilaya yetu ya Igunga kuwa shule hizo zitakuwa zimesaidia kupunguza uhaba wa shule hasa ikizingatiwa kwamba Igunga tayari tuna Shule ya Igunga *Day* na Nanga.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri. Napenda kuchangia katika suala zima la nyumba za Walimu hasa wale wanaoishi vijijini.

Pia ujenzi wa vyumba vya madarasa ya sekondari na msingi hasa ukizingatia katika Wilaya ya Lushoto kuna maeneo mengi vijijini hayana shule kabisa. Watoto wanatoka zaidi ya Kilometa 20 hadi 25. Wakati wa mvua nyingi watoto hawa hawaendi shule mpaka mvua itakapopungua.

Naiomba Serikali yangu Tukufu ijenge shule kwenye maeneo hayo, mfano Lushoto Makanya Kagambe, Mazumbai, Ngindoi, Muheza na Mlola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wetu wanapata mishahara midogo sana ambayo haikidhi haja zao. Naiomba Serikali yangu Tukufu iangalie jinsi gani ya kuwaongezea mishahara Walimu wetu hawa. Pamoja na stahiki zao, walipwe kwa wakati hasa hizi za uhamisho. Sambamba na hayo, makato ya Walimu yamekuwa mengi. Naiomba Serikali yangu ipunguze makato hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la vitabu mashuleni pamoja na miundombinu kwa ujumla. Pia Walimu hawa wapandishwe madaraja kwa wale wote wanaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala la *VETA* ni suala ambalo lipo kwenye ilani, kila Wilaya iwe na *VETA*. Wilaya ya Lushoto ni miongoni mwa Wilaya ambazo hazina Chuo cha *VETA*. Naiomba Serikali ikafungue chuo cha *VETA* Lushoto na kwa bahati nzuri kuna majengo ambayo yako tayari, kwani ni kuongea na TAMISEMI wawape majengo waliyoyaacha na kuhamia kwenye jengo lao jipya. Nia na madhumuni ni kusaidia vijana wetu hawa ambao hawakuweza kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naishukuru Serikali yangu kwa kutoa mikopo kwa wanafunzi hao, lakini wanafunzi hawa wanapomaliza vyuo, Serikali haiwapatii ajira vijana wetu hawa. Hapo hapo Serikali inatangaza wote ambao wamesoma Vyuo Vikuu kwa mikopo wanatakiwa warejeshe mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe binafsi najiuliza, vijana hawa bado hawajapata kazi na huu mkopo wataurudishaje? Naiomba Serikali yangu Tukufu iwapatie Vijana hawa ajira ndiyo waanze kulipa mikopo hiyo. Pia Serikali ijue ya kuwa kuna kundi kubwa sana la vijana ambao wapo mtaani hawana ajira. Kwa hiyo, ni muhimu sana kujenga vyuo vya *VETA* vijana wetu wakimaliza waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri aniangalie kwa jicho la huruma aniletee Walimu wa sayansi. Mungu akubariki mama yangu Mheshimiwa Profesa Ndalichako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anitembelee katika Wilaya ya Lushoto.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri mambo kadhaa katika Wizara hii muhimu katika maendeleo ya nchi yetu ili kuleta tija kwa kizazi hiki na kizazi kijacho, kuboresha maslahi ya Walimu kulingana na umuhimu Mwalimu katika kuboresha elimu nchini ni lazima Mwalimu aweze kulipwa stahiki zinazostahili kulingana na hali halisi ya maisha kwa sasa. Kulipa madai ya Walimu kwa wakati kulingana na Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wanapocheleweshwa kulipwa madai yao kwa wakati inapelekea Walimu wetu wengi kukosa utayari wa kufundisha kama ilivyokuwa mwanzo, wanakata tamaa. Mfano, Manispaa ya Sumbawanga iliyoko Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tabia ya kutowalipa Walimu pesa ya likizo na kupelekea kuona kama wanatengwa. Suala la Afisa Elimu kumwadhibu Mwalimu, hali hii imeendelea kuonyesha manyanyaso makubwa kwa Walimu wetu kwa mfano dalili iliyojitokeza hivi karibuni katika Wilaya ya Sumbawaga Mkoa wa Rukwa. Serikali inachukua hatua gani kwa Afisa Elimu huyu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuleta ufanisi katika Wizara ya Elimu katika Taifa letu, suala hili la kodi kwenye Wizara hii imepelekea ada kuwa kubwa zaidi na hivyo Watanzania wa hali ya chini kushindwa kumudu katika ada husika. Mwingiliano wa Wizara kuwa na chanzo cha tatizo kutokana na changamoto nyingi zinazowapata Walimu wanafuzi pamoja na miundombinu kutokana na mambo hayo kutoshughulikiwa na Wizara moja, imekuwa changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Kitengo cha Ukaguzi kutokuwa na vifaa vya kuweza kuwafikia Walimu na kutimiza majukumu yake na kupelekea kuleta matokeo chanya katika Wizara moja ambayo itashughulikia haya yote, suala la mikopo katika Elimu ya Chuo Kikuu kuna vigezo gani vinavyotumika kutoa mikopo hii ambayo imekuwa na malalamiko makubwa hasa kwa watoto wanaotoka familia za kimasikini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI, upandishwaji wa madaraja katika Sekta hii ni lazima Wizara ifanye marekebisho. Suala hili linaleta mkanganyiko mkubwa hasa katika Manispaa ya sumbawanga. Hii ilitokana tu na uzembe wa vyombo husika. Hatua zichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Waraka Na. 5, elimu bure, liende sambamba na miundombinu, ada elekezi kulipa madai yote ya Walimu, mikopo hata kwa Walimu walioamua kujiendeleza ili kuondokana na ujinga na kukomboa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha elimu tujiulize mambo yafuatayo katika Wizara hii ya Elimu. Nini chanzo cha elimu yetu kushuka? Nini kinazuia kulipa madai ya Walimu? Kwa nini Walimu hawawezeshwi katika matibabu? Kwa nini mitaala yetu ni tatizo? Kwa nini ada elekezi leo? Lini Wizara itatoa Motisha kwa Walimu wa vijijini? Ni lini Serikali italeta mashine ya kuchakata vyeti nchini?

MHE. SALMA M. MWASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja kwenye Wizara hii ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi.

Kwanza niongelee upunguzfu wa Walimu wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Lugha. Pamoja na jitihada za Serikali za kuwapeleka Walimu

wachache kwenye mafunzo ya masomo ya Hisabati na Sayansi lakini bado idadi ni ndogo ukilinganisha na udahili mpya wa wanafunzi katika kipindi hiki cha elimu bure kutoka Elimu ya Msingi hadi Sekondari. Hivyo nashauri Serikali iangalie upya mpango wa kuongeza Walimu hasa katika masomo haya ya Sayansi, Hisabati na Lugha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee pia miundombinu. Kuna tatizo la upungufu wa miundombinu na udhaifu wa miundombinu.

Kwa mfano, upungufu wa madarasa, maabara, nyumba za Walimu na vyoo hasa kwa Mkoa wa Dar es Salaam. Kutokana na idadi ya kubwa ya wanafunzi katika Mkoa wa Dar es Salaam kuna upungufu mkubwa wa madarasa, nyumba za Walimu, madawati na vyoo hasa kwenye Shule za Msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niongelee ubora wa elimu. Ubora wa elimu yetu hasa kwenye shule zetu za Serikali siyo mzuri. Nashauri Walimu wapelekwe Semina na Ukaguzi wa shule ufanyike mara kwa mara ili kuboresha ubora wa elimu. Napenda kujua kutoka Serikalini ni lini shule za Serikali zitaanza kuwa kwenye kumi bora katika mitihani ya Taifa? Kwani sasa shule zinazoongoza ni za binafsi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nakupongeza sana kwa hotuba nzuri sana yenye ufafanuzi mzuri sana wa Sekta ya Elimu. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Wizara ya Elimu na Wizara ya TAMISEMI washirikiane kuhakikisha kwamba suala la madawati linakwisha na wanafunzi wote kuanzia Shule za Msingi na Sekondari wanakaa kwenye madawati siyo kukaa chini. Hii inaathiri sana taaluma na ni suala la aibu, karne ya 21 bado wanafunzi wanakaa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Mpwapwa Sekondari *(Mpwapwa High School)* ilianzishwa mwaka 1926. Hivi sasa shule hiyo imechakaa sana na haifanani kabisa na hadhi ya Shule ya Mpwapwa Sekondari ya zamani. Je, Serikali ina mpango gani wa kuzikarabati Shule za Sekondari Kongwe kama vile Mpwapwa Shule ya Sekondari, Msalato Sekondari na Kilakala Sekondari? Nashauri suala hili wasiachiwe Wizara ya TAMISEMI peke yao, lazima na Wizara ya Elimu ishiriki kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinazotengwa kwa ajili ya chakula cha wanafunzi wa sekondari za bweni ni kidogo sana na kusababisha kila mwanafunzi kupata shilingi 1,500/= kwa siku, yaani chai/uji, chakula cha mchana na jioni. Hela hiyo haitoshi kabisa, dola moja kwa siku. Nashauri Serikali iongeze angalau ifike shilingi 2,500/= kwa kila mwanafunzi wa bweni. Wanafunzi lazima wapate chakula ambacho ni *balanced diet (carbohydrates, vitamins* na *proteins)* siyo ugali na maharage kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kufutwa kwa ada, wananchi wamelipokea suala hilo kwa furaha sana na uandikishaji wa wanafunzi Darasa la Kwanza umeongezeka sana kuliko ilivyokuwa mwanzo. Waliogopa ada na michango mbalimbali. Shule ya Sekondari ya Mpwapwa ni Kongwe lakini mpaka sasa haina gari na ni muda mrefu sana. Je, ni lini shule hii itapatiwa usafiri wa gari? (wapo Wanafunzi 600)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Ualimu cha Mpwapwa kilianzishwa mwaka 1926. Chuo hicho kinahitaji ukarabati mkubwa zikiwemo nyumba za Walimu. Kuna baadhi ya nyumba hazijafanyiwa ukarabati, sasa ni zaidi ya miaka 20, zimechoka sana. Ni lini Chuo na nyumba za Walimu zitafanyiwa ukarabati mkubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa Walimu katika shule zote za Sekondari za kutwa, naishauri Serikali ihakikishe kila shule iwe na Walimu wa kutosha na wa masomo yote ili kuboresha taaluma katika shule hizo. Maslahi ya Walimu yalipwe mapema ili kupunguza malalamiko ya Walimu. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mhshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Awali ni muhimu sana katika kumwandaa mtoto kuanza Darasa la Kwanza kwa mwaka unaofuata, hivyo ni vyema Walimu wa kufundisha watoto hawa wakawa rasmi na kupewa cheti cha kufuzu masomo hayo kwa kufaulu badala ya kuchukua Walimu waliochoka, wasio na taaluma hiyo kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Ufundi ni nyenzo muhimu sana kwa vijana wetu ambao hawakubahatika kuendelea na masomo ya elimu ya juu, hivyo ni jambo la muhimu vijana hao wakapata mafunzo ya ufundi ili elimu hiyo iwasaidie katika kumudu maisha yao, pia kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa Taifa lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tutambue kwamba sera ya Serikali ni kwamba kila Wilaya kuwa na Chuo cha Ufundi *(VETA)* angalau kimoja. Je, sasa

nataka Mheshimiwa Waziri anieleze ni lini sasa Wilaya ya Sumbawanga vijijini itajengewa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi *(VETA)?* Ni lini Mkoa wa Rukwa utajengewa Chuo cha Ufundi *VETA*? Naomba majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ianzishe haraka Kidato cha Tano na Sita ili kwenda sambamba na uanzishaji wa sekondari kila Kata ili wanafunzi wanaomaliza Kidato cha Nne wapate nafasi ya kuendelea na Kidato cha Tano na cha Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia sana na hasa kwa familia masikini ambao wazazi wao hawana uwezo wa kuwapeleka mbali. Nitolee mfano wa Wilaya ya Sumbawanga vijijini, inazo Shule za Kata zinazofika Kidato cha Nne 19, ikiwa tunayo shule moja tu ambayo imepandishwa kufikia Kidato cha Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Mheshimiwa Waziri atukubalie kupandisha shule zifuatazo kufikia Kidato cha Sita; *Vuna Secondary School*, *Mazoka Secondary School*, *Mzindakaya Secondary School*, *Milenia Secondary School*. Naomba majibu ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitengo cha Ukaguzi kimezorota sana ukilinganisha na ilivyokuwa hapo awali, hivyo kitengo hiki kiimarishwe kwa kupewa vitendea kazi kama vile, magari pikipiki, vifaa vya Ofisi na Ofisi zao zijitegemee bila kuingiliwa, kuwe na mafunzo ya mara kwa mara, fungu la kutosha kwa maana ya *OC* ili kuwezesha kitengo hiki kufanya kazi vizuri na kwa uhuru bila mashindikizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapaswa kujipanga juu ya ujenzi wa hosteli ili kunusuru vijana wetu na hasa watoto wa kike ili kuwapa fursa nzuri ya kusoma na kuwaepusha na vishawishi wanavyovipata wanapokuwa huru katika mazingira ya uraiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamejitahidi sana katika ujenzi wa maabara, hivyo tunaomba Serikali itoe vifaa vya maabara ili kuboresha na kuiimarisha, vijana wetu waweze kupata elimu bora katika masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali itoe posho kwa Walimu wanaokwenda kukaa katika umbali na ukosefu wa huduma muhimu kama vile umeme, mabenki, mawasiliano na usafiri. Naunga mkono hoja.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, nahitaji kuchangia katika maeneo machache kutokana na udhaifu na nini kifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu matatizo ya elimu duni nchini na kufeli kwa wananfunzi hasa katika Mikoa inayofanya vibaya kama Mikoa ya Tanga, Tabora na Mikoa ya Kusini. Hii inasababishwa na Walimu kukosa makazi mazuri kwa ujumla na hivyo Walimu kukosa moyo wa kufundisha katika shule walizopangiwa hasa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukosefu wa miundombinu hiyo na umbali mrefu kufika mjini. Mfano, Mkoa wa Katavi inamchukua Mwalimu muda mrefu kufika mjini kufuatilia madai yake kutoka kijijini mpaka mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madai ya Walimu, hili limekuwa ni tatizo kwa nchi nzima. Walimu wanachukua muda mrefu kulipwa madai yao, madeni ya nyuma na kadhalika. Hii imesababisha Walimu kupoteza muda mwingi wakiwa mijini kufuatilia madai yao na hivyo kushindwa kufundisha na muda wa kufundisha wanafunzi unapotea bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kifanyike? Naomba sasa Wizara iweke mipango kwa namna ya kusaidia Walimu hawa wasipoteze muda mrefu mijini kufuatilia madai yao na hivyo wajikite zaidi kufundisha wanafunzi hawa ambao wanasoma katika mazingira magumu. Uchache wa Walimu na Walimu kuishi katika mazingira magumu, hivyo Serikali sasa ihakikishe utekelezaji wa ujenzi wa nyumba za Walimu kwa wakati ili kuondoa usumbufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo la baadhi ya shule hasa vijijini kuendelea kuwanyanyapaa wanafunzi ambao wanakuwa wamepata mimba kwa bahati mbaya (mimba za utotoni) kutokana na mazingira ambayo wanafunzi hao wanatoka. Nini kifanyike? Serikali itoe agizo sasa ili wanafunzi hawa waliojifungua mashuleni, warudishwe waendelee na masomo na wasinyanyapaliwe. Pia Serikali iweke mpango mkakati wa kuhakikisha wanafunzi hao wanaonyonyesha wawe na darasa lao maalum ili wawe huru na wale wasionyonyesha wasije kuharibika kisaikolojia kutokana na kuchangamana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa mabweni ya wanafunzi umekuwa ukisuasua na kusababisha wanafunzi kukosa huduma nzuri za malazi na hivyo wanafunzi kutokana na umbali kushindwa kuingia darasani (utoro) na kusababisha wanafunzi kufeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Serikali iwape nguvu wananchi katika baadhi ya maeneo ambao tayari wananchi wamechangishana pesa kwa ajili ya ujenzi wa mabweni na hivyo wameshindwa kumaliza. Sasa Serikali ione umuhimu sasa wa kuwasaidia wananchi maana wamebeba majukumu ya

Serikali, isiwapuuze wananchi, imalizie majengo hayo (Mabweni) ili kunusuru wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya shule za binafsi zimekuwa zikitoza ada kubwa na kuwaumiza wananchi. Hivyo Serikali iangalie upya ada hizi katika shule binafsi.

MHE. ELIAS J. KWANDIKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara hii kupigania ongezeko la bajeti, pia irekebishe sura yake ya bajeti. Haya ni maoni yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti yetu bado ni ndogo sana, shilingi trilioni 1.4; ni vema tufuate azimio la Abuja *(E.F.A Goals)*. Bajeti ya Elimu ifike ifike 6% ya Tanzania GDP. Mfano, bajeti ya mwaka 2014, *GDP* ilikuwa inakadiriwa kuwa trilioni 100+, hivyo bajeti ya elimu ingekuwa shilingi trilioni 6.055.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bajeti ya Elimu kwa matumizi ya kawaida, kujumuisha mikopo ya wanafunzi, nashauri siyo vema bajeti ya maendeleo kujumuisha mikopo ya wanafunzi; hii ina-*mislead budget structure* ya Wizara. Mbona ununuzi wa magari inawekwa kwenye matumizi ya kawaida?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Idara Ukaguzi wa Elimu itengewe bajeti ya kutosha na iongezewe rasilimali za kutosha ikiwemo rasilimali watu. Kwa sasa mawanda ya ukaguzi ni madogo, yaani asilimia 20 tu. Ni vema ukaguzi uweze kufikia angalau asilimia 30, itasaidia kugundua mapungufu na kufanya marekebisho mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara hii ifanyie kazi tafiti zilizofanyika pamoja na ripoti za *CAG* hususan maeneo ya *value for money,* audit *(VFM Audit)*. Mfano, wanafunzi kutofanya vizuri masomo ya hisabati, viwango vya ufaulu kwa watoto wa kike na kadhalika, Wizara ifuatilie maoni hayo ili tufanye vizuri na kuinua viwango vya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kuanzisha Shule za *High School* katika Jimbo la Ushetu hususan Shule za *Bulungwa Secondary School* (Kata ya Bulungwa) na *Mweli Secondary School* (Kata ya Ushetu). Mimi Mbunge na wananchi tutahamasishana kuongeza madarasa na mabweni, naomba Wizara mtuunge mkono. Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo na utaratibu wa kurudisha vyeti vya vyuo kwa wale wanaopotelewa vyeti vya *NECTA* pale aliyepotelewa akiwa na ushahidi usiotia shaka wa kupotelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ada elekezi za shule hazitekelezeki labda vitu kama michango ya majengo kwa shule binafsi yapigwe marufuku. *Private investiment* inawahusu vipi wazazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuanzishwe Bodi ya Elimu na Walimu wasajiliwe na wawe *responsible* nayo hasa mambo yanayohusu maadili. Vyuo Vikuu viwe *categorized* kwa *level* zake lakini viwe na *specialize* hata kama kutakuwepo na kozi nyingine zaidi, lakini chuo kijulikane kwa *specialization* moja au mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Sera ya Elimu iangaliwe upya, kwani jamii tuliyonayo leo ya vijana kutopenda kazi, kusema uongo na unafiki ni zao la sera isiyokuwa na dira ya wapi tunaenda na nini tunataka ku-*achieve*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango kisichoridhisha cha mshahara wa shilingi 570,000/= haiwezi kukidhi maisha ya mtu, lazima Serikali ibuni njia nyingine za kuwasaidia Walimu vitu kama *Transport Allowance, Accommodation Allowance na Teaching Allowance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upandishwaji wa madaraja kwa Walimu unachukua muda mrefu sambamba na malipo ya vyeo hivyo vipya.

Vile vile nashauri kuwepo na chombo cha kusikiliza rufaa za wanafunzi ambao huwa wanakata pale wanapokuwa hawajaridhishwa na usahihishaji wa *NECTA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Wizara ibuni namna nyingine ya kutambua uwezo wa wanafunzi kwani njia moja tu ya mtihani siyo sahihi. Pia kuna uwezo na vipawa mbalimbali nje na kukariri majibu ya mtihani, kila mtu awe *awarded* kwa uwezo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wa *Nursery School* wasajiliwe na watambuliwe rasmi katika mfumo wa Walimu. Jiji la Tanga ni kati ya mikoa iliyosahaulika na kuwa na vyuo vichache vya Serikali.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *VETA* Wilaya ya Rungwe; Katika Wilaya ya Rungwe hatuna chuo cha ufundi na hii inatupa shida sana katika kuwaendeleza vijana wetu waliomaliza Darasa la Saba na Kidato cha Nne. Rungwe ni Wilaya yenye kutegemea kilimo sana hivyo uanzishwaji wa *VETA* kutasaidia vijana kujifunza elimu ya usindikaji wa mazao, ufundi wa kutumia mzao kama mahindi, migomba majani yake na kuwezesha kupatikana ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mabweni Wilaya ya Rungwe, upatikanaji wa mimba za utotoni ni shida sana katika Kata za Kyimo Masukuru. Je, Wizara haioni umuhimu wa kuwezesha Halmashauri ziweze kujenga mabweni ili kupunguza vishawishi, ulinzi kwa watoto wa Kata hizi. Nashauri Mkoa mpya wa Songwe upatiwe umuhimu wa kuanzisha vyuo, vikiwemo vya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Chuo cha Ualimu Mpuguso. Majengo ni chakavu kabisa idadi ya wanafunzi mabwenini siyo nzuri, miundombinu haifai, vitabu havitoshi kabisa. Pia shule ya sekondari Ndembela, Halmashauri imekuwa na deni la shule ya sekondari Ndembela takribani milioni 700 toka kanisa la Adventista Wasabato barua ya maelezo ya msaada ipo katika Wizara ya Elimu mimi nakumbusha Wizara ione umuhimu wa kulipa deni hilo na kuweka *commitment* kulibeba deni hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho na nauli za walimu. Walimu wamekuwa na madeni mengi sana Serikalini, pesa zao za likizo na nauli wafanyapo kazi nje ya kituo wengi wamekopwa na Serikali kwa muda mrefu sana. Kupandishwa madaraja pia imekuwa tatizo kwa walimu kukaa muda mrefu sana na pesa zao za uhamisho pindi wakipata uhamisho posho hizi zilipwe haraka.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuchangia hotuba ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Ufundi kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu bure ukweli kabisa sera hii imezibagua shule za Kata za kutwa na zile shule za Serikali ambazo zinahudumiwa kwa chakula kwa mabweni yaliyojengwa na wananchi na watoto/wanafunzi kukaa bweni wakati shule hizo bado zinaitwa za kutwa na hawapewi fedha za kununuliwa chakula kutoka nyumbani.

Hivyo ni vema suala hili likaangaliwa upya namna ya kusaidia shule hizo zenye mabweni zipewe chakula kama nyingine za Serikali. Wapiga kura wetu wanapiga kelele juu ya ubaguzi huo wa shule za bweni za wananchi hivyo kuongeza mzigo wa michango ya chakula. Shule hizo ni nyingi sana zilizopo kwenye Kata mbalimbali nchini kuliko shule za Serikali za bweni mfano Semeni, Likumbule, Wamasakata, Walasi, Malumba na Mbega Mchiteka Wilayani Tunduru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya posho za likizo za Walimu na madai ya zabuni mbalimbali. Kuna madai mengi hawajalipwa walimu katika shule mbalimbali kutokana na posho za likizo, uhamisho na posho nyingine mbalimbali. Kuna chuo cha maendeleo Nandembo watumishi wanadai 7,164,000 na wazabuni wanadai 5,447,000 na wametishia kusitisha kutoa huduma zao na kuna mtumishi mmoja Saidi Salanje alifariki mwaka 2011 lakini

warithi wale hawajapata mafao yao ya kiinua mgongo mpaka leo hii. Ni vema madai hayo yakashughulikiwa mapema ili kuondoa malalamiko na kero zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukarabati shule za sekondari za Serikali, majengo ya shule za sekondari Tunduru, masonya na Frank Wiston zilijengwa muda mrefu zaidi ya miaka 30 iliyopita lakini hakuna ukarabati wowote uliofanyika katika majengo na yanatishia usalama wa wanafunzi na walimu wao. Hivyo, tunaomba majengo hayo yafanyiwe ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa walimu wa shule za msingi na sekondari; Kuna upungufu mkubwa sana wa walimu wa sekondari hasa wa sayansi karibu shule zote za sekondari zilizopo Tunduru na walimu wa shule za misingi takribani mia tano jambo ambalo linashusha kiwango cha ufaulu wa watoto wetu katika masomo ya sayansi. Tunaomba tupewe kipaumbele cha kupewa walimu katika ajira ya mwaka 2016/2017 ili kupunguza pengo hilo na mwaka 2015/2016 hatukupewa hata mwalimu mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa vya kufundishia tunaomba Serikali kuliingilia kati suala la vifaa vya maabara ili watoto/wanafunzi wajifundishe kwa vitendo badala ya kuwaachia Halmashauri zetu, kwa sababu uwezo wa Halmashauri nyingi kupata vifaa hivyo kwa kutumia mapato ya ndani ni mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuboresha walimu kimasomo. Tunaomba Serikali itoe fursa kwa walimu wa vijijini kujiendesha kielimu ili kuwapa motisha wa kazi zao za kila siku. Ni vema kuimarisha vyuo vya Ualimu ili kupewa elimu na ujuzi wa kufundishia.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri na Naibu wake pamoja na timu nzima ya Wizara kwa kazi nzuri na hotuba nzuri ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia ya leo ni kama kijiji, hivyo suala la elimu ni muhimu sana kuliko wakati wote uliopita. Tulizoea kulinganisha ubora wa bidhaa *(product competitions)* kwa *brand 'nation brand'* Elimu bora ni muhimu sana kwa nchi yetu kuwa na *nation competitive advantage*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza mindombinu na mitaala ya elimu iboreshwe kulingana na dunia ya leo. Napendekeza elimu kwa vitendo ianze toka shule za msingi elimu ya vitendo ijikite kwenye kilimo ufundi, ujasiriamali na TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za Mashariki ya Mbali, *(tiger countries)* zimefanikiwa sana kwenye uchumi wao kutokana na elimu bora ikiwa na nafasi

kubwa katika orodha ya sababu za hayo mafanikio yao. Pamoja na muundo wa elimu ya nchi yetu napendekeza Wizara iweke mikakati ya kuboresha miundombinu na maslahi ya Walimu. Tunapoenda kwenye uchumi wa kati elimu ni muhimu sana hasa elimu inayowatayarisha vijana kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kwa ufupi tu kuhusiana na maombi yangu ya kupandisha hadhi Chuo cha Maendeleo ya Jamii *(FDC)* kilichopo Tarime Mjini kuwa *VETA*. Chuo hiki kwa sasa kinatoa huduma kwa wananchi wa Tarime nzima Rorya na Serengeti. Hivyo ili kuendana na azma ya Serikali ya Tanzania ya viwanda ni lazima vyuo vya ufundi viwe vingi. Tumekuwa tukiomba chuo hiki kuwa cha ufundi ili tuweze kukidhi hitaji la muda mrefu wa kuwa na chuo cha ufundi, tutashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni wimbi kubwa la walimu toka Kenya wanakuja kufundisha shule binafsi za Tarime. Hiyo tunaomba Wizara iingilie kati maana tunao Walimu wa kutosha kuweza kuajiriwa, hivyo vibali vinatolewaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa elimu kuanzia sera za elimu, mitaala yetu pamoja na miundombinu yetu, inatoa taswira pana ya nini tufanye kama Taifa kwa ufupi tu. Tarime tumejenga Maabara hatuna vifaa wala wataalam wa maabara, tuna uhaba wa Walimu wa Sayansi na ndiyo maana watoto wanafeli. Tusiangalie *Quantity* tuangalie *Quality*. *if we need to have quality education then input* lazima ziwe *effective*. Madaftari, vitabu, madawa, madawati, walimu wenye *motivation,* nyumba za walimu na posho ya ziada, posho ya pango, posho ya safari na usafiri, kupandishwa madaraja, chakula mashuleni, ukaguzi wa shule zetu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi ni hayo, mengi yamechangiwa naomba kuwasilisha.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda wa kuchangia moja kwa moja ni mfupi ninachangia baadhi ya mambo kwa maandishi. Ninaunga mkono hoja. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake, pia ninampa pole Naibu Waziri Mheshimiwa Stella Manyanya kwa kufiwa na mama, Mungu amrehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya elimu ndiyo itafafanua mustakabali wa Taifa letu. Kwa hiyo, wote tu wadau. Ninaunga mkono hoja lakini ninatoa maoni na ushauri ambao Waziri akiufanyia kazi itasaidia sana. Nitajielekeza katika maeneo yafuatayo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waraka Na. 6 wa 2015 kuhusu elimu una mapungufu. Wakati ninaunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais kwamba elimu ya msingi na sekondari ni bure, kwa maana italipiwa na Serikali ili kumpunguzia mzazi mzigo, ninashauri waraka huo uboreshwe. Ni wajibu wa jamii katika kuchangia elimu ili iwe bure huku miundombinu ikijengwa iweze kutekelezeka.

Hali ilivyo sasa inaonekana wajibu wa kuendeleza miundombinu umebaki tu kwa Serikali jambo ambalo ni mzigo mkubwa. Ushauri wangu ni kwamba wajibu wa kuchanga fedha za miundombinu elimu katika Kata uwe wa lazima katika jamii ili tusirudi nyuma. *Momentum* ya kuendeleza shule za Kata nazo ziwe na viwango. Duniani kote elimu huchangiwa na jamii, wazazi pekee hawawezi, Serikali pekee nayo ni vigumu kwa nchi kama yetu pamoja na nia nzuri sana ya Rais wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumuunge mkono kwa kuhamasisha jamii ijenge madarasa, hosteli, maabara, ofisi, vyoo na kadhalika. Aidha, jamii ichangie madeski na mahitaji mengine ya kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya walimu wa sekondari katika Wilaya ya Muleba yanaonesha upungufu wa walimu wa sayansi wakati wa sanaa wametosha na kuzidi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba Wizara itafute misaada ya walimu wote nje ya nchi ili shule ziwe na walimu. Mwaka 1960 Baba wa Taifa alitafuta msaada kutoka kwa Rais wa Marekani John Fitzgerald Kennedy walioitwa *Peace Corps* wakafundisha. Hatuwezi kuacha hii hali ambapo mwanafunzi anamaliza shule sekondari bila kumuona mwalimu wa hesabu. Naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza pia walimu wa ziada waondolewe katika shule za sekondari na pia kupelekwa shule za msingi ambazo bado hazina walimu wa kutosha. Aidha, katika *manpower planning* mahitaji ya walimu wa hesabu na sayansi zipewe kipaumbele. Walimu wanaweza kupewa *retrovining program* na kufundisha masomo yasiyo na walimu. Pia, unaweza ukaweka *mobile teaching teams'* za vipindi vya sayansi, walimu wachache waliopo wanatoka shule moja hadi nyingine. Pia kwa kuwa umeme na simu umesambaa uwezekano wa kutumia *distant learning* kutumia mtandao uangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili litasaidia pia kuboresha viwango. Kwa vyovyote vile walimu wasiohitajika shuleni waondolewe. Muleba imekuwa na tatizo la baadhi ya walimu wa Kiswahili na Historia wasio na vipindi wanabaki kwenye majungu na kuvuruga utulivu na nidhamu shuleni. Hii imetokea shule ya sekondari Bureza ambapo baadhi ya walimu wasio na vipindi vya kutosha

walivuruga nidhamu, jambo la kusikitisha baada ya ukaguzi kuliona hili na kupendekeza wahamishwe ni Mwalimu Mkuu aliyehamishwa katika mazingira yanayotakiwa kuchunguzwa. *District Education Officer* aeleze kwa nini ana muadhibu Mwalimu Mkuu anayefanya vizuri katika Wilaya nzima ili kuwafurahisha walimu wasio na nidhamu. Mheshimiwa Waziri afike Muleba aangalie hali duni ambayo tunayo hairidhishi na haitaleta tija wala matokeo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya kuanza shule kwa hali tuliyonayo vijijini chekechea ianze na miaka 5 hadi 6 na shule ya msingi miaka 7 hadi 8 la sivyo, watoto wanakuwa wengi sana darasani na ukizingatia udogo wa watoto na uchache wa walimu, *service ratios* hazikubali inakuwa na shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ada elekezi katika shule binafsi, mjadala huu ni wa kushangaza, Wizara ya Elimu ina kazi nyingi na mimi sielewi kwa nini hili litusumbue. Wazazi wapewe elimu ya kutosha kuhusu ubora au mapungufu ya shule binafsi wanapopeleka watoto wao ili wapate *value for money*. Lakini kuchukulia shule binafsi kwamba ni biashara ni kushindwa kutambua elimu bora ilivyo huduma. Mimi sina mgongano wa maslahi lakini mdau katika sekta ya elimu. Niko katika taasisi ya Barbo Johnson *Girls Education Trust- JOHA Trust* inayomiliki shule mbili za sekondari; moja Dar es Salaam nyingine Bukoba. Shule hizi siyo biashara kama wengi wanavyodhani; shule hizi ni huduma kuwapa wasichana elimu bora. Shule ina utaratibu wa kutoa ufadhili kwa wasichana wenye vipaji lakini ambao hawana uwezo kulipa ada. Katika shule za *JOHA trust* ada inatofautiana kati ya wanafunzi kulingana na uwezo wao kiuchumi inaitwa *assessed fees*. Kuna wanafunzi wanapewa ufadhili wote na kuna wanalipa kinachoitwa *fees* zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hawa wanapewa ruzuku ya karibu milioni moja kwa sababu gharama halisi ni shilingi milioni 5.5 na *full fees* ni shilingi 4.5 milioni kwa sasa. Mheshimiwa Waziri awasikilize watoa elimu na kuwasaidia. Ni aibu kwa *TRA* kushinda kwenye shule kudai kodi badala ya utaratibu mzuri zaidi kwa kodi za lazima kukusanywa.

Hali ya sasa hivi imelalamikiwa sana na siyo rafiki kwa watu wanaosaidia kuelimisha Taifa letu. Kama kuna shule binafsi ambazo hazina viwango wazazi watazigundua. Kazi ya Wizara ni kutoa taarifa za ufaulu wa wanafunzi na hapa *NECTA* imefanya kazi nzuri ila ninashauri *NECTA* iwe inatangaza *top* 100 *schools* siyo *top* 10 maana shule zimekuwa nyingi, kwa hiyo *top* 10 ni kasumba ya mazoea. Tujue shule bora 100 kwa ujumla na katika vipindi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitabu viwe vinafanana. Mwisho ninashauri kuwa elimu pia inasimiko utamaduni, sasa kama vitabu viko tofauti tutajengaje utamaduni wa Taifa, *culture harmony*. Ninashauri utunzi wa vitabu ubaki kama

ulivyo lakini Wizara iratibu na kuchagua vitabu vinavyofanya wanafunzi, kizazi au rika wawe na *common reference point* kupitia vitabu wavyosoma.

Mheshimiwa Spika naunga mkono hoja.

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nafasi ya Makamu Mkuu wa Chuo ni muhimu sana katika maendeleo ya Chuo Kikuu chochote. Kwa muda mrefu Chuo Kikuu Mzumbe kinaendeshwa na kusimamiwa na Kaimu Makamu Mkuu *(Acting Vice Chancellor),* ninaomba Wizara iharakishe na ikamilishe taratibu za kupata *Vice Chancellor* wa Chuo Kikuu Mzumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uhaba wa walimu wa awali kwa walimu wa awali ambao wamehitimu katika vyuo mbalimbali na wamekuwa wakijitolea kufundisha kwa muda mrefu ingekuwa vizuri waajiriwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya China ilibainishwa nia yake ya kushirikiana na Serikali yetu kujenga chuo cha Veta Mkoa wa Kagera. Naomba Wizara iongeze msukumo ili chuo cha *VETA* – Kagera kianze kujengwa. Eneo la kujega chuo hicho lipo na Balozi wa China Tanzania alishatembelea eneo hilo. Ninaomba pia Mheshimiwa Waziri akipata nafasi atembelee eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna walimu wengi ambao wanapandishwa madaraja lakini mishahara yao haibadilishwi, naomba Wizara ijitahidi kuhakikisha walimu wote wanalipwa stahili zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utaratibu wa kufundisha unaitwa *Montessori* utaratibu huu ni mzuri na una manufaa mengi ukilinganisha na utaratibu wa kawaida tunaotumia. Aidha, hapa Tanzania kuna vyuo vinavyofundisha kwa kutumia mfumo huu. Ninaomba walimu waliofundishwa kutumia mfumo wa *Montessori* waajiriwe na Seikali. Aidha, kwa kuanzia, madarasa ya awali yanaanza kutumia mfumo wa *Montessori* kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya A-*level* kisiwani Ukerewe; Wilaya ya Ukerewe ambayo inaundwa na Visiwa na kwa maana hiyo ki-jiografia iko vibaya lakini tayari Wilaya ina shule za sekondari za Serikali 22 na za binafsi 2. Lakini pamoja na historia ya Wilaya hii kielimu kuwa nzuri hasa kwa kuzalisha vipaji vingi bado hakuna shule ya kidato cha tano na kidato cha sita. Tayari Halmashauri imeandaa shule ya Bukongo sekondari na Pius Msekwa Sekondari kuzipandisha kuwa za *high school* na tayari kibali kimepatikana. Ninashauri Wizara itoe ushirikiano wa kutosha na kufanikisha

uanzishaji wa shule hizi ili kunusuru maisha ya vijana wengi ambao wanamaliza kidato cha Nne na kukosa nafasi ya kuendelea na kidato cha Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho ya mazingira magumu Ukerewe; kutokana na mazingira ya kijiografia kuwa magumu katika Visiwa vya Ukerewe, walimu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana na wakati mwingine wanapopangiwa kuja Ukerewe kwa mara ya kwanza, Serikali haitoi kwa wakati pesa za kujikimu hivyo kuwapa shida sana walimu wetu. Ninashauri Serikali kupitia Wizara hii itoe kwa wakati pesa za nauli na kujikimu kwa walimu wanaopangiwa vituo kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itolewe posho ya mazingira magumu kwa watumishi hasa walimu wanaofanya kazi katika Visiwa vya Ukerewe ili iwape motisha katika kukubaliana na changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upandishaji wa madaraja; Kumekuwa na malalamiko mengi sana toka kwa walimu yanayotokana na ucheleweshaji wa upandishaji madaraja sambamba na mishahara. Ushauri wangu ni kwamba Wizara ilisimamie jambo hili ili madaraja na mishahara vipandishwe kwa wakati kwa walimu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa walimu kiutumishi; Serikali kupitia Wizara ya Elimu iangalie upya namna ya muundo wa utumishi kwa walimu. Hali iliyopo sasa kwa walimu kusimamiwa na zaidi ya Wizara moja ni tatizo kwa watu hawa. Hivyo nashauri walimu wawe chini ya usimamizi wa Wizara moja tu badala ya hali ilivyo sasa ili kuongeza ufanisi wa kada hii.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Suala la Elimu; elimu ya Tanzania bado haijaboreshwa, ni tofauti na nchi jirani. Elimu ya Tanzania inasikitisha sana, ni lazima Tanzania tuwe na elimu bora ili wananchi waweze kukabiliana na changamoto za maisha. Ni vizuri Watanzania wapate elimu bora ili kujenga Taifa la watalaam wa sayansi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijijini hawana elimu bora, shule zipo mbali na makazi ya wananchi, hii inapelekea wanafunzi wa kike kupata mimba za utotoni kwani wanapoenda shule wanakutana na vishawishi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wa kike wanapata taabu sana, wanapokuwa wameingia katika hedhi; kwani shule wanazosoma hazina vyoo vizuri. Vyoo ni vibovu na pengine shule nzima hakuna, kuna vyoo viwili, kimoja wavulana na kimoja wasichana. Ni vizuri Serikali ijenge shule bora na nzuri na wanafunzi watakuwa na bidii ya kusoma na tunaweza kupata wasomi wazuri wenye vipaji mbalimbali, ambavyo vitakuwa ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tupitishe Sheria Bungeni, Wananfunzi wa kike, wanapopata mimba wakiwa shuleni wapewe fursa nyingine, wanapozaa warudi tena kusoma shule au Serikali iwajengee shule maalum kama walivyofanya Zanzibar na hao wanaowapa mimba wanafunzi wachukuliwe hatua kali za Kisheria. Je, ni lini Serikali itahakikisha inarudisha shuleni wananfunzi wa kike waliopata mimba katika umri mdogo? Na ni lini Serikali itajenga shule bora vijijini wanafunzi wa kike wasipate taabu wanavyoingia kwenye hedhi pia vyoo bora iwajengee?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Elimu ya Watu Wazima, baadhi ya wananchi wa Tanzania, ambao ni watu wazima hawajui kusoma na kuandika. Ni vizuri Serikali ikarudisha elimu hii ya watu wazima na ikafika mpaka vijijini. Wakuu wa Mikoa na Wilaya wakaratibu ni wananchi wangapi hawajui kusoma na kuandika na wakawekewa muda maalum wa kusoma. Vilevile, wapewe semina elekezi kuhusu elimu na faida ya elimu kwani katika tawala wa Rais ziliopita akiwepo muasisi wa nchi hii Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, elimu hii ya watu wazima ilikuwepo na watu wazima nao walikuwa wakisoma jioni. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha elimu hii ya watu wazima wasiojua kusoma na kuandika inarudishwa na kuboreshwa hasa vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Vyuo Vikuu ni vizuri Serikali yetu ijenge Vyuo Vikuu vingi hapa nchini ili wanafunzi wanaohitaji kusoma Vyuo Vikuu wasiende kusoma nje ya nchi kwani baadhi ya wanafunzi wakienda kusoma nje ya nchi wanakuwa wanashawishika na kuamua kufanya kazi katika nchi jirani kwani wanakuwa wana vipaji vizuri. Wanafunzi wa vyuo Vikuu wakopeshwe mikopo na hiyo mikopo isikopeshwe kwa upendeleo. Vilevile, ni vizuri Serikali iwekeze katika elimu na wanafunzi wataka kuwa na juhudi ya kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, Chuo Kikuu Huria kwa tawi la Zanzibar liboreshwe, naona kama limesahulika. Wanafunzi wa elimu ya juu kwa upande wa Zanzibar, wapewe mikopo kwa wakati muafaka kwani wanafunzi wa elimu ya juu kwa upande wa Zanzibar wakitaka mikopo ni lazima wafuate Bara. Hii itasaidia kuondoa kero za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Walimu, walimu ni watu ambao wamesahulika! Walimu ambao wako pembezoni bado hawajawa na miundombinu mizuri ya kufundishia, wanafundisha katika mazingira magumu. Makazi wanayokaa hayaridhishi, maji ni taabu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitaka kuwa na elimu bora ni lazima tuwawezeshe walimu kwani wakiwa wanalalamika watakuwa hawawezi kufundisha wanafunzi vizuri. Lazima mishahara yao wapate kwa wakati

muafaka kwani walimu wanaoishi vijijini mishahara yao ni mpaka waifuate mjini na mshahara wenyewe ni mdogo, haukidhi mahitaji na mwalimu anakuwa hafundishi na anaanzisha kufanya biashara ndogondogo ili kujikimu na maisha kama kuuza karanga, ubuyu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi jirani za wenzetu, walimu wanathaminiwa na wanaheshimika lakini hapa Tanzania hatuwajali walimu na hatuoni umuhimu wao. Walimu ni nguzo muhimu ya maendeleo, Je, ni lini Serikali itahakikisha walimu wanapewa kipaumbele na kulipwa stahiki zao kwa wakati muafaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la shule za binafsi, baadhi ya shule za binafsi mazingira yake siyo mazuri! Sehemu wanazolala wanafunzi haziridhishi zina kunguni na kadhalika. Vyakula wanavyokula siyo vizuri kwa afya zao. Naomba Serikali iwe inakagua shule hizi mara kwa mara na zile ambazo hazipo kwenye kiwango zifungwe au kutozwa faini.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua Serikali imejipangaje katika mambo yafuatayo kwa Wizara hii:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Ualimu baada ya kupelekwa *NACTE* vimekuwa vikikosa wananfunzi wa kutosha kulingana na *capacity* ya Chuo na ukilinganisha na idadi kubwa ya wananfunzi wanaosajiliwa katika shule za msingi kutokana na Sera ya Elimu Bure. Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha nchi yetu inakuwa na walimu wa kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Ualimu vimeingia *NACTE,* lakini stahiki za Wakufunzi bado hazijabadilishwa kuendana na mfumo wa *NACTE*. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Wakufunzi nao wanapata stahiki zao vizuri bila ubabaishaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Je, Serikali imejipangaje kuzuia ombwe kubwa la Walimu kuacha kazi na kutafuta kazi nyingine hivyo kupelekea ukosefu wa Walimu hasa katika shule za Vijijini mfano, katika Mkoa wa Mtwara, ambao mimi ninauwakilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vyuo vingi vya Ualimu vinafundisha masomo ya sayansi, lakini havina maabara. Hivyo, kufanya ufundishaji na ujifunzaji uwe mgumu na kadhalika. Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maabara hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliahidi kuwakopesha wanachuo, ambao wanasoma katika vyuo vya ualimu masomo ya sayansi, lakini haijafanya hivyo, ni kwa nini na kuna mpango gani uliowekwa kuhakikisha ahadi hiyo inatekelezeka kwani inawanyima haki wanachuo hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vingi vya Ualimu havina mtandao wa *internet* wa uhakika. Je, Serikali inalijua hilo na imejipangaje kuhakikisha mtandao unapatikana ili kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji unaenda vizuri ukizingatia hakuna vitabu vya kutosha katika vyuo hivyo.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJABU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja, na ningependa kuchangia kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika hoja hii. Elimu ndiyo msingi wa mambo yote hapa Duniani, yapo mambo ambayo yanatakiwa kuboreshwa ili tuzidi kuongeza ubora wa elimu yetu. Kwa mfano, mitaala yetu inabidi iangaliwe upya, tujaribu kuangalia mitaala ya nchi zingine zinazofanya vizuri ili tuiboreshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitengo cha Ukaguzi cha Wizara inabidi kiimarishwe, sikumbuki au kusikia Wakaguzi wamekuja Muheza. Hawa ndiyo wanaweza kuboresha mambo mengi ni watu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu mkubwa wa Walimu Muheza. Ingawa ni suala lililopo TAMISEMI shule za msingi na sekondari zote, ninaomba uliangalie kwa umuhimu wake, kuna shule zingne zina walimu wawili na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara sasa ni vizuri ifikirie kuanzisha mitihani mara mbili kama wenzetu wengi badala ya kungojea mwaka mzima kwa *O-level* na *A- Level*. Pia maslahi ya walimu yaangaliwe kwani inaonekana kama wamesahulika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msisitizo mkubwa naona Muheza *High School* ambayo ni hiyo tu Wilaya nzima ifanywe ya kutwa na bweni ili iweze kuhudumia ongezeko la wanafunzi wa *'O' Level* Wilaya nzima. Shule hiyo ilijengwa kwa nguvu za wananchi na ina uwezo mkubwa wa kuchukua wanafunzi wengi zaidi. Wizara isimamie TAMISEMI kuona vifaa vya maabara shule za sekondari vinapelekwa.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Hata hivyo nianze na kuchangia machache katika sekta hii ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Wizara na Serikali kuzifanya *High Schools* zote nchi nzima ziwe chini ya Wizara ya elimu na TAMISEMI ibaki na *Primary Schools* na *'O' Level Secondary Schools* tu. Hii itasaidia sana Halmashauri za Wilaya na Miji yetu kujikita zaidi kuboresha shule tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 2006/2007 Serikali iliamua kwa maksudi kusaidia Mikoa, ambayo ipo nyuma kielimu. Mikoa hiyo ni pamoja na Kigoma, Singida, Mtwara, Lindi na Katavi. Mikoa hii ilikuwa inapata fedha za ziada kila mwaka shilingi bilioni 1 kwa ajili ya kusaidia kujenga madarasa, mabweni ya wasichana na nyumba za walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zilisaidia sana na kwa Mkoa wa Kigoma hali ilianza kubadilika, ajabu ni kwamba, baadaye 2011/2012 fedha hizo zilisitishwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri sana fedha hiyo, irejeshwe ili Mikoa iliyobaki nyuma kielimu iweze angalau kupiga hatua. Huu ulikuwa mpango maalum ni lazima Serikali iangalie hali hii ili kuweka uwiano mzuri katika nchi yetu na baina ya Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitengo cha Ukaguzi wa Shule; kitengo hiki kimezorota sana na sehemu nyingine shule za msingi na sekondari hazikaguliwi kabisa! Ni vizuri kitengo hiki kiwe kitengo huru na kisimamiwe na Wizara moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu malipo ya Walimu katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu; malipo ya walimu yahakikiwe vizuri na walipwe stahili zao za matibabu, likizo, likizo ya uzazi, kupanda vyeo na kadhalika. Walimu wengi wanalalamika sana, Wizara ya Elimu na TAMISEMI harakisheni uhakiki ili walimu hawa walipwe fedha zao mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Ujenzi wa Maktaba ya Wilaya Kasulu; Halmashauri ya Mji wa Kasulu tulijenga jengo la maktaba lenye ukubwa wa ghorofa mbili. Tulishirikisha wadau mbalimbali wa elimu kama vile *TANAPA* na *UNHCR* tukafika ujenzi wa asilimia 65. Tafadhali Wizara au Serikali saidieni juhudi za wananchi hawa, tupeni nguvu. Tukipata shilingi milioni 200 zitasaidia sana kukamilisha jengo hili na litaanza kutumika. Ni matarajio yetu mwaka 2016/2017, Wizara itaangalia namna njema ya kufanikisha na kukamilisha mradi huu muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ujenzi wa Kasulu *Science Grand School;* Mkoa wa Kigoma wenye Halmashauri Nane tumeanza mradi wa ujenzi wa shule ya Sekondari ya Sayansi. Mkoa wa Kigoma ulianza kazi hii kutuma Suma JKT, kazi imeanza na hadi sasa shilingi milioni 600 zimetumika. Tunaomba Serikali na Wizara ya Elimu isaidie mradi huu muhimu kwa wakazi wa Mkoa wa Kigoma. Tumeanza tusaidieni kukamilisha ndoto yetu ya kujenga shule hii muhimu ya sayansi. Matarajio yetu ni kwamba, shule hii baadaye tutaifanya ni Chuo Kikuu cha Sayansi na kitaitwa Kigoma *University of Science and Technology*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Kasulu tumetoa eneo la ekari 115 kwa ajili ya ujenzi wa shule hii. Eneo hili limepimwa na sasa tuna – *process* hati ya kumiliki ardhi hiyo. Halmashauri ya Mji wa Kasulu, Kigoma tumeanza, tunahitaji msaada wa Wizara ya Elimu ili ndoto yetu iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa sasa wa kushughulikia masuala ya elimu nchini unaofanywa na Wizara mbili (TAMISEMI, na Wizara ya Elimu) umeleta mkanganyiko mkubwa sana. Elimu yetu siku za nyuma ilisimamiwa na Wizara moja na ndiyo maana tulifanya vizuri. Ninashauri Serikali kurudisha mfumo na muundo wa awali wa Wizara moja tu kama kweli tunataka kupiga hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao uhaba mkubwa sana wa walimu wa sayansi kwenye shule zetu hasa za sekondari za Kata. Mwalimu ana nafasi kubwa katika kumsomesha mtoto. Iweje mtoto anaanza *form one* hadi *form four* hajapatwa kufundishwa na mwalimu wa sayansi kisha watoto hao tunawapa mtihani baada ya miaka minne.

Ninashauri Serikali kufanya jitihada za maksudi kuhakikisha walimu wanapatikana. Serikali pia itoe motisha ya mishahara mizuri kwa walimu ili walimu wakae kwenye kazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za sekondari za Kata, mfano; Endallah, Endabash, Baray, Mangola, Upper Kitete, Kansay, Orbochand, Getamock zina walimu pungufu sana wa masomo ya sayansi. Ninaiomba Wizara ipeleke walimu hao Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ada elekezi huu siyo muda wake. Serikali iboreshe shule zake badala ya kutaka kupunguza ada kwa shule binafsi. Niulize, hivi humu ndani ya Bunge nani ana mtoto wake katika hizi shule za Kata? Tumepeleka watoto shule za binafsi baada ya kuona elimu inayotolewa huko ni bora kuliko ile inayotolewa katika shule za Serikali. Serikali iachane na ada hizo na kama kuna wazazi wanaona hizo shule za binafsi ni ghali basi wapeleke watoto wao kwenye shule ambazo ada zake wanazimudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho Halmashauri ya Wilaya ya Karatu ilitoa majengo na maeneo yake Ayalabe karibu na Mji wa Karatu ili kuanzisha chuo cha Ualimu, miundombinu ya chuo hicho iko tayari. Nimwombe Waziri wa Elimu afike, akague chuo hicho ili kianze kutumika.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii kuwapongeza viongozi wote wa Wizara kwa juhudi kubwa za kuendeleza elimu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Walimu Tanzania, CWT ishauriwe kupunguza mchango kwa Walimu au kuondoa kabisa. Pia michango waliochangisha waoneshe ni kwa namna gani imewasaidia walimu ili walimu wanufaike na michango yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodi ipange mpango mkakati wa kufuatilia wanafunzi ambao wamepata ajira au kujiajiri lakini mpaka sasa hawajarejesha mikopo ili fedha hizo zisaidie kuongeza idadi ya wanafunzi kukopeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,, wanafunzi wa kike waliopata bahati mbaya ya ujauzito nashauri Wizara iwaruhusu kuendelea na masomo baada ya kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara isaidie ujenzi wa mabweni ya wasichana katika maeneo ya vijijini ili kuwanusru wasichana wetu wadogo.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani zangu za awali kwa wote walioandaa hotuba hii ya Wizara ya Elimu na hasa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Naibu Waziri.

Matatizo ya Jimbo langu la Bunda Vijijini; moja ni kutoa kibali cha ufunguzi wa sekondari ya *(High School)* ya Makongoro *(Makongoro High School)*. Tunahitaji msaada wa Wizara, wananchi wamejenga vyumba vya madarasa, mabweni na jengo la utawala, tunahitaji shilingi 72,000,000 ili kumaliza ujenzi wa *high school* hii. Tunaomba msaada ili kupunguza makali ya michango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili ni upungufu wa walimu wa sayansi, (kemia, fizikia, biolojia na hesabu). Zaidi ya sekondari 30 wanahitajika walimu 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni matatizo ya mazingira ya vyoo. Zaidi ya shule za msingi 40, zina matatizo ya vyoo vibovu vya shule na tatizo la maji shuleni, hivyo naomba Wizara ya Elimu kupitia mashirika yake ya kutoa huduma za msingi na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na tatizo la vyoo magonjwa ya watoto shuleni yameongezeka sana, *(typhoid, kuhara, U.T.I)*. Naomba msaada wa suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba nne, matatizo ya maabara, madarasa na nyumba za walimu. Wizara iangalie namna ya kusaidia Jimbo hili jipya.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya. Kwa mwelekeo wa bajeti hii inayoonesha wazi Serikali imedhamiria kuboresha elimu kuanzia ngazi ya shule ya msingi hadi elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze uamuzi wa Serikali kuhamishia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(FDC)* kuhamishwa Wizara ya Elimu kwa dhana ya dhamira ya kuvifanya vyuo hivi kutoa elimu ya ufundi, jambo hili litasaidia sana kuwezesha vijana wetu wengi ambao hawajapata fursa ya elimu ya sekondari wapate elimu ya ufundi ambayo wataweza kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo hivi kwa muda mrefu vimekuwa vikiendeshwa katika mazingira magumu sana, vimekuwa havipati fedha za kutosha, dhamira ya kutoa elimu imefikiwa kwa kiasi kidogo.

Sasa Serikali iongeze bajeti kwenye vyuo hivi viweze kutoa elimu bora na wanafunzi bora, yale maeneo ambayo hayana vyuo hivi vya *FDC's* basi Serikali ijenge vyuo vya *VETA*. Mfano ni Jimbo langu la Kilindi halina *FDC's* wala *VETA* japo kwa mwaka wa fedha unaoanza Julai 2016 Serikali imedhamiria nasi tupate chuo cha *VETA*. Naomba nipate uthibitisho wa dhamira ya Serikali katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie juu ya upungufu wa walimu katika shule zetu za msingi na Serikali, japo Serikali kwa sasa inaonesha kutatua tatizo hili hususani katika masomo ya sayansi, hisabati, fizikia na kadhalika. Mfano, katika Jimbo langu la Kilindi shule za sekondari Mafisa, Kibirashi, Kikude hazina walimu wa kutosha, nitaleta ofisini kwa Mheshimiwa Waziri upungufu wa walimu ili Serikali ione namna ya kutatua tatizo hili vinginevyo kiwango cha elimu katika Wilaya ya Kilindi kitashuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nieleze juu ya suala la Maafisa Elimu na Walimu kukaa katika eneo moja la kazi. Jambo hili kwa kweli halileti ufanisi katika utendaji. Mtumishi kukaa eneo moja kwa muda mrefu kunamfanya mtumishi kutojifunza changamoto na morali ya kazi kwa mfano, katika Jimbo langu la Kilindi, Afisa Elimu Sekondari na Elimu ya Msingi wamekaa muda mrefu, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI, tupate watumishi wapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba suala la Wilaya kupata *High School* lipo chini ya Serikali za Mitaa lakini bado Wizara hii inalo jukumu la kusimamia Wilaya ambazo hazina kabisa shule za kidato cha tano na cha sita zinapewa fursa hizo. Mfano katika Wilaya yetu ya Kilindi hatuna hata shule moja,

hii inanyima fursa kwa vijana ambao wazazi wao hawana uwezo kujiunga na shule ambazo zipo mbali na Wilaya ya Kilindi. Wazazi, uongozi wa maeneo hawana nguvu za kiuchumi. Wanafunzi wanachaguliwa mbali na Wilaya ya Kilindi mara nyingi hawaendi. Wizara ituone nasi, itusogezee shule ya wavulana na wasichana katika ngazi za kidato cha tano na cha sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake ya kutoa elimu bure kwa wananchi. Wananchi wa Tanzania na wa Kilindi wamenufaika sana na fursa hii. Naunga mkono hoja.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme elimu kwanza iwe ya darasani au mitaani. Kama Serikali ingekuwa makini katika vipaumbele vya nchi elimu ingewekwa ya kwanza nchini ili kupata matokeo makubwa. Hivi bila elimu hata mimi nisingeweza kuchangia, Daktari, Mbunge, Waziri, Rais, Mwalimu, viongozi na wataalum wote wasingekuwepo. Sasa kwa nini Serikali inafanya mzaha katika suala la elimu? Jamani tusione aibu, tuseme tulikosea sasa tushirikishe wadau tuanze upya ni kweli tumejikwaa na kujikwaa si kuanguka, bado hatujaanguka tujipange.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na matatizo mengi ya walimu nchini lakini naomba nizungumzie matatizo yanayowapata walimu katika Jimbo la Mlimba, pia miundombinu ya shule, upungufu wa walimu na elimu ya awali pia watoto walemavu wanaoishi katika Jimbo la Mlimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shule za sekondari kata changamoto ziko tofauti, kuna uwekaji wa umeme wa jua ambako *REA* haifiki katika shule za sekondari za Kiburubutu, Uchindile, Matundu Hill na Mofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia unununzi wa samani (meza na stuli) za maabara kwa shule zote za Serikali zilizoko katika Jimbo la Mlimba ambazo ni Masagati, Utegule, Mutenga, Kamwene, Mlimba, Tree farms, Chisano, Chita, Mchombe, Kiburubutu, Nakangutu, Mbigu, Mofu na Matundu Hill. Pia ujenzi wa hosteli shule za sekondari za Chisano na Matundu Hill.

Aidha, kuna uhitaji wa madarasa 1,166 yaliyopo 467 hivyo hakuna madarasa 699; nyumba zinahitajika 1,036, zilizopo ni 199, hakuna nyumba 837; vyoo mahitaji ni 897, vilivyopo 290 hakuna vyoo 607

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nitawasilisha hali halisi ya hali ya elimu Jimbo la Mlimba.

Mheshimiewa Mwenyekiti, Jimbo la Mlimba kuna kituo kimoja tu cha ufundi kilichopo Mchombe. Kituo hicho cha ufundi stadi kina changamoto ya uchakavu wa madarasa ya nadharia na vitendo, upungufu wa zana na vifaa

vya kufanyia kazi katika fani zote za useremala, uashi, chuma na sayansi kimu pia walimu. Hivyo naomba ukiangalie kwa jicho la pekee kituo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hali ya shule za awali na msingi ni duni sana, hali ya walimu ndio kabisa, nyumba za walimu ndio usiseme, ukizingatia ni Jimbo la vijijini na miundombinu ya barabara ni mbaya hivyo wanahitaji kuwezeshwa usafiri angalau wa pikipiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kuwa utalipa kipaumbele Jimbo la Mlimba kwa kuwapelekea walimu wa shule za sekondari na msingi katika ajira zijazo. Mahitaji sahihi nitakupatia, ahsante.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Waziri, wewe ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu kama ilivyo kuwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la Wananamtumbo, mtujengee Chuo cha *VETA*. Aidha, mtusaidie Chuo cha Ualimu kilichoanzishwa Namtumbo katika Kijiji cha Nahoro, chini ya mwavuli wa Ushirika wa SONAMCU na Mkufunzi Mstaafu Bwana Awadh Nchimbi kiendelezwe na changamoto zililoko zitatuliwe. Nawasilisha.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza pongezi kwa kuteuliwa kwake Mheshimiwa Waziri na hongera kwa uwasilishaji mzuri, naomba nizungumzie mambo machache yafuatayo:-

Kwanza, Serikali ilitoa waraka wa *responsibility allowance*, lakini mpaka sasa haijaanza kutekelezwa ili kuwawezesha viongozi wetu kwenye Idara ya Elimu.

Pili, kumekuwa na tatizo kubwa sana la madeni ya walimu, Serikali lazima ije na Mpango wa kukomesha madeni ya walimu.

Naomba soko huria la vitabu lidhibitiwe kuendana na mitaala ya elimu. Nashauri kuwe na *formality* moja nchi nzima ya vitabu.

MHE. HASNA S. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu Kigoma Kusini lina jumla ya shule za msingi 119; lakini kati ya hizo tuna shule nne zina darasa moja na zingine

zina madarasa mawili. Kwa kweli hali ya shule hizi inatisha; nyumba za walimu hakuna, nimwombe Mheshimiwa Waziri, aliangalie Jimbo la Kigoma Kusini kwa jicho la huruma ukizingatia miundombinu ya barabara kuwafikisha walimu kutoka wanakopanga nyumba hadi kwenye shule ni mibovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Waziri ahakikishe bajeti ya Halmashauri ya Uvinza inakuja bila kukosa kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017. Wilaya ya Uvinza tuna shule mbili za *A-level* na *O-level* za *Lugufu Boys* na *Lugufu Girls*; nimuombe Mheshimiwa atusaidie kuzisajili kuwa ya bweni ili ziweze kupata mgao wa chakula kwani tangu zianze zimekuwa ni za bweni ilhali zilisajiliwa kama za kutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe pia Mheshimiwa Waziri, atusaidie kusajili shule mbili mpya za sekondari za kata za Mloakiziga na Basanza. Kwani wanafunzi wa kata hizi mbili wanatembea zaidi ya kilometa 15 kufuata sekondari za kata za jirani. Kwa kuwa hizi ni nguvu za wananchi tuiombe Wizara ijitahidi kuzisajili japo kuwa hazijakuwa na miundombinu yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie pia uhaba wa vyoo. Kwenye shule zangu za Jimbo la Kigoma Kusini niombe pesa za ujenzi na ukarabati zielekezwe kama tulivyoomba kwenye bajeti ya Halmashauri ya Wilaya kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia uhaba wa nyumba za walimu ni tatizo kubwa ndani ya Jimbo langu. Sambamba na haya niombe Wizara ituletee walimu kwani Halmashauri ya Wilaya, bado ina uhaba wa walimu hususani walimu wa sayansi na walimu wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nitoe pongezi kwa dada yangu Mheshimiwa Waziri Profesa Joyce Ndalichako, kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais, kuteuliwa kuwa Mbunge na kupewa dhamana ya kuiendesha Wizara hii nyeti ya kufuta ujinga kwa watoto wetu. Nizidi kukuombea afya na achape kazi kwani wanawake tukipewa nafasi tunaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kuchangia kuhusu mtaala wa elimu ya msingi katika ukurasa VIII. Serikali imekiri kuwepo na mtaala uliokuwa ukitumika mwaka 1997. Je, Serikali inaweza kuleta nakala ya mtaala huo hapa Bungeni, kwani nimeutafuta bila mafanikio wakati ni mali ya umma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, malengo ya maendeleo ya milenia ya mwaka 2002, yaliyotajwa katika ukurasa wa pili yalizingatiwa vipi katika kutayarisha mtaala wa elimu ya msingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwaje Mashirika ya Dini yanahusishwa katika tathmini ya mtaala wa elimu ya msingi, lakini sio katika kutathimini mtaala wa elimu ya awali na Serikali za Mitaa kuhusishwa katika tathmini ya mtaala wa elimu ya awali lakini sio katika mtaala wa elimu ya msingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya elimu ya Tanzania katika mtaala wa elimu ya msingi, ukurasa nne ni tofauti na yale yaliyoainishwa katika mtaala wa elimu ya awali katika ykurasa wa tatu na nne, kulikoni?

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na historia ndefu ya elimu ya Wilaya ya Masasi, naomba kiambatanisho namba 1 na 2 vipokelewe kama mchango wangu wa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kudidimia kwa elimu Wilaya ya Masasi. Wakati Tanganyika tunapata uhuru mwaka 1961, kiwango cha elimu *literacy rate* katika Wilaya ya Masasi kilikuwa asilimia 85. Kiwango cha juu kabisa kuliko Wilaya zote za wakati ule; hii haikuwa kwa bahati tu bali ilitokana na juhudi za dhati za wamisionari (wazungu) wa Kanisa Anglikana kwa kiwango kikubwa tangu mwaka 1876 na wale wa Kikatoliki kuanzia mwanzo wa karne ya 1900. Vijiji vyote vikubwa vilikuwa na kanisa (mtaa – Kianglikana au Paroko Kikatoliki). Na vitongoji vilikuwa na makanisa madogo (Anglikana) au vigango (Kikatoliki) vilivyosimamiwa na walimu au Makatekisti.

Vijiji hivi vyote na baadhi ya vitongoji palikuwa na shule za Wamisionari. Shule za Serikali kwa maana ya shule za Serikali ya Mitaa *(district council/native authority)* zilikuwa mbili tu Wilayani, *middle schools* nazo zilianzishwa miaka ya mwanzo mwa 1950 Chiungutwa na Mbemba. Shule hizi zote za vijijini za misheni zilipokea wanafuzi wa dini zote mbili kuu, kikristo na kiislamu. Hivyo ni dhahiri mtandao wa shule hizi za misheni ulikuwa mkubwa Wilayani Masasi, kiasi cha kuwezesha kufikisha asilimia hii kubwa ya 85 wakati tunapata uhuru. Ukaguzi wa hizi shule ulikuwa wa makini na ukifanywa na wamisheni wenyewe (wazungu) na hivyo elimu kuwa bora.

Vivyo hivyo, shule za sekondari na za ualimu katika Wilaya ya Masasi zilikuwa za misheni, sekondari ya Chidya ya Anglikana na Ndanda ya Katoliki pia Chuo cha Walimu wa kike pekee Ndwika na vyuo vya wakunga Lulindi cha Anglikana na Ndanda cha Katoliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masomo ya juu, wanafunzi waliotakiwa waendelee na masomo zaidi walitoka katika shule hizi mbili za misheni kwenda

katika shule kuu mbili za misheni za Minaki (Anglikana) na Pugu (Katoliki). Pia waliweza kwenda shule za Serikali za Tabora, Tanga na kadhalika na baadaye Makerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango vya juu vya nidhamu, uadilifu na uwajibikaji *(commitment)* ndiyo ishara kuu na misingi ya uendeshaji wa shule hizi za misheni kufuatana na maadili ya kidini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio, Makatibu Wakuu, viongozi Ikulu wawili wa kwanza baada ya kupata uhuru, Dunstan Omari na Joseph Namatta walisoma Chidya hata baadae kufika Makerere wakitokea Minaki. Pia enzi za ukoloni Dunstan Omari alikuwa *District Officer* wa kwanza Mwafrika. Rais Mstaafu Benjamin Mkapa pia ni zao la shule ya misheni ya Ndanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya wengine waliofanikiwa kupata uongozi wa juu katika Awamu ya Kwanza kutoka shule za Chidya, Ndada na Ndwika ni kama ifuatavyo:-

1. Mzee Fredrick Mchauru – Katibu Mkuu Wizara mbalimbali na Mshauri wa Rais

2. Nangwanda Lawi Sijaona – Waziri

3. Mama Thecla Mcharoru – Katibu Mkuu UWT

4. Yona Kazibure *MSc (Physics)* wa kwanza Makerere – *Chief Engineer Radio Tanzania*.
5. Mama Anna Abdallah – Mwenyekiti UWT

6. Beda Amuli – *Architect* Mwafrika wa Kwanza Tanzania

7. Mama Kate Kamba - Katibu Mkuu UWT

8. Yuda Carmichael Mpupua – Naibu Katibu Mkuu na *Chief Agricultural Officer*

9. Dkt. Isaya Mpelumbe – *Director of Veterinary Service* na Kamishina wa Kilimo na Mifugo

10. Alex Khalid – Katibu Mkuu

11. Major Gen. Rowland Makunda – Mkuu wa Navy kuanzia vita vya Idi Amin

12. Philip Magani – *Chairman/Managing Director CRDB*

13. Paul Mkanga – Katibu Mkuu

14. Dkt. John Omari – *Fellow of the Royal 1 Surgeons* wa kwanza Tanzania

15. John J. Kambona – *Director of Fisheries Tanzania* na *FAO Headquarters Rome*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia walimu wa kwanza kutoka Makerere walifundisha shule maarufu za Serikali za sekondari tangu ukoloni kama vile Tabora, Old Moshi, Tanga ni Curtius Msigala, Joseph Banali, Peter Nampanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya siasa na hatima. Tangu shule zile za misheni kuwa chini ya Serikali mbali na nyingine nyingi kujengwa, kwa jumla kiwango cha elimu Wilayani Masasi kimezidi kuporomoka. Ufaulu katika shule zote za awali na sekondari umezidi kushuka. Ufaulu wa shule za awali kuingia sekondari umekuwa mdogo na Wilaya kuwa mojawapo ya zile za chini kabisa nchini inashangaza hata shule maarufu kongwe (tangu mwaka 1923) ya Chidya haijapata hadhi ya kuwa *high school* hadi leo, kuna nini? Hili ni jambo lisilokubalika na viongozi, Wabunge, Madiwani na watawala wanawajibika kuelewa *awareness* na kuhimiza kulifanyia kazi kwa nguvu zao zote wakishirikiana na wananchi kurekebisha hali hii mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mwanaharakati aliyeandika kitabu *How Europe Underdeveloped Africa*, si vizuri mwingine akaandika kingine. *How Tanzania Underdeveloped Masasi.*

MHE. ESTHER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango wangu kwa kuzungumza ndani ya Bunge bado nimeona ni vyema niweze kuwasilisha mchango wangu wa maandishi kwa maslahi mapana katika kuboresha elimu ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliposema kuna haja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu kushuka vyuoni kote nchini Tanzania ili kujionea changamoto za walimu pamoja wanafunzi hapa nilimaanisha yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo michango ya wakuu wa vyuo vikuu kutumia madaraka yao vibaya ilhali *universities charter* ikiwa inatoa kinga ya wakuu hawa kutoingiliwa katika utendaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wakuu wa vyuo wamekuwa wakimiliki magari mawili hata matatu wakitengea mafuta lita 500 mpaka 1200 kwa mwezi

kwa ajili ya shughuli za kiutendaji na shughuli za familia zao. Hii ni kukosa utii ku-*abuse* nafasi yao na usaliti wa misimamo ya Mheshimiwa Rais katika dhana nzima ya kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wakuu wa vyuo vikuu wanaolindwa na *security,* mathalani *auxiliary police* 12 hadi 18 kwa siku moja tu na wakati huo wanafunzi wamekuwa na matukio ya kuumizwa na wezi na vibaka kwa kukosa ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoangalia suala la *misuse of public resources* kwa upande wa wakuu wa vyuo vikuu ninapata *feelings* kwamba *at sometimes we need to break the rules for example university charter* inatumika kama sehemu ya kuiibia Serikali kwani pamoja na kutumia nafasi zao kwa maslahi yao binafsi lakini pia tumeona Serikali inavyoibiwa kwa miradi inayoendeshwa na baadhi ya vyuo ambapo Wizara husika inafika hata kukosa taarifa rasmi za kiasi gani chuo husika kinazalisha kwa mwezi kupitia miradi ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo masuala ambayo yana maslahi mapana kwa taifa hili hususan katika dhana nzima ya utumishi uliotukuka. Katika masuala ya TCU ambayo mengi yametugusa mimi binafsi napenda nikiri kuwa nimeridhia kabisa kwa suala la kutodahili wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi 489 wameonekana wamekosa sifa na vigezo katika kudahiliwa kwenye vyuo vikuu, lakini hii haimaanishi tunaitoa *TCU* katika kujibu hoja zetu za msingi.

Mathalani kwa kuwa *TCU* ndiyo inayosimamia ubora wa elimu *(Higher learning institutions)* na ndiyo inayoweka vigezo vya udahili, ndiyo inayokagua na kupitisha mitaala na ndiyo inayokagua ubora endelevu wa taasisi za umma nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani Chuo Kikuu cha *St. Joseph,* ni nini sasa hatma ya vijana hawa 489 ambao wameonekana kukosa sifa na vigezo? Je, watawapeleka shambani wakalime ili ndoto ya ajira kwa vijana hawa ikapate kutimia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninahoja maswali haya kwani kimsingi Serikali imepoteza kiasi cha fedha kupitia udhamini wa mikopo iliyowahi kutoka huko nyuma, lakini pia kibinadamu vijana hawa wameathirika kisaikolojia. Ni vyema Wizara ikawa na mkakati maalum katika kumaliza changamoto za namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na adhabu ya Mheshimiwa Waziri katika kusimamisha Bodi ya *TCU* lakini itoshe kusema adhabu hii haitoshi kwani

katika kusimamisha bodi hii na watendaji wakuu bado mishahara wataendelea kuchukua, hivyo ni vyema Tume ya Uchunguzi ilichukulie hatua stahiki mapema iwezekanavyo ili Mheshimiwa Waziri aweze kupata timu sahihi ya watendaji itakayoweza kwenda sambamba na kiu ya Mheshimiwa Waziri katika kuleta ubora wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hitimisho langu ningependa niombe mwongozo wa Mheshimiwa Waziri kuna sababu gani ya msingi iliyoilazimu Wizara ya Elimu katika kutenganisha mamlaka ya Bodi ya Mikopo na *TCU* kwani kimsingi *TCU* ina kurugenzi zote muhimu zinazoweza kusimamia mikopo ya elimu ya juu tofauti na leo tunapoona *loans board* inatengwa na *TCU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya *TCU* kuna kurugenzi ya udahili *admission, accreditation, quality, assurance* pamoja na *finance*. Nia nini haswa kilichopelekea kutenganisha mamlaka ya *loans board* na *TCU?* Ahsante, naomba kuwasilisha.

MHE. ZUBEDA H. SAKURU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mchango wangu kuhusu hoja ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la siasa vyuoni limeendelea kuwa mwiba kwa baadhi ya vyuo vikuu nchini. Menejimenti za vyuo zimekuwa zikiingilia Serikali za wanafunzi, lakini pia kuwanyima haki wanafunzi wanaoshiriki katika nafasi za uongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mgogoro mkubwa wa uongozi baina ya menejimenti ya Chuo cha Dodoma na Serikali iliyoondolewa madarakani kwa shinikizo la menejimenti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro huu si tu umechochewa na menejimenti ya chuo lakini pia umelenga kuwanyima wanafunzi waliochaguliwa kihalali na wanafunzi kuongoza Serikali ya wanafunzi pamoja na kuwasimamisha chuo kinyume na hukumu ya mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binti Rose Maruchu mwanafunzi wa mwaka wa tatu alichaguliwa na wanafunzi wa *UDOM* alisimamishwa chuo miezi miwili tu kabla ya kumaliza chuo lakini pia wakati kesi ikiwa mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi ilifunguliwa kabla ya tarehe 11/4/2016 lakini cha kushangaza kesi ikiwa mahakamani Bi, Maruchu alipokea barua ya zuio la kuendelea kuwa kiongozi na menejimenti ikaunda Serikali ya mpito kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hata wakati kesi ya zuio inaendelea kusikilizwa mahakamani, wakili wa *UDOM* alitoa barua kuwa Maruchu amesimamishwa chuo tangu tarehe 11/4/2016. Waziri si tu kuwa menejimenti ilidharau mahakama lakini pia imelenga kumkomoa Rose ambaye alichaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa *UDOSO* kihalali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote hukumu iliyotolewa dhidi ya Chuo cha Dodoma ilimpa ushindi Bi. Rose Maruchu na kuamuru chuo kimruhusu Rose kuendelea na masomo pamoja na majukumu yake, Rose hajarudishwa chuo huku akiwa amebakiza miezi miwili tu kumaliza chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki iko wapi Mheshimiwa Waziri? Tunawapaje motisha wasichana waliopo vyuoni kugombea nafasi za uongozi wakati wakiwekewa mazuio na vikwazo vya maksudi? Menejimenti ya *UDOM* inapata wapi jeuri ya kukaidi amri ya mahakama? Kukaa kimya kwa Serikali ndiko kunakoinua malalamiko kuwa inashiriki kushinikiza menejimenti za vyuo kukandamiza na kuingilia Serikali za vyuo hasa zinazoongozwa na wanafunzi wenye mitazamo kinzani na menejimenti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri naomba usimamie haki ya Rose Maruchu, kama Waziri mwenye dhamana lakini zaidi kama mama. *Imagine* unaona ndoto za mwanao zinazimwa kwa kutetea maslahi ya wenzake? Ni uchungu gani mzazi anaobeba kuona ada na jitihada zake kwa binti yake zinazimwa miezi miwili kabla ya kuhitimu miaka mitatu, cha uchungu wa gharama za kusomesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwako si tu kuitaka menejimenti kumrudisha Rose kama kiongozi, bali kutaka menejimenti ya *UDOM* kumrudisha chuo na kumwachia binti huyu haki zake kama mwanafunzi ikiwemo kufanya majaribio (*tests), assignments* zote na mitihani ili ahitimishe miaka yake mitatu. Nawasilisha.

MHE. HASSAN E. MASALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi kwa Waziri na watendaji wake wote wa Wizara kwa kusimamia na kutekeleza majukumu yao. Wizara ya Elimu ni Wizara kubwa na hivyo ina changamoto nyingi sana ambazo Serikali na wadau wa elimu ni lazima wazitafutie majibu ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maboresho katika miundombinu, shule nyingi za kata zimejengwa Tanzania nzima na hivyo kupelekea watoto wengi kupata elimu, lakini shule hizi hazina maabara wala vifaa, nyumba na walimu wa madarasa ni tatizo kubwa hivyo Wizara lazima ijipange kutatua kero hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Wizara kuweka msisitizo kwa elimu ya awali *(pre-school)* ambako watoto wanakosa uwezo wao kiakili na kupata maarifa mapya. Kwa kuwa maandalizi ya mtaala wa elimu ya awali unaendelea ni muhimu kuangalia vigezo kwa vijana waliohitimu na kufanya vizuri katika mitihani ya kidato cha nne na sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaala wetu unahitaji kufanyiwa marekebisho ili uendane na dhana ya uwezo *(competence based)*. Kwa sasa elimu yetu japo tunahubiri *CBC* lakini kinachoendelea mashuleni ni *knowledge based*. Hakuna uhalisia wa matakwa ya mtaala na kinachofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iwekeze katika tafiti kwenye taasisi za elimu ya juu kwa maana zimekuwa chache na taasisi hizi zimeacha moja ya jukumu lake ambalo ni ufundishaji, utafiti na ushauri wa kitaalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la udahili wa wanafunzi wa elimu ya juu liangaliwe upya katika sheria iliyoanzisha *TCU* na ikiwezekana liachwe kwa vyuo husika, na hii ndiyo *practice* ya vyuo vingi duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tujenge nchi yenye wataalam wa kada mbalimbali ni muhimu Wizara ikapiga marufuku vyuo vya kati kutoa shahada. Vyuo hivi vitoe astashahada na stashahada. Kwa sasa nchi inakosa wafanyakazi wa kawaida kwa maana wenye shahada hawawezi kufanya kazi ambazo zinaweza kufanywa na watu wa kata, ahsante.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kama kuna kosa kubwa mtalifanya ni kuviweka vyuo vya walimu chini ya *NACTE*. Kwanza jambo hili litashusha nidhamu za walimu tarajali, jambo ambalo ni hatari kwa mustakabli wa elimu nchini. Pia jambo hili litafanya sekta hii muhimu ya utoaji wa mafunzo kwa walimu kusimamiwa na watu ambao hawana ujuzi wala uzoefu katika masuala ya mafunzo ya walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni suala la kudharau mafunzo kwa vitendo kwa walimu tarajali. Kazi ya walimu inadharaulika, wanafunzi walimu mnawapa shilingi 2,000 wanapokwenda *BTP,* ili wakanunue nini? Sekta ya elimu ni sekta muhimu na lazima Serikali ioneshe *seriousness* katika kuratibu, kusimamia na kuongoza sekta hii.

Mheshimiwa Waziri, jambo lingine ni Idara ya Ukaguzi. Hivi kwa nini Idara hii haiwezeshwi kipesa iweze kufanya kazi ya kusimamia utoaji wa elimu na kudhibiti ubora wa elimu inayotolewa. Tafadhali sana wezesheni Idara ya Ukaguzi ili ifanye kazi yake ipasavyo. Jambo hili ni muhimu sana, ahsante.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Wizara ya Elimu kwa mipango mizuri ya maendeleo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha wanafunzi wetu wanapata elimu bora. Mchango wangu nitauelekeza katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za binafsi ni nzuri sana na zinaisaidia sana Serikali kupunguzia mzigo wazazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyopo ni kupanda kwa ada mara kwa mara. Ada kutozingatia hali ya uchumi wa Watanzania na kutuweka katika matabaka na kuongeza ufisadi kwa wazazi kwa kwenda kinyume na maadili ya utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TCU,* udahili wa wanafunzi wa vyuo vikuu uangaliwe upya, vyuo vya binafsi vinapelekewa wanafunzi wengi kuliko vyuo vya Serikali. Mfano *UDOM* ni chuo kikubwa na kina mabweni mengi lakini wanalala ndege; badala yake wanajazwa kwenye vyuo ambavyo havina hata hosteli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa wanachuo wa *private* kwenda *TCU* ni tatizo kubwa na yawezekana ikawa sababu ya *TCU* kujichanganya hata kuwapa mikopo hata wasiostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali, watu wanaotaka kujilipia vyuo waende wenyewe kwenye vyuo wanavyovitaka na ada walipe kwenye chuo husika. Mfano sisi wengine ni wazee na fedha tunazo za kulipia unapelekwa *TCU* ukafanye nini? Usumbufu usio na msingi na kama ni kuhakiki vyeti acha nikahakikishiwe nipewe barua nimalizane na chuo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za msingi za *english medium*. Shule iliyopo Dar es Salaam ni Olymipio na imezaa Diamond; ni shule zilizokuwepo kwa muda mrefu. Je, Serikali kwa nini haioneshi mpango mahsusi wa kuongeza idadi ya shule hizi angalau tukapata katika Wilaya ya Kinondoni moja na Temeke moja kwa kuanzia. Naomba Serikali iliangalie kwani Jiji la Dar es Salaam limekuwa kubwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya mitihani. Kitendo cha kuwaweka wanafunzi wa shule zetu za kata na shule binafsi zenye uwiano wa mwanafunzi mmoja kwa mwalimu mmoja ni kuwaonea wanafunzi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka kushindanisha mtu ni vyema umshindanishe na yule aliyekuwepo kwenye *level* moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja bajeti ya Wizara ya Elimu changamoto zilizopo zifanyiwe kazi.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshmiwa Spika, naomba kuwasilisha maelezo yangu kwa maandishi na naomba yawekwe kwenye *Hansard*. Naomba mchango wa jana ubadilishe na huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 9 Machi, 1967 aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alichapisha falsafa ya elimu ya kujenga nchi ya kijamaa. Falsafa hii ni elimu ya kujitegemea ambayo ilitaka kuleta mapinduzi ya elimu katika nchi yetu. Mwalimu Nyerere alisema shabaha ya elimu ni kutafsiri maarifa na busara kutoka kizazi kimoja kwenda kizazi kinachofuata na kuwaandaa vijana kwa ajili ya kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi. Falsafa hii ilijenga kutatua changamoto za kutoa elimu yenye ubora tofauti kwa watu tofauti kulingana na kipato chao. Falsafa ya elimu ya kujitegemea ililenga kuondoa ugandamizwaji na wenye nguvu dhidi ya wanyonge na matajiri dhidi ya maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka karibu hamsini sasa tujiulize mfumo wetu wa elimu unatoa maarifa muafaka kwa vijana wetu? Mfumo wetu wa elimu unaondoa matabaka katika nchi yetu? Ni dhahiri kwamba hivi sasa tuna elimu kwa ajili ya watu maskini na elimu kwa ajili ya watu wenye uwezo. Tuna elimu kwa ajili ya sisi viongozi na walimu kwa ajili ya wapiga kura.

Mfumo wetu wa elimu unajenga matabaka ya walionacho na wasionacho na kutokana na hali hiyo Serikali sasa inaanza hata kutaka kudhibiti bei za shule binafsi ili wenye uwezo wasipandishiwe bei zikawa kubwa zaidi hasa baada ya Serikali mpya kubana mianya ya kupata mapato yasiyo halali kuwezesha kulipa ada kubwa. Kazi ya Serikali kimsingi ni kusaidia wanyonge wanaosoma kwenye mashule yenye hali mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike wakati sasa tujiulize maswali magumu kuhusu elimu. Tujiulize changamoto za elimu ya Tanzania nini? Ni suala la bajeti ndogo? Ni suala la ubora wa elimu? Kama ni kuhusu bajeti ni kwa nini uwekezaji mkubwa uliofanywa kwa miaka kumi ya Serikali ya Awamu ya Nne ambapo zaidi ya shilingi trilioni mbili zimewekwa kwenye elimu na haujaboresha elimu yetu? Kama ni kuhusu ubora ni kwa nini tumeshindwa kulitatua na kila siku tunarudia na kurudia na kurudia? Ni nini nyufa katika mfumo wetu wa elimu wa sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti ni dhahiri tumekuwa tukitoa majawabu yale yale kwa tatizo la ubora wa elimu tukitegemea matokeo tofauti. Tumekuwa tukilalamika kuhusu bajeti, bajeti iliwahi kufika 20% ya bajeti mwaka 2008 lakini hakuna kilichobadilika. Tumekuwa tukilalamika kuhusu ughali wa elimu na

tukapanua udahili kwa kiwango kikubwa lakini bado shida za elimu zipo pale pale. Hata sasa tumetangaza elimu ya msingi bila malipo na tunatuma fedha yote kwenye mashule *(capitation grants),* udahili umeongezeka kwenye baadhi ya maeneo mpaka 140%. Lakini elimu bado haitengemai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana niliuliza rafiki zangu kwenye mtandao wa *facebook* kuhusu mambo gani wanayotaka kufanywa ili kuboresha elimu nchini kwetu. Nimeambatanisha maoni yao na kuwasilisha kwako ili yaingie kwenye *Hansards* za Bunge. Maoni ni mengi yanashabihiana na hali halisi ya elimu yetu. Kila Mtanzania analalamika na kutoa mapendekezo ya namna ya kuboresha elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetunga sera mpya ya elimu inayounganisha elimu ya sasa ya msingi na sekondari na kuitwa elimu msingi. Tumeweka miaka kumi ya watoto kusoma elimu msingi. Muono wa sera ni kana kwamba changamoto zetu ni miaka ambayo watoto wanakaa shule. Mwandishi mmoja kuhusu elimu kaandika kitabu cha *Rebirth of Education: Schooling isn't learning*. Mwandishi huyu anaitwa Lant Pritchett. Naomba watu wote wanaopenda elimu nchini na wanotaka kuleta mapinduzi kwenye elimu wasome kitabu hiki. Kimsingi Pritchett anasema kukaa darasani sio kupata elimu, kwenye nchi nyingi zinazoendelea ikiwemo Tanzania tumewekeza kwenye kufikia malengo ya idadi ya watoto wanaoandikishwa badala ya kuwekeza kwenye kutoa maarifa kwa watoto. Ndiyo maana hapa nchini kwetu takribani vijana 60% wanaofanya mtihani wa kidato cha nne hufeli kwa kupata sifuri na kwenye baadhi ya mikoa kama Kigoma 86% hupata sifuri na daraja la nne. Watoto wanakwenda shuleni lakini hawajifunzi, hawapati elimu. Sera ya elimu lazima itoe fursa ya kuzalisha watoto wanaopata elimu na sio kukaa darasani tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa karibuni kabisa unaonyesha ni 40% pekee ya watoto wa darasa la nne wanaoweza kufanya hesabu hii, sita gawanya kwa tatu (6/3) au kuzidisha saba mara nane. Matokeo ya miaka na miaka ya uwezo yanaonyesha hali hiyo pia. Kwa mfano karibu 50% ya watoto wanaomaliza darasa la saba hawawezi kufanya mahesabu au kusoma hadithi ya darasa la tatu. Kwa nini watoto wetu hawajifunzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, visababishi vya hali hii ni vingi sana, lakini kikubwa kuliko vyote ni mwalimu. Matatizo kuhusu mwalimu Tanzania ni lundo lakini tunaweza kuongelea mawili kwa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa walimu katika miaka ya karibuni nchi yetu imepiga hatua katika kusomesha na kusambaza walimu. Lakini walimu wengi waliopo mashuleni hawafundishi. Utafiti wa karibuni kabisa unaonyesha kuwa ukifanya ziara ya kushtukiza mashuleni ni 47% ya walimu waliopo shuleni ndiyo waliopo darasani kufundisha vipindi walivyopangiwa.

Aidha, walimu wanafunzi nusu tu ya muda wanaopaswa kufundisha. Matokeo yake ni kwamba asilimia 50 ya muda wa watoto shuleni unapotea bila kusoma. Kiuchumi maana yake ni kwamba tunapoteza asilimia 50 ya uwekezaji katika elimu ukizingatia kwamba pesa nyingi katika elimu zinaenda katika mishahara ya walimu. Utafiti ambao umetolewa leo uitwao *Tanzania Service Delivery Indicators* unathibitisha kuwa 49% tu ya walimu wanaingia darasani na kufundisha zaidi ya nusu hawapo shuleni kabisa au hawafundishi. Utafiti huu umehoji walimu 3,692 na wanafunzi 4,041 na umefanywa na *REPOA* na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inasababishwa kwa kiasi kikubwa na motisha na usimamizi hafifu kwa walimu. Hivyo ni muhimu kufanya bidii kama nchi kutoa motisha kwa walimu lakini ni muhimu pia walimu wasimamiwe na wapewe mafunzo kazini ya mara kwa mara. Kwa sasa ni asilimia tano tu walimu wanakuambia wamewahi kuhudhuria mafunzo yoyote kazini katika miaka mitano iliyopita. Ndiyo maana tumekuwa tukidai kwa miaka mingi sana chombo cha kitaaluma cha walimu *(Teachers' professional board)* lakini Serikali imegoma kunyang'anywa udhibiti wa walimu. Tuwekeze kwa mwalimu kama ninavyoshauri hapa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya juu hapo ni balaa kabisa, ubora wa vyuo vikuu umeanza kutia shaka. Katika utafiti wa juzi juzi wa *Times Higher Education* hakuna chuo hata kimoja cha Tanzania kilichopo katika orodha ya vyuo bora 30 Afrika. Tupo nyuma ya Makerere na Nairobi ambavyo tulikuwa tunavizidi, hatufanyi uwekezaji katika tafiti. Nchi ilishaamua kuwekeza asilimia moja ya Pato la Taifa katika utafiti lakini hadi sasa Serikali imetoa 0.001%. Vitabu vya bajeti vinaonyesha kuwa bajeti kubwa ya elimu inakwenda elimu ya juu lakini kwenye mikopo. Uwekezaji kwenye utafiti haufanyiki na tutaathirika sana kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini falsafa ya Rais Magufuli katika elimu? Rais anasema Tanzania ya Magufuli ni Tanzania ya viwanda, viwanda kwenye nchi ya wajinga? Nani anafanya kazi kwenye viwanda hivyo? Nani atasimamia mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kijamii na hata ya kisiasa yatakayoletwa na uchumi wa viwanda? Tunaposema tunataka nchi ya uchumi wa kati tunajua mahitaji ya elimu ya uchumi wa kati? Tunaelekeza rasilimali fedha katika kujenga rasilimali watu itakayoendesha uchumi wa viwanda? Tunaposema uchumi wa viwanda tunawasemea watoto wetu hatujisemei sisi, tunasemea kizazi kijacho. Tunakiandaa kwa Tanzania hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mahusiana chanya kati ya elimu na ukuaji wa uchumi, vilevile kuna mahusiano chanya katikati ya ubora wa rasilimali watu (elimu na afya) na ukuaji wa uchumi. Tafiti zinaonyesha kuwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara zinaweza kwenda kwa kasi kiuchumi iwapo zitawekeza

kwenye elimu na afya. Robo ya kasi ya ukuaji uchumi inaweza kuchangiwa ubora wa rasilimali watu pekee.

Hivyo tunapotaka kujenga uchumi wa viwanda na ili uchumi huo uwe na maana ni lazima kuwekeza vya kutosha kwenye elimu. Hata hivyo, ni lazima tuwekeze tukiwa na ushahidi wa kisanyansi kuhusu nyufa za elimu ya Tanzania *(evidence based policy interventions)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ndogo ya elimu ya ufundi peke yake inahitaji Watanzania wenye ujuzi wa juu milioni tatu ifikapo mwaka 2025. Pia Tanzania inahitaji watu wenye ujuzi wa ufundi (kutoka *VETA* na *Technical Schools)* wapato milioni saba ifikapo mwaka 2025.

Ni muhimu sana kufungua macho na kufanya maamuzi mahususi kuhusu elimu. Tunahitaji uwekezaji wa angalau 20% ya bajeti yetu kwenda kwenye elimu kwa miaka kumi ijayo ili kuweza kuleta mabadiliko makubwa kwenye elimu. Hata hivyo, kipimo cha msingi cha mafanikio katika mfumo wa elimu ni kama watoto wanaotoka kwenye mfumo huo wa elimu wana maarifa, ujuzi na uwezo wa ulimwengu watakaoukabili. Hatuwezi kupata mafanikio haya bila kufumua mfumo wetu wa elimu, kupanua demokrasia ya utoaji elimu na kuhakikisha walimu wanapata motisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya motisha tunayoweza kuwapa walimu ni kuwalipa vizuri, kuwasimamia vizuri na kuwapa mitihani maalum kila wakati ili kuwapandisha madaraja.

Napendekeza *salary scale* ya walimu iwe sawa na angalau nusu ya *salary scale* ya Wabunge na viwango vya mishahara kati ya walimu wanaofundisha ngazi yoyote ile iwe sawa kulingana na usawa wa elimu, muda kazini na juhudi *(performance based remunerations)*. Najua haya yaweza kuonekana magumu lakini naamini maneno aliyoyasema mwanaharakati wa elimu nchini Rakesh Rajani aliyepata kusema *more of the same won't cut I anymore*. Kama elimu ndio silaha kubwa ya kuleta maendeleo, ni lazima tufanye tofauti ili kuboresha elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Kamati ya Bunge ya Huduma Maendeleo ya Jamii kwamba Taifa liunde Tume ya Wataalam ili kuweza kutafuta nyufa za elimu yetu na kutoa mapendekezo yanayotokana ushahidi wa kisayansi. Tuunde Tume ya Elimu sasa ili tuweze kuwa na muda wa kutosha wa kutatua changamoto za elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika pendekezo la kuanzisha vyuo vya ufundi kila mkoa natoa maombi maalum kwa mkoa wa Kigoma kuanzisha Taasisi ya Teknolojia ya Ujiji *(Ujiji Institute of Technology – UIT)*. Mji wa Ujiji ni moja ya miji

mikongwe nchini ambayo inasinyaa kama sio kufa. Uanzishaji wa chuo utakaoweza kudahili angalau wanafunzi 5,000 itakuwa ni chachu kubwa ya maendeleo mji huu na Tanzania kwa ujumla. Taasisi ya Teknolojia ya Ujiji itaweza kusaidia sana kuziba mianya ya wataalam wa katika kwenye sekta ya usafirishaji *(logistics)* kwa kuzingatia kuwa Kigoma ni lango la Magharibi la Taifa letu. Napendekeza kuwa Serikali ilitazame kwa kina ombi hili ili kuweza kuongeza wataalam wa kati katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza pia Serikali itazame upya suala la sera ya vitabu ili kuhakikisha kuwa uwekezaji katika uchapishaji unaongezeka nchini. Nadhani ni wajibu wa Serikali kuhakikisha ubora wa vitabu badala ya yenyewe kuhangaika na kuandika na kuchapisha vitabu. Sera ya vitabu inazalisha ajira kwenye nchi na inawezesha Watanzania kutafuta fursa kwenye maeneo hayo pia. Wachapishaji wa ndani wanashindwa kukua kwa sababu Serikali imewabana. Serikali haipaswi kubana, inapaswa kuchochea ukuaji wa sekta ya uchapishaji.

Vilevile napendekeza sana tuwekeze kwenye maktaba za kijamii kwenye kata zetu na miji yetu. Maktaba hizi ziwe na vitabu na tuhamasishe watu wenye vitabu kutoa vitabu kwa maktaba hizi. Tujenge Taifa la wasomaji kwa kuhamasisha usomaji kuanzisha ngazi za chini kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza kuwa mapendekezo ya Kamati ya Bunge kuhusu namna ya kutoa mikopo na kuikusanya yachukuliwe kwa uzito unaostahili. Mikopo isiwe sehemu ya bajeti ya Wizara badala yake Bodi ipewe fedha moja kwa moja kutoka hazina *(direct transfer)* na mfumo wa malipo udhibitiwe. Ni lazima tufanye tafiti kuhakikisha kuwa ifikie wakati Bodi ya Mikopo iweze kujiendesha yenyewe kutokana na fedha zinazorejeshwa. Mfumo wa kutumia *credit reference bureau* na vitambulisho vya Taifa na hata *mobile technology* kuhakikisha mikopo inarejeshwa ni mfumo ambao utakuwa na mafanikio makubwa sana. Serikali ifanyie kazi pendekezo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza pia kuwa pendekezo la Kamati kuanzisha *President Magufuli Scholarship Award* lianze mara moja. Tuchukue watoto waliofanya vizuri angalau 50 kila mwaka na kuwasambaza kwenye vyuo vikuu vikubwa duniani. Ndani ya miaka kumi tutakuwa tumetengeneza mamia ya Watanzania wenye uwezo mkubwa kwenye nyanja zote nchini. Rais atakuwa ameacha jambo kubwa na la kukumbukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ALLY S. UNGANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya tele na kuweza kuwatumikia wananchi

wangu wa Jimbo la Kibiti, nawaahidi sitowaangusha, naomba ushirikiano kutoka kwao, Hapa Kazi Tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi. Kwanza nampongeza Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako pamoja na Watendaji wake wote wa Wizara husika kwa kazi yao nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitaala ya masomo haiendani na changamoto ya maisha ya kila siku. Napenda kuishauri Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi kufikiria kurudisha mitaala kama ilivyokuwa zamani ya sayansi kilimona sayansi kimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kutekeleza ahadi yake ya elimu Bure. Katika Jimbo langu la Kibiti wazazi wameitikia kauli hii kwa kupeleka watoto wengi kuandikishwa katika shule zangu za msingi. Japokuwa zipo changamoto, naamini huu ni mwanzo tu yote yataisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali yangu sikivu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kulipa madeni yote ya Walimu, kuwapandisha madaraja kwa wakati, kuwalipa madai yao ya likizo, kuwalipa posho ya mazingira magumu kama kwenye Jimbo la maeneo ya Kibiti, *Delta*, Mfisini, Mbwera, Kiongoroni, Maparoni na kadhalika

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimba za utotoni. Napenda kumshauri Waziri wangu mchapakazi wa Wizara hii kuangalia suala hili kwa umakini. Moja, aboreshe mazingira ya shule na yawe karibu na makazi ya wananchi.

Pili, mtoto akipata ujauzito baada ya kujifungua apewe kipaumbele cha kurejeshwa tena shuleni. Tatu, kuhakikisha tunajega mabweni ya kutosha katika shule zetu za sekondari zote za kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuyapongeza mashirika ambayo si ya Kiserikali jinsi yanavyochangia sekta hii ya elimu. Nalishukuru shirika la C*AMFED* jinsi linavyotusaidia kwenye suala hili la elimu katika Jimbo langu la Kibiti na wananchi wote tunawaunga mkono.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu ada elekezi, Serikali iwaache wamiliki kupanga bei kwa kuwa gharama za uendeshaji wa shule hizo ni kubwa sana kutokana na michango mingi na kodi. Pia shule hizi hazifanani kutoka moja hadi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nizungumzie kuhusu vibali vya Walimu wa nje. Serikali iangalie namna ya kuondoa vizuizi vya Walimu wa kutoka nje kufundisha Tanzania hasa Walimu wa masomo ya hesabu na sayansi. Urasimu mkubwa wa Serikali wa kupata *working permit* na kodi kubwa inayotozwa na Serikali inakatisha tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Chuo cha *VETA* Geita. Naiomba Serikali kunipatia majibu ni lini chuo cha *VETA* kitajengwa katika Mkoa wa Geita ambao ni mpya na eneo la kujenga chuo hicho lilitengwa toka mwaka 2014. Kwa mujibu wa *VETA,* ujenzi wa chuo hicho ulikuwa umefadhiliwa na *ADB* kwa thamani ya *6.7 billion*, leo miaka miwili hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne ni kuhusu utitiri wa vyuo binafsi. Serikali ichunguze sana viwango vya elimu vinavyotolewa na vyuo mbalimbali vilivyosajiliwa na *NECTA*. Mfano ni Chuo cha Elimu ya Utalii Musoma kimefungua matawi katika wilaya za Kanda nzima ya Ziwa, je, ubora wa *certificate* na diploma hizi unafanana? Hii ni pamoja na matawi ya vyuo vikubwa na vidogo Tanzania ikiwemo *CBE,* Mipango na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, madeni ya wazabuni mashuleni. Serikali itoe taarifa ni lini itawalipa wazabuni fedha zao walizotumia kutoa huduma mashuleni. Hivi sasa hali ya huduma katika shule zetu ni mbaya kutokana na madeni haya ya wazabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, nyumba za Walimu vijijini. Naishauri Serikali kuanzia sasa itoe tamko la kuzuia kabisa halmashauri zote kujenga nyumba za watumishi wa mjini, kuacha kujenga ofisi za vijiji na kuacha kununua magari mapya na kuhamishia pesa yote kwa miaka mitatu kwenye nyumba za Walimu. Nashauri pia ramani ya nyumba *simple* iandaliwe kwa ajili ya nchi nzima mfano vyumba viwili vya kulala, *sitting room* na jiko.

MHE. MASHAKA MAKAME FOUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia afya na kuweza kuchangia Wizara hii ya Elimu. Pia namshukuru Waziri na Watendaji wake wote kwa kujipanga vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali ya CCM kwa kupiga hatua kubwa kwa upande wa elimu. Anayesema Serikali haijafanya kitu, je, haoni kwa macho, hasikii, labda ana lake jambo.

Baadhi ya mafanikio kwa Serikali ya CCM ni kujenga shule za awali kutoka jumla ya shule 10,612 mwaka 2010 hadi kufikia shule 14,783 mwaka 2015 zenye Walimu 13,600. Serikali imeandikia watoto wa miaka 7-13 kutoka wanafunzi 6,499,581 mwaka 2005 hadi kufikia wanafunzi 7,679,877 mwaka 2013. Idadi ya wanafunzi wa vyuo vikuu imeongezeka kutoka wanafunzi 139,638 mwaka 2010

hadi kufikia wanafunzi 218,959 mwaka 2014. Mwaka huu ni mwaka wa historia, Mheshimiwa Rais baada ya kutangaza elimu bure, watoto wengi wamefurika mashuleni, haya ndiyo maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila pawapo na mafanikio na changamoto hazikosi, la msingi ni kujipanga na kuzipatia ufumbuzi. Ufumbuzi wa changamoto kwa upande wa elimu si Wizara peke yake, hili ni jukumu letu sote jamii nzima. Mzazi analo jukumu kwa mtoto kuhakikisha anakuwa na maadili mema kuanzia nyumbani, mzazi ahakikishe mtoto anahudhuria shule na kwa wakati, mzazi ahakikishe mtoto ana afya nzuri na msafi. Serikali ihakikishe kwa kila shule vyombo vitatu viwe vinashirikiana yaani uongozi wa shule, walimu na wazazi kwa ajili ya kumpatia elimu mtoto. Wizara iweke mitaala inayoendana na mapinduzi ya viwanda na kimataifa, vitabu viwe vya aina moja kwa nchi nzima kwa madarasa yote kuepuka kila shule kusomesha mada yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iajiri Walimu wa kutosha ili kuepuka vipindi vingi kwa mwalimu mmoja hasa katika shule za awali. Serikali ihakikishe vitabu vya kiada na ziada ni vya kutosha mashuleni. Walimu waboreshewe maslahi yao ili wafanye kazi kwa hiari. Serikali ifanye ukaguzi wa mara kwa mara kuhakikisha Walimu wanafanya kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Ndalichako na Naibu wake Mheshimiwa Stella Manyanya kwa kazi nzuri zinazofanywa. Nawapongeza pia kwa kushirikiana na watendaji, wameandaa taarifa ambayo inaleta matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kuwa *aspect* ya *quantity* tumefanikiwa sana na sasa tujielekeze kwenye *aspect* ya *quality*. Serikali iwekeze kwenye kuboresha namna tendo la kujifunza na ujifunzaji linavyotaka kwa kuangalia upya idadi ya wanafunzi kwa elimu ya msingi kwani wanafunzi 45 ni wengi ibadilike iwe 35; Walimu wapewe motisha ili waongeze morali; vifaa na vitabu vya kufundishia vipatikane na kuongeza idadi ya Walimu wanaopata mafunzo kazini kwa kutumia vituo vya walimu vilivyopo *TRCS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Udhibiti wa Ubora wa Shule (Wakaguzi wa Shule). Kitengo hiki kipewe fedha za kutosha ili waweze kukagua shule nyingi. Wadhibiti ubora wapewe mafunzo ya mara kwa mara na nyenzo za kufanyia kazi. Vilevile idadi ya shule zimeongezeka muundo wa Wadhibiti Ubora wa Elimu urekebishwe badala ya kuwa kwenye kanda wawepo kimkoa na kuwe na mawasiliano na Katibu Tawala wa Mkoa *(RAS)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ada elekezi. Nashauri Serikali ijielekeze kwenye hoja za wananchi wengi, tuboreshe shule zetu na wananchi wataacha kupeleka watoto shule binafsi. Hali hiyo ikifikiwa wamiliki wa shule watapunguza ada kwa kufuata nguvu ya soko. Serikali ijikite katika kuboresha elimu katika ngazi zote na si vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa mchango wangu kwa maandishi ili na mimi niweze kushauri Serikali katika kuboresha sekta hii muhimu ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara ya Elimu itoe fursa kwa watu binafsi wenye uwezo kuwekeza katika elimu ya ufundi *VETA*. Hii itasaidia kuipunguzia mzigo Serikali unaotokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mimba za wanafunzi, Wizara ilete Muswada Bungeni utakaoonesha jinsi ya kuwabana na kuwawajibisha wale wanaohusika na mimba hizo. Pia Serikali iweke mtaala maalum kwa wasichana wanaozalia shuleni ili tusije wapa haki ya kusoma na kujikuta tunakandamiza haki ya watoto waliozaliwa mfano haki ya kunyonya, kuwa karibu na wazazi lakini pia tusijeleta mzigo mkubwa wa kulea kwa bibi watakaokuwa wakilea watoto hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujitahidi kutoa motisha kwa Walimu ili kuwapa morali katika utendaji kazi wao. Natoa mifano michache ya baadhi ya Walimu niliokutana nao katika Wilaya ya Kyerwa kwenye moja ya ziara zangu. Walimu hawa walipandishwa vyeo miaka miwili iliyopita lakini mpaka leo hawajaongezewa mishahara. Nafahamu changamoto ya bajeti inayoikabili Serikali yetu ila nashauri tusiwapelekee barua za kuwapandisha vyeo kama hatuna uhakika na malipo yao. Baadhi ya Walimu hao ni kama ifuatavyo:-

(1) Rutaihwa Kazoba
(2) Geofrey Kamondo
(3) Rugeiyamu Damian
(4) Selestine Tibanyendera Ishengoma
(5) Erick Twesige Anacleth
(6) Philbert Jeremiah Kazoba
(7) Tabu Herman
(8) Ndyamukama Cylidion
(9) Heavenlight Baguma
(10) Frida Buyoga
(11) Onesmo Alphonce
(12) Philbert Kinyamaishwa

(13) Diomedes Kajungu
(14) Yohatam Samwel
(15) Diomedes Kajungu

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali hao ni baadhi ya Walimu waliopo katika Wilaya ya Kyerwa ambao nilipofanya ziara yangu ya kiutendaji niligundua hao na wengine wengi ambao majina yao sijayataja wamepandishwa vyeo kwa takribani miaka miwili sasa na mpaka leo hawajaongezwa mishahara. Naomba Mheshimiwa Waziri ufuatilie matatizo haya katika Wilaya ya Kyerwa na upatapo nafasi naomba unijibu hoja zangu hizi kwa maandishi ili niweze kupeleka mrejesho kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kumwomba Waziri ashirikiane na Wizara ya TAMISEMI ili kuweza kusukuma vipaumbele ambavyo kimsingi Wizara hii mnakutana navyo moja kwa moja katika kutekeleza Sera ya Elimu nchini. Nakutakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yako, ahsante.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inahitaji kufanya marekebisho ya msingi katika mfumo wetu wa elimu na mafunzo nchini.

Naomba Mheshimiwa Waziri asome kwa makini sana Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, Hotuba ya Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii na ripoti ya Profesa Mchome ya mwaka 2013 kufuatia *mass failure* ya watoto wetu katika mitihani ya *Form* IV mwaka 2012. Naamini hizi zote zitamsaidia katika kazi nzito iliyo mbele yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri alipitie upya suala au sakata la *TCU* na wanafunzi wa Chuo cha St. Joseph. Kwa kiasi kikubwa tatizo liko katika utaratibu ambao Serikali imeuweka. Mabaraza yetu ya *NACTE*, *NECTA* na *TCU* yanatakiwa yafanye kazi zao kwa kuzingatia mipaka yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiutaratibu vyuo viilivyo chini ya *NACTE* vinadahili wanafunzi waliopata *minimum* ya D nne (4) katika mtihani wa *form four* kwa kozi ya *NTA* 4 katika chuo chochote. Wanafunzi waliofukuzwa *St. Joseph College* wamekidhi hili. Tatizo liko wapi? Kupata diploma watasoma miaka mitatu na wakiendelea mpaka digrii watalazimika kusoma miaka mitano, hili ndilo walilokuwa wanafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusema Mheshimiwa Waziri apitie kwa makini taasisi zilizo chini ya Wizara yake ili kuitendea haki nchi yetu na hasa vijana wetu. Lazima iwepo nidhamu na utaratibu maalum kwa taasisi zetu wakati wanatekeleza majukumu yao. Pamoja na nidhamu, uadilifu ni muhimu

zaidi. Vijana wetu wengi wameharibiwa maisha yao au ndoto zao kwa maamuzi ya *NECTA* kwa miaka mingi na sasa tunashuhudia hili la *TCU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *private secondary schools* wasifanye mchujo wa watoto kwa maana ya *slow learners*. *Private schools* wameweka *pass mark* yao tofauti na Serikali. Huanza mchujo kuanzia kidato cha pili hadi *form IV terms* za mwanzo. Hata kama watoto wakifikia kiwango cha "*pass mark*" ya Serikali kama hajavuka cha shule wanazosoma *(private)* huondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo lao matokeo ya mwisho *final exams results* wapate *division I* wengi na *division* II wachache basi, hawataki *division* III, IV na 0. Wanataka soko la shule zao liwe juu kwamba wanafaulisha sana. Huu ni unyanyasaji na ubaguzi wa hali ya juu, ukemewe kwa nguvu zote. Binadamu tumepishana, wengine *fast learners* na wengine *slow learners* lakini wote uelewa wao ni sawa. Ni mbaya sana inaleta pia usumbufu kwa wazazi, huitwa na kuambiwa mhamishe mtoto wako kwa vile hataweza ku-*cope* na wenzake. Hii ni mbaya, mbaya kabisa.

MHE. MAKAME KASSIM MAKAME: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa tukiwa na afya njema. Pia sina budi kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya ya kutumbua majipu na kuongeza mapato, kwa hili hongera sana. pia napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi kwa kazi nzuri ya kuwasilisha hotuba ya bajeti iliyo nzuri kabisa na yenye muamko kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hii napenda niishauri Serikali kuhusu mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Ingawa *ceiling* hairidhishi lakini naomba fedha za mikopo ya wanafunzi zigawiwe angalau 40% zipelekwe kwa wanafunzi walioko Zanzibar ili na wao wafaidike na mkopo huo na waweze kuinua kiwango cha elimu kwa sababu wanafunzi walio wengi ni maskini na wana uwezo mkubwa na kusoma vyuo vikuu lakini wanashindwa kuendelea kusoma kutokana na kikwazo hicho cha ukosefu wa fedha na hatima yake wanabaki mitaani kuzurura ovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Wizara/Serikali ilizingatie hili ili tuandae wataalamu watakaoweza kuendesha uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuweka mfumo mzuri wa elimu kwa wanafunzi wa shule za msingi hususan shule za kule Zanzibar ambao hivi

sasa wanasoma mpaka darasa la sita. Kwa kweli nashauri utaratibu huu urekebishwe au urejeshwe ule ule utaratibu wa zamani kwa sababu mwanafunzi anayemaliza darasa la sita bado ni mdogo mno hatimaye wanakosa elimu ya kutosha na wanafeli na kubaki kuzurura. Nashauri urejeshwe utaratibu wa zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napongeza Mawaziri na Watendaji wote katika Wizara kwa kuwasilisha hotuba ya makisio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubora wa elimu na ualimu. Tumeshuhudia zaidi ya miaka kumi mitaala mingi ikifanyiwa mabadiliko ambayo yameleta shida kwa wananchi kwani ubora wake umeshuka ukilinganisha na miaka ya nyuma. Vilevile kozi ya ualimu imekuwa haizingatii viwango hasa vyuo vya watu binafsi. Walimu katika shule za Serikali na binafsi hawazingatii taratibu na kanuni katika utendaji hivyo Wizara iangalie namna ya kuboresha kanuni ziendane na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Katika hotuba ya Waziri hakutaja Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Msaginya kilichopo Halmashauri ya Wilaya Nsimbo, Mkoa wa Katavi. Taarifa za hivi karibuni ni kuwa kimehamishwa toka Wizara ya Afya. Chuo hiki kina matatizo mengi kuanzia rasilimali watu, miundombinu na madeni ya wakandarasi ambao wamesimama kazi kwa sababu hawajalipwa. Hivyo tunaomba Wizara ifanye malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo kwa vitendo. Katika kuongeza ujuzi wa wanafunzi, tunashauri Wizara iboreshe mwongozo wa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa kuanzia mwaka wa kwanza kushiriki mafunzo haya ili kuwajengea uwezo mzuri wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo. Wizara inahitaji kuboresha utendaji wa Bodi ya Mikopo na hasa kuwawekea malengo kwa kukusanya madeni toka kwa wanafunzi ambao wanadaiwa. Pia muda wa kulipa upunguzwe tena kwa kuwa fedha inahitajika kusaidia wengine na kuondoa mzigo kwa Serikali kutoa fedha kila mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitihara elimu ya juu. Ili kuboresha elimu ya vyuo vikuu nchini tunashauri Wizara itoe mwongozo juu ya mitahara *(course outline)* zenye kuendana na hali ya sasa na pia ziwe zenye ubora na kufanana ili shahada, stashahada zipate ubora duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile utaratibu wa kutunga mitihani na kusahihisha uwe unashirikisha mtu zaidi ya mmoja *(panel)* kuondoa rushwa za aina mbalimbali kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ruzuku vyuo binafsi vya ufundi. Tunashauri Serikali iangalie namna ya kutoa ruzuku kwa vyuo binafsi vya ufundi ili kuviwezesha kutoa elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami niweke yangu tena ya muhimu katika hoja hii iliyopo mezani ya bajeti ya Wizara muhimu na uti wa mgongo ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze na suala zima la *VETA*-Mikumi. Kwa kuwa Chuo cha *VETA* - Mikumi ndiyo chuo pekee kilichopo katika Jimbo la Mikumi na kwa kuwa ukombozi wa vijana wengi wanaohitimu shule za sekondari zilizopo Jimboni kila mwaka hukosa mwelekeo, hivyo ni muhimu kukipa kipaumbele chuo hicho kwa kukiboresha katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kupanua wigo katika fani zinazotolewa ili ziendane na mazingira ya Jimboni, kuongeza fani ya ufundi-kilimo *(agro-mechanics);*

(ii) Kukiongezea uwezo wa udahili kwa kuongeza idadi ya mabweni hasa kwa ajili ya wasichana ili kuendana na sera ya kuleta uwiano katika udahili kati ya wasichana na wavulana;

(iii) Kuongeza idadi ya madarasa na karakana za kujifunzia, pia kupanua wigo wa mafunzo kwa vitendo; na

(iv) Kuongeza na kuboresha vifaa vya kujifunzia ili kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia ili kuwajengea vijana uwezo wa kitaalamu unaoendana na mabadiliko yanayotokea sokoni kila wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijikite kwenye changamoto zinazoikabili *VETA*-Mikumi kama ifuatavyo:-

(i) Baadhi ya watumishi kukaa muda mrefu sana bila kuhamishwa, wapo waliokaa zaidi ya miaka 20, hii inaathiri sana utendaji wa kazi kwa kuwa wanafanya kazi kwa mazoea na ufanisi kupungua;

(ii) Kuna upendeleo katika udahili hasa katika chaguo la pili hivyo kupelekea aidha ndugu wa viongozi au watu wao wa karibu kujaza nafasi hizo huku wananchi wazawa wa Mikumi wakikosa fursa hiyo. Katika udahili mwaka

wa masomo 2016, wananchi wa Mikumi waliopata fursa ni asilimia 10 tu ingawa tunatambua kuwa usaili huwa unajumuisha waombaji kutoka kila kona ya nchi lakini vijana wa Mikumi walipaswa kupewa kipaumbele hasa katika chaguo la pili;

(iii) Kuwepo kwa uongozi usiofuata taraibu, kanuni za utumishi wa umma na utawala bora. Uongozi wenye mfumo kandamizi usiokubali kufanya kazi na watu waadilifu, uongozi unaofanya ubadhirifu na maamuzi yasiyokuwa na tija kwa *VETA* na Taifa kwa ujumla;

(iv) Chuo kimepeleka *mini-bus* kwa matengenezo Dar es Salaam zaidi ya wiki moja katika gereji bubu katika kipindi cha mwezi Mei 2016 bila kufuata taratibu za manunuzi. Pia kukiuka maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kupeleka magari yote ya umma kwa matengenezo *TEMESA;*

(v) Uongozi wa chuo (Afisa Rasilimali Watu na Mkuu wa Chuo) kuwa na mtandao mpana kuanzia *VETA*-Makao Makuu wa kuwakataa, kuwapinga na kuwahamisha watumishi wanaonekana kutokubaliana na mawazo yao ya kibadhirifu.

Kwa mfano Salum Ulimwengu (Mratibu Mafunzo) aliyekaa kwa kipindi cha miaka miwili na kuhamishiwa Arusha baada ya kuvutana na menejimenti baada ya Mkuu wa Chuo kukiuzia chuo gari bovu lililokuwa likimilikiwa na rafiki yake, pamoja na ununuzi wa spea hewa za magari ya mafunzo. Suala hili lilichunguzwa na ofisi ya *CAG* na hakuna ripoti yoyote iliyotoka. Hata hivyo, uuzwaji wa gari hilo haukuhusisha ofisi ya Afisa Mafunzo ila Kitengo cha Ufundi magari bila kufuata taratibu za mamlaka;

(vi) Kukataa kumpokea na kushindwa kumkabidhi ofisi Mratibu wa Mafunzo kwa kipindi cha mwaka mzima kinyume cha *section 3.13* ya *VETA Staff Regulations and Conditions of Service* ambayo inatamka kuwa mabadiliko yoyote ya kiutumishi lazima yafanyike kwa makabidhiano ya kimaandishi (Rejea *Internal Audit Report VETA- Mikumi, March- December 2014*);

(vii) Mkuu wa Chuo na Afisa Rasilimali Watu kushinikiza uhamisho ili kulinda wizi wa mali za umma na ubadhirifu. Mfano mwingine, Msuya *(Stores Officer)* aliyekaa kwa kipindi cha mwezi mmoja na kupelekwa Morogoro. Joseph Riganya *(Stores Officer)* aliyevutana na uongozi wa chuo na kuhamishiwa Ofisi ya Kanda kwa kisingizio cha matibabu. Riganya alipinga ukiukwaji wa Sheria ya Manunuzi na ubadhirifu katika manunuzi unaofanywa na Mkuu wa Chuo na Afisa Rasilimali Watu; mfano katika ripoti ya ukaguzi wa ndani *(internal Audit report)* ya Machi hadi Desemba 2016 inaonyesha kuwa Afisa Rasilimali Watu, Mhasibu na Mwalimu mmoja walipokea vifaa vya thamani ya shilingi milioni 35

kinyume na taratibu kwani Kamati ya Mapokezi ndiyo yenye dhamana ya kupokea vifaa hivyo. Walifanya hivyo ili kulinda maslahi yao binafsi;

(viii) Ukiukwaji wa taratibu za ajira kwa kumpa mkataba Neema Bui ambaye hana sifa na anafanya kazi za manunuzi kwa maslahi ya Mkuu wa Chuo na Afisa Rasilimali Watu kwa kuwa kila Afisa Manunuzi anayeletwa anaondolewa kwa hila ili asizibe mianya ya wizi; na

(ix) Afisa Manunuzi Rogate aliyehamishiwa mwezi Februari 2016 kutoka Tabora amepewa vitisho kwenye kikao cha menejimenti na sasa anafanya mpango wa kuhama kuwapisha wanaojiita wenye chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuwasimamisha kazi Afisa Rasilimali Watu na Mkuu wa Chuo ili kupisha uchunguzi;

(ii) Kuwahamisha watumishi waliokaa muda mrefu sana katika chuo hiki ambao ndiyo chanzo cha kulea ubadhirifu;

(iii) Kuangalia kama ilikuwa halali kumhamisha Afisa Mafunzo, Ndugu Salum Ulimwengu aliyekaa kwa kipindi cha miaka miwili na ambaye amehamishwa mwezi mmoja tu tangu amhamishe mke wake katika Sekondari ya Mikumi, hivyo mtu aliyepigania maslahi ya Taifa kuteswa kisaikolojia na kifamilia;

(iv) Kufanya uchunguzi maalumu juu ya masuala ya manunuzi na fedha katika chuo cha *VETA*-Mikumi; na

(v) Kufuatilia ilipoishia ripoti ya *CAG* ya Oktoba 2015 juu ya Mkuu wa Chuo kukiuzia chuo gari chakavu kinyume na maadili ya utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niongelee suala zima la elimu bure ambapo kumekuwa na changamoto nyingi kama ifuatayo:-

(i) Ruzuku inayotoka Serikalini ya kila mwezi haikidhi mahitaji ya shule mfano mpaka sasa Walimu Wakuu hawana fungu la mlinzi, umeme na maji;

(ii) Idadi kubwa ya wanafunzi ukilinganisha na Walimu, madarasa na miundombinu mingine kuna vyoo, madawati na kadhalika;

(iii) Huduma ya chakula shuleni irudishwe ili kuhamasisha watoto waende shule;

(iv) Upungufu mkubwa wa Walimu wa sayansi kwenye Jimbo la Mikumi;

(v) Walimu kutolipwa stahiki zao kwa muda mrefu na pia wengi kuchelewa kupandishwa madaraja; na

(vi) Hakuna nyumba za Walimu na pia hawalipwi posho za uhamisho na pesa zao za likizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni baadhi tu ya changamoto nyingi za elimu kwenye Jimbo la Mikumi na Wilaya ya Kilosa kwa ujumla.
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ENG. GERSON H. LWENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba yake nzuri na naunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Wanging'ombe haina shule kidato cha tano na sita pamoja na shule za Mount Kipegere, Makoga, Wamihe na Wanging'ombe kukidhi vigezo vyote vya kuanza masomo ya *high level*. Naomba Waziri alitolee maamuzi yanayostahili. Pia shule za Philip Mangula, Maria Nyerere, Mt. Kipegere, Makinga, Wanike, Wanging'ombe, Igachunya, Luduga, Saji, zinayo mabweni na hivyo zipandishwe hadhi ya kuwa shule za bweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Wanging'ombe ina upungufu mkubwa wa Walimu katika shule za msingi na sekondari. Kwa upande wa elimu ya sekondari hatuna Walimu wa hisabati na masomo ya sayansi. Naomba Wizara hii ituangalie kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujengewa Chuo cha Ufundi cha *VETA* eneo la Soliwaya - Wanging'ombe kwani hatuna hata chuo kimoja kwenye Wilaya hii ya Wanging'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya awali kwa shule nyingi imekosa Walimu wa kufundisha kutokana na upungufu wa Walimu. Tatizo hili limetokana na hivi sasa wazazi kuacha kuchangia kuwalipa Walimu hawa kwa hiyo, Serikali ione maana ya kuelimisha kuhusu uchangiaji kwa maeneo yenye mahitaji kama hili la upungufu wa Walimu na hasa elimu ya awali.

MHE. ROSE C. TWEVE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia kwenye Wizara hii nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja niunge mkono hoja iliyoletwa mbele yetu leo na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Sote tunatambua Tanzania kuna uhaba mkubwa wa Walimu hususani kwenye masoma ya *Mathematics* na *English*. Tanzania hatuna Chuo cha Ualimu kinachoandaa Walimu wa *English* watakaofundisha shule za msingi. Maana yake kuna 100% *lack of trained English Medium Primary School Teachers.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Teachers Colleges* za *Primary Schools* zinafundisha kwa Kiswahili. Sasa changamoto inakuja kwamba, pamoja na kuwa Wizara ya Elimu inatambua mapungufu hayo hakuna *coordination* na Wizara zingine kama Wizara ya Kazi.

Wizara ya Kazi ina *charge* $500 kutoa *class B work permit regardless* wewe ni Mwalimu au ni Injinia wa Dangote *Cement* au *Barrick Gold Mine*. Kinachosikitisha zaidi, Wizara ya Mambo ya Ndani yaani Uhamiaji wao wanatoza $2000 *fee* ya *resident permit* kwa hawa Walimu ambao tunawahitaji sana. Hii *fee* imeongezwa kutoka $600 iliyokuwa wanatozwa mwanzo mpaka $2,000 kwa sasa na hii *fee* ya $2,000 ni kwa miaka miwili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli Taifa letu linataka kusaidia watoto wetu, napenda nishauri yafuatayo:-

(i) Hizi *fee* zifutwe ili kuvutia kupata Walimu bora watakaoweza kufundisha vijana wetu; na

(ii) Tuwape *support* ya kutosha hawa ndugu zetu wenye *private schools* wakati Serikali yetu inaendelea kuboresha hizi *government schools* kwa sababu utafiti unaonyesha *private schools* ndizo zinatoa elimu bora zaidi kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, naomba maslahi ya Walimu wetu yaboreshwe ili kuwapa motisha ya wao kuendelea kuwasaidia vijana wetu. Pia tuhakikishe shule za msingi wanapewa madawati ya kutosha hususani Mkoa wangu wa Iringa watoto wetu bado wanakaa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Wizara ya Elimu kudahili Walimu tarajali 5,690 katika vyuo vya UDOM, Kleruu na Monduli. Pamoja na kudahili wanafunzi hao inaonyesha kuna upungufu wa Walimu 22,000 wa sayansi bado tuna hitaji kubwa sana la kudahili Walimu zaidi. Wizara ingefikiria kufanya programu maalum walau miaka nane (8) ili kuzalisha Walimu wa Sayansi nchini kwa wingi kwa kuwapeleka vyuo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa kujenga maabara katika kila sekondari za kata. Naipongeza pia Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuweka bajeti ya kununua vifaa kwa ajili ya maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, inaonekana pia kuna upungufu wa Walimu wa lugha hasa Kiingereza. Je, kwa nini Wizara isirejee utaratibu wa miaka ya themanini hadi miaka ya tisini ambapo Walimu walikuwa wanasoma kwa michepuo? Kwa mfano:-

(i) Marangu – Kiingereza
(ii) Korogwe – Kiswahili
(iii) Mkwawa – Sayansi
(iv) Monduli – Kilimo
(v) Mandaka/Monduli - Kilimo

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa michepuo ulidahili wanachuo kutokana na ufaulu wao. Je, kwa nini Wizara isirejee mtindo huu ili kupata Walimu waliosomea masoma hayo? Wizara iangalie wapi tulikosea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri kuna mradi wa *Education and Skills for Productive Jobs Programme (ESPT)*. Mradi una nia ya kukuza stadi za kazi na ujuzi. Sekta zilizopo ni sita (6) nazo ni za kukuza uchumi, kilimo, uchumi, utalii, uchukuzi, ujenzi, nishati na TEHAMA. Nashauri fani ya ushonaji na upishi nazo ziongezwe. Wizara inaweza kuona fani hii si hitaji lakini fani ya ushonaji/upishi ni fani ambazo zimeinua wananchi wengi katika ujasiliamali. Inabidi wanafunzi waanze kufundishwa fani hizi tangu msingi ili kuwaandaa wakifika *VETA* waweze kupata ujuzi mzuri zaidi na itasaidia vijana wengi kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu maalum wengi wameizungumzia. Nashauri Wizara ifanye utaratibu wa kufanya sensa ya watoto wenye ulemavu kwani watoto wengi wenye ulemavu wanafichwa. Katika ukurasa wa 97, kiambatanisho (6) kinaonesha idadi ya wanachuo wenye ulemavu wanaodahiliwa katika vyuo ni kidogo sana. Tunataka kujenga Taifa lenye uchumi wa kati ni budi Serikali ikaona umuhimu wa kudahili wanachuo wengi zaidi wenye ulemavu ili nao waweze kupata fursa nyingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sula la maslahi ya Walimu *TSD* ambayo sasa ni *TSC* inabidi ipewe nguvu ya kufanya kazi. Ni vema Wizara ya Elimu na TAMISEMI kuona jinsi ya kuipatia fedha za kutosha ili Walimu waweze kuhudumiwa vizuri zaidi. Kwa kuwa *TSC* inasimamia Walimu wa shule ya msingi/sekondari katika masuala ya nidhamu, maadili, kupandisha vyeo, kuthibitisha Walimu kazini na kutoa vibali vya kustaafu, vikao vya kisheria

(statutory meetings) havifanyiki kutokana na ukosefu wa fedha. Inabidi Wizara ya Elimu na TAMISEMI waiangalie *TSC* kwa jicho la pekee ili waweze kutekeleza majukumu yao vizuri kwa ajili ya ustawi wa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wadhibiti Ubora wa shule za msingi/sekondari, ukurasa wa 18. Naipongeza Serikali kwa kusomesha Wadhibiti Ubora 1,435 ambao wamepata mafunzo ya stadi za KKK ili kutoa msaada kwa Walimu wanaofundisha KKK. Pamoja na kuwepo kwa Wadhibiti hao ni vema Wizara ikaweka utaratibu maalum wa kuwapeleka masomoni Walimu kipindi cha likizo ili wapate mafunzo rejea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 10, kipengele cha 5.0, mapitio ya utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2015/16, katika kusimamia utekelezaji na mambo yaliyobainishwa nazungumzia kipengele (v), naomba pia Walimu wa michezo wapewe mafunzo ili waweze kuwafundisha watoto wetu michezo kwani hakuna ubishi michezo ni ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza tena Wizara ya Elimu, Waziri na timu yote. Nawatia moyo waendelee na kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ANNA J. GIDARYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu inakabiliwa na changamoto nyingi sana ikiwepo ya kuandaa miundombinu ya elimu yenyewe. Changamoto nyingine ni:-

(i) Ubora wa elimu kuanzia ngazi ya msingi hadi vyuo vikuu;

(ii) Uhaba wa madarasa na Walimu kwa shule nyingi hasa Walimu wa masomo ya sayansi;

(iii) Upandishaji wa madaraja mserereko kwa Walimu;

(iv) Uhamisho wa Walimu holela pasipo kulipwa haki zao stahiki na hata posho za uhamisho; na

(v) Uhaba wa nyumba za Walimu/mazingira magumu wanayoishi Walimu;

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu yetu Tanzania haina ubora kuanzia ngazi ya msingi kwa kuwa tunabadilisha mitaala ya elimu kila mara jambo ambalo ni kinyume na taaluma halisi ya Walimu waliyosomea. Hii ni changamoto kubwa kwa Walimu hata katika maandalio ya somo. Haya ni mazingira magumu sana kwa Walimu hata katika maandalio ya somo. Haya ni mazingira magumu sana kwa Walimu na wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Manyara ni mmojawapo ya Mikoa inayokabaliwa na changamoto ya uhaba wa Walimu na majengo ya nyumba za Walimu na madarasa ya kufundishia watoto. Walimu wengi wanaishi katika mazingira ambayo ni hatarishi na si rafiki kabisa kwa Walimu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tabia Wizara kuwapandisha Walimu madaraja kwa mkupuo (madaraja mserereko) bila kupandishiwa mishahara. Kwa muda mrefu na hadi sasa bado kero hizo zinaendelea na bado Wizara imekaa kimya bila kutoa tamko kama Walimu hawa watalipwa madai yao ya kupandishwa madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tabia ya Wizara kuhamisha Walimu pasipo kuwa na sababu za msingi lakini pia Walimu hawa hawapewi posho za uhamisho wala *disturbance allowance*. Mpaka sasa katika Mkoa mzima wa Manyara zaidi ya Walimu 160 wanadai hayo madeni ya msingi kwa Serikali hii takribani miaka zaidi ya kumi na mbili (12) bila kufikiriwa na hata kupatiwa majibu yanayoleta matumaini kwa Walimu hawa, wamebaki na maumivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa nyumba za Walimu ni kero kubwa kwa Mkoa mzima wa Manyara. Katika shule moja ya msingi Haraa iliyoko katika Mji wa Babati, Walimu wanaishi katika mazingira magumu na hatarishi. Nyumba yenye vyumba viwili wanakaa Walimu nane (8) wa kiume, nyumba yenyewe haina madirisha wala haijasakafiwa ni nyumba ya udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mapendekezo yafuatayo:-

(i) Serikali itoe rai kwa Wizara ya Elimu kuhusu mambo yote ambayo ni kikwazo kwa sekta nzima ya elimu kushughulikiwa haraka ili kuokoa muda na kuokoa jahazi la elimu;

(ii) Posho za Walimu zilipwe kwa wakati baada ya madai hayo kufanyiwa uhakiki na malipo yafanyike kwa kila Mwalimu anayedai madai yake;

(iii) Nyumba za Walimu zijengwe za kutosha ili kuondoa kero na adha wanayopata Walimu wetu na kuwaondoa Walimu wetu katika mazingira hatari ya ufundishaji; na

(iv) Serikali irudishe utaratibu ule wa mwanzo wa wanafunzi kufundishwa masomo ya elimu ya kujitegemea ili wapate elimu bora ya kukabiliana na mazingira pindi tu wanapomaliza elimu ya msingi na hata elimu ya sekondari na kupunguza mzigo wa kutegemea ajira ya Serikali tu. Ahsante.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikushukuru wewe na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kutoa mchango wangu katika hoja hii muhimu kwa ustawi wa Taifa ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Profesa Joyce Lazaro Ndalichako na timu yake yote kwa kuandaa na kuwasilisha vizuri sana hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2016/2017. Pia natoa pole kwa Naibu Waziri Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya kwa kuondokewa na mzazi wake mpendwa. Naomba Mwenyezi Mungu ampe moyo wa uvumilivu katika kipindi hiki kigumu cha maombolezo na roho ya marehemu iwekwe mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa mchango wangu kwenye makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya elimu, sayansi, teknolojia na ufundi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubora wa vitabu vinavyotumika kufundisha mashuleni, wakati soko huria la utengenezaji na usambazaji wa vitabu likilenga kupunguza uhaba wa vitabu Serikali idhibiti ubora wa vitabu ili kuhakikisha vitabu vinavyotumika shuleni vinakuwa na ubora ili kuzalisha wasomi wazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa nini kifanyike kwenye mtaala wa elimu, Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu itengeneze mfumo ambao vijana wengi watakwenda kwenye Vyuo vya Ufundi na hivyo kuwa na wazalishaji wengi ambao wataweza kuunda vitu mbalimbali na sio kuwa na kundi kubwa la wasomi wa vyuo vikuu ambao watakuwa wanatafuta kazi baada ya kutunukiwa shahada zao. Ni muhimu sana Serikali ipitie upya mfumo wetu wa elimu ambao kwa kiasi kikubwa unawaandaa wasomi wetu kuwa waajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano kwa mujibu wa hotuba ya bajeti ya mwaka 2014/2015, idadi ya vyuo iliongezeka kutoka 26 hadi 50 kati ya mwaka 2005 hadi 2014 na hivyo idadi imeongezeka kutoka wanafunzi 40,719 kwa mwaka 2005 hadi wanafunzi 200,986 kwa mwaka 2014. Wasomi wote hawa wanaandaliwa kuwa watawala ambao wataanza kutafuta ajira na hivyo kusababisha nchi kuwa na wasomi wengi ambao watahitaji kuajiriwa na siyo kuwa wazalishaji kutokana na mfumo wetu wa elimu kuwa na nadharia nyingi na siyo vitendo. Katika karne ya sasa ni muhimu Serikali kufanya marekebisho katika mfumo wetu wa elimu ili uwezeshe vijana wetu kuwa wazalishaji pindi tu wanapohitimu elimu ya vyuo vikuu na hivyo kuweza kujiajiri wenyewe badala ya kusubiria ajira za Serikali na mashirika binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na Wizara zake ielekeze pesa nyingi kwenye miradi ya maendeleo na sio kwenye matumizi ya kawaida. Mfano, kwa mujibu wa hotuba ya Wizara ya Maliasili na Utalii iliyosomwa Bungeni na Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, kwa mwaka 2015 sekta ya utalii peke yake ilitoa ajira rasmi kwa vijana 500 na ajira 1000 zisizo rasmi.

Aidha, kwa mwaka 2016/2017, Serikali iendelee kuboresha mazingira ya utalii kama vile kununua ndege, kujenga barabara na kujenga viwanja vya ndege ili sekta ya utalii ifanye vizuri ziaidi na hivyo kusaidia kupunguza tatizo la ajira ambalo kwa kiasi kikubwa linatokana na mfumo wetu wa elimu, kuzalisha wasomi wengi wenye shahada ambao wanategemea kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika dunia ya sasa Serikali lazima itambue kuwa tatizo la ajira kwa wasomi wetu wa vyuo vikuu linazidi kuongezeka kila siku kutokana na mfumo wetu wa elimu kuwaandaa vijana wetu kuwa waajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwandishi wa kitabu cha Rich Dad Poor Dad Robert Kiyosaki anasema mifumo ya elimu yenye mtazamo wa *go to school, study hard, get good grades and find a safe and secure job* umepitwa na wakati.

Aidha, mwandishi huyu anashauri mifumo ya elimu ya sasa iwe na mtazamo wa *go to school, study hard, get good grades, build your business and become a successful investor.* Serikali itazame namna ya kuhakikisha vijana wengi wanapata elimu ya ufundi ambayo itawasaidia vijana wengi kuwa wazalishaji wa moja kwa moja na siyo kutegemea ajira. Katika nchi zilizoendelea kiteknolojia kama China na Japan vifaa vingi vidogo vidogo vinatengenezwa na vijana ambao kwa kiasi kikubwa wana elimu ya ufundi tu. Ingawa tuna vyuo vya ufundi stadi, bado idadi ya wanafunzi wanaojiunga katika vyuo hivi ni ndogo kama ilivyooneshwa katika kitabu cha hotuba ya bajeti ya Wizara ya Elimu, ukurasa wa 95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa vyuo vya ufundi kila mkoa; umefika wakati sasa Serikali ianzishe vyuo vya ufundi kila mkoa ambavyo vitawasaidia vijana wetu kupata elimu ya kuwawezesha kujitegemea na siyo kutegemea kuajiriwa na Serikali. Aidha, vyuo hivi vitoe elimu kutokana na mazingira ya eneo husika. Mfano, vyuo vitakavyojengwa Mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya vitoe elimu ya ufundi juu ya matumizi ya mazao ya mbao na vile vitakavyojengwa katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa vijengwe vyuo vya kutoa elimu ya ufundi na ujuzi na kusindika samaki. Kama Serikali itaweka mfumo ambao vijana wengi watakwenda kwenye vyuo vya ufundi wataweza kuzalisha samani nyingi ambazo Serikali pia inaweza kununua samani ambazo zitakuwa zinazalishwa na vijana wetu hapa hapa nchini kwa matumizi mbalimbali na hivyo kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kutokana na kununua samani nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais za kujenga Tanzania ya viwanda, ni muhimu vijana wengi wawe na elimu ya ufundi ambao wataanzisha viwanda vidogo vidogo vingi ambavyo vitazalisha samani mbalimbali. Aidha, wasomi wetu wenye elimu ya ufundi wanaweza kuunda viwanda vikubwa ambavyo vitasaidia katika kuleta mapinduzi ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali kwa Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi 2016/2017, je, Serikali imejipangaje kwa mwaka 2016/2017 kutatua changamoto za upungufu wa madawati, upungufu wa nyumba za Walimu na madai ya Walimu ambayo ni muhimu hasa katika kuimarisha sekta ya elimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kifanyike kwa mwaka 2016/2017, katika Wizara hii, baada ya Serikali ya Awamu ya Mheshimiwa John Pombe Magufuli imeanza kutoa elimu bure na hivyo watoto wengi wamejitokeza shuleni na hivyo kusababisha shule kufurika watoto wengi. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili, Wizara ya Elimu na wadau mbalimbali wa maendeleo waweke mpango mkakati wa kutatua changamoto hizi kama vile kushawishi wananchi, taasisi binafsi na Serikali katika kuchangia ununuzi wa madawati na ujenzi wa vyumba vya madarasa ili kuwezesha watoto wengi kupata elimu.

Aidha, kwa mwaka 2016/2017, Serikali iendelee kuboresha mazingira ya kazi na makazi ya Walimu hasa wale walioko vijijini. Walimu wapandishwe madaraja na kulipwa stahili zao bila kucheleweshewa, pia kwa mwaka 2016/2017, Serikali ianze kuwapa motisha ili kuwapa moyo na kuwahamasisha wengine kufanya kazi kwa bidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za kuunga mkono makadirio ya mapato na matumizi Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi 2016/2017 yapitishwe, katika bajeti ya mwaka 2016/2017, Wizara imeomba kupitishiwa jumla ya shilingi trilioni 1.396 huku matumizi ya kawaida yakiwa ni shilingi bilioni 499 sawa na 35.7% ya bajeti yote huku miradi ya maendeleo ikitengewa shilingi bilioni 897 sawa na 69.1%. Ili kuunga mkono jitihada za kuinua kiwango cha elimu kwa mwaka 2016/2017, Serikali imedhamiria kuinua kiwango cha elimu kwani kati ya shilingi bilioni 897, Serikali imetoa shilingi bilioni 620 sawa na 69.1%, ni fedha za ndani huku 30.9% ikiwa ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2016/2017, Serikali ihakikishe kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Elimu zinapelekwa kwa wakati ili kuimarisha kiwango cha elimu nchini. Mfano wa mwaka 2015/2016 hadi tarehe 30 Aprili, 2016 Serikali ilipeleka shilingi bilioni 789 sawa na 72.12% ya bajeti yote. Kwa sababu Serikali ya Awamu ya Tano imejiimarisha katika ukusanyaji wa mapato yanayotokana na kodi ni vizuri kwa mwaka 2016/2017 Serikali ipeleke fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuinua kiwango cha elimu, Serikali imeongeza kiwango cha bajeti kutoka shilingi trilioni 1.094 hadi shilingi trilioni 1.396 sawa na ongezeko la 21.6% kutoka mwaka 2015/2016 hadi 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni ufunguo wa maisha, pia elimu ni bahari na haina mwisho. Hivyo elimu ni muhimu sana katika maisha yote na ya kila mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la elimu kuna changamoto zake zikiwemo za taaluma yenyewe na wanaotoa taaluma hiyo. Nazo ni kama ifuatavyo:-

(1) Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa vitabu vya kufundishia. Hili ni tatizo mojawapo katika sekta hii na suala ambalo linakatisha tamaa kuwa tunataka wanafunzi wafaulu lakini hatuna vifaa vya kuwawezesha kufaulu.

(2) Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa maabara. Hili nalo ni tatizo kubwa katika Sekta ya Elimu. Hii inasababisha hata kutokuwa na Walimu wa sayansi, kwani mambo mengi tunasoma kwa *theory* kuliko *practical,* kwa mfano skuli au vyuo havina maabara z kutosha.

(3) Mheshimiwa Mwenyekiti, mitaala mibovu. Pia hili linachangia elimu kuzorota na hatutafika tunakotaka kufika katika elimu na hata katika Tanzania ya viwanda.

(4) Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya mfumo wetu wa elimu ni mbovu. Wenzetu wamefanikiwa katika nchi zao kwa kuipa kipaumbele elimu, hali hiyo inatokana na kuijengea mfumo mzuri kwa kuwafundisha wanafunzi wao fani maalum wakiwa wadogo na wakubwa yaani *primary* hadi vyuo vikuu. Mfano, wanafunzi "x" wanasomea fani ya ufundi kulingana na kipawa chao na "y" wanasomea fani ya unesi kuanzia mwanzo wa masomo yake hadi mwisho. Leo hii katika Taifa letu tumeifanya elimu kama mzigo wa masomo mengi na kupelekea wengi kukatisha njiani au kusoma kwa kukariri zaidi ile nyanja kuliko kufahamu ili aweze kupata kufaulu tu. Hivyo, huwa tunapata wanafunzi ambao si wafanisi bali ni waigizaji tu, hivyo Serikali izingatie ushauri wetu kwa uzalendo wa Taifa letu.

(5) Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu hawana makazi bora; hivyo Serikali iwajengee Walimu makazi kama inavyofanya kwenye sekta nyingine, mfano, Sekta ya Ulinzi, Sekta ya Jeshi la Taifa na sekta nyingine.

(6) Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wapewe posho za kuwakidhi mahitaji yao kama usafiri na uhamisho kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna changamoto katika Sekta ya Elimu katika Taasisi ya Mikopo kama ifuatavyo:-

(1) Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwafikii walengwa, kama tunavyoelewa kanuni ya mikopo iliwekwa kwa wale wasiojiweza kupata elimu hususan maskini, lakini la kushangaza wanaofaidika zaidi ni watoto wa vigogo kama vile Mawaziri, Wabunge, Maafisa na wengine na kupewa mikopo kwa asilimia 100, lakini wale walengwa hupewa wachache tena kwa asilimia chache kwa mfano asilimia 40, 30, 20 na hata asilimia 10 na wengine kukosa na kushindwa kuendeleza masomo yao.

(2) Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mikopo haifiki kwa wakati na badala yake wanafunzi wanadhalilika kwa kujiuza, kuwa ombaomba kwani huwa wako mbali na familia na hata familia zao zinashindwa kuwasaidia kutokana na hali zao za ugumu wa maisha.

(3) Mheshimiwa Mwenyekiti, kutorejeshwa kwa mikopo hii; Serikali na Wizara ya Elimu hawajajipanga wala hakuna kanuni inayosimamia haya. Kwa mfano, wanafunzi wengi wanaona ni takrima ama hisani imepewa tu jina la mkopo na ndiyo maana toka waajiriwe hawajakatwa hata siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la elimu kwa upande wa Zanzibar, ni mgagaisho mtupu; hatutofautishi elimu ya juu ni ipi na elimu ya sekondari kwani wanafunzi wa *O Level* na *A Level* wanafanya mitihani kutoka Tanzania Bara wakati suala hili ni la Zanzibar. Je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano inapora madaraka ya Serikali ya Zanzibar? Naomba majibu kwenye hili; kama ni suala la Muungano mbona haiwaajiri Walimu hawa kwa Jamhuri ya Muungano na wanaajiriwa na Serikali ya Zanzibar na hawalipwi sawa na Jamhuri ya Muungano wakati wanafanya kazi za Jamhuri ya Muungano isipokuwa kusimamia mitihani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja na Wizara ipokee kwa makini sana mchango wangu ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Nkasi Kusini lina matatizo ya kijiografia linalosababisha wakati wa kufanya mitihani ya darasa la saba watoto hulazimika kuhamia shule nyingine, karibuni shule zaidi ya kumi huathirika na suala hili. Kwa nini Wizara isisimamie kukomeshwa kwa adha hii au basi vyombo vya usafiri majini vinunuliwe ili vitumike kuwasafirisha wasimamizi ambao

wanaogopa kutumia usafiri wa *boat* zinazotumiwa na wakazi wa eneo la Mwambao wa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa Walimu Wilayani Nkasi, hasa eneo la Mwambao wa Ziwa Tanganyika. Jimbo la Nkasi Kusini lina uhaba mkubwa sana wa Walimu wa shule ya msingi na sekondari na hasa eneo la Mwambao wa Ziwa Tanganyika ambako Walimu ni wachache kwa kila shule. Walimu hawa pia hawana nyumba za kuishi pamoja na ukosefu mkubwa wa madarasa katika shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu maalum. Wapo watoto *albino* na walemavu wengine, mashuleni kwetu sekondari na hata shule za msingi pia. Naomba kuwapa msaada wa visaidizi ili waweze kumudu masomo, nina maana wakisajiliwa katika shule ifanyike *assessment* kujua mahitaji yao na shule zielekezwe kuwatimizia mahitaji hayo kutoka kwenye ruzuku hiyo hiyo inayotolewa mashuleni kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za walemavu zitunzwe na tuhimize shule na vyuo walikosoma kufuatilia maendeleo yao ili hatimaye waje wapate ajira. Mtiririko huu uzingatiwe pia mara zinapotoka ajira mbalimbali ili kupunguza utegemezi wa walemavu walioendelezwa na kuwa na sifa za kuajirika, watengewe nafasi kabisa na ziwekwe wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *albino* walindwe, wapewe mafuta ya kuwasaidia na wajulikane walipo na Kamati za Ulinzi na Usalama. Wao au familia zao wapewe simu na Kamati za Usalama za maeneo yao ngazi ya wilaya kwa ajili ya mambo ya dharura kiusalama. Nao hawa wajulikane wanaoendelezwa ili kuwekwa kwenye akiba ili zitokeapo nafasi za ajira wajulikane kwa nafasi walizotengewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wanafunzi waliositishwa masomo kwa makosa yaliyofanywa na *Board,* haikubaliki na lazima Wizara itafute ufumbuzi mwingine na siyo hatua yake ya kuwafukuza vijana vyuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya madawati katika shule za msingi ni kubwa na kuacha halmashauri au wilaya kutafuta wenyewe namna ya kumaliza upungufu kutaathiri miradi mingine mawilayani kama ilivyokuwa kwenye mpango wa ujenzi wa maabara. Ushauri; lazima Serikali itenge fedha kushughulikia tatizo hilo na siyo maagizo ya kutia hofu na kuwafanya Wakurugenzi na ma-*DC* kutafuta mbinu mbadala, hivyo fedha itafutwe Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Maendeleo Chala, Wilayani Nkasi. Chuo hiki tangu miaka miwili iliyopita kilianza kutoa mafunzo ya *VETA;* naomba kiwe miongoni mwa chuo cha kutoa mafunzo hayo rasmi na kiendelezwe katika

miundombinu yake na hasa ukizingatia Mkoa wa Rukwa hauna chuo chochote cha ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya watoto wa kike shuleni. Nashauri, pamoja na changamoto zilizopo mtoto wa kike asinyimwe fursa ya kusoma kwa njia au mfumo rasmi pale anapopata mimba ili atimize malengo yake na pale inapotokea adhabu ya upande wa mwanaume anayesababisha mimba apewe adhabu ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za msingi ziendelezwe au kila kijiji kianzishe shule ya sekondari kwa sababu elimu ya sekondari itakuwa elimu ya lazima kufikiwa kumbe tujiandae mapema kuandaa majengo, uamuzi huu wa Serikali kuwa kila mtoto afikie *form IV* bila malipo utakuwa na matokeo ya kukosa vyumba vya madarasa na miundombinu ya kiwango cha sekondari. Nawasilisha.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kuchangia hotuba hii kwa kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuwa miongoni mwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pili, napenda kuwashukuru wapigakura wangu kwa kuniamini na kunichagua kwa kura nyingi. Natambua imani yao kwangu na nawaahidi kuwatumikia kwa nguvu zangu zote. Tatu, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Magufuli kwa kuonesha imani na uwezo mkubwa wa kuendesha nchi.

Nne, napenda kumpongeza Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa pamoja na Baraza lote la Mawaziri kwa kuonesha uwezo mkubwa wa kuongoza Wizara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii ya Elimu, napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ada za vyuo binafsi nchini. Serikali imekuwa na nia nzuri ya kuruhusu vyuo binafsi nchini, hili ni jambo zuri na la maana; masikitiko yangu katika hili ni pale inapoonekana baadhi ya vyuo kutoza ada kwa kulipa fedha za kigeni badala ya fedha ya Tanzania. Miongoni mwa vyuo hivyo ni Chuo cha Kampala *(Kampala International University)* kilichopo Gongo la Mboto Dar es Salaam. Namwomba Mheshimiwa Waziri kuliangalia suala hili na kuweka utaratibu maalum na kuwalazimisha walipishe wanafunzi kwa pesa za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa utekelezaji wa programu na miradi. Katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 67, 109

imeeleza namna inavyoendeleza kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES II). Huu ni mpango mzuri na napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa jambo hili. Napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri, katika kutekeleza ujenzi wa majengo haya ya sekondari na hata yale ya *primary* ni vyema ikazingatia kujenga majengo hayo kwa kuzingatia kuwepo kwa wanafunzi wenye uhitaji maalum ili na wao waweze kutumia majengo hayo bila ya usumbufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. RISALA S. KABONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na shule za ufundi katika mikoa mbalimbali ikiwemo Shule ya Ufundi Moshi *(Moshi Technical School),* shule hii ya ufundi ilikuwa ikitoa elimu ya ufundi kwa wanafunzi kutoka mikoa mingi Tanzania na baada ya masomo ya elimu ya sekondari wanafunzi hawa walijiunga na Vyuo vya *Arusha Technical* na *Dar Technical* pamoja na *Ifunda Tech.* Kwa sasa shule hizi za ufundi zina hali mbaya sana hasa Shule ya Ufundi Moshi; majengo yamechakaa sana vifaa vya ufundi vingi vimekufa na hivyo umuhimu wa shule hii kama ya ufundi, inaendelea kushusha taaluma za ufundi katika nchi yetu na hasa kipindi hiki ambacho tunakwenda kwenye uchumi wa kati na uchumi wa viwanda ambao unategemea nguvukazi kubwa ya vijana waliopitia taaluma ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri anapohitimisha aniambie ametenga bajeti kiasi gani kwa ajili ya kuimarisha shule za ufundi Tanzania. Hii itasaidia sana vijana wetu ambao wamekuwa wakikosa ajira baada ya kumaliza shule na kujiunga kwenye vitendo visivyo na tija kwa Taifa ambapo wangekuwa na utaalam wa ufundi mbalimbali wangeweza kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakaguzi wa shule. Kumekuwa na changamoto kubwa kwa wakaguzi wa shule ambao wengine wamepewa magari ya kuzungukia na kukagua shule, lakini tatizo la magari hayo wakati mwingine yanakosa bajeti za mafuta ya kuwawezesha wakaguzi kufanya kazi zao kwa ufanisi. Naomba kujua kuwa Waziri amejipanga vipi kuhusiana na changamoto hii na atalitatuaje kupitia bajeti yake ya 2016/2017 ili kuhakikisha wakaguzi wanapata fursa ya kufikia kwenye shule zote nchini na kufanya ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa shule. Uboreshaji wa shule za msingi na sekondari uangaliwe kwa karibu ili kuongeza tija, shule zetu ni chakavu sana, huduma za madarasa, vyoo havifai kwenye shule zetu, hakuna viwanja vya michezo, madawati, nyumba za Walimu. Pamoja na changamoto zote hizo, tatizo la vitabu ni kubwa sana, naomba Waziri anapohitimisha

atuambie amejipangaje kwa bajeti yake ili kuweka sera za kusaidia huduma shuleni kupunguza gharama kubwa kwa wazazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mishahara ya Walimu. Mishahara ya Walimu ni midogo sana ukilinganisha na kazi kubwa anayoifanya Mwalimu. Naomba Waziri aangalie ni namna gani anaweza kuangalia upya suala la mishahara ili kuwapa motisha Walimu wetu. Hali ya maisha imepanda sana, hivyo kupelekea Walimu kushindwa kujikita katika ufundishaji na kujiingiza katika biashara ndogondogo baada ya vipindi vya darasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia suala la elimu kwa watumishi waliopo kazini. Kumekuwa na wafanyakazi ambao wamekuwa wakifanyia kazi idara mbalimbali kwa muda mrefu na baadaye kutaka kujiendeleza kutokana na uzoefu wao wa kazi wanazozifanya. Wanapotaka kujiendeleza wanaambiwa cheti cha *form four,* ambacho pengine wakati huo hakikuwa kizuri ila amekuwa mzoefu wa kazi hata kwa miaka zaidi ya 10. Naomba Waziri anapohitimisha atuambie ni namna gani anaweza kutengeneza mfumo wa elimu ya juu kwa watumishi wa umma wanaohitaji kujiendeleza.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kupata nafasi hii kuchangia angalau kwa maandishi. Nitoe pongezi kwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi.

Naomba kwanza kabisa kuchangia kuhusu umri wa Wahadhiri wa Vyuo Vikuu na hasa Maprofesa wanaofundisha masomo ya *science;* ni kweli namwomba Mheshimiwa Waziri, Serikali iongeze umri wa kustaafu kwa Wahadhiri wanaofundisha masomo au *course* za *science* mpaka miaka 70 au 75 badala ya miaka 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu ni tabu kuwapata Walimu hawa wa *science* katika vyuo vikuu vyetu. Pili, Walimu hawa wanapostaafu kwa mujibu wa Sheria wakiwa na miaka 60 wanakuwa bado wanazo nguvu na afya nzuri na bado wanahitajika katika idara na hata vyuoni mwao. Kiasi wengine wengi kupitia kwenye uhitaji, chuo kinalazimika Mwalimu aendelee kufundisha kwa mkataba wa miaka miwili miwili. Naomba Mheshimiwa Waziri alione hili la kuongeza umri wa kustaafu kutoka miaka 60 mpaka miaka 70, madarasa ya awali yaangaliwe na kusimamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa mwanafunzi kuendelea na kupata elimu nzuri ni darasa la awali, mishahara ya Walimu hawa wa madarasa au shule za awali iangaliwe, Walimu hawa wapate mishahara yao waliyopangiwa kufuatana na daraja lao la ualimu kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo ya wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu. Urudishaji wa hela zilizokopwa na wanafunzi zirudishwe kwa wakati na mara hapo mkopaji na mhitimu wa chuo anapopata kazi, kujiajiri au kuajiriwa kwa mkakati wa wazi na mzuri wa kurudisha hela hizi, kusudi wakopeshe wanafunzi wengine kwani wahitaji ni wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri somo la ujasiriamali litiliwe mkazo kuanzia secondari hadi vyuo vikuu ili vijana waweze kujiajiri kwenye fani mbalimbali bila matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. HALIMA A. BULEMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunajadili bajeti muhimu zaidi kuliko zote nchini. Tunajadili bajeti yenye kuhudumia watu wengi zaidi kuliko bajeti yoyote nchini; tunajadili bajeti ya Taifa la sasa na hasahasa Taifa la baadaye, nawaonesha takwimu kuthibitisha maelezo yangu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inakadiriwa kuwa na watu milioni 50 hivi sasa, asilimia 50% ya Watanzania hawa wapo chini ya miaka 17. Maana yake nusu ya Watanzania ni watoto, hii ni kwa mujibu wa takwimu ya Taifa. Katika watoto hawa takribani milioni 25, watoto milioni 12 wapo kwenye shule za awali, msingi na sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za awali. Utafiti wa hali ya uchumi wa Taifa mwaka 2014 inaonesha idadi ya wanafunzi katika elimu ya awali imeongezeka kwa 1.9% kutoka wanafunzi 1,026,466 mwaka 2013 hadi kufikia wanafunzi 1,046,369.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za msingi. Utafiti huo huo unaonesha 2014, idadi ya wanafunzi katika elimu ya msingi ilipungua wanafunzi 8,202,892 kutoka wanafunzi 8,231,913 sawa na upungufu wa 0.4%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za sekondari. Utafiti huo pia unaonesha mwaka 2014, idadi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita ilipungua hadi wanafunzi 1,704,130 kutoka wanafunzi 1,804,056 sawa na upungufu wa 5.5%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa *Basic Education Statistics (BEST)* watoto wa Kitanzania milioni nane wapo kwenye shule zetu za msingi, milioni nne wapo kwenye shule zetu za sekondari; kwa maana hiyo hapa tunazungumzia robo ya Watanzania wapo madarasani, mashuleni, wengine wamekaa chini kwa kukosa madawati, wengine matumbo hayana kitu kwa

kutoka familia fukara na shule hazina chakula na wengine wanagombania kitabu maana hakuna vitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri robo hii ya Watanzania inafundishwa na Walimu wasio na hamasa kutokana na mishahara midogo, kukosa makazi, kutopandishwa madaraja na hata wengine kuwa walevi wa kutupwa kutokana na *stress* za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia na mamilioni ya watoto wetu wanaweza kuwa wanafundishwa na Walimu walevi, nani atawawajibisha ilhali ukaguzi wa elimu hautiliwi maanani? Nani atathubutu kuwawajibisha ilhali hatuhangaiki kutatua kero zao? Naomba kuwaambia robo ya Taifa letu tumeliweka mashakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, robo ya wananchi wanapata bajeti robo, Wizara ya Elimu ina bajeti ya sh. trilioni 1.3 hivi; tunaambiwa nyingine ipo TAMISEMI, ni vema Serikali ikaweka bajeti nzima ya Wizara ya Elimu pamoja na wazi ili tuweze kujua kwa uhakika kama 25% ya wananchi wanapata 25% ya bajeti yetu ya Taifa, lakini hata tukiweka zilizokwenda TAMISEMI bado bajeti yetu ya elimu ni chini ya 10% ya bajeti nzima. Tunawanyima watoto wetu haki yao ya kupata elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka miwili ya chekechea na miaka mitatu ya shule ya msingi ni muhimu sana, lakini sisi sote tunajua hali ya watoto wa Kitanzania ni mbaya sana, hakuna msaada wowote wa Kiserikali, Kisera au Kisheria kuhusu siku za mwanzo za mtoto. Hali hii inabidi ibadilike kama tunataka kujenga Taifa lililoelimika kwa mujibu wa Dira ya Taifa 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya utafiti ya uwezo yanaonesha kuwa katika kila watoto 10 wa darasa la tatu ni watoto watatu tu wenye kuweza kusoma sentensi ya darasa la kwanza na kukokotoa hesabu za darasa la kwanza, hii inaonesha watoto wetu hawapati fursa ya kusoma vizuri katika miaka yao ya mwanzoni shuleni. Jamani tuwekeze kubadilisha hali hii na tukiweza kuwekeza tutapata kizazi cha watoto wenye uwezo mkubwa wa elimu wenye kupenda kusoma, wadadisi na wabunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 50% ya vijana wanaomaliza darasa la saba hawaendelei na elimu ya sekondari, pia 75% ya vijana wanaomaliza kidato cha nne hawaendi kidato cha sita. Hivi sasa Sera yetu ya Elimu inaunganisha elimu ya sasa ya msingi na elimu ya sasa ya sekondari na yote kwa pamoja kuwa elimu ya msingi kwa miaka 10, vijana hawa wanaomaliza hawaendelei, wanakwenda wapi? Rasilimali hii inapotelea wapi? Hapo ndipo tunapohitaji elimu ya ufundi stadi na ufundi mchundo.

Naipongeza Serikali kwa kuamua kuviunganisha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na *VETA*. Ilani ya uchaguzi ya chama chetu iliahidi kujenga *VETA* kila Halmashauri ya Wilaya toka mwaka 2005. Namwomba Mheshimiwa Waziri tutekeleze ahadi hii ili kuwapa stadi za maisha vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuamue kugeuza Jeshi la Kujenga Taifa kuwa *VETA*, kila Kambi ya Jeshi isajiliwe kuwa *VETA* ili wale wanaokwenda Jeshini kwa miaka miwili, mwaka mmoja uwe wa kupata *skills* maalum za maisha, apewe mkopo wa vifaa, tutoke kwenye maneno twende kwenye vitendo. Tutumie rasilimali za nchi kujenga vyuo, kufundisha Walimu wa vyuo hivi na kujenga Taifa la watu wanaofanya kazi ama kuajiriwa au kujiajiri, suala la *VETA* liwe ni mpango malum na utekelezwe na jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni kuhusu Walimu. Nashauri Kada Maalum ya Elimu ya Awali (Chekechea mpaka Darasa la Tatu) kada hii iwe na mafunzo maalum na motisha maalum, vyuo vikuu vitoe shahada maalum za kada hii na tuwe na mradi maalum wa utafiti wa namna watoto wanajifunza kutokana na kada hii na hawa wasiwe Walimu wa kawaida. Walimu wa watoto wetu wadogo wawe Walimu maalum na mishahara yao iwe malum.

Kama tunataka kujenga Taifa la watu wanaojifunza tuanze sasa kuwekeza kwa Walimu na watoto wetu katika hatua za mwanzo kabisa. Tubadilishe Tanzania ndani ya kizazi kimoja tu kwa kuwekeza kwa Walimu wa watoto wetu kuanzia ngazi za chini; *let us derisk the Nation, let us build the foundation, education at early age is the foundation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja ya Waziri wa Elimu.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha Hotuba yao ili tuweze kuijadili. Yapo mambo ambayo naomba kupata ufafanuzi na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maboresho ya maabara katika shule zetu. Katika Mkoa wetu wa Iringa kuna shule nyingi sana za sekondari bado maabara zake hazijaweza kuboreshwa vizuri ili kuweza kumsaidia mtoto anayesoma masomo ya sayansi. Pamoja na kutokamilika kwa majengo kwa baadhi ya shule, lakini hata vifaa vya kutumia katika maabara kwa baadhi ya shule bado havikidhi haja. Vile vile pamoja na Sera ya Serikali kupeleka umeme wa *REA* katika taasisi kama shule zetu za sekondari na vyuo, bado hakuna umeme. Sasa tunategemea hawa watoto wakifanya mtihani kweli watafaulu kwa mtindo huu, tutapata kweli wataalam wa sayansi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule kongwe na maboresho ya shule maalum. Katika Mkoa wetu wa Iringa tunazo zile shule kongwe za sekondari kama Shule ya Lugalo, Shule ya Tosamaganga, Shule ya Malangali, hizi shule zinahitaji ukarabati wa hali ya juu.

Ningeomba sasa Serikali itoe kipaumbele katika ukarabati wa majengo ya shule hizi tu. Shule ya Sekondari Lugalo sasa hivi ni shule maalum, inachukua watoto wanaofundishwa elimu maalum, kama watoto wenye ulemavu wa ngozi, watoto viziwi, watoto wasioona, lakini inasikitisha sana kuona shule hii hawa wenye elimu maalum hawana vifaa vya kujifunzia. Je, ni utaratibu gani unatumika ili hawa vijana waweze kupata vifaa vya Walimu wao kuwafundishia na vifaa vya kujifunzia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho ya mitaala kwa Walimu. Serikali imekuwa ikibadilisha mitaala lakini Walimu hawapati semina au elimu kwa ajili ya kuweza kuielewa hiyo mitaala ili waweze sasa kufundisha kwa watoto. Hivyo, Serikali kama inabadili mitaala iende sambamba na kuwafundisha Walimu hao hiyo mitaala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya wazabuni. Naomba Wizara ifanye utaratibu wa kulipa madeni yote ya wazabuni. Wazabuni wanapata shida kwa muda mrefu sasa. Ningeomba Waziri anapojibu atueleze mkakati wa Serikali wa kulipa madeni ya wazabuni, yamekuwa ni ya muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ASHA MSHIMBA JECHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Naipongeza Wizara hii kupitia Waziri, Naibu na Watendaji wote kwa kazi ngumu mnayokabiliana nayo katika Wizara hii, kwani kazi ya kusimamia na kuiendeleza taaluma kwa kiwango cha ubora ina changamoto nyingi, lakini penye nia pana njia, msivunjike moyo tuko pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimba kwa wanafunzi wa kike. Umefikia wakati sasa kwa wanafunzi wa kike wanaopata mimba baada ya kujifungua waruhusiwe kuendelea na masomo kama kuna Sheria kandamizi ziletwe Bungeni tuzibadilishe.

Bodi ya Mikopo. Pamoja na jitihada kubwa za Serikali kuwapatia mikopo baadhi ya wanafunzi wanaostahili, lakini kumekuwa na changamoto na kama Wizara/Bodi ya Mikopo haikuzifanyia uchunguzi maalum, basi ile dhana ya kuwapa mikopo wanaostahili haitafikiwa kwa usahihi na mikopo iliyoiva kushindwa kurejeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migomo na maandamano kwa wanafunzi/wanavyuo. Kero ya maandamano na migomo kwa wanafunzi inazorotesha elimu kwani huharibu mazingira na vifaa na wakati mwingine husababisha maafa na hasara kubwa na hata shule kufungwa na wanafunzi kukosa masomo na kurudi majumbani. Wizara ina mkakati gani wa kuzuia changamoto ya maandamano na migomo, hasa kwa yale ambayo yamo ndani ya uwezo wao kwani tumeshuhudia baadhi ya wakati mara tu wanapogoma au kuandamana, kile wanafunzi wanacholalamikia Wizara inawapatia haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dira na Dhima ya Wizara ni nzuri na kama tutaitafsiri kwa vitendo na kuwashirikisha wadau mbalimbali na kila mmoja wetu akitimiza wajibu wake hakuna lisilowezekana. Hivyo, tunaiomba Wizara iandae mipango mikakati ya muda wa kati na muda mrefu ili kubaini ushiriki mpana na wa wazi katika kufikia Dira ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Juu ni suala la Muungano, hivyo pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara kwa kushirikiana na upande wa Zanzibar (Wizara ya Elimu), ipo haja sasa kukaa pamoja wadau wa elimu wa pande hizi mbili za Muungano ili kubaini changamoto na kuzitafutia njia muafaka za utatuzi, hasa ukizingatia tumo katika mchakato wa ushirikiano wa Afrika Mashariki na nchi yetu pia, inakabiliwa na utandawazi. Ni muhimu tujiandae sasa, wakati hautusubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja hii.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipongeze hotuba nzuri ya Waziri wa Elimu. Kwa ufupi naomba nichangie yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uandaaji wa Walimu. Tunaomba Wizara isimamie vyuo vya Walimu kwa karibu kwani vyuo vingi ubora umepungua sana:-

(i) Maabara za sayansi hakuna katika baadhi ya vyuo, kufanya Walimu kukosa umahiri wa ufundishaji; na

(ii) Walimu wa Hesabu. Ubora wa Walimu wa hesabu umepungua na kufanya *output* kuwa hafifu. Nashauri programu maalum ya hamasa kwa Walimu wa hesabu Kitaifa na kutoa zawadi maalum kwa wakufunzi wa hesabu. Hesabu ni tatizo kubwa kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa *VETA*. Tunaomba kuleta maombi ya kujengewa Chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Buhigwe kwani ni Sera ya Wizara yako ya kujenga Chuo cha *VETA* kila Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Nyumba za Walimu/Madarasa. Kwa kuwa, bajeti ya Wizara ya Elimu na TAMISEMI ni ndogo, kwa nini Wizara ya Elimu isishirikiane na *Social Security Fund* (Mifuko) ili iwasaidie kujenga na Serikali kuwalipa *yearly?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TCU* na Bodi ya Mikopo. Nashauri Wizara isiishie tu kufukuza, naomba uchunguzi uende mbele zaidi kwani inaonekana rushwa ipo kubwa kwenye sekta hizi mbili; maamuzi ya kubadili *Secretaries* ni muhimu sana, nao wanaweza kuwa ni chanzo cha rushwa. Bodi ya Mikopo wapewe malengo makubwa ya kukusanya mapato kuliko kuachwa kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri zaidi:-

(1) Fanya ziara za kushtukiza katika taasisi zako.

(2) Komesha siasa mashuleni.

(3) Toa zawadi kwa vyuo bora kwa vigezo vya Wizara.

(4) Toa zawadi kwa wanaofaulu hesabu.

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu. Awali ya yote, nitamke rasmi kwamba naunga mkono hoja. Nina imani kubwa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu. Naomba Bunge lako Tukufu, Waheshimiwa Wabunge tumuunge mkono Mheshimiwa Waziri, kwa nia yake na kwa jitihada anazozifanya kuhakikisha kwamba anarekebisha Sekta hii ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania watakubaliana na mimi kwamba kama Taifa tuna safari ndefu kwenye Sekta hii ya Elimu.

Naweza kusema kwamba baada ya kuwa tulishapiga hatua kubwa, tulipofanya uamuzi wa kuwa na sekondari kila Kata, pamoja na kuwa na ongezeko kubwa katika Shule za Msingi, jambo hili la kuwa pia na vyuo vingi limepelekea nchi yetu kuwa katika hatua ya mpito kwenye elimu. Kwa hiyo, tutakuwa na mambo mengi ya kurekebisha mambo ambayo siyo ya siku moja, mwezi mmoja, wala miezi sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie tu, kwa kutambua hilo, ndiyo maana Mheshimiwa Rais, alitafuta mtu mahsusi, akamteua na kumleta katika sekta hii kwa kuzingatia weledi wake, na kwa kuzingatia uzoefu wake katika sekta hii. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tumpe muda Mheshimiwa Waziri, tumuunge mkono na Watanzania wote tumuunge mkono. Mimi naamini tunakokwenda ni

kuzuri na wote tutakuja kutambua kwamba kweli Mheshimiwa Rais, alifanya jambo jema kwa kutafuta mtu mahsusi katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukirejea kwenye historia, leo hii tunaongele kuhusu shule binafsi, shule za Serikali, ni dhahiri kwamba kinachotambulisha kwenye shule binafsi, ni dhamira ya mzazi. Kile kinachotambulisha kwenye shule ya Serikali, ni uwezo wa mwanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme wazi tu kwamba Ubunge wangu niliupata kuanzia nilipofaulu kwenda sekondari. Yaani kile kitendo cha kutangazwa kwamba nimefaulu na kwenda shule ya vipaji maalum ya Ilboru, Tarafa mbili tayari zilitambua kwamba huyu ni mtu wa tofauti na tangu namaliza walikuwa wanasema ukimaliza kusoma, chagua Ubunge. Kwa hiyo, kiwango na ubora wa shule una umuhimu mkubwa sana katika kutengeneza jamii yetu na mchango wao katika maisha ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, sisi kama Wabunge, ni vyema sana tukaunga mkono jitihada za Serikali; na kwakuwa ni mambo mengi ya kurekebisha, tukatoa fursa kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake, wayafanyie kazi moja baada ya lingine. Nia ya Serikali na nia ya Mheshimiwa Rais mara zote anaposimama na anapotuelekeza, imekuwa ya dhati ya kuhakikisha kwamba heshima ya elimu inarudi kwenye mstari wake kama ambavyo amekuwa akifanya katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge pamoja na Kamati na Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Kuna hoja ambayo ilitolewa kuhusu uchelewezwahji wa fedha za mikopo ya wanafunzi wa elimu wa juu, lakini taarifa zilizoko ambazo ni taarifa rasmi ni kutoka Wizara ya Fedha, zinasema, hadi Machi, 2016 kama ambavyo tunajua kwamba mikopo huwa inaenda kwa *quarter,* Serikali imetoa mikopo ya elimu ya juu yenye thamani ya shilingi bilioni 331.9 kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016, mikopo ya elimu ya juu Bodi ilitarajiwa kukusanya shilingi bilioni 34.7 na hadi kufikia Machi, Bodi ilikuwa imekusanya bilioni 22.9. Kwa hiyo, ukichukua na zile ambazo Serikali imetoa, utaona kwamba tayari shilingi bilioni 354 zilikuwa zimekwisha kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati hapa na pale kunatokea ucheleweshwaji ambao ni wa kiutendaji zaidi katika masuala ya mgawanyo wa fedha, hayo ni ya kiutendaji ambayo mara zote yamekuwa yakirekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge, hali ilivyokuwa siku za nyuma na sasa iko tofauti. Zamani ilikuwa kawaida; na ilikuwa

ni jambo la kawaida mpaka wanafunzi wagome ndiyo mikopo itoke, lakini mtakumbuka kwamba katika miaka ya hivi karibuni na siku za hivi karibuni, jambo hilo linaenda likirekebishwa, hasa hasa yamekuwa tu yakitokea yale ambayo ni ya kiutendaji ya ndani ya usambazaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo lilijitokeza lilikuwa ni fedha za mchango wa Serikali, Mradi wa Mlonganzila, ambao kwa bajeti ilikuwa inatarajiwa zitumike dola milioni 755. Tayari Serikali ilishachangia shilingi bilioni 18 na tayari zilishalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelisema, ni lile ambalo linahusu pendekezo la bajeti ya Wizara ya Elimu pamoja na TAMISEMI angalau kuongezeka kutoka asilimia 11 kwenda 15 hadi 20. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa hesabu zetu tulizozipiga; na hii ni taarifa rasmi kutoka Wizara ya Fedha, kwamba tayari tumeshavuka hiyo asilimia inayopendekezwa na Waheshimiwa Wabunge na sasa tuko asilimia 22 ambayo ni shilingi bilioni 4,777 za bajeti yote. Kwa hiyo, tayari Serikali imeshavuka lengo hilo ambalo Waheshimiwa Wabunge wanapendekeza la kufika asilimia 20, sasa tuko asilimia 22.1. *(Makofi)*

Jambo lingine ambalo liliongelewa ni kuhusu madai ya Walimu yasiyo ya mishahara. Serikali imechukua hatua, tayari imetenga fedha zaidi ya shilingi bilioni 626 kwa ajili ya kushughulikia madeni ambayo yamehakikiwa. Kingine kikubwa ambacho Serikali imefanya ni kuhangaika na mianya iliyokuwa inasababisha malimbikizo ya aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu uliopita, ilikuwa inatokea Waalimu wakitaka kufanyiwa *promotion*, kubandishwa madaraja, walikuwa wanaulizwa. Kwa hiyo, ilikuwa inatokea Mwalimu ambaye amesoma Chuo kimoja na mwenzake, wamepangiwa vituo kwa wakati mmoja; lakini ikitokea yeye akachelewa kupokea barua ambayo inaelezea kuhusu kupandishwa kwake, ilikuwa inatokea Waalimu waliosoma pamoja, wamepangiwa kazi pamoja, wanapandishwa madaraja tofauti kufuatana na kupokea taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali itaenda moja kwa moja kuwapandisha watu ambao wana sifa bila kuwauliza kwa sababu ni dhahiri kwamba hakuna mtu atakataa kupandishwa daraja kama amefuzu sifa zile ambazo zinatakiwa, atapandishwa. Hiyo itaondoa Walimu ambao wamemaliza pamoja na wamepangiwa pamoja kazini, wameanza kazi pamoja kuwa na madaraja tofauti kama walivyopandishwa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kairuki.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami napenda kuunga mkono hoja hii ya Wizara ya Elimu. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na Naibu Waziri wake, lakini vile vile na Uongozi mzima wa Wizara ya Elimu kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijibu hoja chache zinazohusiana na masuala ambayo yako chini ya Utumishi ili kuweza kutoa ufafanuzi kidogo. Hoja ya kwanza ambayo ni kuhusiana na madeni mbalimbali ya malimbikizo ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imekuwa ikiwalipa watumishi mbalimbali wakiwemo Walimu na Watumishi wengine ambao sio Walimu, madai yao mbalimbali ya malimbikizo ya mishahara. Kwa mwaka huu wa fedha kuanzia Julai, 2015 hadi 25 Mei, mwaka huu wa 2016, Serikali imeshalipa madai ya Watumishi 24,677 yenye thamani ya shilingi bilioni 22.9. Kati ya madai haya ya shilingi bilioni 22.9 Walimu 14,366 waliokuwa wakidai takribani shilingi bilioni 10.7, wameshalipwa madeni hayo ya malimbikizo ya mishahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tumeshapokea madai mbalimbali ambayo yalipokelewa *manually* na mengine ambayo yalikokotolewa kwa mfumo wa ni *automatic,* tunaendelea kuhakiki madeni yenye thamani ya shilingi bilioni 11.5 na yatakapothibitika kwamba kweli madai hayo ni halisi, basi yataweza kulipwa bila shaka yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile yapo madeni ya takriban shilingi bilioni 2.3 tayari yameshahakikiwa ya Walimu zaidi ya 1984 na wakati wowote yanasubiriwa kulipwa. Kwa hiyo, ni imani yangu yataweza kulipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze tu, kwamba tangu tuliposimika mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara au *Lawson* mwezi Mei mwaka 2012, tumekuwa tukitekeleza ulipaji wa madai mbalimbali. Changamoto kubwa ambayo tulikuwa tukiipata, kwanza ukiangalia katika mfumo ulikuwa unakokotoa madai haya *automatically,* yaani kupitia mfumo. Wakati huo huo watumishi mbalimbali wenye madai au Walimu wakiwemo, wengine walikuwa wakileta pia taarifa zao *manually* kwa madeni yale yale na mengine unakuta yalikuwa yanaenda tofauti na madeni ambayo yalikuwa ni *automatic arrears*.

Kwa hiyo, hii ilikuwa inatupa taabu, unajikuta umepokea deni huku na huku pia umepokea. Kwa hiyo, ilikuwa ni lazima tuendelee na uhakiki. Nawaomba tu Walimu na Watumishi wengine wawe na subira lakini wajitahidi kuhakikisha kwamba wana-*submit* madai ambayo ni ya kweli na halisi. Aidha,

nawaomba zaidi waajiri wazingatie hili kwa sababu hatuta- *entertain manual arrears,* tuna-*entertain* zaidi *automatic arrears claims* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ambayo imekuwa ikitupata kama Serikali na ambayo imekuwa ikisababisha madai haya ya malimbikizo ya mishahara, mfumo huu tulionao wa taarifa za malipo ya mishahara, hauwezi kukokotoa madai au malimbikizo ya mishahara ambayo yanawasilishwa, watu wanaingia kwenye *payroll* kuanzia tarehe 15. Bado ulikuwa haujajengewa uwezo wa kuweza kukokotoa madai ya siku kwa siku. Mtu anayeingizwa baada ya tarehe 15, labda amekaa siku 14 tu, lakini kwa sasa tunaendelea kulifanyia kazi na ni imani yangu ndani ya muda mfupi suala hili litaweza kuwa limekwisha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ilikuwepo hoja kwamba baadhi ya Walimu na watumishi wengine wamekuwa hawaingizwi katika orodha ya malipo ya mishahara kwa wakati. Kwa takwimu nilizonazo za mwaka 2014 na 2015, tulikuwa na ajira mpya 56,816 na kati ya hizo ajira 57,036 zilishaingizwa katika mfumo wa *human capital management information system* na kati ya ajira hizo, ni ajira mpya 2020 peke yake ndizo tuliwarudishia waajiri ili waweze kufanya marekebisho mbali mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda tu kusema kwamba tayari ajira zaidi ya 57,036 zimeingizwa katika mfumo. Vile vile, nitumie nafasi hii kuwakumbusha waajiri kuhakikishia wanawaingiza waajiriwa wapya mapema katika mfumo huu wa *payroll* pindi wanapokuwa wamepangiwa katika maeneo yao ya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo ilitolewa ni kuhusu kuweka posho ya kufundishia au kuirudisha pamoja na posho ya mazingira magumu. Serikali inatambua ugumu wa kazi ambao wanaipata Walimu, lakini vile vile inatambua umuhimu wa kada hii muhimu. Kwa kutambua hilo, tunayo nia ya kuboresha maslahi mbalimbali ya watumishi ikiwemo Walimu na kuhakikisha kwamba tunawapa mishahara ambayo kwa kweli itakuwa imeboreshwa. Lengo letu ni kwamba badala ya kulipa posho zaidi, tutahakikisha kwamba tunaboresha mishahara. Tumeshaanza zoezi la tathmini ya kazi pamoja na upangaji wa madaraja au *job evaluation* na kama ambavyo nilieleza katika bajeti yetu, zoezi hili litakamilika ifikapo mwezi Februari, mwaka kesho 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itakuwa siyo kwa ajili ya kada ya Walimu tu, bali Serikali nzima kwa ujumla wake kwenye watumishi wa Umma. Tutaoanisha na kuwiainisha mishahara pamoja na posho mbalimbali au marupurupu mbalimbali ambayo wanayapata. Tutaangalia pia aina ya kazi; kama ambavyo nilieleza, siyo kwa Walimu tu, tunatambua umuhimu lakini na

wenyewe pia wataangaliwa kuona namna gani wataboreshewa. Unakuta kuna Mtumishi X, mwenye sifa sawa, elimu sawa, uzoefu sawa kazini labda mmoja ni Mwanasheria *EWURA*, mwingine ni Mwanasheria kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali lakini unajikuta wanapishana mishahara wengine mara tano mpaka hata mara kumi. Tukasema hili haliwezekani. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge tuvute subira, eneo hili tunalipa kipaumbele kikubwa na Walimu tutawazingatia katika uboreshaji wa mishahara yao na maslahi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo limesemewa sana na Waheshimiwa Wabunge ni suala zima la upandishaji wa madaraja kwa Walimu. Serikali imeshawapandisha Walimu 85,533 madaraja yao katika mwaka huu tu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia idadi hii ni takriban asilimia 28.5 ya Walimu wote waliopo katika Utumishi wa Umma. Vile vile, tumekuwa tukiendelea kuboresha maslahi ya Walimu, lakini vile vile kwa kupitia Muundo wa Utumishi wa Walimu wa mwaka 2014 tuliweza kufungulia ukomo wa kupanda vyeo kwa Walimu na Halmashauri mbalimbali zimekuwa zikianza kuwapandisha madaraja waliofikia ukomo na wale ambao walikuwa hawajafikia ukomo. Natambua Halmashauri mbalimbali wanaendelea na vikao kuona ni kwa namna gani basi wanaweza kuhakikisha kwamba watumishi hawa wanaweza kupandishwa madaraja yao kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo imekuwa ikisumbua sana na ambayo inaendana na upandishwaji wa madaraja, unakuta watumishi wengine na Walimu wanapandishwa madaraja lakini mishahara yao wanakuwa hawajarekebishiwa kupata mishahara mipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha ambao tunaumalizia, tumeweza kurekebisha mishahara ya Walimu 57,898 ambao walipandishwa madaraja katika mwaka huu wa fedha. Aidha, katika idadi hiyo kama nilivyoeleza Walimu 4,927 tumekuwa tukihakiki taarifa zao na wakati wowote kuanzia sasa wataweza kurekebishiwa mishahara yao. Vile vile, kwa ambao walipandishwa madaraja, lakini vielelezo vyao vimekuwa havijitoshelezi ni Walimu 23,314.

Kwa hiyo, naomba waajiri mbalimbali waendelee kufuatilia kuhakikisha kwamba Walimu hawa wanaweza kurekebishiwa mishahara yao kwa wakati kwa sababu sisi kama Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, tulishakasimu mamlaka kule kule chini kwa waajiri kwa ajili ya kuboresha huduma na kuisogeza huduma karibu zaidi na watumishi hawa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Simbachawene.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza Waziri wa Elimu kwa kuwasilisha bajeti nzuri, lakini pia kwa kutekeleza majukumu yake vizuri pamoja na watendaji wote wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nachukua nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote wa pande zote mbili, kwa michango yao mizuri ambayo kwa hakika inalenga katika kusaidia Taifa hili kwenda vizuri katika suala zima la uhai wa Taifa kwa maana ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamesemwa mengi hapa na pengine niseme tu, yote haya sisi kama Wizara ya TAMISEMI ambao ndio wamiliki wa shule za Serikali, maana hapa kulikuwa kuna kuchanganya kidogo mambo na pengine nitumie nafasi hii kueleza kwa uwazi; kwa nini tuligatua shule zile za Serikali kutoka Wizara ya Elimu kuleta TAMISEMI? Msingi wake kwanza ni wa kikatiba, ugatuaji wa madaraka ni wa kikatiba. Ukisoma Ibara ya 145(1) na Ibara ya 146(2) zinaeleza juu ya uanzishwaji wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri lakini pia mamlaka hizo zinapewa majukumu ya huduma za jamii, afya, elimu barabara na mambo mengine yote yanayohusiana na jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kulikuwa kuna mjadala mkubwa na ninajua mjadala huu umekuwa ukiendelea hata kwenye ma-*corridor* ambapo kimsingi mjadala huu unataka kuturudisha tulikotoka; kwa maana ya kwamba Wizara ya Elimu isimamie shule zote, isimamie wanafunzi wote, itunge mitihani, itunge vitabu; yaani ishughulikie ithibati, imiliki shule za Serikali, iangalie shule za binafsi, iangalie vyuo, iangalie Vyuo Vikuu, vyote hivi vinarudisha Wizara ya Elimu. Tunarudi tulikotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema tukaangalia kama TAMISEMI imeshindwa, imeshindwa kwa sababu gani? Kwanza nieleze, mgawanyo wa haya majukumu ni upi? Baada ya mafanikio ya *MESS I* na *MESS II,* katika elimu ya sekondari mwaka 2008 Serikali ya Awamu ya Nne iliamua kugatua shule hizi kuzipeleka kwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa. Majukumu ya TAMISEMI ni yafuatayo katika elimu: kusimamia uendeshaji wa elimu msingi, yaani Elimu ya Awali, Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari, Elimu Maalum na Elimu ya Watu Wazima.

Pili, kuratibu upelekaji wa rasilimali fedha na ruzuku za uendeshaji kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, lakini tatu kusimamia matumizi ya fedha na ruzuku shuleni, lakini nne, kuimarisha rasilimali watu kwenye ngazi za shule, Halmashauri na Mikoa na tano kusimamia uwajibikaji wa watendaji wote na

viongozi wote wa elimu kwenye ngazi za shule na Halmashauri za Mikoa; sita, kusimamia uendeshaji wa michezo katika Shule za Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu haya ni majukumu ambayo yamekabidhiwa kwa TAMISEMI. Sasa TAMISEMI ni nani? Ni mamlaka za Mikoa, Wilaya na Halmashauri zetu kwamba leo hii Mkurugenzi yule ndio mwajiri wa Walimu wa Sekondari. Ni rahisi sana kwa mfano shule za kwenye Wilaya yako ya Kasulu kwa mfano kuhudumiwa na Mkurugenzi shughuli zao zote. *Issue* hapa: Je, Mkurugenzi anawahudumia? Kwanini hawahudumii? Ndiyo *issue* ya kujadili. Anashindwa nini? Hana nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kuhamisha! Mnakumbuka ilivyokuwa maandamano Wizara ya Elimu pale, palikuwa hakuna hata mahali pa kukanyaga, tulikuwa tume-*centralize*. Ukisoma hata *democratic development* za *aspects* mbalimbali za kimaendeleo ya kidunia *decentralization* ndiyo mfumo wa kidemokrasia. *If you centralize,* maana yake unataka mtu anayesoma shule ya Kasulu kule, yule Mwalimu Mkuu awe chini ya Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Dar es Salaam. Hizo *allowance* za kumlipa anaposafiri kwenda kucheki kule na kurudi, tutazitoa wapi? Tusirudi kule tulipotoka jamani, kama kuna makosa, tuyajadili hayo. Mimi sisemi kwa sababu nipo leo TAMISEMI, naweza nikatoka kesho, lakini tunataka kurudi kule kwa jazba. Wizara ya Elimu ina majukumu gani? Hebu tuyaangalie. *(Makofi)*

Kwanza huo udhibiti, hapa yanazungumzwa masuala ya vitabu; huo udhibiti tu peke yake, ni majukumu makubwa kweli kweli! Ithibati peke yake ni majukumu makubwa; Vyuo Vikuu peke yake ni majukumu makubwa; Vyuo vya Elimu hivi vya kati vya Diploma na *Certificate* ni majukumu makubwa; Vyuo vya *VETA* ni majukumu makubwa! Leo mnasema na shule turudishe kule. Tunataka kufanya kosa walilolifanya waliopita. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu wali-*centralize* na mambo haya yakashindikana na leo tumeongeza shule, tuna shule nyingi, tuna Walimu karibu laki mbili wa Shule za Msingi, tuna Walimu karibu laki moja wa Sekondari. Hawa wote tunataka waende Dar es Salaam. Tuna wanafunzi hawa; hivi inawezekanaje? Hebu tutafute jibu, kwaniini hatutoi huduma nzuri? Tatizo ni kwamba tuliokabidhiwa ambao ni sisi Wabunge, tupo kwenye Halmashauri, ndipo shule zilipo; tuna Wenyeviti wa Halmashauri, ndio wanaowa-*controll* kwa nidhamu na kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, wanasimamia, rasilimali, zinakwenda? Ndiyo maana Mheshimiwa Rais anasema kama kuna uozo, upo kwenye Halmashauri. Mimi sikatai, ni kweli. Hapa tusaidiane Waheshimiwa Wabunge, hili Taifa ni letu. Tunapofika hatua fulani, lazima tukubaliane wote; na ndio maana nataka nikubaliane na aliyesema hebu siku moja tufungiane kusiwe vyombo vya

habari. Nafikiri alisema Mheshimiwa Mbatia, akasema, hebu tuzungumze mambo ambayo tuna maslahi wote ambayo yanafanana. Tukiwa tunazungumza tuna-*criticize* tu hapa hatuwezi kupata majibu. Kwa mfano, unazungumzia waliosimamia mitihani mwaka 2014/2015 kwamba hawajalipwa baadhi ya fedha zao. Unajua kilichotokea? TAMISEMI wameomba *17.7 billion,* Wizara ya Fedha ikatoa *17.7 billion*. TAMISEMI wanakwenda kupeleka kwenye Halmashauri zile pesa, wanasema hazitoshi. Wanarudi wanaomba *6.8 billion* kwamba hizi hawa wamekosa. Unauliza *6.8, how?* Wanasema, kwa sababu hii na hii; hebu leteni mchanganuo. Mchanganuo unakuja, *1.04 billion*. Sasa hebu niambie, kwanini Waziri wa Fedha asikatae kutoa fedha, aseme ngoja kwanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nasema uozo upo kwenye Halmashauri zetu. Ni lazima wote tujikute tuna majukumu na sisi Waheshimiwa lazima tuhakikishe tunahudhuria vikao vya Halmashauri kwa sababu tumepewa majukumu makubwa. Halmashauri zimepewa majukumu makubwa na ndiyo maana tunawajibika katika hata huu upungufu kwa sababu maamuzi yote tumepewa sisi kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri!

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI: Nasoma mwenyewe!

MWENYEKITI: Unafanya mwenyewe? Si nimeona mtu anakusaidia hapo? Basi sawa, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge zilizotolewa wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2016/2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa *Eng*. Stella Manyanya ambaye kwa kweli tumekuwa tunafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na hata katika kuandaa hii hoja, tumekuwa naye bega kwa bega hadi tarehe 21 ambapo bahati mbaya alipata taarifa za msiba wa mama yake.

Kwa hiyo, nafahamu sasa hivi atakuwa na majonzi mara mbili; anasikitikia kuondokewa na mama yake, lakini anasikitika kwamba hajaweza kuwa pamoja

na mimi katika kuhitimisha hoja hii. Naendelea kumpa pole sana na ninamwombea Mwenyezi Mungu aendelee kumtia nguvu katika kipindi hiki kigumu alichonacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati kabisa Katibu Mkuu wa Wizara yangu, Bibi Maimuna Tarishi kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Kwa kweli ananipa ushirikiano mkubwa sana katika sekta hii ya elimu ambayo wote mnakubali kuna changamoto. Nawashukuru sana Manaibu Katibu Wakuu, Watendaji wa Taasisi, Wakuu wa Vyuo na Watendaji wote katika Wizara ya Elimu kwa ushirikiano wao mkubwa ambao umeniwezesha hata kusimama kuhitimisha hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Peter Serukamba pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuchambua kwa kina bajeti ya Wizara yangu. Kwa hakika niseme kutoka kwenye sakafu ya moyo wangu kwamba nimefarijika na nimefurahishwa sana na maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yao yanaonyesha jinsi gani Kamati yangu imejaa Wajumbe ambao wana weledi mkubwa katika sekta hii ya elimu na wana dhamira ya dhati kabisa ya kuona mabadiliko katika Sekta ya Elimu. Nawashukuru sana na niwaambie tu kwamba mambo yote mliyoyasema tutayazingitia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nichukue fursa hii kumshukuru kwa dhati kabisa *classmate* wangu Mheshimiwa Suzan Anselim Lyimo, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa kuwasilisha vyema maoni ya Kambi ya Upinzani, lakini vile vile kwa ushauri na mapendekezo yake ambayo kama nilivyosema, tunachoangalia ni kuwatumikia Watanzania na kujenga nchi yetu. Kwa hiyo, mapendekezo yote ambayo yana tija kwa Tanzania tutayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa nirudie tena kutoa shukrani za dhati kabisa kwa familia yangu, mume wangu amekuja kuniunga mkono; lakini pia nashukuru kwamba yupo pamoja na mwanangu, tangu jana wamekuwa na mimi hadi leo ninavyohitimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naishukuru familia yangu yote kwa ujumla, wamekuwa wakinivumlia na wananipa ushirikiano mkubwa. Haya majukumu huwezi kuyafanya vizuri bila ushirikiano wa familia. Naomba mwendelee kunivumilia, kazi iliyopo mbele yangu ni kubwa ili niweze kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa majadiliano ya hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge 16 walitoa hoja zao kuhusiana na Sekta ya Elimu. Aidha, baada ya kuwasilisha hotuba yangu Waheshimiwa Wabunge 60 wamechangia hoja kwa kuongea na Wabunge 61 wamechangia kwa maandishi, ninawashukuru sana Waheshimiwa wote ambao mmechangia katika hoja yangu ama kwa maandishi ama kwa kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwashukuru niwashukuru pia hata wale ambao hawakuweza kupata nafasi ya kuchangia nikiamini kwamba yale yaliyochangiwa na wengine yamewakilisha mawazo yao pia. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara yangu itazingatia ushauri uliotolea na Wabunge wote na itafanyia kazi pia mapendekezo yaliyotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikisikiliza kwa makini sana michango ambayo imekuwa ikitolewa, kuanzia kwenye Kamati yangu ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, upande wa Upinzani na kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamezungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kujali itikadi zetu, bila kujali upande gani tumekaa nadhani wote katika hoja yangu tumezungumza lugha moja, tumezungumza lugha moja kwamba, tunataka kuona elimu katika nchi hii inatoa wahitimu wenye ubora, tunataka kuona mazingira ya kujifunzia yako vizuri, tunataka kuona ukaguzi wa shule unafanyika vizuri ili kudhibiti ubora wa elimu.

Tunataka kuona maslahi ya Walimu na stahiki zao zinaboreshwa, tunataka mamlaka za udhibiti wa ubora hizi tunazozipigia kelele *TCU, NACTE* na ukaguzi zifanye kazi zao vizuri ndicho tunachokitaka, tunataka wanafunzi wenye uhitaji maalum wafanye kazi vizuri na mambo mengine ambayo ziwezi kuyaorodhesha lakini wote kwa kauli moja tumeonesha kwamba, haya ndiyo mambo ambayo Watanzania wanayataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kuwa Waheshimiwa Wabunge wamekuwa na mambo mengi mazuri ambayo wameyachangia, labda niseme tu pengine kuna sehemu nyingine tofauti tu ni ile aina ya uwasilishaji na lugha inayotumika lakini mimi kimsingi naangalia hoja ile ambayo inawasilishwa na kama nilivyosema yote yatazingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulialifu Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kwa dhati kabisa katika kuboresha na kuinua ubora wa elimu katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimenukuu katika kitabu changu cha bajeti, na hii haikuwa ni bahati mbaya. Nimemnukuu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania maneno yake ambayo aliyatoa katika Bunge hili siku ya tarehe 22 mwezi wa Novemba, wakati alipokuwa analizindua Bunge rasmi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alisema na ninaomba kunukuu "Serikali ya Awamu ya Tano itajielekeza katika kuongeza ubora wa elimu inayotolewa ikiwa ni pamoja na kuongeza mkazo kwenye masomo ya sayansi" mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wameongea kwa uchungu sana, tena sana wakielezea masikitiko yao makubwa kuhusiana na hali ya elimu ilivyo sasa hivi nchini kila mmoja wetu hapa anasikitika. Waheshimiwa Wabunge, wanaonekana kutoridhishwa kabisa na ubora wa elimu inayotolewa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie kwamba, sasa hilo ndilo jukumu ambalo Mheshimiwa Rais amenikabidhi na nina nia ya dhati, ninao uwezo wa kuweza kuhakikisha kwamba elimu yetu inakwenda vizuri. Kwa hiyo tu nianze kwa kusema kwamba, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge wote mniunge mkono katika bajeti yangu ili sasa nikaanze kufanya ile kazi ambayo wote mnahamu kuona ikiwa inafanyika katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekii, ninawahikishia tu kwamba tunayo dhamira ya dhati na nimefarijika kabisa na michango yenu ambayo inaendana na ile kipaumbele chetu ambacho maneno yake nimeyatoa, siyo kama ninasema tu kwa sababu mmechangia lakini hiyo ndiyo kauli na ahadi ya Mheshimiwa Rais. Ninachoweza kusema tu kumbe katika Sekta ya Elimu tulipoweka kipaumbele cha kuinua ubora wa elimu hakika tumelengesha kwa sababu ndipo Tanzania wanapopahitaji. Ningependa tu niseme kwamba, tunaposema kuboresha elimu maana hiyo ndiyo msingi ya hoja zote ilikuwa katika hali halisi ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaposema kuboresha elimu maana yake ni nini? Maana yake lazima tujitazame tulipo, tuangalie changamoto tulizonazo na mahali ambapo tunataka kuenda. Niwakumbushe tu maneno aliyekuwa anasema Mheshimiwa Rais wetu katika kampeni zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alikuwa anawaambia wananchi kwamba, akichaguliwa anakuja kuleta mabadiliko ya kweli katika nchi hii. Na mimi naomba Bunge lako Tukufu liniruhusu nifanye mabadiliko ya kweli katika Sekta ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana mturuhusu kufanya mabadiliko ya kweli, kwanini ninasema hivyo. Tumekuwa na utamaduni wa kuwa tunatoa mapendekezo na Serikali inakwenda kufanyiakazi mapendekezo lakini baada ya kufanyiakazi mapendekezo wakati mwingine inakuwa inaonekana kwamba, kunakuwa pengine na maoni tofauti.

Mabadiliko ya kweli yanahitaji mabadiliko ya mfumo, huwezi ukawa na mabadiliko ya kweli wakati mfumo ni uleule na hatuwezi kuwa tayari hapa tulipo kama kweli hatuna dhamira ya dhati ya kufanya mabadiliko katika mfumo wetu wa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango kumekuwa na hoja inayojitokeza kwamba kila Waziri anayekuja, anakuja na mitaala yake anakuja na mabadilikoyake. Kwa hiyo niseme tu kwamba, kama hayo ndiyo yatakuwa maoni kwamba, labda sasa katika sekta yetu ya elimu tubaki kama tulivyo inamaana tukubali kubaki na elimu ambayo wote tunailalamikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, pale inapohitajika mabadiliko tutayafanya lakini tutahakikisha kwamba, tunashirikisha wadau wote muhimu ili kufahamu misingi ya mabadiliko, nafikiri hilo ndilo jambo la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapofanya mabadiliko, mabadiliko hata wanataaluma kuna mtaaluma mmoja ambaye amekuwa anaandika sana mambo ya masuala ya mabadiliko, Profesa Fulani amekuwa anasema kwamba kunakuwa na uwoga wa mabadiliko hilo ni jambo la kawaida, mtu anapotaka kufanya mabadiliko kunakuwa na uwoga. Mabadiliko lazima yawaguse watu, mabadiliko lazima yaguse sehemu ambazo pengine niseme kwamba, zinaweza zikaleta maumivu labda kwa lugha ambayo ni nyepesi. Kwahiyo tukubali tunapokuwa tunayafanya hivyo kwa sababu haiwezekani tukatoka hapa tulipo kama tutabaki kama tulivyo.

Mhesimiwa Mwenyekiti, labda nikitolea tu mfano sasa labda kwanini nimeanza na utangulizi huu mrefu, nimeyasema haya yote kwa sababu ninatambua umuhimu wa kufanya mabadiliko katika sekta ya elimu na kwakweli ndiomana nasema nimefurahishwa sana na michango yote ya Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia katika Wizara hii, michango yote ni mizuri sana yenye afya na yenye tija katika sekta ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuwakumbusha tu kwamba, sasa tunaposema tunafanya mabadiliko tunakubali wote kwamba kuna changamoto, kama kuna changamoto lazima tuwe na mahali pa kuanzia na tunaposema mahali pa kuanzia kwa mfano, nikianza sasa kutoa mifano, tunaposema walimu wawe bora ni dhahiri kwamba, kuna baadhi ya Walimu

pengine inawawezekana wakawa wamepita wasiokuwa na sifa ambazo ni stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itakapokuwa inachukua hatua za kukagua na kuhakikisha kwamba walimu waliopo wanasifa mtuunge mkono maana kunakuwa na ile ku-*symphasize* kupita kiasi kwa hiyo mara nyingi tunaonea huruma watu badala ya kuionea huruma nchi na ndiyo matatizo yanakuwa yako mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la wanafunzi wa St. Joseph ambalo limejitokeza sana katika michango ya Waheshimiwa Wabunge wengi walipokuwa wanachangia hoja yangu. Hili suala nimeliongea kwa kirefu katika hotuba yangu na nirudie tu kusema kwa kifupi ni kwamba, hawa wanafunzi nimesikia michango mingine wanasema kwamba walikuwa wanasifa za wakati huo, mimi kwa kweli sijafahamu ni lini Serikali hii kulikuwa na sifa ya mwanafunzi kwenda kusoma digrii akiwa amemaliza kidato cha Nne akiwa na ufaulu wa D nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kuna wengine humu ndani wanafahamu kwa heshima kabisa ili tuweze kwenda vizuri, wanisaidie kwa sababu kuwa Waziri haina maana unafahamu kila kitu, sipuuzi kabisa naheshimu michango ya watu, lakini pengine tuwe tunasaidiana kwa kuonyeshana na lini Tanzania hii tulishawahi kuwa na sifa za mwanafunzi kujiunga na Chuo Kikuu akiwa na ufaulu wa Kidato cha Nne na 'D' mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo majibu niliyoyatoa na maelezo niliyoyatoa mbele ya Bunge lako yanazingatia hali halisi ya elimu na kumekuwa na kuchanganya kati ya sifa ya kujiunga na Chuo Kikuu na sifa ya kujiunga na Cheti cha Ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba, hata katika kujiunga na cheti cha uwalimu hawa wanafunzi walipokuwa wanadahiliwa mwaka 2013/2014 ilikuwa ni ufaulu wa *point* 27 ambazo ni sawa mtu awe na angalau D 6 na C moja ndiyo ilikuwa kiwango cha chini. Kwa hiyo, wale ambao walikuwa wanajua kwamba zilikuwepo sifa za namna hiyo, nikizipokea Wizara yangu itapitia kwa kuzingatia pia na hizo taarifa ambazo mpaka sasa hivi hazipo mezani kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa nataka kusema sasahii ndiyo mfano ambao tunakuwa tunasema tunataka mabadiliko lakini pale ambapo hatua mahsusi zinapochukuliwa za kuonesha kwamba, tunataka kuwa na elimu iliyo bora pia sasa tunakuwa tunapata pingamizi au tunakuwa tunapata

malalamiko. Ninawaomba sana Waheshimiwa mtuunge mkono katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni sawa na kiwanda bahati mbaya ndugu yangu Mheshimiwa Mwijage ana shughuli hayupo hapa maana kila siku ndiyo eneo lake kila akisimama anazungumzia masuala ya viwanda na ndugu yangu Mheshimiwa Mwigulu mambo ya kilimo. Nataka tu kusema kwamba, elimu ni sawa na kiwanda, haiwezekani kama wewe unataka kutengeneza nguo kiwandani ukaanza na pamba iliyo mbovu ukategemea utoe nguo iliyo bora, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kupata *products* nzuri kiwandani lazima na malighafi ziwe na ubora ulio mzuri. Kwa hiyo, hii inakwenda hivyo hivyo hata katika sekta ya elimu. Haiwezekani uwe na wahitimu wazuri wanaoweza kuchangia katika kuleta maendeleo katika nchi hii wakati unaowadahili wana viwango vya chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mwanafunzi amefeli katika somo, katika *level* ya Kidato cha Nne unampeleka akachukue digrii na kwa miongozo ya Wizara ya Elimu, mwanafunzi mwenye digrii ya uwalimu anatakiwa afundishe A-*Level*. Yeye mwenyewe hajafika, yeye mwenyewe hakufaulu halafu anatakiwa akafundisha A-*Level* hivi kweli itawezekana! *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba katika hili mtuunge mkono na kwamba, mturuhusu tuendelee kufanyakazi ambayo wote kwa siku mbili mmekuwa mkichangia kwamba mnataka kuona elimu hii inakwenda vizuri. mtuunge mkono kwamba, huo ni mwanzo tu tutaendelea kusafisha katika elimu, tutaendelea kusafisha katika vyuo vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama wapo ambao wamekwisha maliza wako katika soko la ajira tutafika hata huko. Tusipofanya hivyo tutakuwa tunayasema haya kila siku. Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba, hilo suala tutalifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni utofauti unapozungumzia mtumishi hewa sioni tofauti na mfanyakazi asiyekuwa na sifa akikaa mahali. Tofauti tu ni kwamba, mmoja, ni mtumishi hewa haonekani kabisa, lakini mwingine ni mtumishi hewa amekaa mahali ambapo hastahili na hawezi kuleta tija katika Taifa hili. Kwa hiyo, kwasababu mmekuwa mnachangia kwa siku mbili mfululizo ninaamini kwamba, michango yenu ilikuwa inatoka moyoni na mlikuwa mnachangia kwa dhati kabisa na ndiyo maana nimesema bila kujali mchango umetoka upande gani, kwa sababu haya ndiyo malengo ya Serikali ya Awamu Tano katika sekta ya elimu. Nashukuru kwamba, wote tuna-*share vision* moja na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tuliyoifanya St. Joseph haitaishia hapo, kazi ndiyo imeanza na kwa heshima tu labda ya wale ambao wako kwenye utumishi wanatumi vyeti feki, wanatumia *qualification* feki. Mimi niseme kwamba, mjitoe katika Utumishi wenu kwa heshima yenu, vinginevyo tutawafikia, wajitoe wenyewe, wajisafishe wenyewe kwa sababu tunaposema mnataka mabadiliko basi mkubali mabadiliko ya kweli ni mabadiliko ya kweli ni kuthubutu kuchukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nguvu na ujasiri wa kuthubutu tunao na hatua tutazichukua. Kwa hiyo, hili suala la St. Joseph ni mwanzo tutaendelea kama nilivyosema tutavikagua Vyuo kama vina watu ambao hawana sifa tutawaondoa. Pia kama mlivyoshauri na ninaungana na ninyi kabisa kwamba, tutaangalia na hatua za ziada za kuchukua kwa sababu haiwezekani kufanya utapeli, unawapotezea muda vijana kwa kitu ambacho unajua kabisa mwisho wa siku hawatafika popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kwa kweli ndugu yangu Mwanasheria Mkuu wa Serikali atanisaidia tuangalie hatua gani za ziada zitachukuliwa lakini suala la wale wanafunzi kurudi pale halipo, isipokuwa tutaangalia kuwashauri kulingana na sifa zao, kwa sababu kuna nafasi mbalimbali katika elimu basi wanaweza wakaenda katika nafasi nyingine ambazo zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata humu ndani kama kuna watu wembe ni huo huo. Ni lazima tukubali kwamba Kiongozi ni kuwa mfano, kwa sababu haiwezekani tu tuwe tunakemea. Haiwezekani sisi tuwe wa kwanza kupaza sauti halafu sisi wenyewe tunakuwa na matendo hayo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie eneo lingine ambalo limechangiwa kwa nguvu sana, suala la ada elekezi; Kwanza nimefurahi kuona kwamba humu ndani hata nikiamua kufanya kikao cha kutoa maelekezo kuhusu shule nitapata tu *column* ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa wengi ambao wamechangia wamekuwa wanasema ni wamiliki wa shule, wengi humu ndani wameonyesha ni wamiliki wa shule, ni jambo jema. Lakini tu niseme kwamba ni kwa nini Serikali ilianza huu mchakato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la ada elekezi lilianzia humu ndani ya Bunge lako Tukufu, ambapo Waheshimiwa Wabunge mmekuwa mkitumwa na Wawakilishi wenu muihoji Serikali kwamba, ni kwa nini Serikali inaziachia shule zipandishe ada kiholela? Huu ndiyo msingi na chimbuko la ada elekezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyokuwa nafuatilia mjadala kidogo nikawa nasema ndiyo hivyo, wanasema kila wakati kingereza *every day is a new*

beginning kwamba, kila siku inakuwa na mambo yake, sina maana kama napinga maoni yaliyotolewa lakini tu nilikuwa nataka tukumbuke historia ambapo tumetoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo katika hili suala la ada elekezi tumekuwa na hoja nyingi zimekuwa zinatolewa na wananchi mbalimbali wakilalamika kwamba, viwango vinapandishwa kiholela, humu ndani katika Bunge lako kukawa na ombi au maelekezo kwa Serikali kwamba ije na ada elekezi ili kutoruhusu shule kupandisha ada kiholela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii inaendelea kufanyika ambapo kulikuwa na mtaalam elekezi ambaye anatoka Chuo Kikuu Huria aliyekuwa amepewa kuifanya kazi hii. Hii kazi ilikuwa inafanyika kwa ushirikishwaji wa wamiliki wa shule binafsi na mpaka mwezi Februari kulikuwa tayari na majadiliano yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuifanya kazi hii ni kweli kumekuwa na changamoto hilo lazima nikiri, haikuwa rahisi sana kuweza kufikia viwango kutokana na kwamba shule ziko katika madaraja tofauti tofauti, kwa hiyo mwezi Februari tulikaa kikao cha pamoja na wamiliki wa shule binafsi kwa sababu wao ni wadau tulikuwa tunataka kitu cha ushirikishwaji ambacho tukikitoa wote tunakuwa tunaelewa kwamba misingi na sababu ya kufika tulipofika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kikao kile tulifikia hatua ya wote tulikubaliana hizi shule tulizozikagua viwango viko tofauti. Kwa hiyo, tukawa tumefikia hatua ya kwamba, tuweke madaraja lakini kabla hili zoezi halijakamilika wenzetu ambao tumekuwa tunafanya nao kazi upande wa pili, wamiliki wa shule binafsi wakawa wameona ni vema labda hili suala walifikishe huku. Kamati yangu ya Kudumu ya Huduma za Jamii tulifanya kikao cha pamoja kujadili suala la ada elekezi nafikiri ilikuwa tarehe 15 Aprili na katika kikao hicho hoja za pande zote zilizingatiwa na tukawa tumefikia muafaka kwamba, kwa sasa hivi hilo suala kwa sababu limechukua muda kulikamilisha na kumekuwa na changamoto, Kamati ikawa imetushauri kwamba kwa sasa Wizara tuna changamoto nyingi, hebu hilo tuendele kulitafakari na kuliangalia labda namna bora zaidi ya kuli-*approach* na Serikali ikawa imekubaliana na ushauri wa Kamati, tukawa tumesema kwamba kwa sasa hili suala la ada elekezi tutaendelea kulifanyia utafiti kwa kuzingatia changamoto ambazo zimejitokeza.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nasikiliza michango tu lakini kimsingi tulikuwa tunajadili suala ambalo ukurasa huo ulikuwa umeshafungwa tarahe 15 mwezi Aprili mbele ya Kamati. Ninashukuru hiyo michango mliyochangia tutaizingatia lakini hili suala lilikuwa limeshahitimishwa tarahe 15 mwezi Aprili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimalizie kwamba suala hili la ada elekezi limehitimishwa kivipi, maana hilo ndiyo jambo la msingi. Kwamba kumekuwa na malalamiko ya shule za binafsi kupandisha ada na pia kumekuwa na michango ya kiholela. Kwa sasa hivi tulipofika makubaliano tuliyofika tutatumia taratibu zetu na ukiangalia katika hata Sera ya Elimu kabla ya hii mpya ambayo ilikuwa 1995, imeonyesha kabisa kwamba, shule binafsi zitaweka ada kwa kupata kibali cha Kamishna wa Elimu, kwa sasa hivi ofisi ya Kamishna wa Elimu itaendelea pamoja na Wakaguzi wa Shule kuendelea kuangalia uhalali wa ada zinazotozwa katika utaratibu ambao umeainishwa katika Sera ya Elimu na taratibu za elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Serikali haiwezi ikajitoa kabisa katika hili jambo, kwa sababu humu ndani tunapozungumza tumegawanyika pande mbili. Wengine humu wanaochangia wanasema ni huduma wengine wanasema ni biashara, kwa hiyo tutakachokifanya hatuweki ada elekezi lakini ni ile tu kuangalia uhalali kwa sababu kuna shule nyingine Mwanafunzi anaambiwa kila mmoja mchango wa majengo sasa kama shule ilikuwa haina majengo ilisajiliwa vipi? Kuna michango mingine ambayo haina uhalali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kigezo kimojawapo ili uweze kupata usajili wa shule lazima uwe na majengo na je, unapowachangisha wazazi wachangie majengo yako ya shule na wao watakuwa wabia katika shule yako? Kwa sabaabu shule ni ya kwako mwenyewe. Kwa hiyo kuna mambo ambayo lazima kama Serikali tutayaangalia na kamwe hatuwezi kuyafumbia macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shule zingine zinamtoza kila Mwanafunzi shilingi 100,000 kwa ajili ya Ulinzi, hiyo shule ina Walinzi wangapi? Je, kila Mwanafunzi ana mlinzi wake? Kwa hiyo ninachotaka kusema kwamba, katika msafara wa kenge na mamba wanakuwemo! Kwa hiyo hata katika shule binafsi katika msafara wa kenge…..hivyo hivyo! *(Makofi na Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoendeleza maana ya ada elekezi haina maana Serikali itaacha tu mtu atumie kivuli cha shule, akilala, akiamka anawaambia wazazi kesho mje na kitu fulani. Tutaangalia, tutaenda katika utaratibu ambao tutakuwa tumekubaliana ambao utazingatia kanuni na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie kuhusiana na suala la *VETA* kwasababu hili suala limekuwa linajitokeza kwa wachangiaji wengi. Ni kweli kumekuwa na ahadi ya Ujenzi wa *VETA* ambao labda kasi yake haijaenda kwa kiwango ambacho Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla walikuwa wanatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika hati idhini ya Serikali ya Awamu ya Tano, Vyuo vyote vya Maendeleo ya Jamii vimewekwa chini ya Wizara yangu, kwa hiyo niwaombe kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wabunge mnipitishie bajeti yangu ili sasa niende nikaviangalie vile Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, mmekuwa mnaomba sana mpate VETA tutafanya ukaguzi tuangalie vina hali gani ili tuweze kuanza mara moja kuvitumia hivyo kwa sababu mtaji wa kuanzia utakuwa ni mdogo kuliko kuanza kujenga upya. Ninaamini kabisa hatua hiyo ya Serikali ya kuleta Vyuo vya Maendeleo katika Wizara ya Elimu itaweza kutatua kwa kasi kubwa suala hili la *VETA* ambalo kwa kweli ni muhimu sana.

Waheshimiwa Wabunge ningeomba tu niwasihi na kuwaomba sana, tunapozungumzia *VETA* tusizungumzie kwamba ni kwa sababu ya Watoto waliofeli, hapana! *VETA* ni kwa ajili ya kujenga uwezo, *VETA* ni kwa ajili ya kujenga ujuzi ili Watoto waweze kuleta tija, tusiichukulie kwamba ni chuo cha wale ambao wameshindwa kwa sababu inaweza ikatufanya tusipate watu ambao ni wazuri ambao wanaweza wakalisaidia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie ndugu yangu alikuwa anaulizia kuhusu suala la *VETA* ya Ludewa na akawa anasema kwamba atashika shilingi yangu. Mheshimiwa Mbunge wa Ludewa wala huna haja ya kushika shilingi yangu, mimi na Serikali ni waaminifu, Serikali haiwezi kusema uwongo, tuliahidi tutajenga *VETA* Ludewa tutaijenga na pengine huioni katika kitabu kwa sababu inasomeka kama Chuo cha VETA cha Mkoa wa Njombe. Hiki Chuo cha VETA Mkoa wa Njombe kitajengwa katika Kijiji cha Shaurimoyo ambayo iko Ludewa, kwa hiyo utakuwa na bahati kwamba ni Chuo cha Mkoa lakini kinajengwa sehemu ya Ludewa, inapatikana katika ukurasa wa 59 wa kitabu changu cha bajeti.

Hivyo, Waheshimiwa Wabunge wamechangia na nikubaliane na ninyi kwamba kasi ya ujenzi wa *VETA* haijaenda kwa namna ambavyo tulikuwa tunatarajia, lakini naomba tu kwamba sasa kwa kuwa tumepewa hivi Vyuo vya Maendeleo ya Jamii mniruhusu kwamba nikalifanyie kazi, nikaviangalie vile ambavyo vitakuwa vinaweza kutumika mara moja na mdogo wangu Mheshimiwa Esther Matiko asubuhi alichomekea wakati Mheshimiwa Grace anachangia, kwa hiyo vyuo vyote katika Nchi nzima tutavitazama ili viweze kutumika mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo limechangiwa ni suala la Bodi ya Mikopo, suala la urejeshwaji wa mikopo pamoja na ule uhalali wa Bodi ya Mikopo ku-*charge* zile tozo zinazotolewa kwa Wahitimu. Kwanza kabisa nishukuru kwa michango yenu kuhusiana na suala hili la Bodi ya Mikopo na vilevile Waheshimiwa Wabunge walisema kwamba wana mambo ya ziada ambayo wanaweza wakanipatia ili niweze kuyafanyia kazi. Naomba sana, niko

tayari kupokea michango hiyo na niwahakikishie kabisa nikiipata nitaifanyia kazi kwa sababu hizi fedha ni kwa ajili ya Watanzania na kwa ajili ya kuwakopesha watoto wa Kitanzania ambao hawana uwezo, kwa hiyo ni jukumu letu sote kusaidiana ili ziweze kurejeshwa kwa kasi inayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie tu kwamba ni kwanini kumekuwa na hii *retention fee* katika Bodi ya Mikopo. Suala la *retention fee* linawekwa ili ile thamani ya fedha iweze kubaki pale pale. Nitasema viwango. Inawezekana ikaonekana *60 percent* kwa sababu mtu amekaa nayo muda mrefu, kadri unavyochelewa kulipa ni wazi kwamba ile fedha itaongezeka, lakini kiwango ambacho kinatozwa cha *value retention fee* ni asilimia sita ya mkopo wa mwanafunzi lakini vilevile kunakuwa na *administration fee* ambayo inakuwa ni *one pecent* ya mkopo anaouchukua mwanafunzi. Hivyo, kadri mtu anavyochelewa *retention fee* inakuwa ni kubwa kwa sababu kuna wengine ambao walikopa tangu Bodi ya Mikopo inaanza lakini bado hawajarejesha mikopo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina nia ya kukusanya mapato ya ziada kwa watu, kinachotakiwa, madam watu wanafahamu kwamba kunakuwa na *retention fee,* basi turejeshe mapema ili tusichajiwe kwa sababu ni hiari ya mtu ukirejesha mapema hautachajiwa, lakini wale ambao watachelewa ili thamani ya shilingi yetu iweze kubaki pale pale, ni lazima tuchaji hiyo *retention fee*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la urejeshwaji mikopo, changamoto zake zimezungumzwa kwa kirefu na mimi nikiri kwamba kama nilivyokuwa nimekiri kwenye hotuba yangu natambua kwamba kuna changamoto lakini kuna hatua ambazo tayari tunazichukua na vilevile kuna changamoto pia za kisheria. Baadhi ya maeneo katika Sheria ya Bodi ya Mikopo itakuwa vema kama ikifanyiwa marekebisho ili kuweza kuongeza kasi ya urejeshwaji ili kuwawezesha Watanzania wengi zaidi kunufaika na mikopo inayotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine lililozungumziwa ni suala la utekelezaji wa sera, kwamba kumekuwa na maswali hii elimu ya lazima ya miaka kumi inaanza kutekelezwa lini na kadhalika. Niseme tu kwamba, ukisoma Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, imeainisha wazi kwamba ili utekelezaji wa sera hiyo uwe fanisi, kuna sheria ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho. Sasa hivi tuko katika hatua ya kupitia sheria mbalimbali, kwanza kuna Sheria ya Elimu sura ya 353, kuna Sheria ya Serikali za Mitaa sura ya 287 na sura ya 288 na sheria nyingine ambazo zitawezesha sasa hii Sera ya Elimu iweze kutekelezwa kwa ufanisi. Hivyo, tupo tunafanya kazi na nategemea katika Bunge lijalo, baadhi ya sheria tutazileta na natarajia pia hata katika Bunge hili, Sheria ya Marekebisho ya Bodi ya Mikopo nitaiwasilisha kwenu, kwa hiyo itakapokamilika na taratibu zake zikawa zimewekwa na mikakati ya kuangalia

madarasa na walimu, basi hiyo Elimu ya Msingi ya miaka 10 ndipo itakapoanza rasmi, sasa hivi bado tunaendelea na mikakati ya kuhakiksha kwamba tunakamilisha maandalizi ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo imezungumziwa ni kuhusiana na suala la kutokuwepo kwa mtaala wa elimu ya awali na kutokuwepo na walimu wa kutosha. Ningependa tu kusema kwamba, mtaala wa elimu ya awali unaounganishwa na muhtasari wake umeshaandaliwa. Nikiri tu kwamba mtaala ambao ulikuwa unatumika zamani sasa hivi umerekebishwa na wako katika hatua sasa ya kuandaa vitabu. Pia kuhusiana na idadi ya Walimu kuwa pungufu ni kwamba katika mwaka 2013/2014, Wizara yangu iliongeza idadi ya Vyuo vinavyotoa mafunzo kwa ajili ya walimu wa elimu ya awali kutoka vyuo tisa hadi vyuo 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi tuna wananfunzi 3,200 ambao wanasoma ili wawe walimu wa elimu ya awali, kwa hiyo ninaamini kabisa kwamba jambo hili ni changamoto ambayo tunaikabili lakini tayari kuna hatua ambazo zinachukuliwa na ninaamini kwamba hawa watakapomaliza mwakani hili suala litatatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika mafunzo ya walimu kunakuwa na somo la elimu ya awali ambalo ni somo la lazima kwa kila mwalimu na hivyo basi, pamoja na kwamba wale wanakuwa hawajabobea kwa maana ya *specialization* katika elimu ya awali lakini katika mafunzo yao ya Ualimu wamepata *course* ya elimu ya awali, kwa hiyo naamini kabisa kwa kutumia ujuzi huo wanakuwa wanaweza kuwafundisha vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango mwingine ambao umechangiwa kwa wingi sana na Waheshimiwa Wabunge ni kuhusiana na suala la ununuzi wa vifaa vya maabara. Ni kweli juhudi kubwa sana ilifanyika ya ujenzi wa maabara, na nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wote, Halmashauri zote na watu wote walioshiriki katika ujenzi wa maabara hizi ambazo kwa sasa zimekamilika. Tunatambua kwamba maabara zilijengwa ili zitumike na ninaomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara yangu inafanyia kazi suala hilo kupitia mpango wa *program* yetu ya lipa kulingana na matokeo ambayo hii ni sehemu ya *BRN*.

Katika *BRN* kulikuwa na makubaliano na washirika wetu wa maendeleo kwamba, Wizara tunapokuwa tunatekeleza vigezo ambavyo tumekuwa tumewekewa, tunakuwa tunapata fedha ambazo kwa kweli zinakuwa na msaada mkubwa sana na hizo fedha tunazozipata katika Wizara yangu tunakuwa tunaachiwa uhuru tofauti na fedha nyingine za wafadhili ambazo wanakuwa wamekupangia, hizo ndiyo fedha pekee ambazo wanakupa halafu wanasema panga unavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo pamoja na kwamba jukumu la kununua vifaa vya maabara liko katika ofisi ya Rais - TAMISEMI lakini niseme tu kwamba Wizara yangu imetenga kiasi cha shilingi bilioni 12 kwa ajili ya kununua vifaa vya maabara na tayari hizi ni katika fedha za mwaka unaokwisha, sasa tunavyoongea ni kwamba tumeelezea hata katika kitabu chetu iko katika ukurasa wa 75, kwa hiyo niwahakikishie kabisa kwamba hilo suala tunalitambua, tunataka wanafunzi wajifunze Sayansi kwa vitendo na siyo kwa nadharia kwahiyo shule zote ambazo zimejenga maabara na imekamilika kabisa, naomba niseme vizuri, shule ambazo zimejenga maabara na zimekamilika kabisa mpaka mwezi Februari tulikuwa tumezitambua shule 1,536 hizi zote zitapata vifaa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nichukue fursa hii pia kuzihamasisha Halmashauri nyingine ambazo hazijakamilisha ujenzi wa maabara basi nazo zikamilishe na niseme tu kwamba kwasababu hii *program* ya *pay for results* bado inaendela na kwa kutambua kwamba kipaumbele chetu ni kuboresha elimu yetu inayotolewa, niwahakikishie tu kwamba hizi fedha kila tunapozipata tutakuwa tunazitumia katika kuboresha elimu na tunatambua kwamba hatuwezi kuwa na elimu bora kama hatuna vifaa vya kufundishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la elimu maalum. Limechangiwa vizuri na Dada yangu Mheshimiwa Dkt. Elly Macha amezungumzia suala la kiwanda cha kuchapa vitabu na ile lugha ya alama na kadhalika kuhusiana na elimu maalum.

Naomba tu niseme kwamba, kama ambavyo nilikuwa nimesema katika hotuba yangu, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, elimu maalum itakuwa ni kipaumbele. Tutahakikisha tunanunua vifaa, tayari kuna fedha ambazo tumezitenga kwa ajili ya elimu maalum na ni fedha nyingi takribani bilioni 5 siyo hela kidogo hizo, tunataka kuhakikisha zile kero za msingi katika hii elimu maalum tunaziondoa. Kwa hiyo nirudie kuwahakikishia kwamba umuhimu wa elimu maalum tunautambua na katika bajeti yetu tumezingatia. Tumeweka fedha za kutosha na tutaendelea kuimarisha kadri uwezo wa kifedha unavyojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Kiwanda cha kuchapa vitabu vya wasiiona pia nacho tutakifanyia maboresho na vilevile suala la lugha za alama nililipata nilivyoenda kutembelea Kilimanjaro, kuna changamoto kule kwamba kuna shule ya wanafunzi wanafundishwa lakini wanakuwa wengi wanashindwa kwenda sekondari kwa sababu hakuna wataalamu, tayari tumeshaanza kulifanyia kazi na tunashirikiana na kitengo cha elimu maalum katika Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Wameniandikia andiko la mapendekezo ya jinsi gani ambavyo tunaweza tukatatua hilo suala la lugha za alama ili kuwawezesha wanafunzi hao kuendelea na elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala ambalo limeongelewa kwa kirefu pia sana humu ndani, suala la watoto wa kike wanaopata mimba kuweza kurejea masomo yao. Hili suala la kuwarejesha wanafunzi ni suala ambalo najua limeanza muda mrefu kidogo na nakumbuka nilikuwa na Kamati, Mheshimiwa Zaynab Vullu nakumbuka alikuwa ni Mjumbe wa hiyo Kamati, tulishafanya hata na *presentation* muda, lakini na Mheshimiwa Suzan Lyimo na Margret Sitta wote walikuwa kwenye hiyo Kamati Maalum ilikuwa imeundwa ajili ya kuangalia ni kitu gani cha kufanya na pia walienda hata kutembela hata katika Nchi nyingine kuona, kimsingi pendekezo ambalo lilikuja ni kwamba, hawa wanafunzi wapewe nafasi ya kuweza kurudi shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Waziri mwenye dhamana ya elimu ambaye pia nina dhamana ya kuangalia elimu nje ya mfumo rasmi, elimu ndani ya mfumo rasmi sina pingamizi kabisa na hawa wanafunzi kurudi shuleni. Kitu ambacho tutafanya katika Wizara yangu ni kukaa na wadau ambao ni muhimu katika jambo hili hasa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto, ili tuhakikishe kwamba tunapomuangalia binti arudi shuleni, lakini pia tusimsahau mtoto wake, kwa sababu binti ana haki ya kupata elimu lakini na huyu mtoto ana haki ya kupata malezi. Kwa hiyo, hicho kikao cha kuangalia utaratibu gani utawekwa ili hizi pande zote mbili ziweze kunufaika bila ya kuwa na madhara, tukiweza kuwa na utaratibu mzuri sioni kama kuna tatizo lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema michango ni mingi na nimejitahidi kuongea mengi lakini naona kengele ya kwanza imeshagongwa, siwezi kuyamaliza yote lakini niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba hoja zenu zote tutazijibu na tayari tuna rasimu hii hapa – tumeshaanza kuzijibu, tutamalizia na tutawakabidhi. Kwa hiyo wale ambao pengine hoja zao sijazijibu naomba tu msione labda pengine siyo za muhimu ni kwa sababu ya muda, michango yote kama nilivyosema ni muhimu, michango yote ina tija na mtapata majibu kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa nigongewe kengele ya pili, nihitimishe hoja yangu kwa kukushukuru sana wewe Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kutuongozea majadiliano, nashukuru sana pia Naibu Spika ambaye tulianza naye jana na Wenyeviti wote ambao wameshiriki katika kuongoza majadiliano ya hoja hii. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu na sasa ninaomba sana kwa heshima kubwa mniunge mkono ili nikafanye kazi ambayo mnataka tuifanye. Naomba muunge mkono hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

MWENYEKITI: Ahsante, hoja imeungwa mkono. Katibu!

NDG. NENELWA WANKANGA – KATIBU MEZANI: Kamati ya Matumizi

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

NDG. NENELWA WANKANGA– KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na Kitabu namba mbili Matumizi ya Kawaida ukurasa wa 295, Fungu 46 Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi.

Kif. 1001 - Admn and HR Mgt ……...Sh. 5,491,039,752

MWENYEKITI: Ahsante! Waheshimiwa Wabunge, nimeshapata majina naanza na Mheshimiwa Ester Mmasi.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia wasilisho la bajeti ya Wizara ya Elimu, ni dhahiri kwamba wengi wa Wabunge wetu tuliokaa katika nyumba hii takatifu tumesikitishwa sana, tumeumia sana baada ya kuona pamoja na uwepo wa Taasisi hizi mbili, *NACTE* na *TCU* lakini suala zima la ubora wa elimu ya nchi ya Tanzania bado limekuwa likipuuzwa. Bado limekuwa siyo lenye tija. Tumeona changamoto nyingi sana katika upande huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona changamoto zinazotokana na udahili wa wanafunzi pamoja na mitaala isiyo na tija, lakini mwisho wake tunaona vyuo vingi vinaishia kupewa *clean certificate*. Mambo haya yamefanywa na *TCU* pamoja na *NACTE*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maabara, Wabunge wengi wameongea uhaba wa maabara, wameongea uhaba wa *library* lakini pia wameongelea uhaba wa mihadhara kufundishia wanafunzi wetu kule vyuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yameongelwa masuala ya mafunzo duni kwa wanafunzi wetu chini ya mwavuli wa *NACTE,* lakini pia limeongelewa suala la maslahi duni kwa Walimu wetu wa Vyuo Vikuu ambao walimu hawa leo hii wamegeuka kuwa *laptop Consultants* na hata wamewaacha wanafunzi wetu vyuoni wakifanya mitihani ya *multiple choices* kwa kiwango cha *degree* ya Uzamili na hata Uzamivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumeona pamoja na uwepo wa *TCU* na *NACTE,* lakini pesa imekuwa ikinunua *degree* ya Uzamili, pesa imekuwa ikinunua *degree* ya Uzamivu, hii ni aibu sana kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona pia wanafunzi wetu mashuleni leo wamekuwa wakifanya *assignment* kwa kutumia *Google search*. Mwalimu ana *mark just introduction na conclusion*. Elimu inapuuzwa katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi niliyesimama hapa, kimsingi ninamuomba sasa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana asimame na atueleze, Serikali ina msimamo gani juu ya uwepo wa *NACTE* na *TCU* ambayo kimsingi imeonesha kupoteza imani ya Watanzania tulio wengi, pia taasisi hizi mbili ni taasisi ambazo kimsingi zimekuwa zikifanya jukumu moja. Sasa tunaomba Mheshimiwa Waziri asimame na atueleze msimamo wa Serikali. Ni kwanini tuwe na taasisi hizi mbili ilhali elimu ya Mtanzania inaporomoka…

MWENYEKITI: Ahsante!

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa niseme ninakamata rasmi shilingi. Ninaomba majibu rasmi ya kujitosheleza kwa Mheshimiwa Waziri na tofauti na hapo nitakuwa wa kwanza kushika shilingi yake mpaka pale tutakapopata majibu yanayojitosheleza. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mmasi, unajua mumewe yuko juu kule, sasa hizi pesa mkianza kuzizuia zuia hizi! Mheshimiwa Waziri majibu! *(Kicheko)*

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza katika hotuba yangu na vilevile katika majumuisho kwamba Serikali ina dhamira ya dhati ya kusafisha taasisi hizi. Ni kweli kumekuwa na changamoto ambazo kwa masikitiko makubwa, hata na mimi nimesikitika sana kuona kwamba Serikali inafika mahali inalazimika kuwaondoa wanafunzi ambao tayari walikuwa wamekaa chuoni kwa muda kutokana na uzembe wa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zimechukuliwa na kama nilivyosema Kamati ya uchunguzi imeundwa ili kuweza kubaini chanzo cha tatizo hilo, kwa sababu tumeona tatizo lakini chanzo chake bado hatujakifahamu na tunaamini kupitia Kamati hiyo tukishafahamu chanzo hatua kali za kisheria na za kinidhamu zitachukuliwa. Kwa hiyo, niseme tu kwamba kama Serikali hatuungi mkono vitendo ambavyo vinafanywa, ambavyo vinakuwa vinarudisha nyuma maendeleo ya Sekta yetu ya Elimu na tutaendelea kuchukua hatua na hata kama itakuwa ni hatua kali sana za kuzivunja hizi taasisi na kuziunda upya, tuko tayari kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la hizi taasisi mbili uwepo wake, kimsingi ni kwamba ukiangalia sheria zilizoanzisha taasisi hizo zilikuwa na umuhimu wa kuwepo, tatizo limekuja kwa Watendaji. Umuhimu wa hizi taasisi kuwepo upo, na hivyo basi tutaendelea kuchukua hatua kwa watendaji ili yale majukumu ya msingi yaliyosababisha taasisi hizi kuanzishwa yaendelee kutekelezwa kwa ufanisi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mmasi!

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kusema kwamba msimamo wangu ni mmoja, kwenye hili sijaridhika kabisa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NACTE* inakuja hapa inaomba Fungu litengwe kwa ajili ya *NACTE,* lakini pia *TCU* inakuja hapa inaomba Fungu litengwe kwa ajili ya uboreshaji wa sekta nzima ya elimu, lakini kilio cha Wabunge wote humu ndani ni kuporomoka kwa ubora wa wa elimu nchini Tanzania. Leo Mheshimiwa Waziri ananiambia kwamba Serikali inajipanga. Mheshimiwa Waziri nikutake, nikuombe, tupe *commitment* ya Serikali, ni kwa nini tuwe na taasisi hizo zote mbili ambazo kimsingi Serikali inapoteza mabilioni ya shilingi katika kuhakikisha elimu ya Mtanzania leo inaboreshwa, lakini sasa tumeishia wote tuko gizani, wote tumeishia kwenye vitendawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri atupe *commitment* ya Serikali, ni kwa nini tuwe na taasisi zote hizi mbili wakati elimu ya Mtanzania inazidi kudidimia? Ninaomba nishikilie shilingi hii mpaka Mheshimiwa Waziri atakapotupa majibu ya kujitosheleza. Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mmasi, hivi Waziri akujibu kitu gani zaidi ya alichokwambia? Hata yeye limemgusa, tatizo liko kubwa na sasa hivi taasisi zote mbili hizo zinachunguzwa. *What else do you need her to tell you?*

Mheshimiwa Chumi, Mheshimiwa Dr. Kigwangalla, Mheshimiwa Susan, Mheshimiwa Zitto, kule mwisho kabisa Mheshimiwa Hasunga na Mheshimiwa Ridhiwani maana unaanza kulia sasa! *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Mheshimiwa Susan.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti ni wazi kwamba *TCU* na *NACTE* ni vyombo viwili katika Wizara ya Elimu ambavyo vina majukumu mawili tofauti kabisa. Wakati ambapo *TCU* inashughulika zaidi na Vyuo Vya Elimu ya Juu, *NACTE* inashughulika na vyuo vyuo Kati pamoja na uyuo vya ufundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani hapa ni kweli vimefanya makosa makubwa sana na kwa maana hiyo hatuwezi kuvifuta kwa sababu vina majukumu ya msingi. Nadhani cha msingi ni Serikali kuhakikisha kwamba inaboresha ili viweze kufanya kazi zake kama ambavyo sheria iliyoviunda inavyosema. *(Makofi)*

Kwa hiyo Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani mdogo wangu Ester anachotaka hapa siyo kuvifuta isipokuwa Serikali sasa ihakikishe kwamba vyombo hivi vinaboreshwa, Watendaji wawe na usimamizi mzuri, kwa sababu kwa kweli vijana wetu wamepoteza muda wao na jambo hili linanipa uchungu sana kwa sababu mwaka jana tulilizungumza, kwa maana hiyo *TCU* ilipaswa Wakurugenzi Watendaji wote wawe wamefukuzwa kazi toka mwaka jana au mwaka juzi haya tusingekuwa tunaongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo nadhani Serikali imenisikia na naomba sana *TCU* na *NACTE* vifanyiwe kazi. Tunatambua kwamba hata Mtendaji Mkuu wa *NACTE* alishaondoka kwa sababu naye alikuwa na cheti feki kama sikosei. Unapoona mambo kama haya ni wazi kuna matatizo kila mahali, kwa hiyo ushauri wangu ni huo.*(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimsihi Mheshimiwa Ester Mmasi asiondoe shilingi kwenye mshahara wa Waziri, ninamsihi afanye hivyo kwa sababu anafahamu wazi jitihada zinazofanywa na Serikali yetu kuboresha sekta ya elimu. Anafahamu wazi mabadiliko makubwa yaliyofanyika kwenye sekta hii, anafahamu wazi uwekezaji mkubwa uliofanywa kwenye sekta hii na leo hii tuna takriban vyuo 51 vikuu, tuna vyuo vya kati vingi, anafahamu wazi akiwa kama Mbunge anayewakilisha wasomi humu ndani kwamba majukumu ya *NACTE* na majukumu ya *TCU* ni tofauti kabisa, na kwamba *NACTE* inatoa ithibati kwenye

vyuo vinavyotoa elimu ya ufundi ama ufundi mchundo na mfumo wake ni tofauti, siyo mfumo wa *academic* kama mfumo wa *TCU*, anafahamu wazi akiwa kama Mbunge msomi. Kwa maana hiyo majukumu ya hizi taasisi mbili yana malengo mawili tofauti. Mfumo wa *NACTE* unaendana sana na falsafa ya Serikali ya Awamu ya Tano inayotupelekea kwenye Tanzania ya Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo namsihi asiondoe shilingi ya Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Ahsante! Mheshimiwa Chumi, jiandae Mheshimiwa Zitto

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ester na kwa masikitiko kabisa makubwa napenda kusema kwamba sasa hivi nina hakika hata wanafunzi walioko kwenye vyuo mbalimbali *majority* watakuwa hawajakaa kwa amani kutokana na haya ambayo yametokea St. Joseph.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nieleweke wazi hata mimi katika wasilisho langu lile nilisema ni muumini wa elimu bora na siyo bora elimu. Hii ni kama mtu unakuta mahali kuna sherehe na unaambiwa bwana wewe ingia hata kama hujavaa viatu na unakaguliwa na unaingia. Unaingia ndani, unaanza kushereheka, baada ya muda unaambiwa bwana wewe kuingia kwako ni kwa makosa na kwa hiyo unatakiwa ulipie gharama hizi ambazo mwanzoni uliambiwa kwamba unaingia mle bure na chombo halali. Kwa hiyo naungana na Mheshimiwa Ester.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Chumi, *you have made your point*! Mheshimiwa Zitto.

MHE. KABWE R. Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naungana mkono na maelezo ambayo Mheshimiwa Susan Lyimo ameyazungumza. Ni dhahiri kwamba tuna maeneo ambayo kuna matatizo makubwa katika mfumo wetu wa elimu. Elimu ya Ufundi ni moja ya maeneo ambayo tuna changamoto kubwa. Huwezi kuzitatua changamoto hizo kwa kufuta vyombo ambavyo vipo! Unafuta changamoto kwa kuviboresha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama jinsi ambavyo Waziri Kivuli alimesema kwamba *TCU* wana kazi yao na itakuwa kazi kubwa zaidi, kwa sababu kati ya sasa na 2025 nchi yetu inahitaji wasomi wenye ngazi za digrii, wasiopungua milioni 3. Ina maana tutajenga vyuo vikuu vingine vingi zaidi na umuhimu wa *TCU* utakuwa ni mkubwa zaidi. Kati ya sasa na 2025 tutahitaji mafundi mchundo kwa maana ya ngazi ya kati, milioni 7. Maana yake ni kwamba tutahitaji *NACTE* iwe na nguvu zaidi kuliko ambavyo iko sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nilikuwa nashauri Waheshimiwa Wabunge tuzikubali hizi changamoto ambazo zipo, tuangalie namna gani ambavyo tutakavyoweza kuboresha ili ubora wa elimu uweze kuimarika, badala ya kupendekeza kwamba vyombo hivi kwa sababu ubora ni mbovu haupo. Kama jambo ni hilo, Wizara ya Elimu nzima ifutwe.

MWENYEKITI: Ahsante! Mheshimiwa Hasunga, ajiandae Mheshimiwa Ridhiwani.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kabisa kwamba taasisi hizi mbili zinafanya kazi ambayo inafanana, hili nalisema kwa sababu *TCU* wanasimamia Vyuo Vikuu ambavyo vinaanzia *level 8* mpaka *10. NACTE* wanasimamia Vyuo ambavyo siyo Vyuo Vikuu hata kama vinatoa *degree* lakini viko chini ya *NACTE*, kuna *IFM,* kuna *Dar es Salaam Institute of Technology* na vinginevyo vyote vinatoa *degree* lakini viko chini ya *NACTE* kwa sababu sio *Universities* na *NACTE* wanaanzia *level 4* mpaka *level 10*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa *NACTE* wanaanzia *level 4* mpaka *10*, *TCU* wanaanzia *level 8* kuna haja kabisa ya ku- *harmonize* ili kuwe na udhibiti ambao unafanana. Vyote vinafanya kazi moja na hilo nafikiri ni la msingi sana. Kwa hiyo, lazima tuliangalie. Siyo kwamba *NACTE* wame- *concentrate* kwenye vyuo vya ufundi, tuna maana kwamba ni *specialized education, skills* ambazo zinatakiwa katika soko lakini ni kuanzia *level 4* mpaka *level 10.* Kwa hiyo mimi nafikiri vyote vinafanya kazi inayofanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana *NACTE* wanasimamia *certificate*, wanasimamia Diploma, wanasimamia *Degree, TCU* wanasimamia *degree* tu! Lakini vyote vinafanana, na mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ester. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ridhiwani

MHE. RIDHIWAN J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza niunge mkono hoja aliyotoa Mheshimiwa Susan Lyimo pale na ndugu yangu Zitto. Nafikiri watu hawajaelewa vizuri jinsi ya kutenganisha hivi vyombo viwili, pamoja na hilo nina jambo moja dogo nataka nilizungumze hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshuhudia katika historia ya maisha yangu ya Ubunge kwa mara ya kwanza *conflict of interest* iliyopo kubwa katika maisha ya Bunge hili. Asilimia kubwa ya Wabunge wako walioongea hapa kila mmoja ana-*declare interest* kwamba ana shule, nimeshangaa! Hawa watu wanachangia, hata *mandate* wanaitoa wapi? Unaweza kuwa Mbunge hukatazwi lakini jamani tuogope *conflict of interest,* sisi wengine tumesomea vitu hivyo! Sasa unapofika sehemu Mbunge unashindwa kujua….

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ridhwan, waki- *declare ineterest* Kanuni zinaruhusu. Endelea!

MHE. RIDHIWAN J. KIKWETE: Ah! Ah! Mimi sikatai katika suala la Kanuni. Kanuni zinawaruhusu, sawa! Lakini wanatetea maslahi yao tu! Yaani mtu ana *declare interest* ili apate nafasi ya kutetea maslahi yao. Sisi kama Wabunge humu ndani, *interest* yetu sisi ni kutetea shule za Serikali. Tumezungumza hapa, wakati tunasoma shule zilizokuwepo zinafaulisha sana, kulikuwa na hizi shule ambazo zinaitwa *special schools*..

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ridhiwani kuna hoja ya Mheshimiwa Mmasi.

MHE. RIDHIWAN J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nakuja huko!

MWENYEKITI: Muda wako unakwisha!

MHE. RIDHIWAN J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaniongelesha! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini leo hii tumefika sehemu…

(Hapa muda wa mchangiaji uliisha)

MWENYEKITI: Ahsante! Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyeki, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii, na nashukuru wale ambao wameniunga mkono, na niombe tu kumsihi sana ndugu yangu anirudishie shilingi kwa sababu zifuatazo, nimekiri kwamba kuna matatizo katika *TCU* na *NACTE* ambayo tayari tumeanza kuyafanyia kazi. Pia nakubaliana na yeye kwamba kunakuwa na mwingiliano wa majukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye kuwa kuna mwingiliano wa majukumu kwa sababu, kimsingi ukisoma ile sera ambayo ndiyo ilisababisha Sheria ya Baraza la Taifa la Ufundi kuanzishwa, ile sera imesema wazi kabisa kwamba litaundwa Baraza la Taifa la Ufundi kwa ajili ya kushughulikia mambo ya Mafundi Mchundo *(Technical Education)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Baraza la Taifa la Ufundi yenyewe ikaja kusema ni *technical and education,* kwa hiyo mimi nafikiri, tutakachokifanya ni kupitia labda pengine zile *mandate* na kuangalia yale majukumu ambayo pengine yanaleta kuingilia, kwa sababu hizi *NACTE* inaangalia fani zote ili

tuweze kufanya *harmonization*. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Ester anirudishie shilingi yangu hayo mapungufu tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante umejieleza vizuri Mheshimiwa Ester!

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu nashukuru kwa mchango mzuri wa Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa, yeye ni mtu makini sana kwenye suala zima la elimu, na ameonekana kuwa ni mtu mwenye utu, mtu mwenye kujali, pia tumeelezwa hapa amekuwa ni mchezaji wa kukodishwa mimi naunga mkono hoja, ninaomba kurudisha shilingi ya Mheshimiwa Waziri tuendelee na hoja zilizoko mezani.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Amina Mollel.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuzungumza. Matatizo ya watu wenye ulemavu ni mengi na hasa katika suala zima la elimu kwa watoto wenye ulemavu. Matatizo haya yanaanzia katika jamii. Mfano Kifungu cha 8(1) cha Sheria ya Mtoto namba 21 ya mwaka 2009 kinampa mzazi au mlezi wajibu wa kumtunza mtoto ikiwemo kumpatia haki elimu na malezi. Pamoja na hayo ndipo ambapo matatizo yanaanzia hapo kwa watoto wenye ulemavu, kwa sababu jamii yenyewe inaanza kwa kuwaficha watoto wenye ulemavu na wanakosa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale wanaobahatika kufika shule bado mazingira ni magumu miundombinu siyo rafiki, kwa watoto wengi wenye ulemavu unapokwenda katika shule za msingi, mazingira siyo rafiki kwao na hakuna tafiti zozote ambazo zimeweza kusaidia kutatua tatizo hili ili kuhakikisha watoto wenye ulemavu wanapata elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado vifaa ambavyo ni saidizi, mfano kwa watoto wasioona mashine zile, bado hazipo, hata kama zipo bado ni chache, Walimu wanaofundisha bado changamoto ni nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu ulemavu upo wa aina nyingi, lakini katika ulemavu

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mollel toa hoja yako muda wako umekwisha

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kwanza naomba niseme kabisa kwamba endapo sitopata majibu sahihi, majibu yatakayoniridhisha nitakamata shilingi ya Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Ahsante umeeleweka Mheshimiwa Waziri

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu nimhakikishie Mheshimiwa Amina Mollel kwamba suala la elimu maalumu nadhani nilisema katika hotuba yangu lakini hata katika majumuisho nimelielezea kwamba hicho ni kipaumbele. Nimeona anazungumzia kwamba imekuwa ni changamoto ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba anipe nafasi, kwa sababu hii ndiyo bajeti yangu ya kwanza nimeahidi kwamba nitaenda kutekeleza, anipe nafasi aachie shilingi yangu, ili nikatekeleze yale ambayo tayari nimekwishayaweka, kwa sababu akishikilia ina maana hawa watoto wataendelea kuteseka. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mollel!

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo bado sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri, kwa sababu changamoto hizi ni nyingi na upo Mfuko wa Watu Wenye Elemavu ulianzishwa na Sheria namba 9 ya mwaka 2010. Endapo mfuko huo ungetengewa fedha ungeweza kufanya tafiti mbalimbali na kuibua changamoto za watu wenye ulemavu ili ziweze kumsaidia Mheshimiwa Waziri kutatua tatizo hili bado naendelea kushikilia shilingi Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Ahsante

MHE. AMINA S. MOLLEL: Naomba kutoa hoja na nawaomba Waheshimiwa Wabunge, mnafahamu katika Mjimbo yenu popote mlipo, changamoto ni nyingi naomba mniunge mkono ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya mfuko huu, ili iweze kusaidia matatizo mbalimbali ya watoto wenye ulemavu.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Ikupa, Mheshimiwa Dkt. Macha, wanatosha, Mheshimiwa Ikupa *(Kicheko)*

MHE. STELLA IKUPA ALEX: Mheshimikwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba Serikali itajitahidi kadri iwezavyo kwa habari ya elimu kwa ajili ya kundi hili la watoto wenye ulemavu. Huyu mtoto mwenye ulemavu kama ambavyo Mheshimiwa Amina ameongelea, watoto hawa wamekuwa wakifichwa, kwa hiyo lazima kuwe na juhudi za maksudi za Serikali kuhakikisha kwamba inawabaini watoto hawa na inagundua watoto ambao wamefichwa. Kwa sababu kama yuko ndani atapataje hii haki ya elimu, mimi naunga hoja

mkono ya Mheshimiwa Amina kwamba Serikali ni lazima sasa itoe *commitment* kwamba itatumia njia zipi kuhakikisha kwamba hii elimu, inawafikia hawa watoto.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Ibara ya 11 huu ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba Kifungu cha tatu kuhakikisha kwamba kila mtu anapata fursa ya kupata elimu, kwa hiyo mimi niombe Serikali itoe *commitment* kwamba itafanya juhudi zipi kuhakikisha kwamba watoto hawa wanabainiwa na wanapatiwa hii elimu kama ambavyo Katiba yetu inaeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, Dkt. Macha

MHE. DKT. ELLY M. MACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi pia naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Amina kwamba tunahitaji *commitment* ya Serikali, ni jinsi gani sasa hii haitaendelea kuwa *story* ni kweli kwamba suala la watu wenye ulemavu linatengewa fedha za kutosha, haitaendelea kuwa kwamba ni suala la kuonewa huruma au la kujibiwa kwa kuturidhisha tu, au linaonekana kama hili suala ni la Wabunge wenye ulemavu tu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kaimu Waziri Mkuu, aah! hili suala ni zito linahitaji mtu mzito humu ndani.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Mheshimiwa Amina na wenzake, na Waheshimiwa Wabunge wote waliongea, kuwaeleza tu kwamba Rais wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa maksudi mazima, ameteua Viongozi wa Wizara hii kubwa, nyeti yenye mzigo mkubwa wanawake. Lengo ni kuhakikisha tu kwamba kwa kweli Wizara hii inapewa mwanzo mpya na sasa tuwape *commitment* ipi zaidi kuliko kmwangalia machoni huyu Profesa wa Elimu ambaye amepewa kuongoza hii Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hii ni bajeti ya kwanza kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano nawaombeni mtuamini, ili baada ya mwaka mmoja basi ndiyo mje sasa ku-*question* kama haya yanayosemwa hayatatekelezwa. Nawaomba Wabunge wote mtuamini tutaiweka sekta ya elimu katika sura tofauti kabisa, kwa sababu wote yuko *committed* na tumeshadhamiria kufanya hivyo kama Mheshimiwa Waziri alivyosema. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Kwa mujibu wa Kanuni 104 naongeza muda wa nusu saa Mheshimiwa Mollel.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kaimu Waziri Mkuu, na hapa yuko kwa niaba ya Waziri Mkuu, amelitamka hili na kwa kuwa pia katika Wizara yake ya Katiba na Sheria tunaye Naibu Katibu Mkuu ambaye ni mtu mwenye Ulemavu. Ninaamini na nikuombe tu Mheshimiwa Waziri wewe ni mwanamke, unaujua uchungu wa mwana, uchungu wa mwana aujuaye mzazi. Tunazungumza hivi kwa sababu haya matatizo tumeyapitia huko.

Mheshimiwa Waziri ninakuomba ninakurudishia shilingi yako. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa James Mbatia.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia suala la kisera, kwa sasa Wizara hii ya Elimu mfumo wake wa uandaaji wa sera, halafu ukitoka sera tunaenda kwenye mitaala, tukitoka kwenye mitaala ni muhtasari na vitabu. Katika suala la mitaala imekuweko dhana katika Taifa kwamba mitaala inabadilishwa mara kwa mara, dhana ambayo siyo sahihi. Katika Bunge hili, Bunge lililetewa mitaala ya elimu ikiwa na muhuri na Bunge likapiga muhuri wake kwamba nakala halisi mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 6 Machi, 2013 Serikali ikaji-*commit* kwamba itahariri au watafanyia maboresho, sasa mitaala waliyofanyia maboresho kumbe walikuwa na mitaala mingine ya 2007 wakati wanaleta hii hapa 2013, ni kwamba Wizara haiaminiki, Taasisi ya Elimu inasema uwongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha zaidi Kamishana wa Elimu ambaye yupo sasa hivi alishiriki katika mchezo huu, sasa Spika alivyotuita kwenye ukumbi wake, Serikali, Bunge wote waliokuwepo *Commissioner* wa elimu alikuwepo na amesaini kwenye mitaala huu ambao unaonekana ni wa 2007. Na licha ya maudhui na makosa yaliyoko ndani Taasisi ya Elimu sasa ndiyo imepewa jukumu hili, kazi yote Bunge iliyofanya 2013 bado makosa yako yale yale, ni kwamba hata jukumu la Bunge au Serikali ilivyotoa ahadi yake kwamba imefuatilia yote ya Wabunge wataenda kutekeleza hawakutekeleza, sasa naomba asipotoa majibu ya kuridhisha nitatoa shilingi, sera ya sasa hivi…

MWENYEKITI: Umeeleweka. Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimshukuru kabisa Mheshimiwa James Mbatia nimekuwa

nikimwona jinsi ambavyo amekuwa anafuatilia masuala ya elimu, amekuwa anafuatilia masuala ya vitabu, kwa hiyo anaonesha kabisa ana djhamira ya dhati na mimi namuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hii hoja ambayo ameileta sasa hivi labda ningeomba kwa sababu nyaraka alizonazo mimi sina, sijaziona kwa hiyo inakuwa kwangu ni vigumu kuzungumzia kitu ambacho sina. Kwa hiyo niombe Kiti kama kitaridhia Mheshimiwa Mbatia anipatie hizo nyaraka niziangalie *then* ndiyo nitaweza kuzungumzia hili jambo nashukuru Mwenyekiti. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakubaliana na wewe Mheshimiwa Mbatia utampatia nyaraka Waziri mtakaa, mimi ndiye ninaye *control* hapa, fursa yako endelea.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nyaraka hii Mheshimiwa Waziri unayo na nimeona ukiwa nayo, tuwe wakweli tu sera, nyaraka hizi uko na Wataalamu wako na nimezisema wakati natoa mchango ni za Taasisi ya Elimu unazo Mheshimiwa Waziri, tuwe wakweli tu, ni za Taasisi ya Elimu sijazitoa vichochoroni wala popote, ziko chini ya Wizara yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba tu *with due respect,* aseme kwamba Taasisi ya Elimu haiwezi ikafanya jukumu hili la kisera, jukumu la mitaala, jukumu la mihtasari, mpaka vitabu, na sera ya vitabu ya mwaka 1991 sasa wanarudisha huko huko wakati *EMAK* ilivunjwa hapa mwaka 2013, sasa tunahitaji *commitment* ya Waziri, naomba Wabunge wenzangu waniunge mkono kwenye kushika shilingi ya Waziri, ili jambo hili ni kwa maslahi endelevu ya Taifa ili Taasisi ya Elimu haina tena uwezo wa kusimamia mambo haya.

Mheshimiwa Mwennyekiti, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa AG, Mheshimiwa Suzan, Mheshimiwa Bobali, utaanza Mheshimiwa Mwigulu!

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono msimamo wa Mheshimiwa Waziri, ambao amesema mara nyingi, akiomba Wabunge wampe muda, kwa sababu ndiyo bajeti yake ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili alilolisemea Mheshimiwa Mbatia si hili peke yake ambalo Mheshimiwa Waziri ananuia kuyafanyia kazi, kwa hiyo kwa *modality* ya ili ile ya maeneo mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge wametoa rai kwa sauti kubwa na hili analolisemea Mheshimiwa Mbatia, tumwachie Mheshimiwa Waziri pamoja na mambo na mengine ili ayafanyie kazi kwa ujumla wake. Kwa sababu jambo la kubadilisha vitu hivi ambavyo ni vikubwa vikubwa halifanyikii hapa, bali Mheshimiwa Waziri kwa uzoefu wake na

weledi wake pamoja na timu yake, wataenda kuyafanyia kazi mambo haya yote yanayohusu kurejesha elimu katika ubora wake kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Mheshimiwa Mbatia ukitoa tu shilingi itakuwa haitoshi kusema kwamba ndiyo jambo hilo linafanyiwa kazi, lakini *commitment* ya Waziri kama ambavyo amesema kuanzia kwenye hotuba yake na hivi sasa ambavyo amewaomba Waheshimiwa Wabunge wengine waliokuwa na hoja zingine ni kitu ambacho kinatosha zaidi na kina uzito zaidi kwamba Mheshimiwa Waziri ataenda kufanyia kazi mambo haya kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miezi hii, tangia ateuliwe haingetosha kwa ukubwa na wingi wa mambo ambayo yapo haingetosha kuwa kila kitu awe ameshakifanyia kazi na sasa hivi hii ndiyo bajeti yake ya kwanza anaomba tumpitishie ili akakae na Wataalamu wake kuanza kuyafanyia kazi. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbatia nikuombe, umeshapaza sauti kama ambavyo wabunge wengine wamepaza sauti tumwachie Mheshimiwa Waziri akafanyie kazi mambo hayo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Bobali

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa James Mbatia ya kuendelea kuishikilia shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa kigezo kimoja tu. Kwamba uwepo wa Taifa letu hususani kwenye Taifa ambalo tunalitaka la viwanda, utategemea ubora wa elimu na malalamiko ya ufanyaji kazi usioridhisha wa Taasisi ya Elimu umekuwa ukitolewa mara nyingi ndani ya hili Bunge kwa Bunge la Kumi tulikuwa tunaangalia, lakini pia hata nje huko watu wanalalamika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri katika hili niombe tu uwe *responsible* kwa sababu Taasisi ya Elimu iko chini yako, malalamiko ya Watanzania juu ya chombo hiki yamekuwa ya siku nyingi, nilidhani kabla hujachukua hatua kwa *TCU* ungeanza hata na Taasisi ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naunga mkono hoja kwa sababu ni malalamiko yamekuwa mengi, *public opinion* zimekuwa nyingi, juu ya Taasisi ya Elimu naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Suzan

MHE. SUZAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba niunge mkono kwa dhati kabisa hoja ya Mheshimiwa Mbatia, naunga mkono kwa sababu Serikali haiko *committed* hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili Mheshimiwa Mbatia alilileta huku Bungeni toka mwaka 2013. Na hiyo *EMAK* inayozungumzwa ilivunjwa hapa Bungeni toka 2013 na Mheshimiwa Kawambwa mpaka leo naomba kuuliza Serikali, nani anayehariri na kuhakiki vitabu vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitabu viko hapa, vitabu kama hivi nimezungumza kwamba mtoto mdogo ubongo wake ni kama tabularasa kwamba kile kitu anachokipata mapema, ndiyo hicho hicho kinakaa kichwani. Leo hii kuna hizi picha za kishenzi kabisa, mtoto wa kiume ananyonywa na mtoto wa kike, mtoto wa darasa la nne kweli apewe kitabu kama hiki, siyo sawa sawa kwa hiyo hili analozungumza Mwigulu, kwamba Mheshimiwa Ndalichako amepata ofisi juzi, hii ni Taasisi yeye ni Taasisi, Wizara kwa hiyo mambo haya yalipaswa yawe yamesharekebishwa mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa kweli hoja hapa ni kwamba Taasisi ya Elimu Tanzania, kazi yake ni kuendeleza mitaala na siyo kutunga vitabu. Mimi naunga hoja mkono kwa sababu mitaa ndiyo ya msingi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa AG.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba kushauri nimesikiliza mchango wa leo uliwaunganisha Wabunge wote wa kambi zote mbili na wametoa ushauri mzuri sana kwa Serikali. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Ibara ya 63(2) inasema kwamba Bunge ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii, na kwamba, kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka yake Bunge laweza; (d) Kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, leo Bunge limetekeleza wajibu wake. Moja, wajibu wa kuisimamia Serikali na kuishauri. Waheshimiwa Wabunge naomba kushauri, Mheshimiwa Mbatia ameishauri vizuri sana Serikali, na ana vitabu hapo, ambacho sasa Serikali inaomba kwamba itupatie hivyo vitabu, ili tu…

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Aah! *No! No! No!* hiyo ya kwanza!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kwamba, naomba kushauri kwamba, Mheshimiwa Mbatia akubali…

MWENYEKITI: Mheshimiwa AG, zungumza na Kiti.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa sawa! Mheshimiwa Mbatia, akubali kutoa hivyo vitabu alivyonavyo Serikalini ili Serikali iviangalie. Kwa sababu, kimsingi Waziri ameshaji-*commit* kwamba, Serikali itafanyia kazi mambo haya hakuna sababu ya msingi kwa sababu, Bunge limeshaisimamia Serikali, limeishauri, hilo la kwanza Mheshimiwa! Eeh! Na ndiYo namna sasa unaishauri Serikali.

MWENYEKITI: Ahsante.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wameishauri na Bunge limeishauri Serikali ili itekeleze! Sasa kuna udhaifu anaousema Mheshimiwa Mbatia, kuna udhaifu! Mwenzie anasema leta tutekeleze sisi! Kwa hiyo, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; analolitaka Mheshimiwa Mbatia kwamba, Waziri atamke hapa kwamba, hiyo haina sababu yoyote ya kuwepo! Hili ni suala la Kisera, Serikali inafanya maamuzi ya haya Kisera kwa pamoja, taasisi imeanzishwa kwa sheria! Aah, suala la sheria utaliamuliaje hapa! Waziri ataliamuliaje hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba kumshauri Mheshimiwa Mbatia amrudishie Mheshimiwa Waziri shilingi yake, ili sasa ushauri huu mzuri ambao Waheshimiwa Wabunge wameishauri Serikali, Serikali iende kutekeleza. Na huo ndiyo ushauri wangu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri! Mheshimiwa Zitto, sikukuweka kwenye orodha!

MHE. ZITTO Z. KABWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo. Siyo kwa ajili ya kuchangia, ninauliza kuhusu utaratibu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo la elimu halihitaji ushabiki wa kisiasa, ni jambo ambalo linahitaji tupate jawabu litakalotatua tatizo. Wala hamna sababu ya upande mmoja ku-*panic,* upande mwingine kutoku-*panic!* Hili ni jambo ambalo linahitaji tupate jawabu na busara inahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nakuomba umruhusu Mheshimiwa Mbatia na Mheshimiwa Waziri waje kwenye Kamati tuweze kujadili jambo hili, ili tuweze kulipatia ufumbuzi, *and in the mean time,* Mheshimiwa Mbatia

umuachie Mheshimiwa Waziri ili mtakapokuja kwenye Kamati tuweze kulitatua jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni Makamu Mwenyekiti wa hii Kamati, Waziri Kivuli ni Mjumbe wa hii Kamati inayohusika na elimu, naamini kabisa tutapata suluhisho badala ya kulumbana humu ndani bila suluhisho lolote. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Mwenyekiti tuweze kuendelea. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri Simbachawene!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya tu utukutu nika-*cross* hapa kwenda kuangalia hicho kinachosemwa na Mheshimiwa Susan Lyimo kwamba ni mtoto wa kike anamnyonya mtoto wa kiume! Neno ambalo kwa kweli kusema ukweli, siyo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema ukweli, kinachofanyika pale ni eneo ambalo wanafundishwa huduma ya kwanza…

MBUNGE FULANI: *First Aid!*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *first aid!* kwa hiyo, kinachoonekana pale ni kile kinachofundishwa. Sisi tulioona kwenye mafundisho ya namna hiyo, huwa kinafundishwa hata mtu ikitokea ame-*collapse* hapa unamuongezea *oxygen* kwa kumpulizia! Ni kitu cha kawaida kabisa, haimaanishi iwe ni wa kiume au wa kike, lakini kuonekana neno hili linasemwa na Mbunge ambaye ninamfahamu na kutumia kwamba, anafanya hivyo badala ya kusema anampulizia kwa sababu imeandikwa pale ni huduma ya kwanza! Inaonekana kuna *malice* nyuma yake sasa.

MWENYEKITI: *Point* yako ninakushukuru! *Point* yako ni muhimu. Mheshimiwa Waziri ukubali kuja kwenye Kamati, *simple as that!*

WAZIRI WA ELIMU ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nirudie kusema siyo kwamba ninapingana na hoja aliyoitoa Mheshimiwa Mbatia, lakini nilikuwa nimeleta ombi ambalo nadhani ni ombi la msingi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili niweze kufanyia kazi hayo mambo ni muhimu nikaona kile kilichowasilishwa. Kwa hiyo, niseme tu *commitment* ya Serikali ni

kwamba, tutafanyia kazi hilo jambo baada ya kupata zile nyaraka tutaziangalia na tutafanyia kazi baada ya kuziona, nashukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru. Mheshimiwa Mbatia!

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyokuwa nachangia niliomba sana itikadi tuweke pembeni. Tarehe 04/03/2013 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ikulu nilipeleka vitabu sanduku zima nikamkabidhi Rais! Prof. Eustellah Bhalallusesa ni Kamishna wa Elimu, yupo mpaka leo hii, vitabu vyote alikabidhiwa! Bunge hili lilikabidhiwa vitabu vyote!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, *with due respect,* najua hii ni Serikali nyingine imekuja, lakini muendelezo wa Serikali ni ule ule. Sasa tukiweka itikadi hapa hatuisaidii nchi, mimi nasema kutoka sakafu ya moyo wangu, wala sina itikadi ya aina!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na rai kwamba, tuje kwenye Kamati tuokoe Taifa hili la Tanzania hapa tulipofika sasa hivi. Narudisha shilingi yangu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa George Lubeleje!

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina shida ya mshahara wa Mheshimiwa Waziri, ninachotaka ni maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango wa kukarabati shule kongwe za sekondari saba, sasa mimi nilikuwa namuomba Waziri kwanza azitaje shule hizo halafu vigezo alivyotumia kuchagua hizo shule saba, kwa sababu shule nyingi kongwe zimechakaa ikiwemo Shule ya Sekondari ya Mpwapwa, tangu mwaka 1926 sasa ina umri wa miaka 90! Shule zinachakaa, Bunge linapitisha bajeti, kwa nini hawazikarabati hizi shule, leo unachagua shule saba tu? Nataka maelezo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri maelezo.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka tu kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba, ninaamini yeye kwanza anatoka Jimbo la Mpwapwa. Kwenye Hotuba yangu nimeainisha shule 33 ambazo zitafanyiwa ukarabati awamu ya kwanza na Mpwapwa ikiwemo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema katika hotuba yangu kwamba, katika mgawanyo wa majukumu suala la miundombinu liko TAMISEMI, mimi nimeshika Sera. Lakini kwa kutambua changamoto ambazo ziko katika sekta ya elimu

nikaona kwamba, hata zile fedha ambazo tumeletewa kama Wizara yangu za kuendeleza elimu katika maeneo ambayo ndiyo ya msingi ya Wizara yangu nitumie fedha hii niweze kuboresha miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kwamba, shule zote kongwe tutaziboresha, na kwa kuanzia tunaenda na shule 40, shule 33 ziko katika huu mwaka wa fedha ambao tunaumaliza ndiyo maana hazionekani katika vitabu ambayo na Mpwapwa ipo, hizi saba katika mwaka ujao. Hayo ndiyo maelezo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kafumu!

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mimi naomba kupata maelezo, nilitaka kushika shilingi lakini kwa maelezo ya Mama anaonekana yuko *honest* sana. Naomba nipate maelezo kuhusu ubora wa elimu unavyosimamiwa. Ukurasa wa 18 wa bajeti yake hapa anazungumzia shule 7,882 zilizokaguliwa kati ya 17. Nilifanya mahesabu ni chini ya nusu ya shule zilizokaguliwa, hii haithibitishi kwamba kwa kweli tunasimamia ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mfano wa pili, bajeti yenyewe ni shilingi bilioni 24 kwa ajili ya Idara ile ya Ukaguzi. Tunazo Wilaya zaidi ya 160, tuna Kanda 11, hizi shilingi mishahara ni bilioni 21, kwa hiyo zinabaki bilioni 2 pale ambazo hazitoshelezi kabisa! Tukienda kwenye Wilaya zetu Wabunge wote ni mashahidi, Idara za Ukaguzi zile wamekaa tu hawana gari, hawafanyi kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi naomba Mheshimiwa Waziri utusaidie, ufikirie kuongeza fedha kama inawezekana kwa ajili ya ukaguzi, kwa sababu nawaomba na Wabunge jamani tusaidiane, tumuombe Mheshimiwa Waziri kwa namna yoyote ile atoe *commitment* ya kutafuta fedha. Hata kama baadaye huko mwezi wa kwanza kama tunaweza kuja kwenye bajeti ndogo, basi tufanye hili jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho…

MWENYEKITI: Aah ni jambo moja tu Mheshimiwa Mbunge!

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa swali ambalo ameuliza Mheshimiwa Mbunge. Niseme tu kwamba, suala la ukaguzi tunalipa kipaumbele na katika hii fedha ambayo tumeiweka ukiangalia Fungu 210211, tumetenga fedha ambazo ni bilioni 21 kama anavyosema, lakini pia katika Kifungu cha *Learns*, tunao mpango wa *Learns* ambao una-*support* kusoma, kuandika na kuhesabu. Vilevile kutakuwa na fedha ambazo zitatumika katika kuongeza mafuta, lakini tutakapokuja katika Kitabu cha Maendeleo ambacho hakijafika kwa sasa hivi, utaona kule kwamba, Ukaguzi tumeipatia pia fedha za kuendelea kuboresha. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba, hilo suala la Ukaguzi tutalifanyia kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusiana na idadi ya shule zilizokuwa zimewekwa lengo na shule zilizokaguliwa, nikiri tu kwamba hilo lengo lilikuwa *over ambitious* kwa sababu hizo ndiyo idadi ya shule zote! Haiwezekani ukague shule zote zilizoko nchini kwa mwaka mmoja. Kwa hiyo, tulizokagua 7,000 na kama tukiendelea kwa utaratibu huu, mimi nadhani ni namba nzuri tu ambayo itatuwezesha katika elimu yetu inavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kafumu!

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa maelezo. Naomba basi niendelee kushauri kwamba, Idara ya Elimu muibadilishe kuwa Mamlaka kama mlivyofikiria sijui liliishia wapi? Miaka mingi tumelia!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili la mwisho la ushauri ni kwamba, hizi Kanda 11 mlizoanzisha naomba mzianzishie *Sub Vote* zote kama tulivyofanya Wizara ya Nishati na Madini. Tulikuwa na *Sub Vote* moja kwa Kamishna ilikuwa inahudumia Kanda, ilikuwa ngumu sana, lakini tulipoanzisha *Sub Vote* kwa kila Kanda ilisaidia. Basi na ninyi mkianzisha itasaidia kuhudumia ukaguzi kwenye Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Bobali

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ninaomba kupata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kwenye Vyuo vya Ualimu vya *Certificate* na *Diploma* Walimu hawa tarajali wanafundishwa mafunzo kwa vitendo na yale ya darasani. Mafunzo ya vitendo ambayo ni *BTP (Block Teaching Practise)* kwa miaka miwili yalikuwa yanayumba, yalikuwa yanaendeshwa kwa wiki tatu badala ya siku 60! Kauli ya Serikali ilikuwa ni

kwamba, kilikuwa ni kipindi cha mpito, pesa hazikuwepo za kuendesha mafunzo ya *BTP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze hali ya mwaka huu ikoje? Je, tathmini ya kielimu ikoje kuhusu wale Walimu ambao walipata mafunzo ya *BTP* ya wiki tatu badala ya siku 60 kama ambavyo utaratibu ulivyo? Naomba maelezo ya Mheshimiwa Waziri, nisiporidhika na majibu yako Mheshimiwa Waziri, nitakamata mshahara wako. *(Makofi)*

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana Mheshimiwa Bobali, tunakaa tunatazama, naomba usikamate shilingi yangu! Tafadhali!*(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mafunzo ya wanafunzi, *Block Teaching Practise* mwaka huu yamefanyika kwa wiki 10. Nimhakikishie kwamba, katika mwaka huu pia, tuko vizuri, atakapoangalia katika Kifungu 220800 tumetenga shilingi bilioni 3.9 na kulingana na idadi ya wanafunzi waliopo ili wafanye mafunzo hayo katika kipindi cha wiki 10 kama ambavyo inatakiwa. Naomba usishike shilingi yangu! *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bobali!

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, naye Mama ameniomba sana, utu umeniingia kwa hiyo, ninamuachia shilingi yake, nataka nimshauri jambo moja.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshauri tu kwamba wakati mwingine kunatolewa matamko ambayo yana mkanganyiko juu ya uendeshaji wa hivi Vyuo vya Ualimu. Mwaka 2014 aliyekuwa Waziri wa Elimu alitangaza kufuta Mafunzo ya Cheti ya Ualimu kwa Ngazi ya Cheti, jambo ambalo naona bado linaendelea! Alitangaza akiwa Tabora ilikuwa tarehe 27 mwezi wa Februari. Hili ni jambo ambalo lilizua mkanganyiko mkubwa sana. Kwa hiyo, wewe kwa sababu, umesomea haya mambo usiwe tena na wewe ukaingia kwenye mkumbo wa kutoa matamko ambayo mwisho wa siku yanayumbisha sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Kifungu hiki Kinaafikiwa? Haya, dakika 5 zimebakia, Mheshimiwa Susan!

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo *fair* kwa sababu, tuko ki-vyama na umewapa CCM mara tatu, sisi huku bado!

Mheshimiwa Mwenyekiti…

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan, tunakwenda na *total*.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, lakini nilikuwa naomba maelezo, Wabunge karibia wote humu ndani na niseme wote wameongelea suala la Walimu. Matatizo makubwa ya Walimu hapa nchini kwamba, Walimu hawapati mishahara yao kwa wakati, Walimu hawapandishwi madaraja! Vilevile upungufu mkubwa wa Walimu, ajira hawajapata mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nakumbuka katika Bunge hili, tuliomba na tukaahidiwa kwambwa, Bodi ya Walimu itaundwa *(Teachers' Professional Board),* mpaka leo hilo jambo halijafanyika, naomba kujua ni kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baya zaidi sasa hivi Wizara imekuja na utaratibu mpya wa kuendelea kuwadhalilisha Walimu. Walimu sasa hivi wametoka Wizara ya Elimu wamepelekwa *NACTE*, wametoka kwenye Kitengo chao pale, wamepelekwa *NACTE*! Sasa hivi Walimu watakuwa wanaangaliwa *(treated)* kama Mafundi Mchundo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba maelezo, kama sitapata maelezo ya kuridhisha Mheshimiwa Waziri, nitashuka shilingi ni lini matatizo ya Walimu yataisha?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Utumishi na Utawala Bora amelizungumzia hili suala la maslahi ya Walimu na jinsi ambavyo Serikali imekuwa ikiwalipa Walimu stahili zao pamoja na upandishaji wa madaraja. Mimi ningependa kuzungumzia suala la *Teachers' Profession Board* pamoja na suala la *NACTE* ambalo pia tulikuwa tumeshalizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *Teachers' Professional Board* Wizara yangu inalifanyia kazi na tunakusudia kuwa na Bodi ambayo itakuwa inaangalia viwango vya Walimu. Naomba nitoe *commitment* kwamba, katika Bunge lijalo Wizara yangu italeta hapa Muswada wa kuanzisha *Teachers' Profession Board. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la Walimu wameenda *NACTE* na kwamba, Je, Walimu ni Mafundi Mchundo? Nadhani nilipokuwa najibu hoja ya Mheshimiwa Ester Mmasi nimelieleza Bunge lako kwamba, kuna mambo ambayo tutaenda kuyaangalia, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Susan

Lyimo usishike shilingi yangu, tutafanyia kazi. Hata hili suala la Walimu, maana tunazungumzia hapa na Mheshimiwa Bobali anasema nisiwe mtu wa kutoa matamko! Naomba nisitoe tamko lolote hapa, mniruhusu nikafanyie kazi halafu nikitoa tamko liwe linazingatia na wadau niwashirikishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Susan usishike shilingi yangu tafadhali! *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan umeombwa na Mama! pia wewe mwanakamati mwenzie! *Classmet! (Makofi)*

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri. Ninaamini hili suala la *Teachers' Profession Board* kama alivyosema litaletwa ndani ya Bunge na siyo udanganyifu kama *last time! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kwa kweli, hiki chombo ndiyo pekee kitaondoa matatizo makubwa ya Walimu na ninaamini Wabunge wote huku wanaelewa hilo. Kwa hiyo, naomba sana hili jambo kama halitaletwa nitaendelea kulishikilia mwakani, Mungu akipenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru kwa busara zako, Kifungu hiki kinaafikiwa?

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 *Finance and Accounts*….....Sh. 701,560,140
Kif. 1003 *Policy and Planning*…….....……Sh. 1,029,720,176
Kif. 1004 *Internal Audit Unit*…….....…Sh. 283,481,000
Kif. 1005 *Procurement Mgt Unit*….....……...Sh. 310,491,617
Kif. 1006 *Gvt. Comm. Unit*….....Sh. 70,012,200
Kif. 1007 *Legal Unit*…….....Sh. 97,416,114
Kif. 1008 *Info. Comm.Tech and E-learning*.....Sh. 120,040,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2001 *Basic Education Dev. Office*….....Sh. 61,796,493,390

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwakibete!

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naitwa Frank Mwakajoka.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwakajoka, samahani bwana!

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka nipate ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kutokana na Kifungu hiki kwenye *item* ya 221700. Kwa sababu mwaka jana ilikuwa bilioni 4,400, mwaka huu iko bilioni 10,500. Ongezeko hili ni kubwa sana, lakini na Kifungu hiki inawezekana Mheshimiwa Waziri anaweza akawa amepanga hizi fedha kwa ajili ya kuwalipa Wazabuni wetu ambao kumekuwa na madeni makubwa sana, kwa hiyo tunataka atueleze kwamba fedha hizi atakwenda kuwalipa hawa Wazabuni na fedha zitakazobaki zitawahudumia wanafunzi wetu, zitahudumia vyuo vyetu bila kuwa na madeni tena katika mwaka ujao? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu!

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la fungu hilo kama alivyosema Mheshimiwa ni kwamba tumeweka fedha kwa ajili ya kuweka chakula kwa vyuo vyote 35 vya Ualimu, ndiyo maana ya ongezeko.

(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kutokana na muda tunaingia katika *guillotine* Kanuni ya 104.

Kif. 2002 *School Quality Assurance*……..…..Sh. 24,083,900,324
Kif. 2003 *Reg & Inter.Edu Affairs Coord Unit*.....Sh. 98,413,994
Kif. 2004 *Edu. Sector Perfo. Coord Unit*…….....Sh. 66,244,000
Kif. 3001 *Basic Education*…….....Sh. 306,012,000
Kif. 3002 *Adult Edu. & Non Formal Educ*…....Sh. 745,575,600
Kif. 4001 *Secondary Education*……..…...Sh. 289,140,000
Kif. 5001 *Teacher Education*……..……Sh. 29,518,317,600
Kif. 7001 *Higher Education*…….....Sh. 269,615,100,174
Kif. 7002 *Techn. and Voc. Training Div*…...Sh. 68,377,901,919
Kif. 8001 *Science. Tech. and Innovation*….Sh. 36,271,391,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu – 46 Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi

Kif. 1001 *Adm. and HR. Mgt*….....Sh. 1,500,000,000
Kif. 1003 *Policy and Planning*……..….Sh. 100,012,731,083
Kif. 1008 *Info. Comm.Tech and E-learning*.....Sh. 500,000,000
Kif. 2001 *Basic Edu.Dev. Office*…….....Sh. 156,739,219,546
Kif. 2002 *School Quality Assurance*……Sh. 8,700,000,000
Kif. 3001 *Basic Education*…….....……..Sh. 0
Kif. 4001 *Secondary Education*…….....…Sh. 7,000,000,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif. 5001 *Teacher Education*……..……Sh. 23,000,000,000
Kif. 7001 *Higher Education*……...……Sh. 568,022,572,136
Kif. 7002 *Techn. &Voc. Training Div*….....Sh. 9,200,000,000
Kif. 8001 *Science, Tech. and Innovation*….....Sh. 22,983,024,860

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. NENELWA WANKANGA- KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

(Bunge Lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja taarifa!

TAARIFA

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake. Hivyo basi, naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa mwaka 2016/2017 yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, Bajeti imepita. Ahsanteni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri nachukua nafasi hii kukupongeza na timu yako, nakupa pole kwa Naibu wako, lakini mmefanya kazi nzuri. Changamoto zipo tunaamini kwa namna mlivyojipanga na Serikali hii ilivyojipanga haya mambo yatakwisha. Vilevile nikupongeze wewe mwenyewe kwa uwezo wako umekuwa *women of substance. (Makofi)*

Matatizo ambayo yako kwenye Majimbo yetu Waheshimiwa Wabunge, tujaribu kuisaidia Serikali kwenye Halmashauri, yako matatizo mengi sana kwenye Halmashauri. Tusitegemee kila kitu itafanya Serikali, sisi ni sehemu vilevile ya kutatua matatizo ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninaahirisha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 2.25 Usiku, Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumamosi, Tarehe 28 Mei, 2016, Saa Tatu Asubuhi)